

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 9 Mei, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 120

Kujenga Wodi ya Wazazi Kituo cha Afya Chiwale

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi ya wazazi (*maternal ward*) kwenye Kituo cha Afya Chiwale kwa kuwa wazazi hujifungulia kwenye chumba kilichomo ndani ya jengo ambalo pia hutumika kulaza wagonjwa wa kiume na kike?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMESEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Afya Chiwale hakina wodi ya wazazi na hali hiyo niliishuhudia mwenyewe nilipofanya ziara kituoni hapo mnamo tarehe 9 Januari, 2016 ili kujionea hali ya utoaji wa huduma kituoni hapo. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Halmashauri imetenga shilingi milioni 80 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya, Chiwale. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 20 zinatokana na mapato ya ndani ya Halmashauri na shilingi milioni 60 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu ambazo bado hazijapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuharakisha utekelezaji wa mpango huo, Halmashauri imeshauriwa kutumia fursa ya Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) ili kupata mkopo utakaowezesha kujenga jengo kila maabara na wodi ya kisasa ya wazazi kutokana na ukosefu wa miundombinu hiyo muhimu katika kituo hicho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Nataka kufahamu pia kuhusiana na mgogoro wa wafanyakazi uliopo katika Hospitali ya Ndanda. Serikali iliahidi itaajiri wafanyakazi 85 na wale Wamisionari sasa hivi wameamua kupunguza wafanyakazi 59 kwa sababu Serikali haijatekeleza ahadi yake toka mwaka 2012 hali inayotishia kuifanya Hospitali ya Ndanda isiwe tena Hospitali ya Rufaa katika eneo la Kusini. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kutekeleza ahadi yake ya kupeleka pesa kwa ajili ya wafanyakazi wa Ndanda Hospitali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu pia ni lini Serikali italipa pesa za fidia katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa vile katika vitu vilivyoharibika ni pamoja na gari la wagonjwa la hospitali ya Chiwale ili waweze kujinunulia wenyewe tena lile gari liweze kusaidia baada ya kujenga wodi ya akinamama katika eneo lile? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la changamoto ya watumishi ni kwamba Serikali tumelichukua. Sasa hivi tuna mchakato wa kuajiri watumishi mbalimbali

katika Halmashauri zetu na Wizara ya Afya ina-finalize stage hiyo. Nina imani kwamba siyo muda mrefu ndani ya mwezi huu wa Mei na Juni tutaenda kupunguza hii gape ya watumishi, lakini changamoto ya Ndanda tutakwenda kuifanyia kazi. Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kulifanyia kazi kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *ambulance* zilizoungua, ni kweli na mimi mwenyewe nimefika pale. Pale kuna *ambulance* tatu zilichomwa moto na kwa njia moja au nyingine siyo kwamba Serikali ni ya kulaumiwa. Katika hili, naomba nitoe maelekezo kwa wananchi, inawezekana kwa jazba zetu tunaharibu vitu ambavyo vilikuwa kwa maslahi ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi kile pale Mtwara watu walienda kuchoma *ambulance* ambazo zinabeba akinamama na watoto. Fikiria mtu anachukua kibiriti na *petrol* anakwenda kuchoma *ambulance* tatu mpya, unategemea nini katika mazingira hayo? Kwa kweli ni jambo lenye kuhuzunisha na ndiyo maana nilipofika pale Masasi nilienda kutembelea maeneo yake, kwa kweli ni jambo la kuhuzunisha, lakini Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaangalia jinsi gani tutafanya kwa sababu mwisho wa siku ni wananchi na akinamama ndiyo wanaopata shida zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalichukua hili kwa upana wake lakini kwa kweli kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumesikitika sana kwa sababu ile ni fursa ambapo wananchi walikuwa wanapata huduma kila siku. Naomba nitoe onyo kwa watu wote, tusichukue jazba zetu mbalimbali tukazielekeza katika vitu ambavyo vinawasaidia wana jamii kupata huduma bora katika maisha yao. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Grace Kiwelu.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda kuuliza ni lini wodi ya wazazi katika Hospitali yetu ya Mkoa ya Mawenzi itakamilika kwa sababu imejengwa kwa zaidi ya miaka mitano na inakuwa ni kero kwa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI kuna Waziri anataka akusaidie kidogo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukamilika kwa wodi ya wazazi katika hospitali ya Mawenzi, Moshi ni suala la kipaumbele kwenye Serikali ya Awamu ya Tano. Wiki takribani tatu zilizopita nilifika pale na kuona hatua ya ujenzi iliyofikiwa na tukashauriana na uongozi wa hospitali ile na kukubaliana kwamba kwa mwaka huu wa fedha waombe wapewe bajeti maalum kwa ajili

ya kukamilisha sehemu ya jengo hilo ambayo itatoa huduma kwa akina mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile watumie mikopo inayopatikana kwenye taasisi mbalimbali za kifedha ili wakamilishe ujenzi huo mara moja sasa hivi kuliko kusubiria huu utaratibu wa kutumia bajeti. Tayari wameanza mchakato huo kupitia Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Said Meck Sadick kwa kufanya mazungumzo na Benki ya TIB.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, Halmashauri zinatofautiana kimapato na Kituo cha Afya cha Nyambiti hakina gari, ni utaratibu gani sasa utumike ili kituo hiki kiweze kupata gari kwa sababu uwezo ni mdogo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la upatikanaji wa gari katika vituo vya afya, tulipokuwa tunapitia mchakato wa bajeti yetu ya mwaka huu 2016/2017, tulikuwa tukifanya *analysis* ya halmashauri mbalimbali katika suala zima la sekta ya afya, kila halmashauri iliweka kipaumbele chake. Kuna wengine waliweka kipaumbele cha ujenzi wa miundombinu, kwa mfano kwa ndugu yangu pale zahanati aliyosema ya Chiwale, wametenga karibuni milioni 287 kwa ajili ya kituo kile cha afya. Wengine kipaumbele chao walichoweka ni ununuzi wa gari la wagonjwa. Kwa hiyo, vipaumbele hivi vinatofautiana kati ya zahanati na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Ndassa kwa sababu sijajua kipaumbele walichoweka katika eneo hili, sisi na wenzetu wa Wizara ya Afya tutaangalia katika bajeti ya mwaka huu tumegusa vipi katika eneo hilo. Mwisho wa siku ni kwamba, lazima kwa umoja wetu wote tuangalie jinsi gani tutafanya maeneo kama hayo ambayo wananchi wanapata shida waweze kupata fursa za kuwa na gari la wagonjwa ili mama akipata matatizo aweze kupelekwa hospitali ya karibu kupata huduma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndassa naomba tulichukue hili tujadiliane kwa pamoja na kuangalia bajeti yenu ya halmashauri mlipanga vipi kama vipaumbele vyenu vya awali.

Na. 121

Uwepo wa Wakunga Wanaume katika Zahanati

MHE. RIZIKI S. MNGWALI aliuliza:-

Kwa mila zetu za Kiafrika imezoeleka kuwa huduma ya ukunga kwa akinamama wajawazito wakati wa kujifungua hutolewa na wataalam wanawake:-

Je, Serikali haioni kuwa kwa kuweka Wakunga wanaume katika baadhi ya zahanati za Serikali nchini ni kuwadhalilisha akinamama wajawazito wanaojifungua katika zahanati hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakunga wote nchini wanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Uguzi na Ukunga ya mwaka 2010. Kwa mujibu wa sheria hiyo, Mkunga ana wajibu wa kutoa huduma ya kumsimamia mama mjamzito wakati wa uchungu, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua. Kwa mujibu wa sheria hiyo, Wakunga wote wa kike na wa kiume wanaruhusiwa kutoa huduma ya ukunga baada ya kufuzu mafunzo yao na kupata leseni ya kutoa huduma hizo kutoka katika Baraza la Uguzi na Ukunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, japo Sheria ya Uguzi na Ukunga inampa mtaalam aliyefuzu masomo hayo kutoa huduma lakini kumekuwepo na changamoto kwa baadhi ya wanajamii kutokana na mila na desturi zinazotawala jamii husika. Kutokana na hali hiyo, Serikali itaendelea kuajiri wataalam wengi ili pale penye changamoto iweze kupatiwa ufumbuzi bila kuwakwaza wanajamii husika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Riziki Mngwali swali la nyongeza.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza hasa kwa kuwa majibu hayakutosheleza haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunarudi pale pale kwenye kutoa huduma stahiki na kuajiri wahudumu stahiki, siyo suala la kuajiri wengi bali waajiriwe Wakunga ambao wanaendana na mila na desturi zetu na wale ambao wanakidhi haja. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba Serikali hii ya CCM imekuwa inafanya mambo yake kanyaga twende tu na siyo kwa kufuata taratibu maalum?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali hii ya CCM itakubaliana na mimi nikisema kwamba haiendani na matamko yake? Leo hii gazeti linaandika kuboresha huduma za uzazi lakini wanatuambia wataendelea kutuwekea Wakunga wanaume kwa kuwahudumia wanawake. Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali ya Chama cha Mapinduzi haifanyi mambo yake ya kanyaga twende. Hapa nilizungumzia sheria inasemaje kwa sababu kama Majaji Naibu Spika mna taratibu na sheria zenu. Nimeshangaa sana, kuna sehemu nyingine sasa hivi hata ukiangalia kuna *ma-gyno* wengi sana akinamama lakini siku nyingine wanaenda kwa *ma-gyno* wa pande zote mbili. Niseme kwamba siku zote Serikali inalenga kuona ni jinsi gani itawasaidia wanajamii kupata huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na dhana nzima ya kusema kwamba tuwe tunaajiri watumishi wa kike na wa kiume, nimesema kwamba tutaendelea kuajiri na ndiyo maana nimesema jamii zetu zinatofautiana. Kuna maeneo mengine ambayo inaonekana kwa mila na desturi zao itabidi tuweke watu wa aina fulani na sisi tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge katika Mkutano uliopita aliuliza swali hili hili na nilitoa maelekezo. Bahati nzuri hapa tumepata takwimu wataalam wangu wa afya na RMO wetu wa Mkoa baada ya agizo lile waliweza kufanya mchakato katika kila zahanati takribani nane wameweza kubadilisha wale wataalam kutokana na swali lako mama la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimepata taarifa hizo lakini nitaenda kufanya *verification* mwenyewe kuona hali ikoje, lakini taarifa nilizopata toka wiki iliyopita ni kwamba walifanya mchakato huo na zile zahanati ambazo mwanzo zilikuwa na wataalam wa kiume peke yake sasa hivi wamepeleka na wataalam wa kike lengo likiwa ni kuwasaidia akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa Wilaya ya Mafia, napenda kuwashukuru sana kwa mchakato mlioufanya wa kupata mashine mbalimbali. Tulikuwa na tatizo la *X-ray* na *Ultra-sound machine*, Mbunge wao Mheshimiwa Dau amefanya harakati watapata *Ultra-sound* na *X-ray machine* mpya, zimeshafika Dar es Salaam sasa hivi wanaendelea na taratibu za kuzisafirisha kwenda Mafia. Kwa hiyo, tutaendelea kuenzi juhudi kubwa zinazofanyika lakini Serikali itajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo wananchi wapate huduma bora.

NAIBU SPIKA: Tuendeleo Waheshimiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 122

Ujenzi wa Kiwanda cha Matunda - Muheza

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Wilaya ya Muheza ina utajiri wa uzalishaji wa matunda kama machungwa, maembe, machenza, mafenesi na kadhalika:-

Je, ni lini Serikali itajenga kiwanda Wilayani hapo cha kutengeneza juisi na kuwaondolea usumbufu wakulima hao wa kutafuta soko?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya jukumu la Serikali katika kujenga viwanda ni kwa Serikali kuweka mazingira sahihi na wezeshi ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje wa sekta binafsi kujenga viwanda. Katika kutekeleza hilo, sera na mkakati mbalimbali shirikishi inatoa fursa kwa sekta binafsi na taasisi za uwekezaji kujenga viwanda na kunufaika na vivutio mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga ikiwemo Wilaya ya Muheza wamejaliwa kuwa na utajiri wa matunda aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na machungwa, maembe, machenza, mafenesi, mananasi kwa kutaja baadhi. Kwa kutambua upatikanaji huo wa matunda, Wizara yangu inahimiza na kuhamasisha wawekezaji kutoka sekta binafsi wenye nia ya kufungua viwanda vya juisi Mkoani Tanga ikiwemo Wilaya ya Muheza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa kampuni ya *SASUMUA HOLDING* imeanzisha mradi mkubwa wa kulima matunda katika utaratibu utakaoshirikisha wananchi (*out grower*). Mradi huo ulioko Kwamsisi – Handeni, Mkoani Tanga ni matengemeo yangu kama ukifanikiwa, wawekezaji wengine watafutwa na kuweza kuwekeza eneo hilo la Tanga na sehemu nyingine za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kupitia Shirika la Viwanda Vidogo (*SIDO*) lina utaratibu wa kutoa ushauri jinsi ya kuanzisha mitaa ya viwanda kila mkoa ikiwa ni jitihada za kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuendeleza uzalishaji katika mikoa husika. Hivyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge tushirikiane kuhamasisha na kuwahimiza wadau wakiwemo wananchi na halmashauri mbalimbali nchini kutoa ushirikiano pindi wawekezaji wanapojitokeza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Adadi Rajab swali la nyongeza.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, Kumbukumbu za Bunge (*Hansard*) zinaonesha kwamba swali hili lililwahi kuulizwa mara nyingi na Wizara imekuwa ikitoa maelezo tofauti tofauti ikiwapo na kusema kwamba machungwa ya Muheza siyo mazuri wakati machungwa ya Muheza sasa hivi ni mazuri, tunatumia mbegu ya *Valencia*, *Washington* na Msasa na kwamba machungwa hayo yanapelekwa Kenya na kutengeneza *juice* ya *Del Monte*. Swali langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri atanihititishiaje kwamba hii Kampuni ya *SASUMUA HOLDING* ni kweli inataka kujenga hicho kiwanda Mkoa wa Tanga? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ninao wawekezaji ambao wanataka kufanya Muheza iwe kituo cha matunda. Mheshimiwa Waziri atanihititishia kwamba wawekezaji hao hawatapata usumbufu nitakapowaleta kwake? Nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, unapoulizwa swali na Mheshimiwa Mbunge ambaye amewahi kuwa Kamanda halafu ni Balozi inakuwa shida kumjibu. Nimezungumza na watu wa *TAHA (Tanzania Horticultural Association)* kupita Mkurugenzi Mkuu wao Jacqueline na nimezungumza na *SASUMUA HOLDING*, vifaa vyao kama *earth equipment* vimeshafika Kwamsisi, nimeviona na wamenihakikishia. Jambo la kukupa amani ya moyo Mheshimiwa Adadi ni kwamba mimi na wewe pamoja na Waziri, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Mboni, Mbunge wa Handeni tutapanga twende pale tuone shughuli zinazofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tuna shughuli ya msingi kwamba yule mtu anataka *outgrowers* hekta 3,000 na yeye mwenyewe hekta 17,000 na anasema atawapa service. Kwa hiyo, ni jukumu lako Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Tanga mkiongozwa na Mheshimiwa Mboni, mimi na Waziri mwenzangu pacha twende pale tuone *Kashenamboni*, tuamini au tusiamini mimi na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninalolipenda kuliko yote ni hili swali lako la pili kwamba niko tayari. Leo nina shughuli tena shughuli pevu, nakuomba kesho uniache nipumzike Jumatano walete wawekezaji wako, hakikisha Tanga hakuna vikwazo, mimi saina yangu natembea nayo. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Waziri, amesema kuna wawekezaji ambao wanakusudia kuwekeza pale Kwamsisi, natoa pongezi kwa sababu kiwanda kile kinakuja katika Mkoa wetu wa Tanga. Kwa kuwa ndiyo wanatarajia kuanza kulima hayo mazao ambayo yatalisha kiwanda hicho, je, haoni ni wakati muafaka kwa matunda yaliyopo sasa na hasa ikizingatiwa kwamba Serikali imeshasema itafufua kwanza viwanda vilivyokuwepo hasa kiwanda kilichokuwepo pale Korogwe, ni kiwanda kidogo lakini kinaweza kutengeneza *juice* kikafufuliwa hicho kwanza wakati tunasubiri kiwanda kikubwa? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, waambie wanipige taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mary Chatanda ameuliza maswali mawili katika moja. Ubora wa matunda au matunda tuliyonayo na hii kampuni ya Kwamsisi ambayo itachukua miezi 18 mpaka ianze kutengeneza *juice*, jibu lake ni hivi, kuna kampuni nyingine inaitwa Sayona inajenga kiwanda sehemu ya Tanga karibu na Chalinze, itachakata tani 25,000 za matunda yoyote, hii itakuwa inakidhi haja wakati sisi tunasubiri hiki kiwanda cha SASUMUA. Kwa nini SASUMUA hawezi kuanza, yeye analenga kuanza na mananasi na wanasema wataalam kwamba nanasi litakapopandwa linahitaji miezi 18 kuweza kukomaa. Kwa hiyo, yeye ana masharti yake na utaalamu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la Korogwe kwamba kiwanda kipo na bahati nzuri ameuliza swali siku nzuri, namuagiza Mkurugenzi Mkuu wa *SIDO*

aende Korogwe na mtaalam wa TIRDO watathmini ni kitu gani kinahusika halafu Halmashauri yake ambaye yeye ni Diwani tuje tuangalie ni namna gani ninyi mnaweza kuhamasisha Wanatanga ili muweze kukiendesha, viwanda vingine siyo vya Serikali. Ni nini tatizo, hiyo ni kazi yangu nitabaini, spare atanunua wapi wataalam wangu watamwambia, ni viwanda vya shilingi milioni 60 au 80, halmashauri mnawimudu. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga swali fupi.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Waziri swali dogo. Ni lini Serikali itaacha kuagiza *toothstick* maana tuna miti mingi ya kutosha kule Mbeya na sehemu nyingine. Ni lini Serikali itaacha kuagiza *toothstick*? Ahsante sana. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji nadhani ni *toothpick*. (Kicheko)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo yanayoninyima raha ni kama kuona watu wanaagiza *toothpick*. Mimi nimeleta bajeti yangu hapa lakini haina maana hata ningeisoma kwa mbwembwe namna gani kama ninyi msipoikubali. Ninyi Wabunge mniambie kwamba *toothpick* zisipite Dar es Salaam muone kama zitaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo wa kutengeza *toothpick* ni dola 28,000, ni jukumu lako Watanzania kuwekeza. Kuna Mtanzania mmoja, nawaomba asiyetaka kuwekeza kwenye viwanda na nimelisema mara tatu, kuna Wabunge, kuna watu wanakuja kila siku wanataka kuwekeza, Mtanzania anayeagiza *toothpick* anaagiza *container* 100 ni mtu wa Makete. Mtambo wa kutengeneza *toothpick* ni dola 28,000. Kuna Mbunge Mheshimiwa Lema anafuatilia kuleta mtambo wa *toothpick* kupeleka Kilimanjaro. Watu wanahangaika, msikosoe, msilalamike twende tufanye kazi. *Toothpick* inatumia mabaki ya miti haitumii ubao, *the reject, the unwanted material* ndiyo inatumika. Tuchangamke, twende wote kwenye behewa la viwanda msibaki nyuma. Viwanda ni vita Bwana Msigwa twende kwenye viwanda. *Toothpick* mkiamua zisiagizwe hazitaingia, *TBS* ni yangu nitazizuia lakini na ninyi muwekeze watu wanapenda *toothpick*. (Makofi/Kicheko)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Na.123

Hitaji la Senta ya Michezo ya Riadha - Manyara

MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y. MHE. MARTHA J. UMBULLA) aliuliza:-

Ujenzi wa senta ya Michezo ya riadha katika Mkoa wa Manyara hususani Wilaya ya Mbulu imekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa viongozi na wananchi wa eneo husika kutokana na vijana wengi kuwa na vipaji katika mchezo wa riadha na michezo mingine:-

(a) Je, ni lini Serikali itasikiliza kilio cha muda mrefu na kujenga senta ya michezo ya riadha Mkoani Manyara ili vijana wengi wenye vipaji waweze kunufaika?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kujenga senta ya michezo Manyara itaweza kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana wa Mkoa huo na maeneo jirani kama Singida, Arusha na Dodoma ambako kuna vipaji hivyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Manyara na Wilaya zake una vijana wenye vipaji vya riadha na michezo mingine. Aidha, Serikali inatambua pia umuhimu wa kuwa na kituo kikubwa cha michezo hasa ya riadha ambacho pamoja na mambo mengine kitasaidia kuibua, kukuza na kuviendeleza vipaji vya vijana ikiwa ni pamoja na kuwapatia ajira vijana mkoani humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Massay, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mkoa wa Manyara imepanga kujenga kituo cha michezo cha mkoa mara baada ya kukamilisha mazungumzo na kukubaliana na wananchi wanaomiliki ardhi katika eneo ambalo mkoa wamekubaliana. Aidha, kwa kipindi hiki ambacho uongozi wa mkoa hauna kituo cha michezo, mkoa umepanga kutumia kambi ya michezo ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwa muda, wakati wanasubiri kupatikana kwa

eneo la kudumu la mkoa. Hii ni kutokana na sababu kuwa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ina hosteli na viwanja vya michezo vya kutosha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kujengwa kwa kituo hiki katika mkoa kutaongeza ajira, kutapanua shughuli za kibiashara na hata kukua kwa uchumi wa Mkoa wa Manyara. Serikali inaendelea na mazungumzo na wananchi wamiliki wa eneo husika, yakikamilika na pesa zikipatikana ujenzi wa kituo hiki cha michezo utaanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Massay swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa Mbulu walishapewa ahadi ya kujengwa uwanja na *Olympic* na sasa wale wameondoka na eneo hilo lipo mpaka sasa na wananchi wa Mbulu wamekubali kutoa eneo hilo. Je, Serikali haioni ndiyo sasa wakati wa kuja kuwekeza au kujenga kituo hicho Mbulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wanariadha wazuri ambao wamevunja rekodi ya dunia mpaka leo na haijawahi kuvunjwa mfano Philbert Bai ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa Tanzania, je, Serikali haioni sasa ndiyo muda muafaka wa kujenga kituo hicho Mbulu kwa sababu uwezo wa Mbulu na uoto wa asili na hali ya hewa inawaruhusu wanariadha kuweza kufanya mazoezi na kushinda *Olympic*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inatambua kazi nzuri iliyofanywa na wanariadha wanaotoka Mbulu wakiwemo akina Philbert Bai na wenzake. Tunakubaliana na hoja kwamba kama eneo lipo ambalo kwa kweli halitahitaji fidia na litaondoa hii haja ya mazungumzo ya kupata eneo, tutashauriana na Serikali ya Mkoa wa Manyara kuona namna ambavyo tunaweza kulitumia eneo hilo kwa ajili ya kujenga kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba kwa kutambua mchango wa wanariadha kutoka Mbulu na namna nzuri ya kuwaenzi nadhani ni vizuri tukaangalia namna ya kujenga kituo hiki Mbulu kwa kuzingatia mazingira hayo. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kuna msemu wa Kiswahili unaosema samaki mkunje angali mbichi. Ujenzi wa kituo hicho hautakuwa na maana kama hatujawekeza huku chini. Tunatambua kwamba wakati Serikali inapanua elimu walihakikisha kabisa viwanja katika shule zetu za msingi havipo kwa maana kwamba walijenga shule za pili. Je, Serikali inasema nini kuhakikisha kwamba shule zetu za msingi zina viwanja ili watoto waanze kucheza riadha au michezo mingine ili sasa hivi vituo wanavyovijenga huku juu viwe na maana? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza siyo kweli kwamba Serikali ilihakikisha kwamba shule hizi hazina viwanja. Bahati mbaya iliyotokea yako baadhi ya maeneo ambapo suala la kutenga viwanja vya kutosha halikuzingatiwa wakati wanapanga mipango na maeneo mengine viwanja vilichukuliwa vikabadilishwa matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kusesitiza kwanza katika kila mpango wa ardhi kuhakikisha tunatenga maeneo ya michezo siyo tu kwenye shule, lakini maeneo ya michezo yatengwe kwenye makazi ya watu ili kurahisisha watu kushiriki michezo kwenye maeneo yao ya makazi. Pili, tumeendelea kukagua na kurudisha maeneo ambayo yamevamiwa na kubadilishwa matumizi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge ninyi ni Madiwani tusaidieni mambo mawili. La kwanza, hakikisheni hakuna mipango ya matumizi ya ardhi inapitishwa wakati hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo.

Pili, shule hizi zinaendeshwa na kumilikiwa na halmashauri zetu. Sisi Waheshimiwa Wabunge ambao ni Madiwani tukiwa wakali kwenye kubadilisha matumizi ya maeneo yetu bila shaka viwanja vitapatikana na michezo yetu itaendelea. Nakubaliana na wewe michezo ili iendelee lazima ianze ngazi ya chini, habari ya kuanzia ngazi ya juu tutapoteza muda wetu bure. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango.

Na. 124

Benki ya TIB Katika Kupunguza Umaskini

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA aliuliza:-

Kwa miaka mingi sasa *Tanzania Investment Bank* na *TADB* imekuwepo ila mchango wake katika kupunguza umaskini haufahamiki zaidi hata kwa

Waheshimiwa Wabunge. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Benki za *TIB* na *TADB* zinajielekeza kwenye utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM kwa sababu ndiyo mkataba wa mpango kazi wa maendeleo ya nchi yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa Benki ya *TIB* na *TADB* kama benki za maendeleo ni kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kwa lengo la kufadhili miradi ya kimkakati. Katika kutimiza azma ya kufadhili miradi ya kimkakati ya kufungua fursa za kiuchumi na kupunguza umaskini, *TIB* imetoa mikopo katika maeneo yafuatayo:

Mradi wa Maendeleo ya Makazi (Temeke na Kinondoni); Mradi wa Maendeleo ya Miji kupitia *NHC*; Viwanda vya Kubangua Korosho; maghala; mabomba ya maji; sukari na kilimo cha miwa; kukoboa na kusindika kahawa; kusindika matunda; mifuko ya kuhifadha mazao; nyaya za umeme; vinu vya pamba na uzalishaji wa mafuta yatokanayo na mbegu za pamba; na mahoteli. *TIB* umewezeza katika mashirika ya umma kama vile Shirika la Reli (*TRL*), imeiwezesha *TPDC* katika mradi wa gesi na kuipatia *TANESCO* mkopo kwa ajili ya fidia kwa wananchi ili kuweka njia mpya ya kusafirisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwaka jana (2015), *TIB* imewawezesha Watanzania wengi kupambana na umaskini kwa kutoa mikopo ya zaidi ya shilingi bilioni 550 katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Katika sekta ya kilimo, *TIB* imewasaidia wananchi wengi kwa kusimamia mikopo iliyotolewa na Serikali kupitia Dirisha la Kilimo inayofikia shilingi bilioni 58.8 hadi mwishoni mwa mwaka 2015. Mikopo hii ilitolewa kupitia makampuni binafsi yapatayo 121, taasisi ndogo ndogo za fedha zipatazo 11 na *SACCOs* 78.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TIB* pia imetoa mkopo wa shilingi bilioni 489.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 181 ya kusambaza umeme vijijini kupitia *REA* na kaya 257,000 zimenufaika na mradi huo. Aidha, vikundi 17 vya wachimbaji wadogo wadogo vimenufaika na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya *TIB* kwa sekta na taasisi mbalimbali imesaidia kwa kiasi kikubwa kutoa ajira mpya na kuendeleza zilizopo. Pia mikopo ya *TIB* imetumika kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje kama

vile maua, kahawa na dhahabu. Pamoja na Benki ya Kilimo kuchelewa kuanza kutoa mikopo ni wazi kabisa kuwa Benki ya TIB imejielekeza kwenye utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM pamoja na utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo kama vile Dira ya Taifa (2025), Mpango wa Pili wa Maendeleo na Maendeleo Endelevu 2020 pamoja na Ajenda ya Afrika 2063.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bashungwa swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, lakini kwa upande wa kahawa, Jimbo la Karagwe tunalima kahawa sana na zao la kahawa bado lina fursa kubwa sana kuwainua kiuchumi wakulima wa kahawa na uchumi wa nchi kwa ujumla lakini mikopo ya TIB imekuwa ni kidogo mno kwenda kwenye kukopesha walimaji wa kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu ni kama ifuatavyo: Kwa vile miche ya kahawa ni ya zamani sana, imepandwa toka enzi za wakoloni na mababu zetu, je, Benki ya Kilimo ina mpango gani wa kuwakopesha wakulima wa kahawa pesa ile waweze kununua miche wakiwemo vijana ambao wana tatizo la ajira na kama miche ikipatikana wanaweza wakajikita kwenye kilimo cha kahawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa vile kabla ya kuanzishwa kwa Benki ya Kilimo, TIB ilikuwa ikitoa mikopo kwenye sekta ya kilimo kupitia Dirisha la Kilimo, kwa nini hii *portfolio* isitoke TIB ikaenda Benki ya Kilimo ili hii fedha shilingi bilioni 58.8 itumiwe na Benki ya Kilimo kukopesha wakulima wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Uvuvi na Mifugo.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Innocent Bashungwa kwa kufuatilia suala la miche ya kahawa na kusema kuwa imechakaa na kwenye hotuba yangu nilisema katika Wilaya na Mikoa inayolima miche ya kahawa wajitahidi kupanda miche 5,000 kwa kila hekari ili kuweza kurejesha heshima ya zao hilo la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ombi lake hili la kuangalia uwezekano wa vijana kukopeshwa fedha kwa ajili ya kupanda miche mipya, niseme tu nitajielekeza Benki ya Kilimo wawasiliane na Mheshimiwa Mbunge na wapangilie safari ya kuweza kufika huko ili wakaangalie mazingira sambamba na vile ambavyo tulishakubaliana watafika pia Kitulo kwa ajili ya kuangalia uwezekano

wa kukopesha uzalishaji wa mitamba ili wananchi waweze kupata mbegu za mazao haya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge na naelekeza uwasiliane na Benki ya Kilimo ili waweze kuwakopesha vijana wapande miche mipya ili kurejesha heshima ya zao hilo la kahawa. Zao la kahawa litaendelea tu kama tutalipokea kutoka kwa wazee wetu na sisi vijana tukaona ni zao la fursa kwa ajira na kwa ajili ya biashara. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

MHE. ESTER N. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza Naibu Waziri wa Fedha kwa makini, kwa jinsi alivyojibu ametutajia *figure* kubwa sana ambazo zimeenda katika sekta ya kilimo, lakini ni wazi na Waheshimiwa Wabunge wanajua bado wakulima wetu kilimo chao ni cha kusuasua na wanalima katika mazingira magumu. Hata wale ambao wanajitokeza katika kilimo cha umwagiliaji wakiwemo watu wangu wa Tamau, Nyatwali na maeneo mengine wanakosa vifaa. Mna mkakati gani wa kuhakikisha hizi *figure* zinaendana na hali halisi ya mkulima mmoja mmoja? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru kwa kuelewa kwamba kiasi hiki nilichokitaja ndicho ambacho kimetoka Benki ya *TIB (Tanzania Investment Bank)* kwenda katika miradi ya kilimo na miradi mingine niliyoitaja. Mimi kama Naibu Waziri wa Fedha na Mipango jukumu langu ni kuhakikisha pesa hizi zinafika kwa wale wanaomba pesa hizi. Kwa hiyo, naamini tutafanya kazi kwa ushirikiano mzuri mimi na Waziri wa Kilimo, mtani wangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ili tuhakikishe sasa pesa hizi zinawanufaisha walengwa na zinaweza kukidhi mahitaji yale waliyoomba.

NAIBU SPIKA: Tuendeleo Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata.

Na.125

Kuanzisha Ofisi za TRA Kwenye Maeneo Mbalimbali Nchini

MHE. OMAR M. KIGUA aliuliza:-

Ulipaji kodi ni chanzo kikuu cha mapato ya nchi kwa ajili ya maendeleo na Serikali inao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba wafanyabiashara,

wakulima na wafanyakazi wanalipa kodi kwa mujibu wa sheria na ili Serikali iweze kukusanya kodi kwa ufanisi mkubwa ni lazima kuwe na Ofisi za TRA katika maeneo mbalimbali nchini:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Ofisi ya TRA katika Wilaya ya Kilindi?

(b)Kwa kutokuwa na Ofisi za TRA Serikali haioni kama inadhoofisha maendeleo ya Wilaya hususani katika suala la mapato?

(c)Kwa kuweka Ofisi za TRA Wilaya ya Handeni na kuacha Wilaya ya Kilindi, Serikali haioni kama inawajengea wananchi tabia ya kukwepa kulipa kodi kutokana na umbali uliopo kati ya Wilaya hizo mbili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kufungua Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Wilayani Kilindi kama ilivyo katika Wilaya zingine. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ina mpango wa kufungua ofisi za Mamlaka ya Mapato katika Wilaya mbalimbali nchini ikiwemo Kilindi baada ya kukamilisha zoezi la utafiti na uchambuzi wa kina kuhusu fursa za mapato ya kodi zilizopo katika Wilaya zote ambazo hazina ofisi za TRA.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha ofisi za Mamlaka ya Mapato katika Wilaya ni fursa mojawapo ya kuleta maendeleo katika eneo husika. Aidha, uamuzi wa kufungua ofisi ya Mamlaka ya Mapato unazingatia zaidi gharama za usimamizi na ukusanyaji wa mapato. Kwa msingi huo, Serikali haidhoofishi maendeleo ya Wilaya ya Kilindi isipokuwa ni lazima tufanye utafiti kwanza kubaini gharama za usimamizi na ukusanyaji wa mapato kabla ya kufungua ofisi.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Kigua kuwa uwepo wa ofisi za Mamlaka ya Mapato katika maeneo yetu unaongeza ari ya wananchi kulipa kodi kwa hiari. Napenda kutoa rai yangu kwa wananchi wa Wilaya ya Kilindi na Watanzania wote kwa ujumla kuendelea kulipa kodi kwa hiari na kwa mujibu wa sheria. Aidha, wananchi wasiache kulipa kodi kwa kutumia kisingizio cha maeneo yao kukosa ofisi za Mamlaka ya Mapato kwani

kwa kufanya hivyo watakuwa wamevunja sheria na kuikosesha Serikali yao mapato ambayo yangetumika kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigua, swali la nyongeza.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni takribani miaka 13 toka Wilaya hii ya Kilindi imeanzishwa. Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba, pana umbali mkubwa sana kati ya Wilaya ya Handeni iliko ofisi ya Mamlaka ya Mapato na Kata mbalimbali za Jimbo la Kilindi hususani katika Kata ya Pagwi. Je, ni lini sasa utafiti huu utakamilika ili wananchi wa Kilindi waweze kunufaika na huduma hii? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa ametaka kujua ni lini utafiti huu utakamilika. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba pamoja na utafiti huu kukamilika pia tunaangalia *potentials* ya ukusanyaji yaani *cost and benefit analysis* ya kuanzisha ofisi hizi kila Wilaya. Kwa sasa hivi nguvu nyingi tunazielekeza katika kuanzisha ofisi za Mamlaka za Mapato katika mikoa mipya ambayo imeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naendelea kusema kwamba namwomba Mheshimiwa Kigua aendelee kuongea na wananchi waendeleo kulipa kodi kupitia Wilaya yao ya mwanzo kabla ya Kilindi kuanzishwa. Pia tutakapokamilisha utafiti huu na tukaona kwamba kuna *potential* kubwa ya kupata mapato ya kutosha Wilaya ya Kilindi, basi hatutasita kuanzisha ofisi hii katika Wilaya ya Kilindi na wilaya nyingine zote za Tanzania ambazo hazina Ofisi.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na.126

Miradi ya Maji Chini ya Benki ya Dunia

MHE. MPAKATE D. IDDI aliuliza:-

Katika Wilaya ya Tunduru kuna miradi mingi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia ambayo imesimama kwa muda mrefu bila kukamilishwa na wakandarasi kwa sababu ya ukosefu wa fedha:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kumaliza miradi hiyo ambayo wananchi wanajua kuwa fedha zilitolewa na Benki ya Dunia lakini hazijulikani zilikwenda wapi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mpakate Daimu Iddi, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambapo ugharamiaji wa maji chini ya programu hii hutokana na fedha za Serikali na wadau wengine ikiwemo Benki ya Dunia. Hivyo, upelekaji wa fedha kwenye halmashauri hutegemea upatikanaji wa fedha kutokana na bajeti ya Serikali na fedha za wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu hii, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 11. Hadi sasa jumla ya miradi miwili katika Vijiji vya Nandembo na Nalasi imekamilika na inahudumia wananchi 21,224. Miradi minne ya Vijiji vya Lukumbule, Amani, Mtina na Matemanga ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mradi wa maji katika Kijiji cha Mbasa umesimama kutokana na mkandarasi kukiuka masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha miradi hiyo inakamilika, mpaka kufikia Februari 2016, Wizara imeshatuma kiasi cha shilingi milioni 537.2 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa ajili ya kuendelea kukamilisha miradi hiyo. Aidha, miradi minne katika Vijiji vya Majimaji, Muhuwesi, Nakapanya na Mchoteka haijaanza kutekelezwa kutokana na kukosa vyanzo vyenye maji ya kutosheleza. Miradi hii itatafutiwa vyanzo mbadala katika utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Mpakate swali la nyongeza.

MHE. MPAKATE D. IDDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini katika miradi miwili aliyosema imekamilika, mradi wa Nandembo na Nalasi tarehe 22 Julai, 2014, Rais wa Awamu ya Nne alifungua miradi ile, lakini cha kusikitisha hadi leo maji hayatoki katika miradi yote miwili. Je, yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kuangalia miradi ile kama alivyosema imekamilika wakati maji hayatoki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mradi wa Mbesa umesimama kwa takribani kwa mwaka mmoja na nusu na vifaa viko pale, vina-hang hovyoy bila usimamizi wowote. Je, ni lini Serikali itapeleka mkandarasi mwingine ili aweze kumaliza mradi ule? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, miradi miwili niliyoitaja amesema kwamba miradi hiyo haitoi maji. Nitafanya mawasiliano na Mkurugenzi wa Halmashauri husika ili aweze kutupatia maelezo kwa nini miradi hiyo haitoi maji ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakamilisha pale ambapo pamepungua kuhakikisha hiyo miradi inatoa maji. Pia kwa ridhaa yako, ridhaa ya Mheshimiwa Spika na Waziri wangu wa Maji na Umwagiliaji, hatuna matatizo kabisa, tukimaliza Bunge tunaweza tukaambatana naye ili kwenda kuangalia utekelezaji wa hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza kuhusu mradi wa Mbeso. Mradi huu ulikosa chanzo cha maji lakini kama mnavyofahamu Mheshimiwa Wabunge ni kwamba tumeanza Programu ya Pili ya Maendeleo ya Maji ambayo imeanza Januari, 2016, baada ya kukamilisha programu ya kwanza. Ie miradi yote tuliyoi-earmark kwenye Programu ya Kwanza ambayo ilianza mwaka 2007 na haikukamilika ndiyo tutaanza nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika bajeti ambayo itasomwa na Mheshimiwa Waziri mwezi huu kwanza tunalenga kukamilisha miradi ambayo tulianza na haikukamilika na miradi ambayo pengine haikuanza lakini ilikuwa imependekezwa itekelezwe katika Programu ya Kwaza tutahakikisha kwamba miradi hii tunaikamilisha kabla hatujaenda kwenye miradi mipya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii miradi yote 11 katika Programu ya Pili tutahakikisha kwamba inakamilika kabla hatujaingia kwenye miradi mingine.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kemi Luota.

MHE. KEMIREMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la maji Wilayani Misungwi kwenye Kata za Mbarika, Nyangomango na Iyerere ambako chanzo cha maji cha Ziwa Viktoria kinapita maji yaendayo Shinyanga na Kahama. Je, ni lini Serikali itapitisha maji kwenye vijiji hivi ambavyo vinayaona maji tu yanapita, lakini wao hawana maji? Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilikamilisha mradi wa kutoa maji Ziwa Viktoria kupeleka Shinyanga. Katika bajeti inayokuja ambayo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ataisoma, tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha upelekaji wa maji kwenye vijiji ambavyo vimepitiwa na hilo bomba kuu lakini havikuweza kupatiwa maji katika hiyo Programu ya Kwanza. Hii itakwenda sambamba na huu mradi ambao unaanza Shinyanga kuelekea Wilaya za Nzega na Mkoa wa Tabora na kwenda Igunga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi, tunalifahamu hilo, sehemu zote ambazo hazijapatiwa maji kupitia mradi huo tutahakikisha kwamba tunaongeza vijiji ikiwemo vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge umevitaja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduma ni lango kuu la nchi za Kusini na Kati mwa Afrika na kwa sababu Mheshimiwa Waziri amenihakikishia kwamba mradi mkubwa wa maji utajengwa kwenye Mji wa Tunduma lakini kuna mradi ambao ulijengwa mwaka 1973, mradi wa maji wa kutega kwenye Kijiji cha Ukwire ambapo ulikuwa unahudumia Kata za Mpemba, Katete na Chapwa na sasa hivi mradi ule hautoi maji ya kutosha. Ni lini Serikali itakwenda kukamilisha mradi ule wa Mpemba ambao unalisha kata tatu katika Mji wa Tunduma? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mji wa Tunduma tayari *study* imeshafanyika kwa ajili ya kuweka mradi mkubwa wa maji. Tuna mfadhili ambaye ameshajitokeza, tunaongea naye, Serikali bado inafanya mazungumzo na yeye kwa sababu alikuwa amekuja na masharti ambayo yanaweza yasiwe na manufaa kwa upande wa wananchi wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja, tunaweza tukapitia mradi huo mkubwa unaokuja, lakini pili ni kwamba mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano inahakikisha kwamba inakarabati miradi yote iliyokuwa imejengwa hapo awali ili kuondoa upungufu ukiwemo mabomba ya maji ambayo yamechakaa, mitambo ambayo imechakaa na vilevile kuongeza huduma kwa sababu kila kunapokucha watu wanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika programu hiyo tutahakikisha kwamba, hayo maeneo Mheshimiwa Mbunge ambayo anayataja nayo tumeyapitia ili kurudisha upatikanaji wa maji ambao umepungua kwa sasa na hasa kwa kuzingatia kwamba Mji wa Tunduma unapanuka sana. Nafikiri upunguaji huo wa upatikanaji wa maji ni kutokana na kwamba watu wameongezeka katika Mji wa Tunduma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aisharose swali fupi.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi hii. Asilimia 90% ya wakazi wa Mkoa wa Singida wanategemea maji ya visima ambapo vingi vya *pump* za mkono na wengine wanachota maji kwenye malambo na mabwawa na hasa maeneo ya vijijini, lakini maji hayo hayakidhi viwango na pia hayatoshelezi mahitaji. Je, Serikali haioni imefika wakati wa kutafuta wawekezaji wakubwa ili kupunguza adha hii ya maji katika Wilaya zote za Mkoa wa Singida na hasa ikizingatiwa Wilaya ya Singida ni wilaya ambayo ina hali ya ukame kijiografia? Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sitaki nibishane naye kuhusu takwimu anazosema kwamba asilimia 90% ya wananchi wa Singida wanatumia *pump* za mkono. Hili ni jambo ambalo kitakwimu itabidi tulizungumze na nitalileta wakati nawasilisha bajeti yangu, atajua ni wangapi wanatumia *pump* za mkono na wangapi wanatumia taratibu zingine ili kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la msingi ni kwamba katika Programu ya Maji, wa kuamua chanzo cha maji cha kutumia tuliwaachia wao wenyewe wananchi hasa halmashauri kulingana na teknolojia na gharama za mradi, kwa hiyo, maeneo mengi walichagua visima lakini katika programu hii tulikuwa hatutumii *pump* za mkono. *Pump* za mkono ni katika miradi ile ambayo inafadhiliwa na wafadhili kama *Water Aid* na mashirika madogo madogo kama yale au *NGO's*, ndiyo wamekuwa wanatoa *pump* za mikono. Kama Tigo nimekwenda juzi Singida nimefungua mradi wa vijiji 12 kwa *pump* za mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Programu ya Maji tunatumia aidha ni *pump* za umeme wa *generator* au kama kuna *grid* karibu ndiyo wanaunga, kitu cha namna hiyo. Kwa hiyo, tutajaribu kuangalia, kuna baadhi ya maeneo ambayo wako karibu na mito, tunaweka mradi mkubwa ambao unaweza kwenda kusambaza maji katika vijiji vingi. Sasa ili kusudi Mheshimiwa Mbunge upate jibu zuri, naomba unisubiri nitakapowasilisha bajeti yangu, nitaonesha ni miradi ya namna gani inakuja kwa Mkoa wa Singida kuangalia vyanzo na nini tutatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na.127

**Barabara ya Oldean Kujengwa kwa
Kiwango cha Lami**

MHE. QAMBALO W. QULWI aliuliza:-

Barabara ya Oldeani *Junction* - Mang'ola – Matala - Manuzi ni kiungo muhimu sana kwa kuunganisha Kanda ya Kaskazini (Mkoa wa Arusha) na Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Simiyu):-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika muda wote?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Oldeani *Junction* - Mang'ola - Matala - Manuzi ambayo pia hujulikana kama Kolandoto - Oldeani *Junction* yenye urefu wa kilometa 328 umeanza na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zitaanza baada ya kukamilika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaoendelea na kupatikana kwa fedha za ujenzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Qambalo swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Tunayo sera katika nchi hii inayotoa kipaumbele kwa ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara zinazounganisha mikoa. Barabara hii tunayoongelea inaunganisha Mkoa wa Arusha na Simiyu. Kutokana na jioografia ya maeneo hayo, barabara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake anasema barabara hii itajengwa fedha zitakapopatikana. Sasa naomba swali, kutokana na sababu hizo za kiseru na kijiografia, je, utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii umefikia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na mvua nyingi zilizonyesha katika maeneo ya barabara hii na hata ile inayounga Mji wa Karatu na Mbulu, zimeharibika sana na usafiri umekuwa wa shida na maeneo mengine barabara zimekatika. Kwa kuwa mvua sasa zinaelekea mwisho, ukarabati na ujenzi wa barabara hii utaanza lini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, suala la upembuzi yakinifu na usanifu wa kina haujakamilika, ndiyo kazi inayoendelea. Hatuwezi kuanza kutafuta fedha kabla hatujajua tunahitaji fedha kiasi gani katika ujenzi wa barabara hii. Tunaposema mara baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika ni wazi hatua inayofuata ni ya kujenga kwa kiwango cha lami na hapo ndiyo fedha tunaziongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili itakumbukwa kwamba nilipojibu swali la nyongeza wiki iliyopita, nilitoa maelekezo kwa TANROADS pamoja na Mameneja wote wa Mikoa Tanzania nzima, kwamba sasa mvua zimekatika sehemu nyingi, tuelekeze nguvu katika kurudisha mawasiliano kwa barabara zile ambazo ziliathiriwa sana na mvua na kuleta changamoto ya mawasiliano. Hii ni pamoja na hii barabara anayoongelea Mheshimiwa Qambalo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Karatu linalingana kabisa na tatizo la Korogwe Vijijini hasa kwenye barabara inayotokea Korogwe - Kwashemshi - Bumbuli - Soni imekatika na barabara hii iliamuliwa na Serikali kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami na sasa hivi mawasiliano hakuna. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuitengeneza barabara hii haraka haraka ikarudisha mawasiliano ya dharura ambayo yalikuwa yameshakatika kwa muda mrefu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu awali, barabara zote ambazo zimekatika hivi sasa TANROADS pamoja na Mameneja wa Mikoa wa TANROADS wote Tanzania nzima waanze kuelekeza nguvu katika kurudisha mawasiliano kwa barabara zile zilizokatika ikiwa ni pamoja na barabara hii ya ndani ya Jimbo la Korogwe Vijijini kwa Mheshimiwa Ngonyani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA. D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Katika Awamu ya Nne Mheshimiwa Rais aliyepita aliwahi kutoa ahadi ya kujenga kiasi cha kilometa takriban mbili hadi nne za lami katika Mji wa Karatu na hasa ukizingatia Mji wa Karatu ni mji wa kiutalii kwa sababu ni lango la kuelekea Ngorongoro. Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa sana kumaliza utamu wa hotuba ya Waziri wangu ambayo inakuja Jumanne wiki ijayo. Ningeomba Mheshimiwa Mbunge asubiri hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo itakuwa inajibu kiu yake hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu pekee ambacho naweza kumhakikishia ni kwamba ahadi zote zilizoko katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo Serikali hii inaitekeleza, ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akiomba kura sehemu mbalimbali za nchi, ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Wabunge, tutaziangalia na kuhakikisha kwamba zinatekelezwa kwa sababu zote kwa pamoja ni ahadi za Chama cha Mapinduzi.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 128

Ujenzi wa Barabara ya Chaya – Tabora

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Hali ya kipande cha barabara ya kutoka Chaya - Tabora ni sehemu ya barabara ya kutoka Urambo – Kaliua:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hizo utakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Chaya – Nyahua na Urambo – Kaliua ni sehemu ya barabara ya Manyoni – Tabora – Urambo – Kaliua – Malagarasi – Uvinza - Kigoma yenye jumla ya kilometa 843.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuunganisha Mkoa wa Singida, Tabora na Kigoma kwa barabara ya kiwango cha lami. Katika kutimiza azma hiyo, tayari ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya yenye urefu wa kilometa 89.3 pamoja na Tabora – Ndoni yenye kilometa 42, Kigoma – Kidahwe yenye kilometa 28, Kidahwe – Uvinza yenye kilometa 76.6 pamoja na daraja la Malagarasi na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 48 umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea kwa sehemu ya barabara zifuatazo na utekelezaji umefikia asilimia kama nitakavyoieleza. Sehemu za Tabora - Nyahua yenye urefu wa kilometa 85.4 ujenzi umefikia 90%. Sehemu ya Ndoni - Urambo yenye urefu wa kilometa 52 ujenzi umefikia 87%. Sehemu ya Kaliua - Kazilambwa yenye kilometa 56 ujenzi umefikia 63%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Nyahau - Chanya yenye urefu wa kilometa 85.5 na Urambo - Kaliua yenye urefu wa kilometa 28 utanza katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 kufuatia kukamilika kwa usanifu wa kina wa barabara hizo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchemba swali la nyongeza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye kutia matumaini makubwa, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara hizi zimeathirika kiasi kikubwa wakati huu wa mvua ambazo zimenyesha kwa wingi na kwa kuwa mpaka hivi sasa barabara hizo hazipitiki, je, Serikali iko tayari kutengeneza sehemu korofi ili usafiri uendelee kama ilivyokuwa zamani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kasisitiza kwamba vijana wetu wa TANROADS pamoja na Mameneja wa TANROADS Mkoa hivi sasa waelekeze nguvu katika kufungua mawasiliano kwa sehemu zote zilizoathiriwa na mvua. Hii ikiwa ni pamoja na barabara hii ya Nyahua - Chaya ambayo imekatika kwa kipindi kirefu kidogo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kuna umuhimu wa kuunganisha barabara za mikoa na wilaya na kwa kuwa barabara inayounganisha barabara ya Iringa na Morogoro inapitia kwenye milima Kitonga na kwa kuwa linapotokea tatizo katika milima hiyo inakulazimu upite Dodoma, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutenga fedha kuunganisha barabara nyingine ambayo ni fupi inayoanzia Kidabaga – Idete – Itonya - Mhanga ambayo inaenda kutokea Mbingu kule Morogoro? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili eneo la Kitonga likiwa na matatizo wasafiri wa upande wa barabara hii wanayoitumia kutoka Dar es Salaam – Mbeya na kwenda Tunduma wanapata matatizo sana na wakati mwingine wanalazimika kupitia njia ambazo ni ndefu zaidi. Ni kweli vilevile hii barabara iliyoongelewa na Mheshimiwa Mwamoto inayoanzia Kidabaga na kuingia Morogoro ni barabara fupi sana na sehemu ya kuunganisha ni kilometa zisizozidi 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahakikisha eneo hili tunalifanyia kazi kwa haraka ili azma ya halmashauri zilizokuwa zinafungua barabara pande zote za kutoka upande wa Morogoro na upande ule wa Iringa iweze kukamilika kwa kumalizia hicho kipande kidogo kilichobakia cha kuunganisha mikoa hiyo miwili. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 129

**Barabara ya Mlalo – Makanya – Mashewa
Kupandishwa Hadhi.**

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Barabara ya kutoka Mlalo kupitia Ngwelo – Mlalo – Makanya – Mlingano – Mashewa ni ya muda mrefu sana na ipo chini ya halmashauri licha ya kwamba barabara hiyo ni kichocheo cha uchumi kwa Majimbo manne:-

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kupandisha hadhi barabara hiyo na kuwa chini ya TANROADS?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya kupandishwa hadhi barabara ya Mlalo – Ngwelo – Makanya – Mlingano hadi Mashewa kuwa barabara ya mkoa yanaendelea kufanyiwa kazi na Wizara yetu sambamba na maombi kutoka mikoa mingine. Aidha, kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) itaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hiyo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marwa Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ndani ya Wilaya ya Serengeti hatujawahi kushuhudia mvua kubwa kama hizi zinazoendelea kunyesha. Barabara za halmashauri hususan madaraja yamesombwa na maji na ruzuku tunayopata kutoka *Road Fund*, haitoshi. Je, Wizara iko tayari kutusaidia kujenga madaraja yale ya halmashauri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ombi lake na kwa kweli kabla hatujaiandaa bajeti

itakayokuja kusomwa na Waziri wangu hapa, bajeti hiyo imezingatia matatizo makubwa ya uharibifu wa madaraja na barabara sehemu mbalimbali nchini na hasa kwa kuzingatia viwango tulivyojiwekea vya mgawanyo wa fedha za *Road Fund* za 30% kwa 70%, siyo rahisi sana kwa upande wa Serikali za Vijiji kuhakikisha kwamba madaraja yote yaliyobomoka pamoja na barabara zote zilizokatika znarudishwa katika hali yake ya kawaida. Tusubiri majibu atakayoleta Mheshimiwa Waziri wakati bajeti itakaposomwa.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shekilindi, samahani nilikuwa nimekusahau, naomba ulize swali lako la nyongeza

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya kuanzia Mombo - Soni – Lushoto ni nyembamba hata mvua zikinyesha magari hayapiti, kuna maporomoko ya mawe na magari ambayo yana mizigo mikubwa na upana mkubwa hayawezi kupita. Je, ni lini sasa Serikali itafanya upanuzi wa barabara ile?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara ndiyo kichocheo cha uchumi wa nchi yetu, je, ni lini sasa barabara ya kuanzia Nyasa - Gale Magamba - Mlola itajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upanuzi wa barabara ya Mombo pamoja na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Nyasa - Mlola, naomba Mheshimiwa Mbunge suala hili tukalitafakari ndani ya Wizara, tuwahusishe wataalam ili tuweze kuleta majibu ya kitaalam. Kwa sababu hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge alilete swali lake rasmi kama swali la msingi ili liweze kushughulikiwa kikamilifu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha. Nitaleta kwenu matangazo machache kabla hatujaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni kutokuwepo kwa Waziri Mkuu Bungeni na hapa Dodoma. Nafasi yake kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni inakaimiwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (Makofi)

Tangazo la pili, nitawaleta kwenu wageni. Tunao wageni 31 wa Naibu Spika ambao ni viongozi kutoka Jumuiya za Wanawake wa Vyama vya Siasa nchini (ULINGO). Nitawasoma wachache wao, Ndugu Saumu Rashid ambaye ni mwakilishi wa Makao Makuu; Ndugu Leticia Mosole, Makamu Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi; Ndugu Zaituni Okororo, Makamu wa Rais wa Chama cha TADEA; Ndugu Mwaka Mgimwa, Katibu Mkuu CHAUSTA; Ndugu Nancy Mrikaria Katibu Mkuu TLP; Ndugu Queen Sendiga, Naibu Katibu Mkuu ADC na Ndugu Georgia Mtikila, Katibu Mkuu DP. Hawa ndiyo wanaoongoza wageni hawa 31 kutoka ULINGO. (Makofi)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, anaitwa Raouf Bakry, huyu ni *Executive Manager* wa *Topic Company* kutoka Cairo Misri. Huyu ni mwekezaji wa Kiwanda cha *Sulphur* Mtwara. Mheshimiwa Kuchauka naona hupigi makofi si utatembelewa na wewe na hiki kiwanda? (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Vicky Kamata Likwelile, Mbunge wa Viti Maalum ambao ni Ndugu Maimuna Mingisi, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Geita. Tunaye pia Ndugu Amina Kanyogoto, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbogwe. Tunaye pia Ndugu Habiba Msimu, Katibu UWT Mkoa wa Geita (Makofi)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Aysharose Matembe ambao ni viongozi wa UWT kutoka Mkoa wa Singida wakiongozwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, Ndugu Aziza Kiduda na Ndugu Anjela Milembe. (Makofi)

Pia tunao wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 96 na Walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya St. Irene Medel, Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni la kikao cha Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Wajumbe wa Kamati hii wanaombwa saa saba na nusu mchana wakutane katika Jengo la Utawala, chumba namba 229. Mwenyekiti wenu anaomba mhudhuria bila kukosa.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM, kwamba leo tarehe 9 saa mbili usiku mara baada ya kuahirishwa kwa kikao cha Bunge kutakuwa na kikao cha Wabunge wanawake wote wa CCM kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Nyote mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 50, Mheshimiwa Spika, amepolekewa maombi ofisini ya Mbunge anayeomba kutoa Maelezo Binafsi ya Wabunge. Ukipitia Kanuni inayohusu orodha ya shughuli za Bunge atapewa

nafasi sasa ya dakika 15 kutoa Maelezo yake Binafsi chini ya Kanuni ya 50(1)(2). Huyu ni Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, sasa nakupa nafasi ya kutoa Maelezo Binafsi.

**Maelezo Binafsi ya Mbunge Kuhusiana na baadhi ya Wabunge kutumia lugha za matusi, kejeli, dharau, kudhalilisha na kuudhi wakati wakichangia mjadala wa hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria
Tarehe 5 Mei, 2016**

MHE. MAGRARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa Maelezo Binafsi Kuhusiana na Mambo Yaliyojitokeza ndani ya Bunge hili tarehe 5 Mei, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge hili tuna Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania unaojulikana kama TWPG ambao ulianzishwa mwaka 1993. Umoja huu una malengo mbalimbali yakiwemo yafuatayo:-

- (i) Kulinda hadhi na utu wa mwanamke;
- (ii) Kuwa msemaji na mtetezi wa haki za wanawake ndani na nje ya Bunge;
- (iii) Kuwa na sauti moja bila kujali itikadi za vyama;
- (iv) Kuwasilisha hoja, Miswada Binafsi ya Sheria Bungeni na kupitia Mikataba ya Kimataifa inayohusu maslahi ya wanawake kwa madhumuni ya kuondoa na kurekebisha sheria zinazomkandamiza mwanamke;
- (v) Kuhamasisha Bunge na Serikali kuwa na mtazamo wa kijinsia katika utungaji wa sera na sheria;
- (vi) Kuhamasisha wanawake, wanaume na jamii yote nchini juu ya masuala ya jinsia na maendeleo yao; na
- (vii) Kulinda haki za binadamu na kuhakikisha utumiaji mzuri wa sheria nchini katika kulinda haki za wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na malengo ya TWPG, tumeona ni muhimu kutoa maelezo haya baada ya tukio la tarehe 5 Mei, 2016 ambapo baadhi ya Wabunge walitumia lugha za matusi, kejeli, dharau, kudhalilisha na kuudhi wakati wakichangia mjadala wa hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria. Ni dhahiri kuwa maneno yaliyotumika yamedhalilisha utu na hadhi ya wanawake na kufedhehesha jamii kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, TWPG imetafakari kwa kina na kuona kwamba pamoja na Kiti chako kuamuru maneno yafutwe baada ya mwongozo na maelezo kutoka kwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani na Mnadhimu wa Serikali, TWPG inalaani vikali na kamwe haikubaliani na tabia ya baadhi ya Wabunge kutumia lugha za matusi, kejeli, dharau na udhalilishaji wa wanawake ndani ya Bunge na nje ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, TWPG inawashauri Wabunge wote kuzingatia Kanuni zote za Bunge hasa Kanuni ya 64(1)(f) na (g), kwa ruhusa yako, naomba kunukuu:-

"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(f) Hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote.

(g) Hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine".

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hizi zimeeleza bayana umuhimu wa Mbunge kutumia lugha ambazo hazitaleta maudhi kwa Mbunge mwingine. TWPG inashauri kuwa mara inapotokea Mbunge amekiuka Kanuni hizi, Kiti kichukue hatua za haraka kudhibiti hali hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, lengo la kuleta na kutoa Maelezo haya ni kuhitimisha mjadala wa kilichojitokeza Bungeni tarehe 5 Mei, 2016, tukiamini kwamba jambo hili halitajirudia tena. Aidha, tunashauri Wabunge wote kuheshimiana ili kulinda hadhi ya Bunge letu na sisi Waheshimiwa Wabunge tuwe mfano wa kuigwa katika jamii yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, TWPG inaamini kwamba tukio hili litakuwa la mwisho. Wakati huo huo liwe fursa kwetu sisi Wabunge wanawake kuimarisha umoja wetu na kamwe tusikubali kugawanywa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namalizia maelezo yangu kwa kurudia kulaani lugha chafu za matusi, kejeli, dharau na udhalilishaji zisizoendana na utamaduni wa Mtanzania zilizotumika Bungeni tarehe 5 Mei, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, Mungu libariki Bunge letu, Mungu ibariki TWPG, Mungu ibariki Tanzania. Ni mimi kwa niaba ya TWPG, Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Margaret Sitta. Katibu.

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa orodha za wachangiaji kutoka vyama vyote vinavyowakilishwa humu Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila, huyu ni Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, halafu Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ajiandae. Mheshimiwa Maftaha Nachuma, karibu.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo Mezani leo hii ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kusema lolote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunibariki kuwa na afya njema. Kwa kuwa katika kuchangia Wizara hizi, hii ni mara yangu ya kwanza nitumie fursa hii pia kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtwara Mjini na niwaeleze kwamba naendelea kupambana vizuri na nitawawakilisha vyema kwa kipindi chote cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hotuba hii ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, nianze tu kwa kusema kwamba mkakati wa Wizara hii wa kuhakikisha kwamba nchi ya Tanzania inakuwa ni nchi yenye uchumi wa viwanda kupitia bajeti yake hii, kimkakati ni jambo zuri sana. Wenzetu nchi nyingi duniani, ukisoma historia, nchi za Ulaya ziliweza kuendelea kwa kiasi kikubwa kupitia sekta hii ya viwanda. Tangu karne ya 15 kule nchi zote za Ulaya ziliweza kufanya mapinduzi ya viwanda na kuweza kuondoa umaskini na hata kuitawala dunia kwa kutegemea sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ya Tanzania, baada ya uhuru, Mwalimu Julis K. Nyerere alijitahidi kwa kiasi kikubwa sana, aliweza kuanzisha viwanda vingi sana. Wakati huo ikumbukwe kwamba tulikuwa katika mfumo wa

ujamaa na kujitegemea, uchumi wetu ulitegemea kwa kiasi kikubwa sekta hii ya viwanda, lakini kwa bahati mbaya kabisa, Serikali ya Chama cha Mapinduzi mwaka 1995-1996 iliweza kuingia katika mfumo wa uwekezaji, mfumo ambao haukufuata kanuni, sheria na taratibu za kiuwekezaji na hatimaye zaidi ya viwanda 446 viliweza kuuawa kwa kupewa wawekezaji ambao hawana sifa ya kuwekeza Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze tu angalau kwa kifupi sababu zilizopelekea kuuawa kwa viwanda ikiwa ni kwamba tuliwapa wawekezaji ambao *they were not credible buyers* katika nchi yetu ya Tanzania, walikuwa hawana uwezo na ujuzi. Jambo lingine lilikuwa ni mazingira yenyewe ambayo tuliyatengeneza hayakuwa rafiki kwa kuweza kuuza viwanda vyetu. Mwisho wa siku leo hii tunasema tunahitaji kufufua uchumi wa viwanda, wakati hatuna utaratibu, hatuna mkakati wowote ili Taifa kama Taifa liweze kuwekeza katika sekta hii ya viwanda kwa kuwapata wawekezaji ambao tunasema ni *credible buyers*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Viwanda, Uwekezaji na Biashara amewasilisha bajeti yake hapa lakini nimepitia hii bajeti takribani kitabu chote hiki sijaona hata sehemu moja ambapo ameeleza ni utaratibu gani ambao utatumika katika kuhakikisha kwamba uwekezaji wa ndani ya nchi unakuwa ni uwekezaji wenye tija. Ameeleza tu kwamba tutahakikisha kwamba wawekezaji wa ndani na viwanda vidogo wanapewa kipaumbele lakini sijaona utaratibu wowote ambao wameuweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nizungumzie suala zima hili la mashirika ya umma na hasa mashirika ya hifadhi za jamii. Kuna mashirika ambayo yana mkakati wa kuwekeza ndani ya nchi lakini katika uwekezaji wao wanatumia mamilioni ya fedha kinyume na utaratibu. Wizara kama Wizara sijaona mkakati wowote ambao wameueleza ni namna gani watadhibiti mashirika haya kutumia fedha za umma hovy hovy.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Shirika la GEPP wakati tunapitia mpango wao ule wa uwekezaji katika Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaweza ukashangaa kuona kwamba wameweka mkakati wamenunua viwanja kwa mfano kule Mtwara wamenunua *square meter* moja kwa shilingi laki moja na elfu arobaini na nne na *something*, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kiwanja hiki sijui wamenunua mbinguni au wamenunua wapi, ni uwekezaji ambao hauna tija. Nazungumzia suala hili la uwekezaji kwamba lazima kama Wizara wahakikishe kwamba wanaweka *mechanism* iliyokuwa bora kabisa ili waweze kuhimiza uwekezaji wenye tija na Taifa letu liweze kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia kuna kiwanja kimenunuliwa Mwanza ambapo *GEPF* wanaenda kujenga *shopping mall* lakini ukiangalia *square meter* moja wamenunua shilingi laki moja na elfu kumi na tano kana kwamba hicho kiwanja kina dhahabu. Hapa nazungumzia suala zima la uwekezaji wenye tija kwa sababu Wizara hii kazi yake ni kuhakikisha kwamba inachochea Watanzania na mashirika ya ndani ya nchi yaweze kuwekeza uwekezaji wenye tija na siyo uwekezaji wa kifisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo suala zima la viwanda. Waziri hapa kazungumzia kwa kiasi kikubwa sana na alikuwa anaruka sana wakati anazungumzia kwamba sasa hivi Taifa letu litajenga viwanda vya kutosha na nchi yetu itaondokana na umaskini kupitia sekta hii ya viwanda. Nizungumza hapa wakati ule tunachangia Mpango wa Serikali kwamba viwanda hivi lazima viwekewe utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba Watanzania walioajiriwa wanafanya kazi kwa tija ili waweze kuondokana na umaskini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia Kiwanda cha Dangote, nimekuwa nikilia sana kwenye Bunge lako hili, ambacho kipo Mtwara Mjini pale, kile kiwanda kimewekezwa na wawekezaji kutoka nje, mwekezaji kutoka Nigeria anaitwa Aliko Dangote, lakini mashirika yaliyopo mle ndani ambayo yanaajiri Watanzania ambao ndio leo hii tunawazungumzia hapa kwamba waondokane na umaskini kile kiwanda kinanyanyasa kwa kiasi kikubwa Watanzania waliopo mle ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata namna ya upataji wa kazi, wananchi wa Mikoa ya Kusini wa Mtwara na Lindi ili wapate kazi mle ndani lazima watoe rushwa kuanzia shilingi laki tatu na elfu hamsini. Nilizungumza hapa na nilimwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anaunda Tume Maalum ije Mtwara ifanye ukaguzi wa haya ninayozungumza na mwisho wa siku waweze kuwachukulia hatua wale watu, lakini kama Waziri anarukaruka na kusema kwamba tunawekeza katika viwanda wakati hivyo viwanda vichache vilivyopo, watu wananyanyaswa, wanapewa mshahara mdogo, wanapewa shilingi elfu sita kwa siku badala ya shilingi elfu kumi na mbili halafu tunasema kwamba tunataka tuondoe umaskini kupitia viwanda! Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anatembelea kiwanda hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la ajabu kabisa kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini, hiki Kiwanda cha Dangote kimeanza kuzalisha *cement*, *cement* inazalishwa kwa wingi sana. Cha ajabu ni kwamba, bei ya *cement* Mtwara na Lindi ambako ndiko *cement* yenyewe inatoka ni shilingi elfu kumi na tatu na mia tano ukija Dar es Salaam, *cement* ile ile inayotoka Mtwara mpaka Dar es Salaam kilomita zaidi ya mia tano inauzwa shilingi elfu kumi na mbili, huku sio kuwadharau wananchi wa Kusini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunazungumza sana kwamba, tumenyanyasika sana Wanakusini lakini tukizungumza mnatupiga mabomu, mnatuletea Wanajeshi. Haiwezekani na haikubaliki hata kidogo na wala haingii akilini kwa watu wenye akili, kiwanda kiko Mtwara, halafu kinazalisha cement, pale pale Mtwara shilingi elfu kumi na tatu na mia tano, ikisafirishwa kwenda Dar es Salaam na maeneo mengine shilingi elfu kumi na mbili na mia tano, huku ni kuwadharau wananchi wa Kusini na wananchi wa Kusini tunasema tutachoka hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo suala zima la Viwanda vya Korosho. Viwanda vya Korosho kwa mfano pale Mtwara, kulikuwa na kiwanda kidogo kinaitwa Kiwanda cha OLAM, lakini kwa usimamizi mbovu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kile kiwanda kimeachwa kinahamishwa badala ya kutengeneza mazingira rafiki, hiki kiwanda niseme tu kwamba kilikuwa kinaajiri takribani akinamama 6,000 ambao walikuwa wanabangua korosho, lakini hakikutengenezewa mazingira rafiki, kikafanyiwa hujuma, mwisho wa siku yule mwekezaji amekihamisha hiki kiwanda na kukipeleka Mozambique. Halafu tunasema kwamba tunataka tuweke mazingira rafiki!

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja anafahamu kwamba kama kweli Serikali ingekuwa makini ikajikita katika kuwekeza na kufungua viwanda vidogo vidogo vya korosho, tunaamini kabisa umaskini ungeweza kuondoka katika Mikoa yetu hii ya Kusini na Tanzania kiujumla. Tunasema tu kwenye makaratasi, mikakati yetu haioneshi kwamba kweli tuna nia ya dhati ya kuhakikisha tunajenga viwanda hivi ili tuweze kuwakomboa wananchi wetu ambao ni maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, kama kweli tunahitaji kufufua viwanda ili viweze kuleta tija kwa Watanzania, tujenge Viwanda vya Korosho. Korosho yenyewe, kama unavyojua kwamba, kila kitu kinachotoka kwenye korosho ni thamani. Maganda yenyewe ni thamani, mafuta ni thamani, korosho zenyewe ni thamani! Tuhakikishe kwamba tunayenga viwanda vya korosho maeneo ya Kusini na Tanzania kiujumla ili tuweze kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie kwa kusema kwa mfano tuna madini ya *Tanzanite*, nilikuwa nafanya utafiti mdogo tu, nilikuwa naingia kwenye maduka kuangalia ni madini gani sasa hivi yana thamani. Ukiingia dukani ukakuta *Tanzanite* unaona ni miongoni mwa madini ambayo yana thamani kuliko madini mengine sasa hivi. Nashauri tujenge viwanda vya kufanya *processing*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nachuma muda wako umekwisha.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anatropia Lwehikila, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nichukue fursa hii kuwapongeza akinamama wote waliokuwa wanaadhimisha siku yao jana na kipekee kabisa wanawake wa UKAWA kwa namna tulivyoshikamana dhidi ya dhuluma na dharau yoyote inayoweza kujitokeza kwa mwanamke. Pia, nitoe masikitiko kwa Naibu Spika ambaye ni mwanamke alionekana kindakindaki kutopenda kukemea kilichokuwa kinatokea na hata tulipoomba nafasi ya kuonesha hisia zetu, alionekana kuiminye, nitoe masikitiko sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, *na-declare interest*, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Viwanda na Biashara, kwa hiyo, nimeshiriki sana katika kipindi hiki cha Ubunge wangu katika Kamati husika. Nimeona kwa vitendo ni namna gani tunamaanisha tukisema tunataka kujenga uchumi wa viwanda na ni namna gani tunawahadaa Watanzania tukitaka kuwaeleza ukweli juu ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe masikitiko yangu kwa sababu watu wengi wamepongeza hotuba, ukiiangalia hotuba kwa maneno tu siyo mbaya, lakini ukienda kwenye *money value* ya kile wanachokisema kwamba wanaenda kukitekeleza, ni vitu viwili tofauti. Pia, kwenye Kamati nilimwambia Waziri nikasema ni bora tuseme ukweli kuliko kuwahadaa Watanzania kwamba tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, ila tuseme siku moja tunaweza kwenda kwenye uchumi wa viwanda. Kwa bajeti ya mwaka huu ambayo ni shilingi bilioni 81 ukiisoma na uki-analyse kipengele kwa kipengele hatuwezi kwenda kwenye uchumi wa viwanda ila tunaweza kuanza kwenda kwenye uchumi wa viwanda pengine miaka 20 au 30 ijayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, tofauti yake na bajeti iliyopita ni ipi? Tofauti ya bajeti iliyopita ilikuwa ni shilingi bilioni 87. Kwa masikitiko kabisa bajeti ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 35, lakini mpaka Machi ilikuwa imetoka shilingi bilioni moja tu ikienda kwenye viwanda. Hao hao ambao tukonao leo wanaosema kazi tu ndiyo walikuwa kwenye madaraka, je, nini kilitokea? Kama bajeti imepangwa kwa 100% ambayo ni shilingi bilioni 35 ya kuendesha viwanda, lakini inapatikana 5% tu ambayo ni shilingi bilioni moja ya kuendesha viwanda, je, tunaweza kwenda tunakotarajia kwenda? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi nimesoma Dira na Dhima ya Wizara ya Viwanda, inaongea wazi kwamba inataka kutengeneza mazingira wezeshi ya ukuaji wa biashara. Ikaja kwenye Dhima inasema kutengeneza msingi shindani wa viwanda wenye kuwezesha biashara ulimwenguni na maeneo mengine. Unaona kwamba *plainly* Wizara imejikita katika kuandaa mazingira. Sasa kama tunaandaa mazingira, tunaandaa mazingira namna gani? Ni kwa kutengeneza sera ambazo ni rafiki kwa wawekezaji, ni kwa kutengeneza sera ambazo zitawezesha ushindani, ni kwa kutengeneza sera ambazo zitaweza kuwa-*accommodate* wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu. Kwa hiyo, sasa ambacho tungekuwanacho hapa ni kujadili sera ambazo zitasaidia kuleta viwanda. Hicho ndicho nilichokiona kwenye bajeti ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi sehemu kubwa ya ziara tuliyoifanya kilio kikubwa cha maeneo tuliyoenda ni maeneo ya uwekezaji hususan kupata maeneo ambayo tunaweza tukafanya uwekezaji kwa ajili ya maandalizi sasa ya viwanda. Tulienda EPZA wakatuambia kwamba katika bajeti ya mwaka jana walipaswa kulipa fidia ya shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kupata maeneo ya uwekezaji lakini ni shilingi bilioni moja ilitoka na kwa *inflation rate* tunapaswa kulipa shilingi bilioni 190.9 *almost* shilingi bilioni 191. Ile iliyokuwa shilingi bilioni 60 mwaka jana *inflation rate* imeenda mpaka leo tunahitaji kulipa shilingi bilioni 191! Hiyo fidia tu inazidi bajeti ya Wizara ambayo ni shilingi bilioni 81! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza kuwahadaa watu tunavyoweza, lakini uhalisia utabaki, tutarudi hapa mwaka kesho tutaanza kuogopa kuangaliana usoni kwa sababu hatuwaambii watu ukweli, ni usanii unaoendelea. Pesa iliyotengwa haiwezi kukidhi haja ya tunachotaka kufanya. Kwa hiyo, nasema ni bora tuseme uhalisia kwamba tuna *plan*, tunafikiria kutengeneza nchi ya viwanda, lakini bado hatujafika huko kwa sababu ya bajeti tuliyokuwanayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimeangalia ile miradi ambayo itakuwa vichocheo ambapo moja kati ya miradi hiyo ni kilimo. Ukiangalia kilimo na bajeti ya kilimo husika huwezi kuona *coloration between* kuwa na viwanda na kuwa na bidhaa zitakazosaidia viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilienda mbali zaidi kuangalia kweli nchi yetu iko *serious* inathamini kilimo? Nikaangalia ajira tu zilizoelekezwa katika sekta ya kilimo ilikuwa ni aibu kwa sababu Waziri, Mheshimiwa Angellah Kairuki alisema kwa mwaka jana kulikuwa na ajira takribani 3,000 ambapo kwenye kilimo ilikuwa ni robo ya ajira hizo 3,000 zilizokuwepo kwa mwaka jana. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni kwa namna gani hatujajipanga wala kuwekeza kwenye kilimo ambapo tunataraji kilimo kiwe ni kichocheo kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi ukiangalia 80% ya wananchi wetu kwa maana ya Watanzania ni wakulima ambao wanaishi katika *absolutely poverty*, katika umaskini wa kiwango cha juu. Wakaenda mbali zaidi wanaonesha kwa miaka 15 iliyopita uchumi wa mkulima ambao ni 80% umaskini umepungua kwa 3.4% ambayo ni kidogo sana. Hawa wakulima maskini ndiyo tunawatarajia wawe *catalyst* katika kuendesha viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati niliuliza, je, tumejiuliza ni kwa nini viwanda vili-*fail*? Ni kwa nini viwanda vilikufa? Takwimu ziko wazi! Viko viwanda 34 ambavyo vimekufa na vimegeuzwa kuwa maghala. Nilitaraji Waziri aje atuambie ni kwa nini vile vilikufa na tumeandaa mkakati gani kwa ajili ya kufufua tena hivyo viwanda? Mheshimiwa Waziri ameandika kwenye kitabu chake kwamba sababu kubwa ni kwamba watu walikopa pesa wakikopea hivyo viwanda na bahati mbaya vikageuzwa maghala lakini hiyo Serikali ya Hapa Kazi Tu ilikuwepo na hatujaona mkakati mahsusi wa kuzuia kurudi nyuma tulikotoka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea kidogo hujuma za dhahiri tunazofanya au Serikali inazofanya dhidi ya hata vile viwanda vidogo ambavyo vinajitahidi kuchechemea. Kama Kamati tulitembelea kiwanda cha TANALEC, wale ni wazalishaji wakubwa wa *transformer*. Hiyo kampuni ya TANALEC Serikali ina hisa ya 30%. Cha kushangaza Serikali imewahi kutoa tenda ndogo sana ya kuzalisha *transformer* 3,000 ambayo wanadai kwamba ni 10% ya *transformer* zinazohitajika nchini na tenda zilizokuwa zinabaki wamepewa nchi za nje, India, China na wengine. Hivyo kile kiwanda wanalalamika kwamba kukosa tenda za Serikali wamelazimika kupunguza ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wafanyakazi takribani 55 walilazimika kuacha kazi kwa sababu walishindwa kuwalipa kwa lengo la ku-*stabilise*, lakini kama haitoshi wameendelea kushindwa kujiendesha. Swali ni je, Serikali inajihujumu yenyewe? Kama sisi Serikali tuna hisa kwenye kiwanda kile kwa nini tunazidi kujihujumu? Moja kati ya hasara tunayopata tunashindwa kupata *Pay As You Earn* kwa sababu watu wametoka kazini. Tungewaajiri watu kwa sababu kile ni kiwanda chetu tungepata *Pay As You Earn* lakini pia tungeweza kusaidia familia mbalimbali za watu wale ambao wameajiriwa katika eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikubwa ambacho tulikiona ni mlundikano wa titiri za *regulatory authorities*. Ningependa Waziri atuambie nini tofauti ya *TFDA* na *TBS*? Wanafanya *almost the same function*! Kinachoonekana pale ni kuongeza mlolongo ili wale wafanyabiashara wakate tamaa. Nataka kujua pia tofauti ya *OSHA* na *Fire*! Kwa sababu *OSHA* wakifika kwenye kiwanda wanaangalia zile *fire extinguisher*, wale *Fire* wenyewe wakija wanaangalia *fire extinguisher*! Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie ni namna gani inaweza

ikapunguza mlolongo wa zile *regulatory authorities* kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa wafanyabiashara au wale wenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nimekiona ni changamoto, wale wafanyabiashara wanasema wanavyofika bandarini Serikali au mamlaka imekuwa ikipandisha bei kutegemea wao wanavyojisikia. Wanadhani kama mtu amechukua *container* la bidhaa fulani kutoka nchi jirani amekuja amepata punguzo kutokana na *competition* alivyoweza kupata, akifika bandarini wanamwambia kwa uzoefu wetu huwa inauzwa hivi. Kwa hiyo, imekuwa ni changamoto ya kuwapandishia bei wafanyabiashara kutegemeana na mahitaji ya yule anayefanya tathmini. Kama haitoshi vigezo haviko dhahiri ni kwa namna gani hiyo pesa imekuwa inaongezwa katika hizo bidhaa zao ambayo imeendelea kuwa changamoto.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mheshimiwa Ally Seif Ungando ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, kwanza naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi kwa kunipigia kura nyingi sana katika kugombea nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (NEC). Nawashukuru sana kwa kunipa kura nyingi na naahidi nitawafanyia kazi, sitawaangusha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kwa ufupi nimpongeze mama yangu, Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kazi nzuri aliyoifanya. Kwa kweli inadhihirisha wazi kwamba tunapokuwa na watu wazima basi mambo hayaharibiki. Tunamshukuru sana mama na akinamama wote kwa juhudi mlizozifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea labda nirekebishe wasemaji wenzangu waliomaliza kuongea sasa hivi, Mheshimiwa Anatropia aliyekaa sasa hivi alikuwa anajaribu kuongea kuhusu deni la EPZA. Ni kweli EPZA wanadaiwa kutoka shilingi bilioni 60 kwenda shilingi bilioni 190, ongezeko la deni hili si kama anavyosema ni kwa sababu ya *inflation*, hapana! Deni limepanda kwa sababu

interest rate imepanda siyo *inflation rate*. Kutokulipa deni hili kunafanya *interest* inapanda matokeo yake ni kwamba leo EPZA wanashindwa kulipa deni hilo kwa sababu ya ucheleweshaji wa kupeleka pesa! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali na mimi niungane naye, ipeleke pesa ilipe madeni ya EPZA waendeleo ku-facilitate yale maeneo na wawekezaji waje wawekeze pale. Wananchi wanadai fidia zao mpaka leo hawajapewa pesa, deni linabaki kwa wale wenye maeneo wanadai, Serikali na yenyewe ongezeko la deni linaongezeka kutokana na *interest rate*. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifanye juhudi maalum kwa ajili ya kwenda kulipa deni hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kuchangia siku za nyuma kuhusu maendeleo ya viwanda lakini naendelea kusisitiza. Upande wa viwanda na hasa viwanda vidogo-vidogo, tunaomba Serikali iweke mkakati wa kutosha, tuna vijana wengi nchini wanamaliza vyuo, wanamaliza shule lakini hawana mitaji, wana ujuzi mbalimbali, hawana pa kuanzia! Wakienda benki *interest* inayotolewa ni kubwa ni *more than 25%*, ni 17% mpaka 25%! Ukienda kwenye *commercial bank* kwa mtu wa kawaida hawezi akakopesheka na hasa vijana wetu kwa sababu kwanza wanakosa *collateral*, inakuwa ni vigumu wao kupata mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Serikali ije na mkakati maalum kwa vijana, iweze kutoa mikopo kupitia dirisha la TIB, mikopo maalum kwa ajili ya vijana, ikiwezekana wapunguziwe *interest rate*, yaani ile pesa ya riba, kutoka 25% inayotolewa na mabanki wapewe upendeleo maalum. Ikiwezekana wapewe 1% - 3% ili wakopesheke waweze kufanya kazi ya kuanzisha viwanda vidogovidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye masuala ya *agro processing*, tumezungumza vitu vingi sana kwamba tutaanzia na mazao yanayozalishwa na wakulima. Ni kweli, tuanze huko lakini kuna tatizo la kodi kero. Nami na-declare *interest*, tumezunguka kama Kamati ya Viwanda na Biashara tumekuta mfano, ukinunua alizeti kutoka Bariadi, Mkoa wa Simiyu kupeleka Singida kwa ajili ya kukamua pale Mkoa wa Simiyu anakutana na geti anatoa ushuru. Akifika Maswa anakutana na geti anatoa ushuru. Akifika Shinyanga anakutana na geti anatoa ushuru. Akifika Singida anakutana na geti anatoa ushuru, ndipo anapofikisha kwenye kiwanda. Huu ushuru mdogo mdogo unafanya *production* inakuwa ina-high cost, matokeo yake bidhaa unapoipeleka sokoni huwezi ku-compete na mtu anayeingiza mafuta ya kupikia kutoka nchi za nje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbuka mafuta yanayoletwa hapa kutoka nchi za nje (*crude oil*) ina kodi ndogo sana. Sasa huyu mtu anayemnunua alizeti

kwa ajili ya kukamua anakuwa ameingia gharama kubwa ya kulipa kodi ndogo ndogo. Hizo kodi wakati mwingine zinapokusanywa hazifiki mahali husika. Kwa hiyo, ni bora kodi hizi zingefutwa ikawezekana huyu mzalishaji ukampa kodi moja kubwa ya mapato kuliko kuingia gharama ya kulipa kodi ndogo ndogo na kero. Tunaomba hili suala lifanyiwe kazi kwa haraka kwa kweli ni kero kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niliwahi kuongea nalisitiza tena, tutafute mbegu bora, mbegu za kisasa ambazo zina mazao mengi. Kwa mfano, alizeti tunapata 70% tu ya ku-extract mafuta kama ukikamua, tunaomba mbegu bora. Ufanyike utafiti maalum kwa kuleta mbegu bora za uzalishaji kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Ufugaji. Mbegu zenyewe siyo za mazao tu, hata za mifugo, tunataka mbegu bora ili tuweze kuvuna mavuno bora. Tunasisitiza tena na hili liingie kwenye kumbukumbu na Serikali ifanye juhudi maalum kwa kazi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la viwanda vinavyoajiri watu wengi na hasa viwanda vya nguo (*textile*). Ningekuwa naongea na Mheshimiwa John Pombe Magufuli leo ningemwambia katika mambo ambayo unatakiwa uyaanzishie Wizara ni Wizara ya *Textile*. Tungeanzisha Wizara au Idara Maalum kwa ajili ya *Textile* maana kwenye *textile* kuna mambo mengi, huwezi ku-produce shati bila kuweka vifungo. Huwezi ku-produce shati bila kuwa na *material* ya *plastic*, kuna vitu vidogovidogo vingi ambavyo vinaweza kwenda kutoa shati na suruali na vitu vingine. Tukiwa na Idara Maalum au Wizara Maalum basi itahakikisha sisi Tanzania tuna-specialise kwenye masuala ya *textile* tu. Pamba tunayo, watu tunao, maeneo tunayo, tuna uwezo wa kufanya *production* ya nguo kuliko nchi nyingine yoyote kwa *East Africa* na Bara zima la Afrika. Tunaomba hilo nalo lifanyiwe uangalizo maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Kiwanda cha Urafiki. Tulitembelea kiwanda hiki, 51% inakuwa owned na China na 49% ni Tanzania tunamiliki. Wachina hawafanyi *production*, *capacity* ya Urafiki ni kuzalisha mita za nguo milioni 30 kwa mwaka lakini *production* ya leo ni milioni tano kwa mwaka. Ukienda kwenye store ya Urafiki nje kuna magari yanasubiri *production* iishe ili wapakie kanga wapeleke Kariakoo. Ina maana *demand is high*, *production is low*. Wachina mkakati walionao siyo ku-modernize tena kile kiwanda, wanachotaka wao kufanya ni kuondoa kiwanda na kufanya iwe ni *shopping mall*, waweze ku-import product kutoka China, wapeleke ajira China, Tanzania tumelala. Mheshimiwa Waziri naomba kwa suala la Urafiki mtoe mkakati tusaidiane, nunueni hizo 2% za Urafiki *ownership* irudi Tanzania tuendeleze kile kiwanda tufanye *production* inayoeleweka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la TANALEC, mwenzangu Mheshimiwa Anatropia kaliongea. Ukienda Kenya tulisoma tenda *document* za Kenya TANALEC wanafanya *production* ya transfoma lakini hakuna upendeleo wa nchi yetu kufanya TANALEC iweze ku-*supply* transfoma Tanzania. Wenzetu wa Kenya niliona *tender form* wanazotoa, wanatoa tenda za transfoma kwa vifaa vya umeme na wanatoa elekezo kwamba hii itajazwa na *local manufacture* tu. Sisi Sheria yetu ya PPRA inaangalia bei, turekebishe, TANALEC imekosa kazi kwa sababu ya sheria hii. Tulimwita *Director General* wa TANESCO akatuambia tunashindwa kununua TANALEC kwa sababu ya Sheria ya PPRA. Tunaomba sheria hii iletwe mapema turekebishe, tu-favor viwanda vyetu. Tunazungumzia viwanda halafu tenda tunapeleka India maana yake nini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la uwekezaji, tunaomba zitoke *special incentives* kwa wawekezaji wanaokwenda kuwekeza mikoani. Sasa hivi eneo zuri la kuwekeza ni Dar es Salaam lakini limejaa, hakuna nafasi. Tunaomba watu wapewe *incentive* wakawekeze nje ya Dar es Salaam, wapewe *special incentive*. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Seif Ungando atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Mheshimiwa Azzan Zungu ajiandae.

MHE. ALLY S. UGANDO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika mada hii ya viwanda. Kwanza, niwashukuru sana wananchi wangu wa Kibiti kwa kunipa kura nyingi sana na nawaahidi sitowaangusha. Pili, napenda kuwashukuru na kuwapongeza akinamama wote kwani tunafahamu bila ya mama tusingekuwa hapa duniani, kwa hiyo, hakuna mtu kama mama. Napenda pia kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwenda kujielekeza katika mada hii ya viwanda. Mada hii ya viwanda ni muhimu sana kwani inagusa sana maisha ya mwanadamu hususani vijana katika soko la ajira. Angalizo langu ningeanza kwa kusema kwamba Waziri mwenye dhamana aangalie ni maeneo gani ya kuanzisha viwanda kutokana na malighafi zinavyotoka sehemu husika. Mfano katika Jimbo langu la Rufiji, tunalima sana mananasi, mpunga, mihogo na korosho. Kwa hiyo, tuna kila sababu lazima tupate viwanda sambamba na

mazao hayo. Atakapotuletea viwanda hivyo naamini wakulima wetu sasa watapata soko lenye tija sasa hivi soko la mazao ya matunda ni moja tu kwa Bakharesa, wananchi wetu wakipeleka mazao yao wanakaa foleni kubwa matokeo yake mazao yao yanaharibika na mkulima anapata *short*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rufiji tuna Kiwanda cha Kusindika Samaki Nyamisati, lakini kiwanda hiki hakifanyi kazi. Naomba Waziri mwenye dhamana tukutane naye ili tuangalie changamoto ni nini ili kiwanda hicho kianze kufanya kazi. Unapozungumzia *prawns* lazima utaigusa Rufiji kwani *prawns* wengi wanapatikana Nyamisati na kiwanda hiki kipo sehemu yenye kina kirefu cha maji. Unapozungumzia kiwanda huna budi urekebishe na uboreshe maeneo ya kufanyia kazi ikiwemo kupeleka maji, umeme na barabara ili mwekezaji anapokuja apate urahisi wa kuwekeza katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kutoa ushauri kwa Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwamba hivi viwanda vinavyoagiza mitambo kutoka nje iangalie ni jinsi gani ya kupunguza kodi. Kwani kodi mkiweka kubwa, hawa jamaa watakaokuja kuwekeza katika viwanda hivi wataona kama mzigo mkubwa ambapo wataona haina tija kuwekeza katika nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rufiji tuna Bonde la Mto Rufiji lakini naliona kwamba halina tija yoyote. Sasa hivi tuna uhaba wa sukari, lakini katika bonde hili tungelima miwa na kuweka viwanda vya sukari hata hii shida ya sukari hapa nchini naamini ingeepukika kabisa au kupungua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia viwanda lazima uboreshe mazingira ili yawe rafiki kwa watu watakaokuja kuwekeza katika maeneo husika. Angalizo langu ni kwamba wawekezaji wa nje wanapokuja ni lazima wananchi wa maeneo au wazawa wa maeneo yale wafaidike. Tunachoogopa wasije wawekezaji kutoka nje wakafikia mjini wakachukuliwa na *master plan* wale wananchi wanaozunguka maeneo yale wakawa hawafaidiki na sekta hii ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuzungumzia mikopo katika taasisi za kibenki, naomba wazawa wapewe elimu ya ujasiriamali ili waweze kujiajiri wao wenyewe. Katika elimu hii ni vema tukaboresha vyuo yetu vya VETA na viwanda vyetu vidogo vidogo (*SIDO*) ili wananchi wapate jinsi ya kujifunza ili waweze kujiajiri wenyewe na kujitegemea katika sekta hii ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nipende kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa utendaji wake wa kutumbua majipu. Wadengereko wote wa Rufiji wanasema wako pamoja naye na wanamuunga mkono kwamba aendee kutumbua majipu ya nchi hii kwa

sababu wananchi sasa wanahitaji maendeleo hawataki maneno. Wameona utendaji wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwamba unaleta tija kwa nchi hii. Nasi tunamwomba kwa Mwenyezi Mungu apate afya njema aendelee kutumbua majipu ili kila mmoja afuate taratibu zinazotakiwa katika utendaji wake wa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia viwanda lazima unagusa maisha ya watu wa hali ya chini. Kwa hiyo, bajeti hii naiunga mkono mia kwa mia, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Ungando kwa kutunza muda. Hata hivyo, ilikuwa uongezewe dakika kadhaa kama ungekuwa hujamaliza kuchangia. (Makofi)

Sasa tutamsikia Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Azzan Zungu ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba nianze kwa kumuuliza swali Waziri wa Viwanda na Biashara. Waziri wa Viwanda na Biashara nataka ulijibu Bunge letu, unataka kujenga viwanda vya nini? *Focus* yetu ni viwanda gani? Maana unapotaka kujenga viwanda, ukisema unataka kila kitu niweke kiwanda tumeanza na kushindwa. Nilidhani umefika wakati tuamue *focus* yetu iwe kwenye maeneo ambayo tuna *comparative advantage*. Ukiambia leo tunaweza tukashindana na China, India na nchi zile ambazo zimefanya vizuri tutapata tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, atuambie kwa hali ya dunia inavyokwenda, Tanzania tunaweza tukaanza na viwanda vya namna gani. Ukienda leo pale *Silcon* wameanzisha teknolojia lakini wana *invest* kwa ajili ya teknolojia hii, wanafanya *research*, wameandaa mazingira kwa ajili ya viwanda vya teknolojia. Ukienda *Auto Mobile* duniani inajulikana, siyo wote wana *Auto Mobile*. Ninachouliza kama Tanzania tunatakiwa twende kwenye viwanda vya namna gani? Mimi nimesoma hapa, ukiangalia mwanzo mpaka mwisho sioni tunakwenda kwenye viwanda vipi, yaani *focus* yetu ni nini. Tusipokuwa na *focus* tutarudi kule kule tulikotoka miaka ya nyuma. Ndiyo maana unasema leo mara unataka uanzishe hiki, uanzishe hiki, hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niulize, maana yako mambo ambayo tusipoyaweka sawa tutakuja kushindwa huko baadaye. Mimi nasema kama nchi tunge-*concentrate* kwenye viwanda vya *agro-industries* kwa sababu tuna

malighafi. Leo tukiamua kama nchi, maeneo manne tu tufanye kweli kweli, mfano Kiwanda cha Mbolea, kiwanda kikubwa ambacho tuna uhakika tutazalisha mbolea ambayo itatumika *Sub-Sahara Africa*, tutapata fedha nyingi sana kama nchi na tuta-save dola nyingi sana za ku-import mbolea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili, ni viwanda vya sukari, hizi kelele hizi ni kwa sababu hatujaamua ku-invest kwenye viwanda vya sukari. Tukiamua ku-invest kwenye viwanda vya sukari Tanzania tuna hekta karibu milioni nne unazoweza kufanya *irrigation*, tunaweza kuzalisha karibu tani milioni mbili za sukari, tutatumia ndani na nyingine tutauza nje na tutafaidisha sana wakulima wetu ambao wako kwenye hayo maeneo. Namba tatu, mafuta ya kula, tuna michikichi, tuna alizeti, tu-concentrate hapo kwa kuanzia. Namba nne ni *leather industry* kwa sababu tuna mifugo mingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akija hapa anasema kila mtu atajenga kiwanda awe na uhakika atashindwa, kwa sababu viwanda vinahitaji Serikali tuungane, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Nishati na Madini lazima wote tuongee lugha inayofanana. Ukisoma vitabu hapa, ukasoma Mpango, lugha haifanani. Sasa tunataka kujenga viwanda gani? Imefika wakati lazima tuambiane, tunawaunga mkono lakini lazima kuwe na *coordination unity* ambayo inawaunganisha tujue *direction* ya namna moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha anataka kukusanya kodi, lakini kuna wakati lazima tutumie kodi kutoa *incentive* ili viwanda viweze kujengwa. Ili viwanda viweze kujengwa wenzetu wamefanya *research*, kuna mambo lazima tuhangaike nayo, lazima uangalie *micro-stability* ya nchi. *Micro-stability* yetu inasemaje? Kama huangalii hili *investor* haleti fedha zake! Lazima uangalie *skills and education*, hapa kwako mambo ya elimu yakoje? Lazima uangalie *infrastructure* kwa maana ya umeme, maji na *transport system*. Lazima uangalie teknolojia, hali ya *innovation* na teknolojia wewe unafanyaje, kwako pakoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya kupata teknolojia ziko njia tatu, moja kutoka nje, mbili *through FDI*, tatu *research and development* ili kupata teknolojia ambazo ni *locally made*. Kama viwanda tutasema tu tutarudi kule tulikotoka na nina hakika hatutoweza kufanikiwa. Tukiamua kuungana tukajiweka kwenye viwanda ambavyo malighafi tunazo Tanzania ambazo ni *agriculture* tutabadilisha maisha ya watu wetu vijijini na nchi hii itaweza kupata fedha nyingi za kigeni na tutaweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa ni Waziri wa Viwanda na Biashara, hali yetu ya biashara ni mbaya. Ukiangalia *cost of doing business in Tanzania*, kwa ripoti ya *World Bank* ya 2016 tuna *rank* ya 139 katika nchi 189, hili siyo jambo

jema. Kwa hiyo, lazima Waziri wa Viwanda na Biashara ufanye kazi ya kufanya biashara zikue Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi wamesisitiza kuhakikisha tunaanzisha Bodi ya Kusaidia biashara ndogo ndogo (SMES) wala sioni ukieleza *thoroughly*, kwa sababu hiyo ndiyo itakayowaokoa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo, wataajiri watu wengi, tutapata kodi nyingi sana. Kama haturasimishi biashara tunalo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwambia Mheshimiwa Waziri kwa mfano, wanasema ukitaka kuanza biashara Tanzania sisi tunachukua nafasi ya 129 katika nafasi 189, ukitaka kupata *construction permit* tunakuwa wa 126, kupata umeme wa 83, ku-*register property* wa 133, kupata *credit* wa 152, kuwalinda *minority investors* wa 122, kulipa *tax* wa 150, *trading across borders* wa 180 kati ya 189, *enforcing contract* wa 64 na *resolving insolvency* sisi ni wa 99. Waziri wa Viwanda na Biashara lazima uhangaike kuhakikisha unajenga mazingira ya biashara kukua Tanzania. Tusipojenga mazingira ya biashara kukua Tanzania maana yake ni moja tu, hata hivyo viwanda tunavyoviongea havitapatikana, wawekezaji hawatapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema Waziri anaposhughulika na suala la viwanda na biashara lazima ajue analo jukumu la kuhakikisha biashara inaenda vizuri isidumae. Ili isidumae lazima uondoe hizi *bottlenecks*! Tanzania tumeumbwa tuna nchi karibu nane zinatuzunguka, hii ni *advantage* kwetu kiuchumi, je, tunaitumiaje? Lazima mipango yetu iende *towards* kwenye kuleta biashara na siyo tu biashara hata kufanya biashara Tanzania isiwe tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waziri wa Viwanda ukae na Waziri wa Fedha, *concentration* yetu isiwe kukusanya kodi tu, lazima tutumie kodi kukuza uchumi. Unakuza uchumi kwa wafanyabiashara, kwa kuweka mazingira ya watu kuleta fedha zao kwako na hatuwezi kuamini kwamba tunaweza tukaleta mageuzi ya viwanda kwa kutumia fedha za bajeti, haiwezekani! Tukidhani unaweza ukatumia fedha za bajeti mjue tunaelekea kwenye kushindwa. Ili mwenye fedha zake aje, asiende Mozambique, Kenya, Rwanda lazima uweke mazingira ya kumkaribisha aone kwamba Tanzania nikienda nitapata zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumehangaika kule Kigoma, Wahindi wanataka kuleta Kiwanda cha Sukari, wamezungushwa mambo ya ardhi karibu sijui miaka mingapi, inawezekanaje? Huku tuna matatizo ya sukari *in the country*, kuna mtu anataka kuja kuweka kiwanda anazungushwa tu. Lazima haya Waziri wa Viwanda uhangaike nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Serikali iunde *committee* ambayo itahusisha watu wa Wizara ya Fedha na Mipango; Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Viwanda, Biashara na Uwekezaji; na Nishati na Madini, ili mkikaa muwe mnajua hali inavyokwenda nchini kwa maana ya kuhakikisha mnaondoa *bottleneck* za biashara nchini ili watu waweze ku-*invest* Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema Waziri nakuunga mkono, lakini nasema ukisoma mipango yako naona unataka kuanzisha kiwanda *everywhere as if* viwanda ni jambo rahisi, suala la viwanda siyo rahisi kama tunavyotaka kuiweka, unaweza ukaweka viwanda kesho vyote vikafa. Ndiyo leo unataka kufufua *General Tyre, is it our priority?* Huo mpira wenyewe umeanza kuulima? Maana unaweka bajeti leo kwa ajili ya *General Tyre* shamba hujaanza kulima, je, hayo matairi yako yanaweza yaka-*compete* kwenye biashara nyingine duniani, unaweza u-*compete* na wengine? Ukiangalia *cost* zako unaweza uka-*make money* ama tunataka kurudisha *General Tyre out of prestige* kwamba na sisi tumefufua, *prestige!* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara jamani ni *economics* tuache kuchanganya siasa, biashara na viwanda. Suala la viwanda na biashara, tukachanganya na siasa, nina hakika, hatutakwenda tunakotaka kwenda. Nakuamini Waziri, Serikali ina nia njema, lakini kaeni muwe *more focused*, tuanze vile tunavyoviweza ambavyo *raw materials* zake ziko Tanzania na tukizalisha vizuri tutaweza kuuza angalau *regionally* kabla hatujaenda huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Azzan Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah wajiandae.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniweka kwenye orodha ya leo ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja ya Waziri. Nachukua nafasi hii vile vile kupongeza jitihada zinazoendelea kufanywa na Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli katika kupambana na kuhakikisha nchi yetu inakuwa kwenye mstari sahihi. *Desperate times desperate measures.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni ndogo tu, ni namna Wizara ya Biashara inaweza ika-*sensitize*, ikashirikiana na mikoa yote, ni namna gani ya kuweza kusaidia na kunyanyua *informal sector* katika nchi yetu. Sekta ambayo siyo rasmi kama mama lishe, bodaboda, machinga, *welders* na vinyozi. *Informal sector* kwenye nchi jirani hapa, hawa bodaboda, machinga, matatu, *welders*, mama lishe, vinyozi huchangia dola bilioni nne kwenye pato la Serikali. Pesa hizi

zinatumika kuwasaidia tena hawa hawa katika kuwaboresha zaidi ili kuweza kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano kwa Mkoa wa Dar es Salaam tuna wafanyabiashara wa *informal sector* sio chini ya milioni mbili. Fanya kila mmoja analipa shilingi mia tatu tu kama ada ya ushuru kwa siku mamlaka zinazohusika zitapata milioni mia sita kwa siku, kwa mwezi ni shilingi bilioni 18, kwa mwaka shilingi bilioni 216. Kama kuna programu ya kuhakikisha wanawekwa katika mazingira mazuri tunapata shilingi bilioni 432 kwa kipindi cha miaka miwili tu kwenye *informal sector* kwenye Mkoa wa Dar es Salaam. Pesa hizi zinakuwa *ringfenced*, zinalindwa, wanaanzishiwa majengo mapya ya kisasa na kufanya biashara katika mazingira mazuri. Pesa hizi zinaweza zikatumika kuanzisha benki ya wafanyabiashara wadogo wadogo, pesa hizi zinaweza kutumika wafanyabiashara hawa hawa wadogo ambao ndiyo *shareholders* wakaji-*involve* kwenye masuala ya biashara ya kilimo. Ethiopia wameweka programu ya kuwafanya vijana kupenda kilimo. Wamechukua vijana 10,000 miaka minne iliyopita, wamewaonesha kilimo cha kisasa na sasa hivi wanafanya kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta isiyokuwa rasmi ikiwezesha nchini mwetu, ni dhahabu na ni *goldmine* katika mikoa yote ya Tanzania. Nataka kujua kuna *networking* gani inayofanywa katika Wizara ya Nishati, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Biashara? Wizara hizi tatu lazima ziwe pamoja kama alivyosema Mheshimiwa Serukamba lazima, tuwe na *raw materials* na vitu vyote vitapatikana kwa *networking* ya Wizara hizi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kutazama sekta isiyo rasmi ambayo tunaiona ni bugudha, tunaiona ni sekta ya kufukuzana nao mitaani, tunaiona kama ni sekta ambayo ni *parasite* wakati sekta hii ikisimamiwa vizuri inaweza ikatoa mchango mkubwa sana kwenye Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la alizeti mwaka huu nchi nzima kila mkoa uliolima alizeti wamepata *bumper harvest* lakini wanakatishwa tamaa na mafuta yanayoagizwa nchi za nje. Naomba Serikali ijaribu kudhibiti tunyanyue watu wetu, tuzuie *product* kutoka nje na tuweze kuwasaidia katika *agro-industries*. Soko la mafuta ya chakula linapatikana DRC, Rwanda, Burundi na katika *region* yote hii ya East Africa na ni soko kubwa sana ambalo litawanyanyua hawa wakulima. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Waziri wa Biashara yuko hapa ajaribu kutazama masuala haya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali mjaribu kutazama namna gani mtanyanyua *informal sector*. Mjaribu kutazama namna gani one

stop center ya kuleta wawekezaji nchini mwetu itarahisisha uwekezaji kwa kuangalia policies na sheria ambazo zitawavutia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya machache, mimi sina mengi, mara nyingi nachangia kidogo kuwaachia nafasi watu wengine, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Esther Midimu ajiandae.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hii hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyoonyesha na kwa muonekano wake, anaonekana amejiandaa na yuko tayari kulitumikia Taifa hili katika kuhakikisha kwamba katika kipindi chake cha miaka mitano basi suala la viwanda linakuwepo katika nchi yetu, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi yake nzuri ambayo anaifanya. Mahali popote unapopita, kwa kweli kila mmoja anaona kwamba sasa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimeanza kwenda mchakamchaka. Sisi kazi yetu ni kuendelea tu kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, aendelee kuwa na maisha marefu, lakini na kazi yake iweze kuendelea vizuri kwa kadri inavyoonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kumwomba Mheshimiwa Waziri, pale kwangu kwa maana ya Jimbo la Musoma Mjini, kwa bahati mbaya sana tuko pembezoni. Huwezi kupita Musoma kwenda mji wowote ule, ili uje Musoma lazima ufunge safari ya kuja Musoma na hatuna economic activity yoyote zaidi ya biashara ndogondogo na viwanda. Ombi langu la kwanza, nimwombe kabisa Mheshimiwa Waziri hebu apange, tukae siku kama tatu hivi pale Musoma maana tulikuwa tunasaidiwa na Kiwanda cha *Mutex*, Kiwanda cha Nguo, nacho hivi leo ninavyozungumza kinaenda kwa kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, viko viwanda kama vinne vya samaki, kwa bahati mbaya sana sasa hivi tunacho kiwanda kimoja tu nacho kinasuasua. Kwa hiyo, kwa maneno mengine, watu wa Musoma Mjini leo hawana ajira, vijana hawana kazi za kufanya, matokeo yake sasa ni kuongeza vibaka lakini na uchumi wa mji unaendelea kudorora. Kwa hiyo, hilo ni ombi langu la kwanza ambalo naomba kwamba hebu tufike kule ili tuweze kusaidiana tuone tutafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Mutex kilipobinafsishwa, kuna mafao ya watumishi ambayo nimeyapigia kelele katika Bunge hili toka mwaka 2005 hadi leo, wale waliokuwa wanadai wengi wao wamepoteza maisha, lakini hata watoto wao wanaendelea kudai. Kwa hiyo, nimwombe kabisa Mheshimiwa Waziri tutakapofika pale, tupate nafasi ya kuzungumza nao na Serikali sasa itoe majibu yao ya mwisho ili wajue kama hayo mafao yao wanayapata au la kama hawayapati basi waweze kufahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili zoezi la kuendeleza viwanda, tunavyo viwanda vya ngozi hapa nchini. Hivi viwanda vinaonekana vimekufa kwa sababu mpaka leo ukiangalia kwa wafanyabiashara au wachinjaji ngozi zao wanatupa bure. Kwa sababu leo anauza kilo ya ngozi kwa bei isiyozidi sh. 200, tafsiri yake ni kwamba, hakuna wanachokipata. Kwa hiyo, tunadhani na hili nalo Mheshimiwa Waziri ajaribu kutuambia, hivi viwanda vilivyopo mkakati wake ni nini katika kuwasaidia wananchi wetu wa Tanzania maana vinginevyo tutajikuta wale Watanzania tulionao ambao wanafanya biashara hizo basi wanaendelea kufilisika siku baada ya siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo na kwa ufupi hili suala ambalo Serikali imezungumza kwamba tunahitaji kukuza viwanda. Mchango wangu ni kwamba, kama leo tunakubaliana kwamba Tanzania tunahitaji iwe ya viwanda, lazima tukubaliane hivi viwanda tunavyovihitaji ni viwanda vya aina gani. Leo ungeniuliza mimi vile viwanda vikubwa vyote vinavyokuja, kwanza vingi ni *automation*, utakuta kiwanda ni kikubwa lakini watu kinaowaajiri ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu la kwanza pamoja na kuanzisha viwanda na kwa kuwa lengo letu ni ajira tungeiangalia vizuri sana *SIDO*, tuangalie namna ya kuiwezesha kwani kule vijana na akinamama wanapata mafunzo mbalimbali. Ni imani yangu kwamba yale mafunzo wanayoyapata, ukiangalia wanaweza kuzalisha bidhaa nzuri sana, zile bidhaa zinaweza zika-*compete* katika masoko mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuendelea sasa ni vizuri Mheshimiwa Waziri akawa na mkakati maalum, kwanza kuhakikisha kwamba wataalam wanaendelea kuwepo *SIDO* na mafunzo yanaendelea kutolewa. Bahati nzuri *SIDO* ipo karibu katika kila mkoa, kama ni vijana pamoja na akinamama tayari wameshajifunza, wamepata mafunzo sasa tuna nafasi ya kuwapa mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni kwamba hata vile viwanda ambavyo tunaona vinaleta bidhaa nyingi, maana Mheshimiwa Waziri leo amejibu hapa kuhusiana na suala la *toothpick*, amesema kwamba kile kiwanda kinagharimu siyo zaidi ya dola 28,000, wako Watanzania wengi tena wenye

uwezo wa kawaida wanazo hizi fedha, lakini tatizo letu sasa ni kwamba hawa Watanzania wengi hawana exposure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe kinachotakiwa sasa, tukishatoa haya mafunzo, wakati mwingine Mheshimiwa Waziri hawa Watanzania hebu waulizwe, naamini watakuwa tayari kupata exposure kwa fedha zao, waende kwenye nchi za wenzetu kama India, China na hizi nchi Asia, viko viwanda vidogo vidogo huko ambapo wakirudi watavianzisha hapa kwa fedha zao na kwa kusaidiwa na benki na vingi viwe vile ambavyo vinaweza kuzalisha bidhaa zinazoweza kutumika humu nchini. Kwa hiyo, tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo tunaweza kusaidia Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo mimi binafsi nalifahamu na hizo ni hisia zangu, ni kwamba, Serikali yetu haijawa tayari kuhakikisha kwamba inawasaidia hawa Watanzania ambao wanaibukia kwa kuwajengea uwezo ili na wao waweze kufanya biashara. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tukienda kwa utaratibu huo hii *SIDO* itafanya kazi nzuri. Hebu tuzalishe zile bidhaa ambazo tunaweza kuziua humu humu nchini na kwenye hizi nchi za jirani kuliko kuanza kupambana na yale masoko ya wenzetu, masoko ya Ulaya ambayo ushindani ni mkubwa kwa hali yetu kusema ukweli siyo rahisi sana tukaweza kuingia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye nchi za wenzetu mfano kama Syria, kila mwaka kuna bidhaa ambazo wanaleta hapa nchini. Zile bidhaa zote zinatengenezwa na viwanda vidogo vidogo kama *SIDO*. Ukienda kwenye nchi jirani ya Kenya, kuna hivi viwanda wao wanaita Juakali, Juakali ina mchango mkubwa sana Kenya na inatengeneza bidhaa nyingi, nzuri na ambazo zinaweza zikashindanishwa katika masoko mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu ni hilo kwamba hebu tuangalie namna ya kuweza kuisaidia *SIDO*, watu wapakata mafunzo na baada ya kupata mafunzo tuone namna ya kuwasaidia, lakini namna wanavyoweza kupata exposure na wakaja kufanya biashara zao mbalimbali na tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo basi tutakuwa tumewasaidia sana Watanzania wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mchango wangu kwa leo, lakini niendeleo tu kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, kusema ukweli wale watu wetu wa Musoma kule wanahitaji msaada mkubwa wa Serikali ili waweze kuendelea. Nina uhakika vijana na akinamama wakisaidiwa wanaweza kujikwamua. Maana hayo mengine nazungumza kutokana na uzoefu wangu kwamba pale tulipojaribu kuwasaidia vijana, pale tulipojaribu kuwasaidia akinamama wanaweza kwenda, lakini tatizo kubwa ni kwamba vijana hawana ramani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA. Mheshimiwa Esther Lukago Midimu atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga wajiandae.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa namshukuru Waziri kwa hotuba yake nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kuchangia mchango wangu. Mkoa wetu wa Simiyu ni wakulima wazuri wa pamba lakini cha kusikitisha zao hilo linaenda kufa kabisa, wananchi wamekata tamaa kabisa kwa sababu ya bei kushuka. Suluhisho pekee la bei ya pamba ni kutuletea kiwanda cha nguo na nyuzi. Mkituletea kiwanda cha nyuzi, nina imani vijana wengi watapata ajira na bei ya pamba itapanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Simiyu tuna viwanda vitano vya kuchakata pamba. Naona na wenye *ginneries* wamekata tamaa, nashindwa kuelewa kwamba zao la pamba likifa viwanda vile vitafanya kazi gani. Naomba mtuletee kiwanda cha nyuzi na kiwanda cha nguo, nina imani hata wao watauza marobota yao karibu zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mkoa wetu ni wa wafugaji, tunaomba mtuletee kiwanda cha nyama. Nasema hivyo kwa sababu wafugaji wetu wanaibiwa sana, wakipeleka mnadani ng'ombe mmoja anauzwa shilingi laki mbili mpaka shilingi laki tatu lakini ng'ombe huyo huyo ukimlisha na kumnenepesha ukimpeleka kiwandani unamuza shilingi laki nane mpaka shilingi milioni moja, naomba mtuletee kiwanda cha nyama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu kuna akinamama wajasiriamali wakubwa na wazuri sana, wana vikundi vikubwa. Naomba Serikali iwalettee viwanda vidogo vidogo vya *SIDO* vya kusindika mazao ili waweze kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu yalikuwa ni machache tu ya kuomba viwanda, Serikali yangu ni sikivu, naomba ituletee viwanda hivyo katika Mkoa wetu wa Simiyu. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Midimu ahsante kwa kututunzia muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ajiandae.

MHE MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri iliyojitosheleza. Namfahamu sana Mheshimiwa Mwijage, nilijua na niliamini ataleta hotuba nzuri ambayo imejitosheleza kama alivyoisoma hapa. Pia Waziri huyu ni msikivu na ni mfuatiliaji sana na Wizara hii inamfaa kwa sababu amekuwa akitushauri, amekuwa akitufuatilia kwenye mikoa yetu kuona kipi kinafaa ili tuweze kufanikiwa. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa azma yake ya kufanya Awamu ya Tano kuwa ya viwanda. Hii analenga kutubadilishia uchumi tulionao wa chini na kutupeleka kwenye uchumi wa kati. Hivyo tuungane sisi Mheshimiwa Wabunge kumwomba Mheshimiwa Rais na Serikali yetu ili tufikie hapo tunapokwenda na tusiwe watu wa kukatisha tamaa, tuwe watu wa kuwapongeza na kuwashauri ili tuweze kufikia pale tulipokuwa tumejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu niliongelea kuhusu suala la tumbaku lakini kwa umakini wa suala hili, naomba niongee tena. Nimkumbushe pia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Tabora tunalima tumbaku kwa asilimia 60 lakini Serikali imewekeza pesa nyingi sana kwenye reli na barabara, hii pia inasaidia sisi Mkoa wa Tabora kupata viwanda kwa sababu sasa tutakuwa na reli na barabara nzuri, tumbaku tunalima asilimia 60, sioni sababu gani inayoweza kufanya sisi Tabora tusiwe na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepiga kelele sana kuhusu viwanda vya tumbaku Tabora, lakini hata kiwanda cha ku-process hatuna. Wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu niliongea, namshukuru sana Mheshimiwa Mwijage, alinifuata na akaniambia kwamba amepata mwekezaji wa Kichina na atakuja hapa sisi Wabunge wa Mkoa wa Tabora tutaongozana naye kwenda Tabora. Nimwombe sana Mheshimiwa Mwijage atutimizie hilo neno alilotuambia ili sisi Wabunge wa Tabora angalau tuonekane sasa tunajali wananchi wetu maana hawatuelewi na wana Wabunge humu ndani zaidi ya 12. *(Makofi)*

Wabunge wa Tabora sasa tuna mkakati mkubwa wa kuhakikisha Tabora tunapata kiwanda cha tumbaku, wote tumekubaliana tuhakikishe Serikali inatupa kiwanda cha tumbaku au hata cha ku-process tumbaku. Nimshukuru Waziri Mwijage ametuahidi kwamba atatuletea Mchina. Mheshimiwa Waziri hali ya ajira Tabora ni mbaya, vijana wetu hawana ajira wakati sisi ni wakulima wakubwa wa tumbaku, naomba tupate kiwanda. Sijui nani alitoa wazo nchi hii la kupeleka kiwanda cha tumbaku Morogoro wakati tumbaku inalimwa Tabora!

Kwa kweli huwa najiuliza hata sipati jibu, sioni sababu. Kibaya zaidi juzi tena kimejengwa kiwanda kingine cha sigara Morogoro, kwa kweli hii inatumiza sana kama wananchi wa Mkoa wa Tabora. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kuhusu Kiwanda cha Nyuzi. Pale Tabora kuna Kiwanda cha Nyuzi cha muda mrefu, lakini kiwanda hiki kimekufa muda mrefu. Naiomba Serikali yangu, kama kweli inaheshimu wakulima wa pamba, wahakikishe kiwanda hiki kinafufuliwa na kinaanza kufanya kazi. Naomba sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, nini hatima ya kiwanda hiki? Kiwanda hiki kimeanza kupigiwa kelele na Wabunge wengi waliotutangulia ambao leo hii hawamo humu; nasi pia toka mwaka 2011 mpaka leo tunakipigia kelele, lakini hatupati hatima yake ni nini, hakitengenezwi, hakifunguliwi!

Mheshimiwa Naibu Spika, leo namwomba Mheshimiwa Waziri wakati ana-*windup* atuambie ana mkakati gani kuhusu Kiwanda cha Nyuzi cha Mkoa wa Tabora? Nasi pia vijana wetu wanahitaji ajira, hawana ajira, hali ya uchumi inakuwa mbaya kila siku, mpaka kuna baadhi ya watu wanatucheka kwamba Tabora hakuna maendeleo. Ni Serikali haijatuletea hayo maendeleo, tunalima tumbaku lakini hatuna viwanda, lakini pia tuna Kiwanda cha Nyuzi ambacho kimefungwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba tena Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ageuze sasa zao la asali liwe zao la biashara. Watanzania wengi humu ndani ya nchi yetu wameshajua nini maana ya kutumia asali na naamini watu wengi sasa hivi wanatumia asali. Pia zao hili lina soko kubwa nje ya nchi yetu. Namwomba sasa Mheshimiwa Waziri aliboreshe zao hili, awe na mkakati maalum wa kuboresha zao la asali ili liwe zao la kibiashara; lakini pia tupate viwanda vya ku-*process* asali ili vijana wetu wafaidike na zao la asali na pia wapate ajira ili na sisi kama watu wa Tabora tupunguze huo umaskini. Naomba sana Mheshimiwa Waziri akija ku-*windup* atuambie pia mkakati wake alionao katika kiwanda cha ku-*process* asali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea EPZ ndani ya Mkoa wa Tabora. Sisi kama watu wa Tabora tumeipa Serikali heka 200 ili kujenga viwanda vinavyotokana na mazao ya kilimo, ikiwemo tumbaku, asali pamoja na viwanda vya ufugaji. Naiomba sana Serikali, ile ardhi tumewapa bila kulipa fidia, bila gharama yoyote ile ili waweze kutusaidia kutafuta wawekezaji tupate viwanda. Nia yetu ni kupata viwanda ili tuweze kupata ajira za vijana wetu na hatimaye na sisi tuweze kuondoa umaskini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipiga kelele sana Wabunge wa Mkoa wa Tabora, kwa kweli Mkoa ule ni wa siku nyingi, lakini cha kushangaza na cha kutia masikitiko makubwa, Mkoa ule hauna kiwanda hata kimoja. Malighafi zinazopatikana, Tabora zinapelekwa mikoa mingine kuwekewa viwanda na watu wa kule ndio wanaofaidika. Kitu hiki kinatumiza sana sisi Wabunge wa Mkoa wa Tabora na kuonekana kama vile hatuji kuwasemea na kuwasaidia waliotuweka madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kusema kwamba tumtie moyo Mheshimiwa Waziri, tuitie moyo Serikali yetu ya Awamu ya Tano, iendeleo na mkakati wake wa kuhakikisha Awamu ya Tano inakuwa Awamu ya Viwanda, hatimaye tutoke kwenye uchumi wa chini na kuingia kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wenzetu wanaosema kwamba huu Mpango hauna maana yoyote, hatuko kwenye dhana ya viwanda...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Washindwe na walegee. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili la bajeti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Napenda nichukue fursa hii pia kumpa pongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hoja yake, lakini pia na kwa utendaji mzuri wa kazi katika Wizara yake. Nina imani kwamba chini ya uongozi wake, nchi hii itaingia kwenye uchumi wa kati, uchumi ambao utaongozwa na ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga nchi ya uchumi wa kati, ikiasisiwa na

ujenzi wa viwanda, ni mwelekeo mzuri sana, kwa sababu huu ndiyo ukombozi. Vijana wetu wengi wa kiume na wa kike wanapata madhila makubwa sana kwa kukosa fursa za ajira na fursa za kujijiri zinazotokana na nyenzo zile ambazo zipo kama kuna fursa za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na viwanda vingi, maana yake ajira zitakuwa nyingi na fursa za kujijiri pia zitakuwa nyingi zaidi. Kwa hiyo, hii itatupa heshima kubwa sana kwa vijana wetu wanaochipukia hivi sasa, lakini pia kulijengea Taifa uwezo wa mapato makubwa zaidi na kuwaondolea wananchi wetu umaskini. Tunaunga mkono jambo hili, tunawatakia heri Serikali yetu ya Awamu ya Tano waweze kufanikiwa katika jambo hili kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na nategemea kwamba tutapata mafanikio katika ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika mradi wa EPZ. Mradi huu ni wa Kitaifa na kule kwenye Jimbo langu, Bagamoyo tunao mradi huu, ni mradi ambao tunautarajia kwamba kwa sababu ya eneo kubwa ambalo limetwaliwa kwa ajili ya kujenga viwanda vya uchakataji wa bidhaa kwa ajili ya kusafirisha nje; tutapata ajira nyingi na nchi yetu itapata mafanikio kuelekea kwenye uchumi wa kati. Ni jambo kubwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linawatesa sana wananchi wa Bagamoyo ni kwamba tangu mwaka 2008 walifanya tathmini ya ardhi hii ili iwe *free* kuweza kutumika kwa ajili ya kujenga viwanda. Mpaka hii leo, miaka tisa baadaye, bado wananchi wale wanadai fidia ya ardhi ambayo wameitoa na mali zao. Hili ni jambo zito sana, kwa sababu hakuna kiwanda ambacho kitaweza kujengwa kama wananchi hawa hawajapewa fidia yao na ardhi ile iwe *free* ili mwekezaji anapokuja, apate ardhi ambayo haina tatizo lolote; ni ardhi ambayo iko tayari kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka tisa hii ya ukosefu wa fidia, imewafanya wananchi wawe na hasira; wana hasira na Mbunge wao, wana hasira na Madiwani na wana hasira na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Wananchi hawa hamna namna ambayo naweza sasa hivi kama Mbunge kusimama na kuwaambia kwamba tuendeleo kusubiri zaidi. Miaka tisa hii ni miaka ambayo tumepotea fursa nyingi ambazo tungeweza kuzipata wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008 fidia ilikuwa imetathminiwa kwamba ni shilingi bilioni 60; hivi leo ninaposimama hapa miaka tisa baadaye bado wananchi wanadai shilingi bilioni 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine Mheshimiwa Waziri amesema ni zaidi ya hapo, lakini siyo zaidi ya hapo kwasababu ameichanganya na fidia ya Bandari. Tunasema hii ni fidia ya EPZ, shilingi bilioni 60 mwaka 2008, bado wanadai bilioni 47 hivi sasa, kwa maana ulipaji umekuwa mdogo sana. Hatuwezi kupata uwekezaji wa viwanda kabla hii ardhi haijawa *free* na haiwezi ikawa *free* kabla hatujawalipa fidia hawa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012/2013, Bunge hili Tukufu lilipitisha bajeti ya shilingi bilioni 52 kwa ajili ya kulipa fidia na zikawa *ring fenced* lakini hazikutoka. Mwaka wa fedha wa 2013/2014, tukapitisha shilingi bilioni tisa zikatoka shilingi bilioni sita; mwaka 2014/2015, sifuri; mwaka 2015/2016 sifuri; hii bajeti sasa hivi 2016/2017 nayo pia sifuri. Sasa Mheshimiwa Waziri anapojipanga kujenga viwanda na eneo liko pale, hajaweza kulitwaa lile eneo kwa sababu tu hajalipa fidia, tutafikaje kwenye viwanda kama hatutaweza kuwalipa wananchi hawa? Wananchi hawa wanapokuwa na hasira, mimi kama Mbunge nafahamu ni kwa namna gani wana hasira kwa sababu hawajalipwa fidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri namtegemea sana, namwamini kwa juhudi zake, nina imani kwamba hili jambo atalitafutia dawa hivi karibuni. Aliniambia wakati fulani atakopa, lakini sasa hivi siyo wakati wa kusema tutakopa, kwa sababu jambo la viwanda kwetu na kwa Awamu ya Tano ni *priority*. Ni jambo kubwa kwamba tutakopa, haiwezi ikawa sasa hivi ni mpango. Sasa hivi kama tulivyotenga bajeti, mwaka 2012/2013 na 2013/2014 bajeti ndogo, ndiyo hivyo ambavyo Serikali inabidi ioneshe msukumo mkubwa sana ili tuweze kuvuka hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda kusema kwamba, tathmini imefanywa mwaka 2008, huu ni mwaka 2016, miaka tisa baadaye. Thamani ya ardhi mwaka 2008 sio thamani ya ardhi mwaka 2016. Sasa hivi ardhi ya ekari moja ya shilingi milioni tatu na nusu Bagamoyo huwezi kuipata mahali. Mwananchi ananiuliza mimi, Mheshimiwa Mbunge hivi milioni tatu naenda kununua kiwanja mahali gani tena kwa ekari moja? Namwomba Mheshimiwa Waziri waangalie upya uthamini mpya kama vile Sheria ya Ardhi inavyoelekeza. Uthamini ufanywe upya, muda umepita sana ili kuhakikisha kwamba wananchi hawa tunawatendea haki na sisi tunapata mambo yaliyokuwa mazuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu wa viwanda lazima uunganishwe na ujenzi wa bandari na uunganishwe pia na ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, kwa sababu viwanda bila bandari na miundombinu ya usafirishaji kama barabara, reli na kadhalika itakuwa ni jambo ambalo haliwezi likawa na mafanikio.

Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ya Awamu ya Tano ijihakikishie kwamba barabara zile za ahadi, Bagamoyo - Mlandizi mpaka Vikumbulu kwa ajili ya kuunganisha viwanda na barabara ya Morogoro ijengwe na kumalizika; lakini barabara pia ya Saadani - Pangani mpaka Tanga nayo ijengwe ikamilishwe ili kuweza kuunganisha viwanda na kaskazini mwa Tanzania na hatimaye nchi jirani ya Kenya; na zaidi ya hapo, pia ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge* na kuunganisha reli ya kati na viwanda hivi Bagamoyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia mradi wa Kiwanda cha Sukari Bagamoyo ama wengine tunakiita Bagamoyo *Eco-energy*. Kiwanda cha Sukari Bagamoyo kimeasisiwa muda mrefu. Mimi nimepata Ubunge mwaka 2006 tayari tulikuwa tunaongelea Kiwanda cha Sukari Bagamoyo. Kina uwezo mkubwa! Kina uwezo wa kuzalisha tani 150,000 kwa mwaka, lakini pia kina uwezo wa kuzalisha umeme *Megawatt* 100,000 kwa mwaka pia *ethanol* kwa *meter cubes* 12,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sukari ni jambo la kimkakati, shida kubwa tunayoipata sasa hivi ni kwamba ni aibu kwa nchi, ni pale ambapo wananchi wana uhaba wa chakula. Sukari tunaitumia kwenye vyakula vyetu, tangu chai asubuhi na katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kama soda na vitu vingine, ukitaja ni vingi tu. Ndiyo maana sasa hivi tupo kwenye mtikisiko na Mheshimiwa Rais ana kazi kubwa sana ya kuhangaika na watu wanaohodhi sukari katika magodauni.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri amwondolee adha hii Mheshimiwa Rais ya kugombana na watu wanaotaka kuhodhi sukari kwenye magodauni yao. Asimamie kiwanda hiki ambacho kina uwezo wa kupunguza uhaba wa sukari kwa asilimia 50. Tunataka sukari tani 600,000, tuna-*produce* sasa hivi tani 300,000; tuna tofauti ya tani 300,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda hiki peke yake kina uwezo wa tani 150,000. Kwa nini Mheshimiwa Rais ahangaike? Ana mambo makubwa zaidi kuliko kuzungumzia sukari sasa hivi, kugombana na hawa watu. Tengeneza sukari ili waendeleo kuhodhi, viwanda viweze kuwapa tu sukari nyingi na zitoe ajira nyingi. Hana haja ya kuhangaika, maana ana mambo makubwa zaidi ya muhimu ya kuongelea zaidi ya kuongelea mambo ya sukari. Huu siyo wakati wa kuzungumzia sukari tena! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mradi huu tumeanza kuuzungumzia mwaka 2006 huu ni mwaka wa 11. Miaka 11 ya kusubiri ili Serikali yetu iweze ku-*support* ujenzi wa kiwanda hiki kikubwa cha sukari; ardhi tumetoa jumla ya hekta 7,800 kwa maana ni ekari 19,500. Ni ardhi kubwa, nzuri inapakana na mto Wami. Ni ardhi ambayo inafaa kwa umwagiliaji. Serikali lazima iite huu ni mradi

wa mkakati. Kuna miradi mingine ya mkakati lakini huwezi kufananisha na mradi huu wa mkakati. Huu unahusu chakula cha binadamu, chakula cha Mtanzania, kumwondoa katika aibu ya uhaba wa chakula ndani ya nchi yake; anaangaliwaje Mtanzania tunavyoambiwa kwamba hatuna sukari katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unahitaji kila *support* ili fursa hizi za miaka tisa iliyopita tangu shamba dogo la mfano lilipoasisiwa mwaka 2008 na kiwanda kutegemewa kuanza kujengwa miaka michache baadaye, miaka tisa sasa tumepoteza fursa chungu nzima za uwekezaji. Waliokuwa wanataka kuwekeza kwenye sukari, kwa sababu ya kutokupata *support* ya kutosha kwenye mradi huu, hawakuweza kujenga viwanda, labda wamekwenda kujenga kiwanda cha sukari sehemu nyingine, sisi tunaendelea kupata tabu ya sukari hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumekosa fursa nyingi sana za ajira; kiwanda hiki kimepangwa kitoe ajira *direct* 2,300. Ajira za *out growers* ama wakulima wa kimkataba kati ya 1,500 hadi 2,000, lakini ajira zinazoendana na ujenzi wa kuwepo kwa kiwanda hiki ni ajira 16,000. Maana yake tumepoteza fursa ya ajira 20,000 kwa vijana wetu wa kike na wa kiume kwa kipindi chote hiki cha miaka tisa ambayo hatujaipa msukumo wa kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia kwenye hotuba yake ukurasa wa 18, mradi wa mkakati hamna! Nimeisoma tangu mwanzo mpaka mwisho, nimeona Liganga, Mchuchuma na kadhalika. Tunahitaji umeme, lakini kwanza tumboni kabla hata hatujafika huko; sikatai lakini huu ndiyo mradi ambao ningeuona ni mradi wa mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia pia kwenye kitabu cha maendeleo cha bajeti, hakuna kitu chochote kwa ajili ya mradi huu. Namwomba Mheshimiwa Waziri akumbuke kwamba, vijana wanazihitaji hizi ajira 20,000 ambazo zinatolewa kama fursa ya kuwepo kiwanda hiki. Watanzania wanataka sukari, Watanzania wanataka umeme...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kawambwa muda wako umekwisha.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mwaifunga atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, halafu Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli ajiandae.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hii. Nitakayoyazungumza ndiyo ambayo tumekutana nayo na ndiyo yaliyopo. Mheshimiwa Waziri hotuba yake ni nzuri sana ukiisoma, lakini uhalisia uliomo humu haumo, kwa sababu ukienda kule uraiani, kule kwenye viwanda kuangalia uhalisia, haupo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeingia ubia na viwanda tofauti tofauti, lakini Serikali haiangalii hivi viwanda vinafanyaje majukumu yake na mwisho wa siku tunajikuta kila siku tunapoteza mapato, kila siku tutapoteza wawekezaji kwa kudhani kwamba tunaweza kufanya miujiza hii nchi iendelee kuwa ya viwanda, hakuna! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya nchi hii inatakiwa kwanza ilinde viwanda tulivyonavyo. Kabla hatujasema tunakwenda kutengeneza viwanda vingine ama kuanzisha viwanda vingine, vilindwe hivi vichache vilivyopo ambavyo vinazalisha kwa chini ya asilimia 50. Viwanda vinazalisha chini ya asilimia 50, leo tunafikiria tutengeneze viwanda vingine eti Tanzania iende kuwa nchi ya viwanda, wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vipo, lakini wafanyabiashara wenye viwanda wana matatizo mengi kweli kweli! Naishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri, narudia tena, waendeele kukaa na wafanyabiashara wenye viwanda, wasikilizeni hoja zao, matatizo yao ili hawa basi, waliopo hapa leo waweze kuwa mabalozi wa wawekezaji wengine ambao tunawategemea waje hapa. Hatuwezi kutegemea kuleta wawekezaji wengine, wakati hawa waliopo wana matatizo lukuki ambayo yanawakabili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kwanza tutoe haya tuliyonayo hapa, tuyarekebishe, hawa wafanyabiashara leo watakuwa mabalozi wa kwenda kututangaza vizuri nchi ya Tanzania ili iweze kuwa nchi ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, tumekwenda kama Kamati kwenye Kiwanda cha TANALEC, tumekuta *transformer* zaidi ya 2000 zinatengenezwa zinakwenda Kenya. Tanzania tunaagiza *transformer* kutoka India, *transformer* 200, Mkoa wa Katavi zimelipuka baada ya kuwashwa tu! Halafu TANESCO wanawaomba TANALEC wawatengenezee zile *transformer* ambapo TANALEC wamegoma! Nasi tukawaambia, haiwezekani, wapeleke huko huko walikonunua *transformer* hizo zitengenezwe ndiyo wazirudishe hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala wanasema sijui Sheria ya Manunuzi; sidhani kama Sheria ni Msahafu! Sheria zinabadilika! Hebu Waheshimiwa Wabunge tusaaidiane basi kuangalia hizi sheria wapi ni mbaya, wapi zinatatiza ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara zao wakiwa huru, wasifungwe na hizi sheria ambazo zinawatatiza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwanda cha Nondo Tanzania, wanazalisha nondo nyingi kweli kweli, lakini hawana masoko! Miradi ya Serikali inakuja mikubwa mikubwa, nondo zinaagizwa kutoka nje! Tunafanya nini? Tunasema nchi ya viwanda, viwanda gani kama hivi vilivyopo havifanyiwi kazi! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku kwenye viwanda watu wanaondoa wafanyakazi kwa sababu hakuna biashara! Hawa vijana waende wapi? Matokeo yake ndiyo tunakabwa kila kukicha kwa sababu vijana hawana ajira na ajira nyingi tunategemea zitoke kwenye viwanda, leo viwanda vinafungwa, hawa vijana waende wapi? Akinamama waende wapi? Hizi panya-road zitakwisha lini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kama kweli Serikali ina dhamira ya dhati ya kutaka nchi hii iwe ni nchi ya viwanda, iende kwenye huo mfumo ambao mnasema ni wa kati, yaani watu wetu wawe na maisha ya kawaida, basi ni lazima tuboreshe viwanda nyetu vya ndani ili viwanda hivi vikifanya vizuri wawekezaji watakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nikiiangalia bajeti hii ya Serikali, *TIC (Tanzania Investment Center)* hawana bajeti zaidi ya mshahara. Wanafanyaje majukumu yao? Wataletaje hao wawekezaji? *TBS*, mamlaka nzito, kubwa inafanya kazi kubwa; ukiangalia, hawana fedha zaidi ya mshahara. Tunafanyaje mambo haya ndugu zangu? Tutafika kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunazungumza suala la *EPZ*; kwanza hii *EPZ* nafikiri sisi Wabunge hapa ambao tunaelewa ndiyo tunafahamu *EPZ* ni nini. Huko kwetu watu hawaelewi chochote. Unapowaambia habari ya *EPZ*, hawakuelewi! Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya uraia, angalau hata tunapokwenda kuomba maeneo, Watanzania wawe wanajua kitu gani ambacho kinaombewa haya maeneo ili wasiwe wagumu kutoa maeneo yao yaweze kuwekezwa hivi viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, nenda *EPZ* leo, hakuna chochote kinachonunuliwa kutoka Tanzania, hakuna! Nimeuliza na nikamwuliza hata Mtendaji Mkuu pale, kwa nini hakuna chochote kinachonunuliwa hapa? Tukaambiwa tunazalisha chini ya kiwango.

MBUNGE FULANI: Aaah!

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, hadi vifungo ambavyo wanatengenezea mashati, suruali, wanasema tunaagiza nje! Nikauliza, tunanufaika na nini hapa kama Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, wako vijana na wanawake wamewekwa pale, ukiuliza mshahara wao, utalia! Je, hawa watu baada ya kuondoka, wanatuachia nini? Kuna teknolojia yoyote Watanzania ambayo tutabaki nayo ili kesho na kesho kutwa watoto wetu waweze kuikuta hiyo teknolojia, waweze kufaidika nayo? Hakuna! Wamejaa wenyewe pale, wako wenyewe tu. Mheshimiwa Waziri unajua, tunaomba sana Serikali ihakikishe inawasaidia Watanzania kuelewa na kufahamu kabla hatujafanya maamuzi. Maamuzi tunayafanya juu, lakini huko chini Watanzania hawana taarifa nayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna deni kubwa! Deni la shilingi bilioni 60 limezaa shilingi bilioni 190! Mheshimiwa Waziri ukija hapa kumaliza, tuambie hizi shilingi bilioni 190.9 imekuwaje mpaka zimefikia hapa kwa mwaka mmoja, eti ni fidia! Watazitoa wapi ikiwa bajeti yenyewe ni shilingi bilioni 81? Ndugu zangu tunadanganyana hapa! Hatuna kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri, watu wa Tabora tunahitaji viwanda, tuwekee hata hicho kimoja tu kwanza, halafu mambo mengine yatafuata wakati ukiwa unaendelea na mikakati yako mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niiombe Serikali sasa, iangalie kwa umakini bajeti ya Wizara hii. Hii Wizara ni mtambuka; ni Wizara ambayo inaingiza vitu vingi sana ambavyo vipo. Hebu basi Serikali ibadilike na ione uwezekano wa kuiangalia bajeti ya Wizara hii ili kweli tuweze kufika kwenye nchi ya viwanda kama tunavyofikiria. Kama tutaendelea kusuasua, mipango ikawa mingi, mikakati mingi, fedha hakuna, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba basi sasa ifike mahali tuamue, kama tunataka kutengeneza viwanda, tuamue tunaanza na nini? Haya mambo leo kuna hiki, kuna hiki, kuna hiki kwa bajeti ya shilingi bilioni 41 ambayo ni ya maendeleo, tunawadanganya Watanzania, hatutafika. Tunasema leo, tunaishauri Serikali leo, lakini mwisho wa siku haya maneno yataendelea kuwepo kwa sababu hakuna kinachokwenda kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, yangu yalikuwa hayo. Ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa kwa kututunzia muda. Mheshimiwa Riziki Said Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kupata afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nashukuru kwa hoja iliyowekwa mezani, ni nzuri, lakini namwonea huruma sana shangazi yangu Mheshimiwa Mwijage kuwa atapambana na kazi kubwa sana katika suala la viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *na-declare Interest*, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Uwekezaji. Nimeangalia Uwekezaji na Ubinafisishaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi zake kama ni mwiba unaoitafuna nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeingia katika uwekezaji tukikurupuka, mikataba mibovu, usimamizi mbovu, *corruption* ndiyo imesimama. Leo tuna Taasisi zaidi ya 200 katika uwekezaji, lakini mpaka sasa hivi ni mashirika machache sana ambayo yanaweza yakatoa faida katika nchi hii. Taasisi hizo naweza nikazitaja ambazo angalau zimeonesha zinaweza zikatupeleka mbele katika dira ya maendeleo ya uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni TANAPA. Inapeleka ruzuku katika pato la Taifa; Ngorogoro inatoa Ruzuku katika pato la Taifa; *National Housing Corporation* inatoa ruzuku katika pato la Taifa na NSSF. Sasa tujiulize, Taasisi nyingine zinategemea ruzuku kutoka Serikalini, kulikuwa na haja gani ya kubinafsisha wakati bado wanakula fedha ya Serikali na zinaingia katika mashirika yao? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuangalia Taasisi nyingi tulizokuwa nazo, hazina Bodi. Bodi ni dira, sasa kama Shirika halina Bodi unategemea nani ataendesha usukani wa Shirika lile? Nani atasimamia matumizi katika shirika lile? Kwa nini tumekaa na mashirika kwa muda mrefu yakiwa hayana Bodi? Nataka nipate majibu katika Taasisi zote kwa nini hazina Bodi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia Taasisi nyingi hazina *Business Plan*, uliingiaje katika mkataba wa ubinafisishaji na uwekezaji hakuna *Business Plan*? Matokeo yake unakuta mashirika ambayo hayahusiki na ujenzi wa majumba, sasa hivi wanakimbilia kujenga majengo. Sasa *National Housing* ipo, *NSSF* ipo, kwa nini unajenga nyumba sasa hivi? Ni kutokuwa na mwelekeo wa *Business Plan* yake; sivyo inavyokwenda! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingia katika suala la Mashirika mbalimbali ambayo tumeangalia. Katika kuyaangalia kwa kweli unapata huruma! Mashirika mengi yana uwezo mdogo wa Watendaji, inaonekana hawana

capacity ya kulingoza Shirika. Kwa nini umempa taasisi mtu ambaye hana uwezo? Matokeo yake, yale mashirika haya-perform. Kama hamjafanya kazi ya kuangalia nani ana-perform, nani ha-perform ina maana tutaendelea kuwa na business as usual. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilizungumzie Shirika la TANESCO. Shirika la TANESCO wameingia wawekezaji wakubwa, mmojawapo IPTL, Songas, Symbion, wako pale kulila lile shirika. Tufikie mahali tujiulize, nani aliweka ule mkataba mbovu mpaka kufikia hili shirika lisiweze ku-perform? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa kila mwaka; mkataba wa Songas unasikitisha, anasema, mimi nimechukua mkopo, hivyo sitarudisha mkopo ule niliochukuwa Tanzania mpaka kwanza TANESCO anilipe. Bei anayotoa na ya kununulia ni vitu viwili tofauti. Anatoa Dola 13, huyu analipa Dola 21; jamani ni mkataba gani huu? Mnampa mkataba huu mpaka 2020/2025 toka alipoanzia, hana ruhusa ya kuguswa. Jamani, Watanzania tunajipenda hatujipendi! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna huruma na nchi yetu au hatuna huruma na nchi yetu?

WABUNGE FULANI: Hatunaaa!

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Tumeifilisi nchi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika Bodi ya Sukari. Bodi ya Sukari imekaa pale tu kama bodi lakini haina meno, kazi inafanywa na Wizara. Wizara ndiyo wanatoa vibali vibovu vyote vya sukari. Sukari inaandikwa inakwenda nje ya nchi, kumbe inauzwa Tanzania hapa hapa, sukari inaletwa kama malighafi, siyo malighafi, iko katika viwanda. Wanachofanya, inatembea karatasi, sukari ikishateremshwa karatasi inapita katika vituo vyote kama Lorry hii imepita na sukari mpaka inafika Tunduma, lakini sukari iko bado mjini hapa! Kwa faida ya nani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize na sisi Watendaji ambao Watanzania wote wamekosa uzalendo, ndiyo maana wenzetu Kenya wanatupita au Rwanda wanatupita; uzalendo wa Watendaji ni mdogo sana! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika upande wa viwanda. Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani tulikuwa na Viwanda vya Korosho 13, vile viwanda vyote vimefungwa. Matokeo yake, kama Mkoa wa Lindi, hatuna ajira kwa viwanda hivyo. Hata kiwanda kimoja Lindi hamna! Unategemea wale Wamachinga watakwenda wapi? Wakija Dar es Salaam wanafukuzwa! Lindi viwanda mmevifunga, wanakwenda wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ile korosho sasa, ule ndiyo mwiba, amepewa sura pana ananunua korosho vijijini sasa hivi! Wanapewa kununua ufuta vijijini! Hivi jamani panya umemwingiza kwenye ghala, unategemea nini? Ufuta sasa hivi hauna bei maalum, ufuta umelimwa vya kutosha, lakini sasa hivi unaambiwa sh. 1,300/= ukienda hapa sh. 2,000/=. Matokeo yake hata soko la ufuta hakuna! Tunategemea kuletewa mafuta mabovu kutoka nje! Hivi jamani mnazona cancer zilizojaa Tanzania? Magonjwa ya figo mnayaona yalivyojaa Tanzania? Tunakula mafuta machafu, ufuta wetu tunaupeleka nje ya nchi. Tujiulize, tuna vision? Tuna mission? Are we responsible? We are not responsible. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefikia mahali tuko *business as usual*. Naomba tuambiwe, ule ufuta ambao umezalishwa, maana yake sasa hivi Tanzania ni nchi ya pili kuuza ufuta duniani, lakini tunaagiza mafuta kutoka nje; kwa sababu gani tunakula mafuta mabovu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mnatuendeleza mpaka leo tunakula mafuta machafu wakati tuna ufuta, karanga, pamba na alizeti; ni kwa sababu gani mnatufanyia mambo kama haya? Mko serious? Hamko serious, mmekaa kuangalia corruption, nitapata bei kiasi gani, nitapata fedha kiasi gani, basi! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, masikitiko yangu makubwa, naangalia vijana ambao wanayumba yumba. Hizi korosho zinapelekwa nje kama *raw material*, tunapeleka ajira nje! Wanafanya makusudi kuhakikisha Mtanzania hapati ajira katika nchi hii. Wakiwa na viwanda vyao, Mtanzania hana nafasi! Ufuta wetu ambao ni bora, korosho zetu zilizokuwa bora, pamba tunapeleka nje ili kutoa ajira nje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka majibu, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kumalizia aniambie, ajira ya vijana kwa viwanda mlivyofunga itapatikana lini? Tujiwekee *time frame* kwa vile viwanda vilivyofungwa vya Mtwara, Masasi, Nachingwea, Lindi na Kibaha vitafunguliwa lini ili tuone kweli makucha yapo? Kama havijafunguliwa, mwakani nitauliza tena swali hili hili! Vijana wanazurura, wanahangaika!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda Nachingwea, tulikuwa katika msafara wa viongozi, maghala yale ndani mna mbao mpaka juu. Jiulize, yeye amepewa kiwanda kwa ajili ya korosho, zile mbao zinafanya kazi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vya Urafiki; tumekwenda Urafiki vile viwanda ndani kumejaa ma-pampers na vitu vingine. Je, tuna vision na biashara zetu? *Business Plan* zetu zinasema nini? Yule wa Kiwanda cha Urafiki

alikuwa atengeneze nguo, amejaza na viwanda; amechukuliwa hatua gani? Tunataka tujue, hatua gani amechukuliwa? Kama hatujajua amechukuliwa hatua gani, itakuwa ni watu ambao wanaachwa. Anakamatwa na pembe, mnaambiwa, bwana, hajui Kiswahili, ndiyo maana yake tunavyofanya sasa hivi! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu havina thamani, vimekuwa maghala, watu wanaweka vitu vingine; hivyo kilichowekwa pale siyo. Tunataka tujue *Action Plan*, *Business Plan* zetu zinakwendaje? Tupo kwa kujenga au tupo kuwaachia wageni na uwekezaji wao uwe wa kutubomoa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuruni sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Leonidas Gama na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kidogo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kupongeza Baraza zima la Mawaziri na Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa ni Tanzania ya Viwanda. Nawapongeza sana! Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kuhakikisha kwamba tunafikia azma ya kuwa na viwanda au kufikia uchumi wa viwanda katika nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba hatuwezi kufikia huo uchumi wa viwanda bila kufikiria Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo ndiyo sekta mama ambayo itatuwezesha sisi Watanzania kuingia kwenye uchumi wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua sote kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima, sasa huwezi kuiacha sekta hiyo ya kilimo ukaingia kuwekeza viwanda vya aina nyingine na ukataka kufika kwenye uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, ni lazima tuitazame Sekta ya Kilimo, tufikirie kuwekeza kwenye viwanda vya kilimo. Historia inatuambia kabisa kwamba hata nchi zilizoendelea, tunafahamu wote nchi za Uingereza, Ujerumani na Marekani walianza kwanza na viwanda vya Sekta ya Kilimo; *Agro Processing Industries* ambavyo vilikuwa vinaongeza *value* ya mazao au thamani ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasi Watanzania tukitaka twende huko kwenye uchumi wa viwanda ni lazima tuangalie wakulima wetu waweze kuwa na viwanda ambavyo vitaongeze thamani ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishakamilisha kuwa na viwanda vya uongezaji wa thamani ndipo hapo sasa hawa wakulima watahitaji zana mbalimbali, watahitaji magari ya kusafirisha, basi itafanya sasa kuwe na *demand* ya vitu vingine ambavyo hivyo sasa vitahitaji viwanda vya *mechanical industries* na baadaye tutaingia pengine kwenye *Chemical Industries*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nami nasema kwamba, ni muhimu Waziri wetu wa Viwanda aanze sasa kuangalia maeneo hasa ya uzalishaji ili kuwavutia Wawekezaji ili waweze kuwekeza viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuongeza thamani ya mazao, kwanza kabisa itatusaidia kutoa ajira kwa vijana wetu. Tunatambua vijana wengi wako huko vijijini na sasa hivi wanakimbilia mijini wakifikiria kutafuta kazi kwenye Maofisi au kwenye viwanda mbalimbali na wakifika huko wanakosa hizo ajira. Sasa tuanze kufikiria kuanzisha viwanda hivi vijijini ili vijana wetu wengi waweze kuajiriwa kwenye viwanda hivyo, wabaki kule na kufanya kazi ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata changamoto moja kubwa; mimi natokea Jimbo la Lupembe ambapo tunazalisha chai, kahawa, tunazalisha mazao ya matunda, kama mananasi, ndizi, machungwa na matunda mengine mengi tu, lakini kule Lupembe mpaka sasa hivi wale wananchi hawawezi kuuza mazao yao vizuri kwa sababu ya tatizo moja na hata Wawekezaji hawapendi kuwekeza maeneo yale kwa sababu ya tatizo la miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tunapofikiria uchumi wa kati, tunapofikiria uanzishwaji wa viwanda kama nilivyosema lazima tuhakikishe kwamba kwenye maeneo ya uzalishaji ambapo huko ndiko tunategemea kuanzisha viwanda, ni lazima miundombinu ya barabara, tuhakikishe kwamba tunakuwa na barabara nzuri ambazo zinapitika muda wote ili watakaowekeza waweze kusafirisha hizo bidhaa kirahisi zaidi na hatimaye kufikia soko au kufikia maeneo ambayo wanaweza wakaongeza thamani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lazima tufikirie kuwekeza kwenye umeme. Kwa hiyo, unaona hapo Wizara nyingi sana zinahusika. Ni lazima tuwe na umeme wa kutosha kwenye maeneo haya ili tuweze kuwavutia wawekezaji waweze kuwekeza kwenye maeneo haya ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni lazima tuwe na maji. Tukiwa na maji ya kutosha *automatically* tutavutia wawekezaji, kwa sababu naamini kwamba, siyo Serikali itakayokwenda kujenga viwanda, wanaojenga viwanda ni wawekezaji wa ndani na nje. Sasa hawa lazima kuwe kuna huduma hizi muhimu. Huduma za maji, umeme, lakini pia huduma za afya ni lazima ziwe za kutosha ili wawekezaji waweze kuwekeza kwenye maeneo ya vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa kwenye maeneo mengi ya uzalishaji, watu hawapendi kwenda kuwekeza kwa sababu hizi huduma muhimu hazipo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, tunapotaka kuwekeza, ni lazima tufikirie mambo hayo muhimu na hasa tufikirie kuwekeza kwenye kilimo ambacho kwanza viwanda vyenyewe ni vya bei ndogo, ni rahisi kuwekeza, lakini pia vinaweza vikaajiri Watanzania wengi na katika sera yetu tumesema kwamba lazima tuanzishe viwanda, tuanzishe shughuli ambazo zitawaajiri vijana wengi kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ili tuweze kupata uwekezaji mzuri na hatimaye uwekezaji ukawa na tija, ni lazima tufikirie maeneo ya kuwekeza, hasa maeneo yale ambayo kuna uzalishaji, maana tunaweza tukawekeza kama ilivyokuwa kwenye viwanda vile vya tumbaku, badala ya kuwekeza Songea na Tabora ambako tumbaku inazalishwa, vikawekezwa Morogoro. Hatimaye utakuta wakulima wanakata tamaa kwa sababu hawawezi kusafirisha mazao yao kuyaleta Morogoro. Kumbe viwanda hivi vingekuwa vimewekezwa sehemu zile ambazo wanazalisha, basi wakulima wangeweza kupata faida kubwa na wangehamasika kuzalisha hilo zao na hatimaye nchi kupata faida kubwa au uchumi wetu kuweza kukua kwa kuwa viwanda vimewekwa kwenye maeneo ya uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunapoweka viwanda kwenye maeneo ya uzalishaji tunawasaidia wakulima wetu kuweza kupata faida katika kilimo. Ilivyo sasa hivi wanaofaidika sio wakulima, wanaofaidika ni wale *middlemen*, wale watu wanaonunua mazao toka kwa wakulima na kwenda kuwauzia watu watu wenye viwanda.

Kwa hiyo, haiwasaidii wakulima kama tutawekeza viwanda vyetu mbali na kule wanakozalisha. Kwa hiyo, tuweke jirani na eneo la uzalishaji ili wakulima wetu waweze kuuza mazao yao na kupata faida na hatimaye Taifa lipate faida kupitia viwanda na ajira hizi ambazo tumewekeza kupitia viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nijaribu kuongelea suala la kodi. Mara nyingi kumekuwa na kodi nyingi sana kwenye mazao, hasa mazao ya biashara. Kwenye zao la chai, kahawa, tumbaku na pamba, kuna kodi nyingi au kuna utitiri wa kodi. Utakuta kodi za mazao haya hufika mpaka 20 nyingine mpaka 25 au 27. Sasa mwisho wa siku anayekuja kulipa hizi kodi zote ni mkulima. Kwa hiyo,

utakuta kupitia hizi kodi, tunamnyonya huyu mkulima ambaye kwanza anapata shida sana kuzalisha hili zao na soko lake halina uhakika; sehemu ya kuuzia kwenye kiwanda, hakina uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku anauza zao lake; anauza chai yake, kahawa, pamba au tumbaku yake kwa bei ya chini kwa sababu ya kuwa na kodi nyingi. Kwa hiyo, tunapofikiria viwanda au uzalishaji ni lazima tufikirie pia na hizi kodi, tujaribu kuzipunguza ili angalau mkulima aweze kupata faida. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu wawekezaji wazawa. Mara nyingi tumekuwa tukiwavutia wawekezaji wa nje tunawasahau wazawa. Tunasahau kuwahamasisha wananchi wale wanaotaka kujiunga kwenye vikundi vidogo vidogo na kuanzisha viwanda au kuna maeneo mengine tayari kuna wakulima ambao wameonesha nia ya kuwekeza kwenye kilimo na kwenye viwanda, ni vizuri Serikali tuwe na utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunawawezesha kwa kuwapa mikopo au kwa kuwasaidia kuweza kupata mikopo rahisi na kuweza kuwekeza kwenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu kuna mkulima mmoja anataka kuwekeza kwenye kiwanda cha chai, kwenye *processing industries*, lakini anashindwa kupata utaratibu gani mzuri ili aweze kupata mkopo na hatimaye aweze kufungua kiwanda cha chai. Kwa hiyo, naomba tunapofikiria uwekezaji, tuwafikirie sana Watanzania wenzetu ambao wanataka kuwekeza kwenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wangu wa viwanda ajaribu kuhamasisha au kututafutia wawekezaji wengi kwenye mazao ya chai. Kule Lupembe tuna viwanda viwili tu na vile viwanda haviwezi kutosha, havikidhi mahitaji ya chai ya Lupembe. Lupembe tunazalisha chai nyingi na vile viwanda viwili haviwezi ku-process ile chai yote, matokeo yake chai nyingi zinamwagwa na wananchi wanapata hasara kubwa sana. Kwa hiyo, naomba, kama kutakuwa na mwekezaji wa kiwanda cha chai, tunaomba aje awekeze Lupembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye matunda, nanasi na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hongoli muda wako umekwisha!

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leonidas Gama, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa.

MHE. LEONIDAS T. GAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa mpango mzuri. Labda nianze mwanzoni tu niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na mpango mzima wa ujenzi wa viwanda kwa kuzingatia na uzalishaji na hasa dhamira ya Serikali ya kutumia viwanda kwa ajili ya kuinua kilimo. Ukiangalia kwenye mpango ni kwamba, viwanda hivi vinatazamiwa vijengwe ili kuwawezesha wakulima wazalishe zaidi na malighafi ya mkulima ndiyo itumike katika uendeshaji wa viwanda hivi. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana programu hiyo. Nafikiri itasaidia sana kwa wakulima wetu ambao kwa muda mrefu ama wamekuwa wakizalisha wasipate masoko au wanapozalisha, uzalishaji unapungua kwa sababu ya kukosa masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sisi Songea, Jimbo langu la Songea Mjini na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla tunazalisha sana mahindi. Kwa takwimu za mwaka 2015 tu inaonyesha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma walizalisha zaidi ya tani 685,000, lakini uwezo wa NFRA wa kununua mazao hayo ulikuwa ni chini ya tani 50,000. Kwa hiyo, maana yake wakulima walibakiwa na zaidi ya tani 600,000. Ukichukua tani ambazo wametumia kwa chakula, hazivuki tani 300,000 na kwa maana hiyo tani 300,000 za mahindi yao zimepotea, hazina soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niungane na Serikali, niombe rasmi kwamba, Serikali ifanye juhudi za makusudi kwa wakulima kama wale kuwawekea viwanda vya usindikaji. Kwa hiyo, naomba Serikali ione umuhimu wa kuweka viwanda vya usindikaji Songea ili uzalishaji wa mazao ya mahindi uweze kupata vile vile soko la usindikaji kutokana na viwanda vitakavyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, usindikaji unahitaji umeme, viwanda vinahitaji umeme. Mji wetu wa Songea na Mkoa wetu wa Ruvuma kwa ujumla hauna umeme wa uhakika. Kwa hiyo, sambamba na hilo, Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha umeme wa *grid* ya Taifa unafika Songea ili uweze kusaidia juhudi hizi za kuanzisha viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Songea tulikuwa na uzalishaji mkubwa sana wa zao la tumbaku. Kama ilivyo Tabora, vivyo hivyo Songea, lakini uzalishaji wa tumbaku umepungua sana hasa baada ya kiwanda pekee ambacho kilikuwa kinasindika tumbaku katika Mji wa Songea kufungwa kutokana na kuhamishwa,

usindikaji kwenda Mkoani Morogoro. Kwa niaba ya wananchi wa Songea, naomba Serikali isimamie kurejesha kiwanda kile ili kuongeza uzalishaji wa tumbaku ambao umepungua sana baada ya kiwanda kile kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Songea kwa kukosa kiwanda cha tumbaku hauna kiwanda cha aina yoyote. Kwa hiyo, Songea maana yake mzunguko wa pesa ni mdogo, hali ya upatikanaji wa pesa ni mdogo, wananchi wanategemea kilimo tu na kilimo ambacho hakina viwanda vinavyoweza kusindika. Kwa hiyo, maana yake wananchi wa Songea ni wananchi maskini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipofanya ziara mwezi wa 12 katika Mkoa wa Ruvuma, alipata nafasi ya kutembelea kiwanda hiki na ametoa maelekezo rasmi kwamba kiwanda kile kiangaliwe ili kiweze kufufuliwa. Naomba nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia Viwanda, ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage, aone namna ya kufufua kile kiwanda ili uzalishaji wa zao la tumbaku urudi upya. Hivi sasa bado uzalishaji upo, lakini kwa kiwango kidogo sana; hasa ndugu zetu wa Namtumbo, zao kubwa la biashara walilokuwa wanategemea ni zao la tumbaku; na vile vile Songea kuna maeneo ambayo yanalima zao la tumbaku. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mwijage afanye juhudi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mwijage kama kuna uwezekano aone namna ya kufuta ile kauli yake. Kuna kauli moja aliitoa hapa, nadhani tarehe 19 ile mwezi uliopita; alisema, anawaomba wananchi wa Lindi wazalishe muhogo kwa wingi, umepata soko China. Sasa kwa maelezo haya ambayo ameyatoa, tukipeleka muhogo China, maana yake tunahamisha ajira kuzipeleka China. Kwa nini tusifanye utaratibu, kama viwanda vya kuchakata muhogo vipo China, visije Tanzania vikajengwa kule Lindi au Songea ili mchakato wa usindikaji wa muhogo ufanyike Tanzania badala ya kufanyika kule China? Kwa hiyo, niseme simuungi mkono Mheshimiwa Mwijage katika hilo la kusafirisha muhogo kwenda China badala yake muhogo usindikwe hapa hapa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba sana Mheshimiwa Mwijage, tunaomba viwanda Songea, lakini viwanda hivi haviwezi kuja endapo hatutakamilisha zoezi la kukamilisha ulipaji wa fidia katika eneo la EPZA ambapo pale Songea Mjini lipo eneo la Mwenge Mshindo, eneo limeshatengwa, wananchi zaidi ya 1,015 hawajalipwa fidia zao, lakini wananchi hawa wamefanyiwa tathmini mwaka 2008, mpaka sasa ni miaka nane. Nina imani kwamba gharama walizokuwa wanadai 2008, leo zitakuwa zimepanda zaidi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye juhudi ya hali ya juu ili wananchi walipwe fidia zao ili nafasi ile ipatikane kwa ajili ya kuwekeza viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni wananchi wale wamefanya mikutano kule, wana wasiwasi kweli juu ya maeneo yao; wanashindwa kuyaendeleza, wanashindwa kufanya shughuli zozote za maendeleo. Juzi walikuwa wameamua kufanya maandamano ya kuja Dodoma. Nikiwa hapa Bungeni nimejulishwa hivyo na nimefanya juhudi za kuwazuia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake, anipe uhakika wa lini wananchi wangu wa Songea, hasa eneo la Mwenge Mshindo na maeneo mengine yanayozunguka pale, watalipwa fidia zao ili waweze kuondoka katika eneo lile? Kama kuna uwezekano, Serikali ifanye utaratibu wa kuwapatia maeneo mengine ili watakapokuwa wametoka pale, wawe na uhakika wanakwenda wapi na wanakwenda kuendesha maisha yao katika maeneo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kuunga mkono hoja na naomba hizo hoja zangu ambazo nimezisema, namtaka Mheshimiwa Waziri anijibu pale atakapohitimisha. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deogratius Ngalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuzungumza na kuchangia hoja ya Wizara ya Viwanda. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Mawaziri wote kwa namna nzuri wanavyofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu inajikita zaidi kwenye maeneo ya biashara. Hoja ya nchi kutaka kwenda kwenye viwanda ni nzuri, lakini kitu ambacho nakuwa na wasiwasi nacho ni namna ya utekelezaji wa hoja zetu. Ninavyojua, suala la viwanda ni mtambuka, sasa sijajua kwamba Serikali imejiandaa katika kuhakikisha kwamba inawaandaa Watanzania katika mapokeo hayo. Ki-*mind set* Watanzania bado hawajawa tayari kwenye hilo, hivyo wanahitaji *training* ya namna gani ya kuweza kuipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapozungumza, tuna wafanyabiashara wengi sana ambao wako *informal* na kundi hili la wafanyabiashara ni kubwa. Asilimia 70 ya wafanyabiashara wote wa Tanzania wako kwenye kundi ambalo ni la *informal*. Kwa hiyo, bado Serikali haijafanya mchakato mzuri wa kuhakikisha kwamba tunawaandaa wafanyabiashara wetu ili mwisho wa siku waweze ku-*formalise* biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini hizi biashara ziko *informal*? Ziko *informal* kwa sababu sheria haziko *friendly*. Tuna kundi kubwa la wafanyabiashara ambao wanashindwa ku-*formalize* biashara zao kwa sababu ya usajili; namna ya kuzisajili zile biashara inakuwa ni ngumu; na namna ya kupata leseni inakuwa ni ngumu. Leo hii tunaambiwa *TIN number* ni bure lakini ukijaribu kuangalia na kwenda, kupata hizo *TIN number* kwa ajili ya kufanyia hizo biashara, zile *TIN number* zina usumbufu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii unaambiwa, unapotaka kuanza kufanya biashara zako ni lazima kwanza utoe kiwango fulani cha hela hata kabla hiyo biashara hujafanya. Sasa lile linawasumbua sana wafanyabiashara wetu mpaka inafikia kipindi kwamba anaamua acha afanye biashara kiholela, Serikali inakosa kodi na watu wanaweza wakafanya biashara nje ya mfumo sahihi. Nadhani umefika wakati sasa tuendeshe *training* na ikiwezekana hawa watu wetu tuwatengenezee namna ya kujua fursa za biashara zilizopo na ikiwezekana tupate elimu nzuri ya namna hawa watu wetu watafanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la elimu ya ujasiriamali na fursa za biashara bado tuko nyuma. Kuna fursa nyingi ambazo vijana wetu na watu wetu wanazo na wanatakiwa kuzifanya, lakini hawajawa *exposed*. Nadhani ifike wakati sasa Serikali ifanye hatua za makusudi kuendesha *training* kwenye vijiji, kwenye mitaa, ili mwisho wa siku watu wajue ni vitu gani wanaweza kufanya. Kwa sababu fursa zipo zinawazunguka, lakini watu hawajui wafanye nini na mbinu gani watumie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tuna Maafisa Biashara kwenye Manispaa zetu, kuna Maafisa Biashara kwenye Halmashauri zetu, lakini tukijaribu kuwauliza Mpango Kazi wao ni upi? Walio wengi wala hawajui. Waulize Maafisa Biashara kwenye Halmashauri zetu, kuna wafanyabiashara wangapi ndani ya Halmashauri? Hawezi kukupa takwimu. Kwa hiyo, hili nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ifike mahali Serikali lazima itambue ina wafanyabiashara wangapi? Hata tunapozungumza kwamba kuna mfumo ule PPP maana yake nini? Kwa sababu kuna watu wengine hawajui. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo, maana yake kwanza tutawatambua wafanyabiashara na mwisho wa siku ni kwamba hata unapoamua kupanga kodi, unapanga kodi kwa watu ambao unawafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la viwanda. Kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 52, umezungumzia mradi wa kasi mpya wa kuzalisha chuma ghafi. Mara nyingi huwa napata shida, pale unapozunguza kwamba utatekelezwa halafu usiseme utatekelezwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ndiyo tupo kwenye bajeti ya kwanza ya utekelezaji wa miaka mitano kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Naamini unapozungumza mradi, lazima uwe na mahali pa kuanzia na mahali ambapo panatakiwa kuishia. Kwa sababu ukiileta *statement too general* unakuwa hujatupa *tool* ya sisi kuku-assess wewe, kwa sababu hata mwakani tukija, utasema hivi hivi, kwamba mradi huu utatekelezwa na Kampuni ya Maganga Matitu Resources Development. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ifike mahali sasa unapozungumza mradi, hata kama utataka kuutekeleza mwaka 2018, *mentioned*, kwamba mradi huu utatekelezwa muda fulani na unatarajia labda kwisha muda fulani, hivyo tutakwenda vizuri. Kitu chochote unachokiita ni *project* lazima kiwe na mwanzo na lazima kiwe na mwisho. *That is a project.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *statement* zisiwe *too general*. Leo hii unasema unatekeleza mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma kuendeleza utekelezaji wa mradi unganishi wa makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga, kwenye ukurasa wako wa 161. Chuma cha Liganga tumeshaanza kukisikia toka 1906, kwa hiyo, ni kabla hatujazaliwa na inawezekana hata kabla babu zetu wengine hawajazaliwa. Kwa hiyo, ifike kipindi sasa Serikali iseme, wakati tunauliza swali hili kwenye Wizara ya Madini walituambia kwamba fidia itaanza kulipwa mwezi Juni, mwaka 2016 na mradi utaanza mwezi Machi, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa natarajia kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ange-*mention* hii kitu, kwamba mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga utaanza Machi, 2017 kama swali lilivyokuwa limejibiwa na Naibu Waziri wa Nishati na Madini ili tuwe tunakwenda kwa takwimu. Kwa sababu usipotoa takwimu na muda (*time frame*) maana yake hatutaweza kuku-assess na kuku-*pin*. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii Serikali tumeshazungumza kwamba ni Serikali ya viwanda na tunatarajia kwamba tutaenda kwa kasi kubwa. Natamani kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, aseme kinaga ubaga, kwamba tutaanza muda fulani ili tutakapokuja hapa mwakani tuwe na maswali ya kumuuliza. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, hivi viwanda vya kimkakati kwa sababu ameshasema ni *National Flagship Project*, haitakiwi kuwa na majibu *general*. Leo hii watu hawajaandaliwa kwa maana hii miradi itahitaji *support*. Licha ya ukubwa wa hivi viwanda vinavyokuja kule, nilikuwa natarajia kwamba Mheshimiwa Waziri angesema, kwa sababu makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga inaanza, kutakuwa na vitu vya ku-*support* patakuwa na

SIDO; hawa watu tuwaandalie uwezo wa kiufundi ili mwisho wa siku waweze kuji-engage kwenye zile bidhaa au kazi zitakazofanyika na hiyo miradi mikubwa inayokuja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunavyozungumza hakuna barabara ya lami inayoelekea huko. Wimbo huu umekuwa ukiimbwa muda mrefu na hata marehemu Mheshimiwa Deo Filikunjombe alikuwa akiizungumzia kwa kasi sana hii kitu. Mungu amlaze mahali pema peponi. Haijafanyiwa kitu chochote! Kwa hiyo, tuombe kwamba hivi vitu vingine lazima viwe na *support* ya sekta nyingine ili kuhakikisha kwamba hili gurudumu linakwenda. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngalawa muda wako umekwisha.

MHE. DEOGRATIAS F NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jitu soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar,

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia leo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa juhudi na kazi kubwa wanayoonesha na tumeona ushauri mbalimbali ambao unaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuomba Serikali ikubali na Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iwe ndiyo chombo cha kuunganisha Wizara zote, kwa sababu leo hii hakuna chombo cha kuratibu. Kila Wizara inakuwa inafanya kazi kipekee. Muunganike mfanye kazi kama Serikali moja yenye lengo moja. Wizara hii ndiyo iwe mratibu (*coordinator*), ndiyo iwe kiunganishi, kwa sababu masuala yote ya biashara na uwekezaji inapitia katika sekta hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu kuliko yote, tuwe na mabadiliko ya fikra (*mind set change*) na tukishakuwa na mabadiliko hayo ya kifikra, naamini haya yote tunayotarajia itawezekana. Wote tuondoe ile dhana kwamba Serikali itakwenda kuweka kiwanda kidogo cha nini hapa na cha hii; Serikali iweke Sera nzuri, iweke namna ambayo watu wote tutaweza kwenda kuwekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara, badala ya wataalam wote wa ngazi ya Wizara na ngazi ya Mkoa, kuwa wanaandika tu hizi leseni na kuchukua

tozo, wabadilike wafanye kazi ya namna ya kutushauri. Wako Watanzania wenye mitaji yao kuanzia midogo na mikubwa waweze kuwekeza. Kwa mfano, hivi mtu anayewekeza kwenye *Petrol Station* kwa shilingi milioni 600, ni viwanda vingapi vya alizeti? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi ya Wizara ibadilike; badala wale wataalam kukaa na kuandika leseni, hata mtoto wa darasa la saba anaweza kutuandikia leseni. Wao waanze kutushauri, wenye mitaji wapo, mtuambie fursa ziko wapi, Watanzania watawekeza wenyewe. Serikali ibaki kwenye ile ya mradi mikubwa, yaani kwenye zile *flagship projects*. landae miundombinu, sera nzuri, Watanzania waweze kuwekeza kwenye viwanda vidogo na vya kati, wataweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la muhimu ambalo linatakiwa kufanywa ni kuangalia sera mbalimbali; *Regulatory Bodies* zimekuwa nyingi mno. Leo hii Wizara ingefanya utafiti kwamba kwa nini leo tumesema tupandishe kodi kwenye ngozi ghafi na kwenye korosho ghafi, tumeongeza kodi nyingi za *export levy*, kwa nini bado tuna-export mali ghafi ambayo bado haijasindikwa? Kwa sababu hata pamoja na kuwa umepandisha kodi, ukijumlisha, ukizalisha ndani ya nchi, kodi zote zile za *Regulatory Bodies* na tozo mbalimbali ni kubwa kuliko hiyo kodi iliyopandishwa ya ku-export. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wasipokaa na kubadilisha na kuangalia kwa kulifanyia utafiti, bado hii dhana kwamba tutaelekea kwenye uchumi wa viwanda, hatutafikia. Leo hii kwa mfano kwenye mbegu, kwenye madawa ya kilimo, mifugo na chanjo, ukizalisha ndani ya nchi ina kodi zote na ina tozo. Ukitoa nje kuleta ndani vitu hivyo hivyo, havina kodi? Hasa je, hapo unafanya kwamba watu wazalishe ndani ya nchi au tunafanya tuzalishe nje. Kwa hiyo, sera ndiyo kitu muhimu kuliko yote. Sera zikiwekwa vizuri na uongozi (*lead*) uchukuliwe na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naamini Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalam wataweza kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la muhimu ni suala la *BRELA*, tunaomba iwe kwenye kanda na iwe kwenye kila mkoa. Tuanze na kanda ili usumbufu wa kuja mpaka Dar es Salaam kupata huduma hiyo, ingawa mko *online* lakini bado lazima uje Dar es Salaam. Ni vizuri tuwe kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *Regulatory Bodies* nyingi zinafanya kazi za aina moja; nashauri kwamba zote zisiruhusiwe kutoza. Tozo iwe sehemu moja; ukishakata leseni, unalipia kila kitu huko, Serikali ndiyo ipeleke OC huko kila mahali. Hapo ndiyo tutaweza. Mfanyabiashara hataki bughudha, siyo kama anakaa kulipa, lakini bughudha ya kila wakati isiwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tulikuwa tunasema tuwekeze kwenye elimu, kwenye masuala ya VETA. Tumeweka kodi ya 5% SDL, tumeigawa ile kwenda leo kulipia mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Naomba asilimia yote tano iende kwenye VETA zetu. Tunahitaji kuwa na hawa *technical skilled people* ili kwenye hivi viwanda vidogo vidogo na kati tuweze kwenda huko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine muhimu tena ni Sheria ya Manunuzi. Bila kubadilisha Sheria ya Manunuzi haraka, huo mwelekeo tunaoutaka hatutaweza kuufikia. Ni lazima Serikali iangalie namna ya kulinda viwanda vyake vya ndani. Nchi zote zinatoa ruzuku, zinalinda viwanda vyao vya ndani, leo hii katika bidhaa ambazo tunaagiza kutoka nje, naomba muweke *dumping charge* kubwa. Kwa mfano, kwenye chuma, nondo na bidhaa nyingine za chuma, iwekwe *dumping charge*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika mafuta ya kula ambayo yanaagizwa kutoka nje, waweke kodi na ile kodi iwe *ring fenced* iweze kutumika kwenda kuendeleza mazao ya kukamua mafuta ya ndani. Kwenye VAT wanaozalisha mafuta ndani ya nchi, waondoe ile VAT, kwa sababu wanafanya watu waondoke kwenye *formal sector* na kurudi kuwa *informal*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lingine ambalo wafanyabiashara wengi wangependa ni kuwa na *one stop center*. Nikilipa sehemu moja, basi sihangai shwi kwenda ofisi mbalimbali na wakati wanapokuja kukagua, wakague wanapotaka, saa yoyote lakini waje kama timu. Kama mtu wa *weights and measurement*, *TFDA*, *TBS* wote wawe humo humo, wakija wataalam wanakuja mara moja, basi siyo kila siku. Leo amekuja huyu, kesho huyu, kwa hiyo, hayo wakiyaweza, naamini huko tunakotaka tutaweza kufika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ifanye uchambuzi na *research*. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, tukubaliane, nimependekeza kwamba sh. 50/= kwa kila lita ya mafuta iende kwenye Mfuko Maalum kwa ajili ya utafiti, yaani *research*. Tukifanya hivyo, tutapata karibu shilingi bilioni 90 kwa miezi sita. Leo tumeweka kama shilingi bilioni nane kwa utafiti Tanzania nzima. Mfuko huu wa utafiti ukiwepo kwenye kilimo, mifugo, afya kila mahali, hata viwanda na biashara, wote watakuwa na hizo fedha za *research*, kwa sababu bila *research* nchi hii hatutakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara tungependa wale wenye viwanda, wale wenye biashara, wataalam wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji waje wawashauri kwamba hapa fanya moja, mbili, tatu utapunguza gharama ya uzalishaji, fanya moja, mbili utapata tija zaidi. Hiyo ndiyo iwe kazi

ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa sababu wawe *regulators*, wawe washauri, wawekezaji wapo katika sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia leo hii kwa nini, tujiulize kwa mfano, Sekta ya *horticulture* ambayo ndiyo sehemu kubwa kwenye kilimo inayoongeza mapato mengi, leo bidhaa zote tunapitishia Kenya kwa malori. Kwa nini hatutumii KIA? Watu wa Nyanda za Juu Kusini, Songwe, tumejenga uwanja kwa mabilioni ya fedha, kwa nini hautumiki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi ya Wizara hii inatakiwa ndiyo iwe ya kuhakikisha kwamba ushauri unaotolewa, Serikali inakalisha Wizara zote ambazo zinahusika ili ku-*regulate* na kuangalia namna bora na kuweka mazingira wezeshi kwa watu kuwekeza ndani ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Taasisi kama TEMDO, CAMATEC, TIRDO, kuna taasisi nyingi ambazo zinafanya utafiti mbalimbali; nyingi katika hizo zinafanya kazi moja. Hebu mziunganishe ziwe moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukija kwenye Bodi ya Mazao, nashauri badala kila zao kuwa na bodi yake, wavunje bodi zote. Hii ni manyanyaso kwa wakulima na kwa walaji. Wekeni bodi moja na kwenye hiyo bodi moja pawe na idara; kama ni tumbaku, kahawa na nyingine, gharama zile zitapungua na kero kwa hao wakulima na hao wanaofanya biashara itapungua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yao kubwa iwe kushauri namna ya kuboresha biashara, pamoja na hiyo, wakifanya labda kuagiza kama ni pembejeo kwa bei nafuu, faida inayopatikana ndiyo itumike kuendesha zile bodi, isiwe makato kwa wakulima, wavuvi na wafugaji. Kwa hiyo, la muhimu, bado tunarudia pale, ni sera. Kwa hiyo, tunaomba na naamini Mheshimiwa Waziri uwezo huo anao na timu yake kwa kupitia Dkt. Abedi, Katibu Mkuu, waweke Sera bora. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jitu muda wako umekwisha.

MHE. JITU V.SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, kuchangia katika hoja ya viwanda na biashara. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai mpaka leo kwamba nimepata nafasi ya kuweza kumshukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuchangia kwangu ni mara ya kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Newala, kama wanayofanya wenzangu, kumsifu Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi na kazi anazozifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Rais wa Zanzibar, ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kuwasifu Waheshimiwa Mawaziri ambao wameteuliwa ambao kwa kweli uchapaji wao wa kazi unaendana na hali halisi tuliyonayo Tanzania sasa hivi. Maana Tanzania ya leo tulikuwa tunahitaji viongozi wa *design* hii, maana tulishafikia mahali pabaya sana ambapo wananchi walikuwa wamekosa imani na Serikali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite katika mchango wangu kwa Wilaya ya Newala. Wilaya ya Newala inalima korosho takribani tani 80,000 hadi 70,000 wakati korosho ambazo tunasafirisha nje zinakuwa ni tani 150,000. Kwa hiyo, karibu nusu ya korosho ambazo zinasafirishwa zinatoka Newala na Tandahimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Newala tuna viwanda viwili vya kuchakata korosho. Kuna kiwanda kimoja au viwili vyote tulikuwa tumepata kwa mkopo wa Benki ya Dunia ambao naamini mpaka leo tunalipa zile fedha nyingi sana. Vile viwanda vilifanya kazi takriban kwa miaka miwili tu. Hivyo viwanda vikawa vimesimama, haviendelei tena kufanya kazi. Kwa hiyo, nashindwa kuelewa, kama viwanda viwili vipo na tunazalisha korosho zaidi ya tani 70,000, kinachofanyika ni nini? Kwa sababu kinachofanyika hapo unaona kwamba watu ambao wanazalisha korosho wapo, maana yake *product* zipo na vile viwanda vipo, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonyesha ni kwamba hapa tatizo labda ni *management*. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje atueleze hapa, kwamba uchakataji wa korosho katika Wilaya ya Newala utaanza lini? Sambamba na Wilaya ya Newala, kuna viwanda vingine kwa mfano vya Mtama, Likombe pale Lindi, Mtama viwanda vyote hivyo vimesimama na hawa watu wanazalisha korosho, ni kitu gani kinachofanya kwamba tusiendeleo kuchakata hizi korosho?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaingia katika mchakato mwingine wa kujenga viwanda vingine vya pili. Kwa nini tunaendelea kujenga viwanda vingine wakati vile ambavyo Mwalimu Nyerere alikuwa amevijenga tunashindwa kuvisimamia na kuchakata korosho? Ni kitu gani kinachofanyika? Kama kweli tumeshindwa, basi tunge-*hire management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonyesha ni kwamba sisi tunashindwa kuzalisha, basi tukodi *management* ili hivi viwanda vianze kufanya kazi. Ukiangalia kiundani, utaona kabisa kwamba hivi viwanda vyote vinatumika kama maghala leo. Wengine wameondoa mashine zile, wameuza au wamekata chuma chakavu. Sasa Mheshimiwa hapo nashindwa, tutaendaje kwenye hivyo viwanda vingine vya kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo kama haitoshi, kuna wananchi wangu pale wa Newala baada ya kuona kwamba hizi korosho sasa hazichakatwi tena, wale akinamama wameanzisha vikundi vidogo vidogo ambavyo kwa kweli sasa wanachakata kwa kutumia mikono yao; lakini zile korosho ndiyo korosho ambazo ni nzuri *in the world*, lakini sasa zinapatikana kwa kiasi kidogo. Watu wa nje wanakuja wanataka zile korosho, lakini zinakuwa ni kiasi kidogo kwa sababu ile *process* wanayoitumia kuchakata inakuwa ni finyu kwa kuwa wanatumia mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba ana mkakati gani? Kama vile viwanda ameshindwa kuviendesha, je, anawezeshaje akinamama ili waweze kuchakata korosho kwa wingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, pale Nachingwea kuna kiwanda kikubwa sana cha kuchakata ufuta, alizeti pamoja na karanga. Sasa sisi tunalima ufuta kule, ule ufuta unalimwa kwa kiasi kikubwa sana; ni kitu gani ambacho kinazuia tusichakate ufuta tukapata mafuta ambayo ni *the best in the world*? Maana inasemekana kwamba mafuta ya ufuta hata wale ambao wanasumbuliwa na *pressure* iwe ya kushuka au kupanda, ukiyatumia kwa muda mrefu inasaidia kuweka afya yako kuwa nzuri. Kwa nini tusiendeleo au tusifufue kiwanda hiki tukawa na *process* tena ya kuchakata huu ufuta au alizeti? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Farm Seventeen* pale, kwa wale ambao labda hawajafika Nachingwea, kuna *Farm Seventeen*, *Farm Twenty One*, yale yalikuwa ni mashamba ya Wajerumani ambao walikuwa wanalima karanga. Sasa Mheshimiwa Waziri aje atuambie, kama kile kiwanda kipo na yale mashamba yapo, ana mpango gani wa kutafuta watu? Maana wale Wajerumani walilima karanga pale, japokuwa wao walikosa *time*, lakini leo Jeshi

la Wananchi wanatumia eneo lile kwa ajili ya mazoezi. Yale yalikuwa ni mashamba kwa ajili ya karanga!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwamba je, nchi yetu ina mpango gani wa kutumia yale mashamba kulima karanga ili tuweze kupata mafuta? Pia kile kiwanda kilichopo pale Nachingwea kuna mpango gani wa kufufuliwa badala ya kula mafuta mabovu mabovu ambayo tunaletewa kutoka nje? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Diwani pale Kinondoni. Kwa hiyo, mchango huu ni wa Kitaifa. Kwa mfano, pale Ilala kuna Kiwanda cha *Bulb*. Kile Kiwanda cha *Bulb* kimefungwa! Leo tuna-*import bulb* kutoka nje, hivi hii siyo aibu kweli? *Bulb* za kuweka juu; kile kiwanda leo wanatumia watu wa TATA kwa ajili ya ghala la kuuzia magari. Ile mitambo yote imeng'olewa. Hivi ni nani ambaye alichukuwa kile kiwanda na kwa nini ile mitambo iliondolewa? Kwa nini sasa badala ya kutengeneza *bulb*, watu wanatumia kama maghala ya kuuzia magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na *East Afrika Cables*. Leo wana-*import* badala ya kutengeneza zile nyaya ambazo zilikuwa *the best* katika dunia hii kutegemeana na hali halisi ya Tanzania, kwa sababu wale ma-engineer walikuwa wanajua hali halisi ya Tanzania ikoje. Leo wana-*import* nyaya kutoka nje, kwa nini wameshindwa kutengeneza zile nyaya ndani, leo wana-*import* kutoka nje? Hivi ni vitu ambavyo nadhani Mheshimiwa Waziri ayaangalie kabla hajaingia katika viwanda vingine ambavyo anasema anaweza kuhamasisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, utakuta viwanda zaidi ya 300 au 400 havifanyi kazi. Kwa nini hivi viwanda vimegeuzwa kama maghala? Kwa nini wasitafutwe wawekezaji ambao utawaambia kwamba mimi leo nina viwanda vya *design* fulani halafu wale wakaja ukawapa yale maghala wakaweka tu mitambo badala ya kuwatafutia ardhi ambayo haina chochote? Huoni kama huo utakuwa ni utendaji mzuri zaidi kuliko leo unaanza kutafuta ardhi lakini wale watu leo wana maghala na hayo maghala wanayatumia kwa kuhifadhia mali badala ya kuzalisha? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika *TIC*, yaani huu uwekezaji; uwekezaji *should be epically* ina maana kwamba huu uwekezaji maana yake lazima umnufaishe Mtanzania. Wawekezaji wengi wanapokuja hapa Tanzania, hawawanufaishi Watanzania, wao, wanaangalia rasilimali zao. Hamna nchi yoyote duniani ambapo unaweza uka-*import* vitu kutoka *outside* halafu hapa ndani ukaviuza vile vitu kwa dola. Kwa nini hawa wawekezaji zile rasilimali zao wanazozileta hapa ndani wanauziuza kwa dola? Hicho ndicho chanzo kikuu

cha kushusha thamani shilingi yetu, kwa sababu sisi wenyewe tumeshaidharau fedha yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda India, China, nenda mpaka zile hospitali za Wilaya, haiwezekani wewe kule ukafika na dola wakakubali. Watakwambia kabadilishe upate fedha za nchi ile. Hata China, ni lazima ubadilishe zile fedha za Tanzania iwe ni dola, uibadilishe upate fedha ya nchi ile *then* uende ukanunue. Leo hapa tunaletewa magari ya TATA unauziwa in US Dollars. Maana yake *exchange rate* ya hayo magari yanabadilika kila siku kutegemeana na shilingi yetu inavyoshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kama kweli tungekuwa tunauza kwa shilingi, basi zile gari ambazo zimeingia mwaka 2015, mwaka huu zisingeweza kupanda bei. Leo gari ambayo imeingia mwaka 2015 kwa dola fulani, labda *exchange rate* ilikuwa shilingi 1,200/=, mwaka huu kila siku unauziwa kwa *rate* ya leo; uone hapo fedha yetu inakosa thamani. Kwa hiyo, tuangalie kwamba Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji washirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, waone ni namna gani tutakuwa na sheria za kuweza kudhibiti fedha yetu ikawa na thamani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nitayasoma majina ya wachangiaji watakaomalizia kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Tunao Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mheshimiwa Zitto Ruyagwa, Mheshimiwa Yosepher Komba, Mheshimiwa Anthony Komu, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Sabreena Sungura, halafu tutakuwa na Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Hamida Mohamed, Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi na Mheshimiwa Leah Komanya. Hawa ndiyo watakuwa wachangiaji wetu mchana, watakaomalizia uchangiaji wa hotuba ambayo iko mbele yetu.

Pia ninalo tangazo dogo hapa kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *sports club* anawatangazia kwamba Wabunge wote ambao ni wanamichezo kutakuwa na Kikao kesho saa moja na nusu asubuhi baada ya kumaliza

mazoezi uwanja wa Jamhuri, anaomba atakayesikia tangazo hili amjulishe na mwingine. Japo simwoni hapa ndani, naona kama ametubagua tunaowahi kuondoka uwanjani, maana ameweka saa 1.30.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

(Saa 7.02 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tundaendelea na uchangiaji. Tunaanza na Mheshimiwa Mtolea,

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukupa uwezo wa kunipa nafasi ya mimi kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara kwa niaba ya wananchi wa Temeke na kwa maslahi mapana ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukimsikiliza hapa Mheshimiwa Waziri ni kwa namna gani anapenda kuona Tanzania ambayo imesheheni uwekezaji katika sekta mbalimbali ili kuifanya nchi hii iwe ya kipato cha kati. Hili ni jambo zuri na kila mtu angependa siku moja kuona Tanzania hiyo. Wakati pia tunajipanga kuwakaribisha wawekezaji kwa kiasi kikubwa, ni vizuri pia tukawa na mpango maalum wa kuona ni kwa namna gani tutawasimamia wawekezaji hao ili uwekezaji wao uwe na tija kwa Taifa hili na kwa wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano michache ya wawekezaji ambao sasa hivi wapo, inatutia mashaka kweli kweli. Haioneshi kama uwekezaji wao una tija na malengo mazuri kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Jimboni kwangu Temeke, eneo la viwanda Chang'ombe lina wawekezaji wengi, lakini kwa masikitiko makubwa yamekuwa ni maeneo ya mateso kwa Watanzania, maeneo ya mateso kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wananyanyaswa kwa kiasi kikubwa sana katika viwanda na makampuni hayo, kwa kulipwa mishahara midogo sana, kufanyishwa kazi ngumu kwa masaa mengi, hawana vitendea kazi; unamkuta mtu katika kiwanda pengine cha kuyeyushia chuma hana vifaa vya kufanyia kazi. Yupo tumbo wazi, mikono mitupu, hana mask, anafanya kazi kwenye moto mkubwa kiasi hicho. Wawekezaji wanawaambia kabisa, kama

hutaki kazi acha, kuna wenzio 300 mpaka 400 wanasubiri hiyo kazi yako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofikia mahali wawekezaji wanawanyanya wananchi kwa sababu tu kuna tatizo kubwa la ajira, ni lazima tufikirie mara mbili, ni namna gani tujipange tuweze kuufanya uwekezaji huu uwe na tija kwa wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tungependa tuwe na wawekezaji wenye masikio yanayosikia wawekeze kwa kufuata sheria na taratibu za nchi hii. Hapo hapo Chang'ombe, kuna wawekezaji wamejenga viwanda na ma-godown yao juu ya mifereji ya kutiririsha maji machafu. Yaani wanaziba miundombinu ya kutolea maji mitaani kwa maana ya uwekezaji. Unajiuliza, ni kweli tunasimamia huu uwekezaji? Kwa hiyo, kuna wananchi pale Chang'ombe kwa muda wa miaka 12 sasa, kila ikinyesha mvua kwao ni mafuriko, kwa sababu tu kuna watu wamejenga magodauni yao na viwanda vyao, wameziba mifereji ya maji na hakuna mtu wa kuwaambia kwamba hili mnalolifanya ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, wanatiririsha maji ya kutoka viwandani yanaingia mitaani unajiuliza hawa wanaoitwa NEMC wako wapi? Wanaandikiwa barua, wanapigiwa simu, hakuna kitu wanachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akafahamu kwamba Taasisi zinazomzunguka zina mchango mkubwa sana wa kuzifanya ndoto za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati, zitimie au zifeli. Ni vizuri akaziangalia tena upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Sandali ambayo nayo ipo katika Jimbo hili hili la Temeke, ambayo inapakana na viwanda vya Vingunguti vilivyoko katika Jimbo la Segerea, kuna mfereji unaotiririsha maji ya sumu yanayonuka vibaya na yanayoathiri mazingira kuanzia Januari mpaka Desemba. Wananchi wa Mitaa ya Mamboleo 'A', Mamboleo 'B', Kisiwani, Usalama wakijenga nyumba ukaezeka bati leo, baada ya miezi sita, zile bati zinakuwa zimetoboka zote na ukizigusa zile kuta za nyumba, yale matofali yanamong'onyoka. Sasa jiulize, afya za wananchi wa hapo zikoje? Kama mabati yanatoboka hivyo, afya za wananchi zikoje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akimaliza bajeti yake hapa, afanye utaratibu afike Temeke ajionee. Twende nikakuoneshe yanayofanyika, uone wananchi wanavyoteseke na uwekezaji ambao tunautaka uingie sasa hivi. Upite na kwenye ma-godown uone. Kwa mfano, kwenye viwanda labda vinavyotengeneza unga, wakisikia watu wa TBS wanakuja, siku hiyo utatengenezwa unga maalum kwa ajili ya kuwaonesha TBS,

lakini siyo ule unaotengenezwa kila siku. Kwa hiyo, kumbe hata afya zetu kwenye hizi bidhaa zinazozalishwa, ni matatizo (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna raia wengi wa kigeni wasiokuwa na *documents* za kukaa hapa nchini, wamefungiwa kwenye hayo ma-godown wanafanya kazi ambazo Watanzania wangezifanya. Kwa hiyo, kuna miradi mikubwa ya watu, kuwaficha watu, kuwatumikisha wakidhulumu nafasi za Watanzania. Lazima tuyatoe haya, ndiyo uwekezaji utakuwa na tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hawa watu wa viwanja vya biashara vya Saba Saba na uwanja wa Mpira wa Taifa; uwanja mkubwa wa Taifa na Uwanja wa Uhuru; hawa watu hawalipi kodi. Hawalipi malipo wanayostahili kuilipa Halmashauri ya Temeke. Hawalipi *property tax* wala *service levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Halmashauri iweze kutekeleza majukumu yake ya kuboresha huduma za kijamii ni lazima ikusanye kodi. Unapokuwa na wawekezaji au watu wanaofanya biashara ambao hawakulipi, unakuwa ni mzigo mkubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa nafasi yake, aongee na hawa watu wa Saba Saba na Uwanja wa Taifa. Tumewapelekea *invoice* kwa muda mrefu na hawajalipa. Sasa akawaambie nitawajazia watu siku siyo nyingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawakusanya wananchi wa Temeke twende tukazuie kufanya biashara zao, twende tukazuie mechi zisichezwe Uwanja wa Taifa. Najua tutapigwa sana mabomu, lakini *I am very proud* kwamba watu wa Temeke wakilitaka lao, hawaogopi mabomu. Kwa hiyo, tutayafanya hayo endapo wataendelea kukaidi kutulipa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia fedha za Halmashauri kusafisha yale mazingira baada ya mechi kucheza, baada ya maonesho ya Saba Saba; kwa nini tutumie fedha yetu na wao hawataki kuchangia? Hatuhitaji uwekezaji wa namna hiyo. Kwa hiyo, wafikishie taarifa, waambie kwamba tutakuja tuyafanye hayo. Tutazuia moja kati ya maonesho Uwanja wa Saba Saba, lakini tutazuia moja ya mechi Uwanja wa Taifa nao waione hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wakati wengine wanahitaji viwanda, sisi Temeke tunahitaji masoko. Tuna viwanja vikubwa vya kujenga masoko kwenye kila Kata na wafanya biashara wako tayari kufanya biashara katika masoko hayo. Tuletewe wawekezaji watujenge masoko ya kisasa na fedha yao itarudi haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie NSSF waache kujenga madaraja, waje wawekeze kwenye masoko, fedha yao itarudi haraka sana. Waambe

National Housing waache kwenda kujenga majumba maporini wanahangaika kutafuta wapangaji, waje kuwekeza sokoni.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umemaliza Mheshimiwa Mtulia.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea Mheshimiwa Zitto Ruyagwa, atafuata Mheshimiwa Josepher Komba.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na nina maeneo machache kama matatu au manne hivi kama muda utakuwa umeniruhusu ili niweze kuchangia uboreshaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza katika Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Komu, amezungumzia suala zima la *discrepancy* iliyopo kati ya vitabu vya Wizara, vitabu vya Wizara ya Fedha, kwa maana ya kitabu Na. 4 cha maendeleo na randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusiana na mradi wa *General Tyre*, ambapo mpango wa maendeleo unasema fedha zitakazotengwa ni shilingi bilioni mbili, randama ya Viwanda na Biashara inasema fedha ni shilingi milioni 500 na kitabu cha bajeti ya maendeleo kinasema shilingi milioni 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niikumbushie hoja hii kwa sababu nadhani ni hoja muhimu sana ili tuweze kufahamu tunapopitisha bajeti hii ni nini hasa tunachokipitisha. Kwa sababu ni vyema tukajua ni shilingi milioni 150 itakayopitishwa na Bunge, ni shilingi bilioni mbili ambayo ipo kwenye Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya *General tyre* au ni shilingi milioni 500 iliyoko kwenye randama ya vitabu vya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nami nataka kurejea kauli ambayo Wabunge wenzangu Wamezungumza kwamba tunataka kujenga viwanda gani, kwa sababu ni lazima tuwe na *focus* na tuweze kuhakikisha kwamba tunaendana na ile *focus* ambayo tumeiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilipokuwa napitia hotuba ya Waziri, nimeona katika Ibara ya 191 ya hotuba yake, anazungumzia malengo ya mwaka 2016/2017. Katika haya malengo yote, sioni lengo ambalo linaelekeza nchi yetu kwenda kuzalisha bidhaa ambazo wananchi wengi wanazitumia na hapa nazungumzia sukari, mafuta ya kula na nguo. Hizi ni bidhaa ambazo

wananchi wanazitumia kila siku. Hata hivyo, katika malengo tisa ya mwaka wa 2016/2017 ya bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, sioni jambo hilo. Sasa nashindwa kuelewa, Wizara haioni kwamba kuna tatizo katika maeneo hayo na kwamba tuna haja ya kufanyia kazi jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha zaidi ni kwamba kuna tatizo la Wizara kutokusomana; yaani Wizara ya Kilimo inachokisema, hukioni kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Viwanda vyetu sisi kimsingi vinategemea sana malighafi za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nina hotuba mbili, nina hotuba ya Wizara ya Kilimo na nina hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Katika hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara, sukari siyo *priority* kabisa. Haitajwi kabisa! Katika hotuba ya Wizara ya Kilimo ukurasa wa 25, 44 na 63, anazungumzia mikakati ya kuondokana na tatizo la uhaba wa sukari. Mpaka kwenye kiambatanisho namba sita cha hotuba ya Wizara ya Kilimo, kuna mikakati na miradi mingi na mpaka mradi wa Mheshimiwa Kawambwa ambao ameuzungumzia leo wa Bagamoyo na changamoto zake, imeelezwa. Hiki unachokisoma huku, haukisomi Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kujua, Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu yuko hapo, *cabinet* haikukaa kuweza kuwianisha Kilimo na Viwanda? Kwa sababu Waziri wa Kilimo akilima miwa, haiwezi kuwa sukari bila viwanda. Ukiangalia humu, miradi ambayo imeainishwa kwenye Wizara ya Kilimo, ni miradi ambayo inaweza kuzalisha tani milioni moja na nusu za sukari. Maana yake ni kwamba tutaweza kutumia ndani na kuuza nje na kwa bei ya sukari ya jana, tunaweza tukauza mpaka Dola za Kimarekani milioni 500 kulingana na miradi ambayo iko humu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiyo miradi ambayo ipo humu, huioni kwenye viwanda. Tunasema kwamba sisi tunachokitaka ni kuanza na bidhaa za kilimo ili wananchi wetu wapate ajira tuongeze thamani na kadhalika na nadharia za uchumi zinaonesha hivyo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba tukubaliane kitu kimoja ambacho kimo ndani ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, hata tukimpitishia Waziri fedha zake zote sasa hivi, tutarudi mwakani, sifuri. Kwa sababu hakuna tutakachoweza kuki-solve. Iwapo Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, wakioanisha mipango yao, ndani ya miaka mitatu hatuna shida ya sukari tena nchini. Wala hatutamwangaisha tena Mheshimiwa Rais kutembea barabarani anatoa amri kuhusu sukari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anatoa amri kuhusu sukari kwa sababu Mawaziri hawafanyi kazi yao. Kwa sababu matamko ambayo Mheshimiwa Rais anayazungumza kuhusu sukari, ni matamko ambayo yalipaswa kuzungumzwa na Mawaziri. Kama kungekuwa na *coordination* kati ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara wala tusingekuwa na shida leo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa ibara ya 69 ya Kanuni zetu za Bunge, Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu, kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba Waheshimiwa Wabunge na hapa tuwe *beyond party politics*, yaani tuwe zaidi ya Vyama vyetu. Nawaomba tuiombe Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ziende zikakae, wafanye marekebisho ya Bajeti ya Viwanda na Biashara, halafu ndiyo baadaye turudi, kujadili suala zima la Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Vinginevyo hapa tunakuwa tumecheza. Bahati mbaya sana, tumeshapitisha Wizara ya Kilimo. Ilitakiwa zote mbili hizi, tusizipitisha kwanza, wakae, wazungumze watuletee *program*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 69 ya Bunge, mjadala huu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji uahirishwe. Hulikuti jambo hili kwenye sukari peke yake, unalikuta kwenye nguo, Wizara ya Kilimo inazungumzia pamba, lakini uzalishaji wa pamba umeporomoka kwa asilimia 47. Wizara ya Viwanda inasema itaimarisha viwanda vya nguo, utatoa wapi pamba ya kuingiza kwenye viwanda vya nguo. Pamba imeshuka *by six and seven percent*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji haijazungumza kabisa suala la bidhaa ya mafuta ya kula. Leo hii ukitembea unakwenda Singida, unawakuta wananchi wetu wanapigwa na jua barabarani wanauza mafuta kwenye madumu. Mafuta ya alizeti leo bei yake ni kubwa kuliko bei ya petroli katika Soko la Dunia, lakini hamna mpango, hakuna *links* kati ya kilimo na viwanda.

Kama tunataka tuzungumze kuwafurahisha wananchi kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda tuendeleo kupitisha hii bajeti. Kama tunataka angalau Bunge hili lifanye *value addition* katika kazi ambayo Serikali inafanya, tuombe hawa ndugu zetu watoke, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda waende wakakae wawianishe mipango yao watuletee tuweze kupitisha. Tukipitisha hivi hivi, hatutaweza kufanya chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitoe hoja kwamba mjadala wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji uahirishwe ili Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Kilimo waende wakakae waweze kuwianisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, viwanda vinahitaji vivutio. Nitatoa hoja mwishoni. Kuna umuhimu mkubwa sana, maana yake nasikia sasa hivi kuna mvutano kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda kwa ajili ya kutoa vivutio kwenye viwanda vya kimkakati. Sasa Mheshimiwa Rais yuko barabarani, anapiga kelele kuhusu sukari; mwekezaji anataka kujenga kiwanda cha sukari; mnatakiwa mkubaliane mtoe vivutio kiwanda kile kiweze kujengwa, Wizara ya Fedha inakataa. Maana yake nini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais analaghai wananchi? Haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana nasema kuna haja kubwa sana hawa watu wakakae tena. Naomba nitoe hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 69, kwamba Bunge hili liahirishwe shughuli za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji mpaka hapo watakapoainisha mipango ya kilimo na mipango ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja na naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Komba na baadaye atafuatia Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tu kienyeji na Mheshimiwa Zitto, anajua hoja hii siyo kwa bajeti. Kwa utaratibu wa kanuni ya bajeti, mnayo nafasi nyie viongozi wa Bunge wa kukutana na Spika na Wenyeviti wote kujadiliana juu ya haya. Wewe umechangia, subiri ushike Shilingi ya Waziri. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea. Mheshimiwa Yosephu Komba halafu Mheshimiwa Stephen Ngonyani na baadaye atakuja Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Samahani, jina langu ni Yosepher Komba sio Yosephu. Nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu cha Waziri ukiangalia na uhalisia, hakuna kitu. Kwa sababu gani nasema hivyo? Inaonekana Tanzania ya viwanda ipo hewani, haina mizizi. Huu msemu ni msemu wa kisiasa ambao hauna mizizi. Kwa sababu gani nasema hivyo? Wameongea Wabunge waliopita kwamba hakuna uhusiano wa viwanda na mahitaji ya viwanda; hakuna uhalisia wa viwanda na mahitaji ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa *nature* ya nchi yetu, tukubali tukatae, kama tunataka viwanda, ni lazima viwe ni *agro-industries*, viwanda vinavyotegemea kilimo, vinavyotegemea mazao yanayotokana na kilimo, lakini hakuna uhusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wakulima wanahangaika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliwahi kusema kwamba jembe tutalikuta makumbusho. Hizo ni lugha za kisiasa. Tumefikia Tanzania kutokutumia jembe! Tumefikia Tanzania ambayo hatutegemei mvua kwa ajili ya kilimo! Viwanda vinahitaji malighafi muda wote, lakini kilimo chetu cha kutumia mvua; isiponyesha hakuna kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, pamoja na kukaa na kupanga, kuna utaratibu mzuri na uhusiano mkubwa na sekta nyingine. Tusiongee kama sisi, tuongee kama nchi, tuongee kama Wizara ambazo zinafanya kazi pamoja. Kila mtu asiwe na *personal interest* kwenye Wizara yake; kila mtu anaongea anavyojisikia. Waziri wa Viwanda wewe huwezi kukamilisha lengo lako kama huna uhusiano mzuri na Waziri wa Kilimo, huna uhusiano mzuri na Waziri wa Ardhi, huna uhusiano mzuri na Waziri wa Miundombinu na sekta nyingine. Hakuna kitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua mahitaji ya viwanda kama malighafi na teknolojia. Tuangalie suala la teknolojia. Ni kwa kiasi gani hivyo viwanda vitakavyojengwa vitaweza kukidhi teknolojia ambayo wananchi wetu wanayo? Tumelenga viwanda vidogo na viwanda vya kati ambavyo kwa asilimia kubwa ni wananchi wa kawaida, wenye elimu ya kawaida. Tumeongea kuhusu VETA, tumeongea kuhusu maeneo mbalimbali ambayo yangeweza kutoa ujuzi kwa wananchi wetu; hilo halijafanyika. Mheshimiwa Waziri anatuambia Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea miaka mitano hii ungetumia nguvu nyingi sana kutengeneza miundombinu ya viwanda, lakini siyo viwanda kwa

maana ya majengo, tunadanganyana. Tungetengeneza miundombinu ambayo inge-*facilitate* viwanda. Tunasema uwekezaji, tunasema Serikali haijengi viwanda, tunawaita wawekezaji. Tujiulize, miaka yote wawekezaji walikuwa wapi kiasi kwamba Mheshimiwa Waziri amefanya lipi kubwa la kumvutia mwekezaji katika kipindi ambacho yeye amekuwa Waziri? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni yale yale ambayo miaka 20 au 30 iliyopita wawekezaji walishindwa kuja kuwekeza. Hata yale maeneo ambayo viwanda tulivibinafsisha, vingi vimekufa. Mimi natokea Mkoa wa Tanga, kuna viwanda vingi. Tulikuwa na viwanda vya chuma, viwanda vya blanketi, viwanda vya matunda, viwanda vya mafuta, viwanda vya kila aina, vimekufa. Tanga ilikuwa ni Mkoa wa Viwanda miaka ya 1980, lakini sasa hivi Tanga imekuwa ni magofu. Viwanda vingi vilivyokuwepo wameiba mashine, wameiba kila kitu, wengine wamehamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunategemea zao la mkonge, tulikuwa tuna mashamba kwa ajili ya kuzalisha mbegu za mkonge, yamekufa. Tulikuwa na *estate* nyingi sana, zimekufa. Wawekezaji wameshindwa, wamerudi kwenye nchi zao, yale maeneo wananchi hawayatumii kwa kilimo, yamebakia kuwa mapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunataka viwanda, viwanda vipi ambavyo haviangalii malighafi? Tunajua bei ya katani katika Soko la Dunia; tunajua bei ya mkonge, tunajua thamani yake kwenye Soko la Dunia; lakini tunataka viwanda ambavyo tutawadanganya wananchi kwa maneno, kwenye uhalisia hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tujiulize, Mheshimiwa Waziri anapotuambia nchi ya viwanda, anataka ku-*compete* na nani? Amejiandaa ku-*compete* na nani? Anaposema Tanzania ya viwanda, ajue kwenye dunia hii kuna nchi kibao ambazo zipo katika hiyo *level* ya viwanda. Amejiandaa ku-*compete* nao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 91, kuna hili Shirika la Viwango (TBS), naomba ninukuu baadhi ya maneno aliyoyaandika hapa. TBS imekuwa ikishirikiana na Jeshi la Polisi na Taasisi nyingine za Serikali kama *TFDA*, *TRA FCC*, *GSLA* na *EWURA* katika kufanya ukaguzi wa kushtukiza sokoni ili kuhakikisha kuwa bidhaa dhaifu zilizo chini ya kiwango na ambazo siyo salama kwa afya au matumizi ya mlaji zinaondolewa sokoni.

Kwa hiyo, sasa TBS wanaenda kuvizia sokoni. Wanaenda na Polisi, TRA na FDA kuvizia sokoni. Wakati zinaingia, hakuna utaratibu wa kuhakikisha kwamba haziingii. Hii kauli inajidhihirisha, hata Mheshimiwa Rais juzi amesema.

Wafanyabiashara wanavizia sukari ambazo zinaelekea kuharibika, wanazinunua, wanaziingiza Tanzania. Viongozi mnalijua hilo, mnangoja ziingie, zikifika sokoni, mnaenda kuzitafuta. Wangapi watakuwa wameathirika na hizo bidhaa? Tunajua bidhaa zinazotoka nje ni za hali ya chini; zinakuwa na bei ya chini kutokana na ubora pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanazalisha bidhaa ambazo ni bora, lakini inakuja kwenye bei kutokana na hali halisi ya Mtanzania hawezi kununua kitu cha sh. 10,000/= wakati kuna kitu hicho hicho kwa sh. 5,000/=. Kwa hiyo, Watanzania wengi kutokana na hali ya uchumi, hatuangalii ubora, tunaangalia uwingi. Kwa hiyo, hakuna namna kama hamjaweka mkakakati mzuri, kuhakikisha kwamba wazalishaji wa ndani wanalindwa kuanzia kwenye utaratibu wao wa uzalishaji. Wanatumia gharama nyingi sana, mwisho wa siku sokoni lazima bidhaa yake iwe na bei ghali. Mtanzania anashindwa kuinunua, anangoja inayotoka nchi za nje. Tunalalamika, tunataka viwanda, tuna nchi ya viwanda, naona hiki ni kitu ambacho hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi nasoma shule ya msingi, kulikuwa kuna kitu tunaita mazingaombwe. Anakuja mtu, tunachangia shilingi hamsini hamsini, tunaingia, tunaonyeshwa namna ya kutengeneza shilingi elfu kumi. Sasa naona mazingaombwe yale ambayo nilikuwa naamini ni utoto kudanganywa, yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, tunajua ipo kwenye ilani, ipo kwenye maneno ya viongozi wako; Mheshimiwa Rais na viongozi wengine kwamba Tanzania ya Viwanda. Mkoa wa Tanga tuliahidiwa Tanga ya Viwanda mwaka 2010 na aliyekuwa Rais wa Awamu ile ya Nne, sasa leo hii ukisema Tanzania ya Viwanda, watu wa Tanga hawatakuelewa, kwa sababu walishasikia Tanga ya Viwanda, haikuwezekana. Tanzania ya Viwanda ni ndoto! Kwa miaka hii, kwa utawala huu ambao hauna uhusiano katika Taasisi zake, ambao kila mtu anataka kujinufaisha yeye kutengeneza jina lake! Ukiwa Waziri, cheo cha kisiasa kiweke pembeni. Ukiwa Waziri, jaribu kusikiliza wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba Waziri anakuwa mkuu kwenye Wizara yake kushinda mtaalam, kushinda mtu yeyote hata kama hana utaalam wowote, kwa sababu tu ya cheo. Hiyo imekuwa ikiathiri sana mapendekezo na nia ambayo tunayo Watanzania. Naomba Mawaziri, Mwanasiasa yeyote anayejiamini na mwenye nia njema na nchi yake, lengo lake hata kama hana ujuzi wowote ni kuhakikisha wenye ujuzi wanafikia matamanio yao. Mwanasiasa lazima ahakikishe kwamba binadamu hafi; lazima ahakikishe mkulima anapata mazao mazuri kwa sababu ndiyo lengo la mkulima; ahakikishe kwamba *engineer* anatengeneza barabara nzuri; siyo kuwa na amri kwenye kila kitu ambacho hatuna utaalam nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la masoko. Tunajua wakulima wetu wanavyolima kwa shida na hilo jembe la mkono ambalo tumeambiwa litakuwa historia, sijui ni mwaka gani. Tangu mwaka 1961 tunapata uhuru lilikuwepo, hatujui limepungua kiasi gani, lakini tunaambiwa na Waziri wa Kilimo litakuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania kwa kilimo cha jembe la mkono wamejitahidi sana hapo walipofikia. Masoko yamekuwa ni shida! Masoko yamekuwa ni tatizo! Sijui ni kwa namna gani na kwa kiasi gani mnawaandalia masoko wakulima hawa ili hayo mazingira ya viwanda yawe rahisi kwao? Kwa sababu gani nasema hivyo? Masoko yanaendana na miundombinu, masoko yanaendana na bei, yanaendana na gharama za uzalishaji,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yosepher muda wako umemalizika.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya hotuba ya Upinzani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na baadaye atafuatia Mheshimiwa Hawa Ghasia na baadaye atakuja Mheshimiwa Taska Mbogo.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Serikali pamoja na Waziri wa Viwanda kwa hotuba yake nzuri ambayo inaleta changamoto na watu wote tunaipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili wana msembo wao, wanasema: “asiyesikia la mkuu, badala yake, huvunjika mguu.” Kwa nini nimesema hivyo? Nimesema hivyo kufuatana na mazingira ya maongezi. Tunapokaa hapa, ni kwa ajili ya kuchangia mawazo ya wananchi waliotutuma. Kwa hiyo, usiposikiliza mawazo ya wananchi waliotutuma, matokeo yake ni kwamba tutakuja kuvunjika miguu, utakaporudi kwenye uchaguzi unakuwa huna la kwenda kuongea kwa wapiga kura wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la viwanda. Bahati nzuri Wizara ya Viwanda ina Waziri makini na Watendaji wake makini. Tunasema hivyo kwa nini? Kwa muda mfupi tumeona Katibu Mkuu pamoja na Waziri wamezunguka sana katika maeneo kuangalia viwanda gani vimekufa na vipi viamshwe. Naomba sana na nataka nirudie kauli yangu ambayo nilitoa wakati

ule wa mipango, hapa hatupo kupendezana, tupo kwa ajili ya kujenga nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba mwaka huu tunataka Tanzania ya Viwanda, sikatai, naiunga mkono mia kwa mia; lakini naomba nirudie Mheshimiwa Waziri. Tunaposema viwanda, tunaviangalia viwanda vilivyokufa; na kama tunaangalia vilivyokufa, ni namna gani tutavianzisha viwanda vilivyokufa ili vije vijengwe viwanda vingine? Leo hii kiwanda cha *General Tyre* Arusha kingekuwa kinafanya kazi, Watanzania wengi wangukuwa wanaingia pale kufanya kazi, badala yake tunasema tunajenga viwanda. Tufufue *Arusha General Tyre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kiwanda cha kutengeneza magodoro Dodoma, kilikuwa kiwanda kikubwa na wananchi wa Dodoma walikuwa wanakitegemea sana, badala yake kiwanda hiki kimehamishiwa Dar es Salaam. Wale wafanyakazi ambao wangeweza kusaidia au wangeweza kupata kazi hapa, Dodoma watapata kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Tanga nimemsikiliza mchangiaji mwenzangu pale, katika mikoa ambayo ilikuwa ni mikoa ya viwanda; ilikuwa kama mikoa mitano au minne; Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Sasa hivi ndiyo imekuwa mikoa maskini kuliko mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Kiwanda cha Foma kimeondoka Tanga kinakwenda Dar es Salaam. Kwani Tanga hakuna wananchi? Leo hii Kiwanda cha Chuma, kilikuwepo Tanga, hakuna! Leo hii hata Viwanda vya Mkonge, wanafanya kuungaunga maskrepa ili kufungua viwanda vya mkonge ambapo mkonge mmeweka katika zao la biashara. Leo hii ninapokwambia, kuna viwanda vya mkonge, acha viwanda ambavyo vinataka kujengwa, wafanyakazi wake wanayanyaswa kama watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii shamba la Kwa Shemshi, kuna Kiwanda cha Mkonge ambacho wafanyakazi wametoka bara; *imagine* kama mimi Maji Marefu, nimetoka Songea, nilikwenda kule kama Manamba; na wengine wametoka Kigoma, wengine wametoka Usukumani, wamekwenda kule kama Manamba; lakini Manamba yake ilikuwa ni kwenda kufanya kazi. Leo hii shamba hilo linabadilishwa na watu zaidi ya watatu; wametumia kigezo gani? Wametumia sheria gani? Hatua ya mwisho, wafanyakazi wanafukuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninapomwambia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, shamba la Kwa Shemshi wafanyakazi wamefukuzwa na wanaambiwa hawalipwi na shamba hilo limeingiwa na Mwarabu, alipotoka hajulikani; kwa mkataba gani, haujulikani. Sasa mnaposema kwamba

Watanzania wanatakiwa wakafanye kazi, watafanya kazi gani? Sina maana kwamba Mwarabu ni wewe Mheshimiwa Keissy, hapana, naona unaanza kujitutumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naona huyu ananisumbua kwenye message zangu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nairidhia sana Serikali yetu hii, naomba sana tuangalie kwa mfano Kiwanda cha Urafiki Dar es Salaam, kilikuwa kina wafanyakazi chungu nzima, wako wawekezaji wa Tanzania wana uwezo, kama akina Mheshimiwa Bakhresa, Mheshimiwa Mengi, na Waheshimiwa wengine ambao wanafanya kazi vizuri, hakuna upungufu. Leo tunaleta Wachina, tunawaambia waje wafanye biashara. Badala ya kufanya biashara, wanafanya ni kiwanda cha kutengeneza mbao. Kilikuwa kiwanda cha kutengeneza nguo, kinabadilishwa kinakuwa kiwanda cha kutengeneza mbao. Ndiyo mikataba yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya kuendeleza viwanda vyetu ni nini? Maana yake ni kwamba viwanda ambavyo havifanyi kazi, ambavyo vilikuwa vimekufa vipewe watu ambao ni wazawa wenye uwezo wa kufanyia kazi, badala ya kutegemea majitu yanayotoka nje, yanakuja hapa kuchukua viwanda vyetu kwa ajili ya kukopa pesa zetu, wanapeleka huko, halafu wanatuambia Watanzania ni walalahoi. Nani mlalahoi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga kulikuwa kuna Kiwanda cha Saruji, hakipo; kulikuwa na Kiwanda cha Mbolea, hakuna; kulikuwa na Kiwanda cha Sabuni ambao ni Gardenia, hakuna; kulikuwa kuna Kiwanda cha Foma, kimehamishiwa Dar es Salaam; kulikuwa kuna Kiwanda cha Chuma, hakuna; kulikuwa kuna Kiwanda cha Matunda Korogwe, mpaka scraper zimetolewa; kulikuwa kuna kiwanda cha kutengeneza *ceiling board* kipo Mkumbara, lakini cha kushangaza kiwanda kile sasa kimekuwa cha kuchoma mkaa. Maskrepa yameondolewa yamepelekwa sehemu nyingine. Morogoro kulikuwa kuna viwanda chungu nzima, badala yake vinakuwa ni nyumba za kufugia mbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu zangu, Mheshimiwa Waziri yupo makini na bahati nzuri safari hii Mawaziri wote wapo makini. Mnafanya kazi kwa kujituma bila kuangalia itikadi ya Vyama. Naomba sana, tusianze kusema tunajenga viwanda vingine, nendeni Bagamoyo mkaanzishe Kiwanda cha Sukari. Hizi kesi tunazopata za sukari, hatutazipata. Nendeni kule APZ, nendeni Kigoma, kaangalieni Kiwanda kile cha Mawese, kimefikia wapi? Kaangalieni viwanda vya kutengeneza samaki, hebu tuangalieni ukanda huu wa Pwani, ni wapi kuna kiwanda cha kutengenza samaki? Vipo kule ziwani, Mafia hakuna.

Hebu tufanyeni. Tusifanya kazi kwa mazoea. Tufanye kazi kulingana na mazingira ya Watanzania, wanatakaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaseme haya kwa sababu naipenda sana Serikali yangu na ukimkuta mtu hapa kazi yake ni kuja na kuiponda Serikali na kuitukana, nafikiri ana upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacholilia sana ni kwamba tuifanye kazi yetu, wote tuungane, tusiangalie itikadi ya Vyama, tujaribu kukupa mawazo mazuri. Mheshimiwa Waziri, mtu anapokupa mawazo mazuri, usiangalie Chama chake, angalia huko tunakotoka, tuna matatizo gani? Tukisema tuangalie kwamba huyu anatoka sehemu nyingine, hatutapata nafasi nzuri ya kuwa na viwanda vizuri na bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kama kuna tatizo kubwa, Mheshimiwa Waziri anza kuangalia Mkoa wa Tanga ambao ulikuwa ni Mkoa wa viwanda. Viwanda ambavyo vipo, vinaweza kupokea vijana zaidi ya 20,000 badala ya kujenga viwanda vipya ambavyo havitakuwa na maana, havitatusaidia lolote wakati viwanda vya zamani vipo na majengo yake yapo. Hapa kwanza inapunguza gharama ya watu kuanza kutafuta utaratibu mwingine. Una viongozi wazuri ndani ya Wizara yako, wote ni watu watendaji. Nimewapitia kupitia Kamati yangu ya PAC, tumewaona ni wazuri. Naomba tuzitumie nguvu zetu kwa kushirikiana na sisi Wabunge ili mwone tutafanyaje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza kuna matunda, kiwanda hakuna. Kiwanda cha Gossage Tanga kimekufa; Sumbawanga huko ndiyo usiniambie, walikuwa na Kiwanda cha Maziwa, hakuna kitu. Sasa niliona niyaseme haya kwa sababu Kilimanjaro kulikuwa na Kiwanda cha Kahawa, hakipo tena; kulikuwa kuna Kiwanda cha Magunia hakuna; leo tunataka tujenge vingine. Tuanze vya magunia Kilimanjaro, tuanze kile cha Kahawa Kilimanjaro, tukimaliza hivyo ndiyo tunajenga viwanda vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, sitaki kupoteza muda sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ngonyani kwa kujali muda. Sasa hivi tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia, baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Antony.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uzima na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimshukuru na kumpongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kutuletea mwekezaji ambaye ana nia ya kujenga Kiwanda cha *Sulphur* kule Mtwara, namshukuru kwa hilo. Nampongeza kwa hotuba nzuri ambayo siyo tu imeandikwa vizuri, lakini pia amewasilishwa vizuri sana na kila mtu atakubaliana na hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema Serikali ya Awamu ya Tano ni ya viwanda na tunaunga mkono sana hilo. Ushauri wangu kwa Serikali yangu ni kuhakikisha tunatoa vikwazo vyote vile ambavyo wawekezaji wanakumbana navyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Mtwara, naomba nianzie huko. Tunaye mwekezaji ambaye ameonesha nia ya kutaka kujenga Kiwanda cha Mbolea na tayari wenzetu wa EPZA wamemuonesha eneo la kujenga kiwanda tangu mwaka 2015 Aprili, lakini mpaka tunapozungumza sasa hivi, anashindwa kuanza kujenga kiwanda kwa sababu Wizara ya Nishati na Madini wameshindwa kumhakikishia upatikanaji wa gesi kwa zaidi ya miaka minne ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi wakati watu wa EPZA wanakuja kumuonesha eneo, walikuwa hawajazungumza na Wizara ya Nishati na Madini? Mwekezaji anaomba uhakika, kiwanda kile kitachukua zaidi ya miaka minne kukamilika, anaomba ahakikishiwe baada ya miaka minne kupewa gesi, mpaka leo Wizara ya Nishati na Madini haijampa uhakika kama watampa hiyo gesi. Kwa kweli kama Mwanamtwara, nasikitika sana, kwa sababu kiwanda hiki ni cha mfano. Mwekezaji alikuwa anafanya ubia na Halmashauri zote za Mkoa wa Mtwara na tayari tulishakubali, eneo wamepewa, lakini gesi hajapewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja, atueleze amefanya juhudi gani za kumsaidia mwekezaji huyo kupata gesi ili Kiwanda cha Mbolea ambapo nchi inaagiza mbolea kwa zaidi ya asilimia 90, lakini anakuja mwekezaji anataka kujenga hapa, tunamwekea vikwazo. Hivi tuelewe kuna lengo gani ambalo sisi wengine hatulifahamu? Haiwezekani gesi itoke Mtwara lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza hakuna kiwanda hata kimoja kimepewa gesi katika mkoa ule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka kulichangia, ni suala la maeneo ya EPZA. Kama kweli tunahitaji kuwa na Serikali ya Viwanda, ushauri wangu ni kuiomba Serikali itafute fedha, ilipe fidia maeneo yote ambayo wanakusudia kuwa ni maeneo ya uwekezaji kwa maana EPZA na SES ili wawekezaji wanapokuja wasipate usumbufu wa aina yoyote wa kutafuta maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waziri atakapokuja atuambie, ana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba maeneo ya EPZA yote yanalipwa fidia kwa wakati ili yawe tayari, yasafishwe, yawekewe uzio tayari akija mwekezaji unamwonesha kwamba eneo la kuwekeza ni hili hapa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianzisha ushuru wa korosho ambayo inasafirishwa ghafi kwenda nje, yaani *export levy* ili kuhakikisha kwamba, badala ya wafanyabiashara kupeleka korosho nje, wazibangue hapa. Lengo la ushuru ule ilikuwa ni kuwakatisha tamaa wale wanaopeleka korosho bila kuzibangua ili wawekeze viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze tangu tumeanzisha *export levy* mpaka sasa hivi ni viwanda vingapi vimeweza kujengwa. Kama hakuna kiwanda chochote, ameshauri nini, kwamba kodi ile iongezwe kwa kiasi gani? Wasiwasi wangu ni kwamba, labda ile *export levy* ni ndogo kiasi kwamba hakuna sababu, mtu anaweza akalipa na bado akapeleka nje kuliko akizalisha korosho ndani ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulichangia ni suala la kulinda viwanda vyetu. Kama tumeamua kweli kuwa nchi ya viwanda, ni lazima suala hilo liende sambamba na ulindaji wa viwanda vyetu vya ndani. Tanzania tuna uwezo wa kujilisha au kujitosheleza sisi wenyewe kwa mafuta ya kula, tuna uwezo wa kuzalisha alizeti. Tunayo Mikoa kama Singida, Tabora, Dodoma na kanda nzima ya kusini huku, tuna uwezo wa kuzalisha alizeti na kuweza kuzalisha mafuta ya kujitosheleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yatategemea iwapo tutakuwa tumeweka sheria ya kulinda viwanda vyetu. Kuna mafuta mengi sana ya kula yanatoka nje, wakisingizia kwamba mafuta hayo hayajakamilika, yaani yanakuja kusafishwa huku kwetu, lakini kimsingi yakifika hapa wanakuja tu kuya-*park* na kuanza kuyauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Viwanda na Uwekezaji, watuambie wana mikakati gani ya kulinda viwanda vyetu vya mafuta ya kula hapa nchini? Wenzetu Uganda wanafanya, Rwanda wanafanya, kwa nini sisi tuwe ni eneo ambalo mtu yeyote anayetaka kuleta mafuta ya aina yoyote ambayo hatuna hata uhakika wa usalama wa afya zetu, tunaruhusu watu kufanya hivyo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumsikia Mheshimiwa Waziri anatuambia katika upande wa viwanda vya mbolea na korosho kule Mtwara anatuletea viwanda vingapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, namwomba tu Mheshimiwa Waziri ajiandae kuja kuniambia kiwanda kile cha mbolea ana mikakati gani au anamwezesha yule ili aanze kujenga kile kiwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Hawa Ghasia. Tunaendelea na Mheshimiwa Anthony Komu na baadaye atafuata Mheshimiwa Taska Mbogo akifuatiwa na Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi.

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nianze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa masikitiko kwamba kwa kweli ukiitazama hii hotuba yake kuanzia mwanzo mpaka mwisho pale anapokwenda kuomba pesa. Ukijiuliza kwamba ni kitu gani kimoja ambacho kitakuwa kimekamilika baada ya kwisha mwaka huu wa fedha ambao tunauzungumzia, hakuna hata kimoja kitakachokuwa kimekamilika kinachoweza kutupeleka kwenye uchumi wa viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge na Serikali kwamba tunapojadili haya mambo, tuwe *serious* kidogo. Tuangalie kwamba ni wapi tunataka kupeleka nchi hii? Kama ni suala la kujaribu kuwa *masters* wa kila kitu halafu mwisho wa siku tunajikuta kwamba we *are master of none*, kwa kweli tutakuwa tunawadanganya wananchi wetu. Hilo ndilo ninaloliona, kwa sababu tunasema kwa mfano tunataka kuwa na viwanda vya kimkakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kwa miaka nenda rudi kuhusu Mchuchuma na chuma cha Liganga. Tunasema hivi ni viwanda vya kimkakati, lakini ukienda kuangalia fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kwenda kufidia ili watu wapishe maeneo yale kwa ajili ya ujenzi. Ni kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu; lakini tunasema mwakani miezi mitatu ijayo tutaanza uzalishaji. Huu ni uongo! Haya ni maigizo! Hizi ni nyimbo! Sasa nyimbo za aina ya namna hii ni lazima tuachane nazo tuzungumze vitu ambavyo ni *tangible*, yaani vitu ambavyo vinashikika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba hivi ni viwanda vya kimkakati, lakini *share* zetu sisi kwenye chuma cha Liganga na Mchuchuma tuna *share* 20. Sasa *share* 20 nafasi yetu ya ku-*influence* mambo kwenye hiyo miradi, iko wapi? Kwa hiyo, bado tunakwenda kucheza kwenye mikono ya wabia wetu ambao ndio watakaokuwa na *influence*. Kwa hiyo, hatuwezi kujidai kwamba hivi ni viwanda vya kimkakati wakati hatuna mkakati wowote wa kuhakikisha vinaanza, hatuna makakati wowote wa kuhakikisha kwamba, tunavimiliki ili tuwe na *influence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, Waziri atakapokuja hapa atuambie ni mikakati gani ambayo ni *tangible* (inayoshikika), ambayo ni mahususi ya kutufanya kweli twende kumiliki hayo maeneo ambayo yanaitwa ni ya kimkakati na ni lini haya maeneo kweli kwa maana ya fedha kwa maana ya bajeti yanaweza yakaanza na tukaona hapa kweli tunapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kwenda kwenye uchumi wa kati, wakati huo huo tunazungumza habari ya kuwa na *private sector* yenye nguvu, lakini ukiangalia Serikali yetu ndiyo ambayo inajitahidi kwa nguvu zake zote kuua *private sector*. Ukienda kwenye deni la Taifa, unakuta tunadaiwa zaidi ya shilingi triloni 29 sijui, kama sijakosea *figures*, lakini 1.3 *trillion* ni madeni ya ndani ambapo ni Wazabuni mbalimbali waliofanya kazi na Serikali, watumishi wa Serikali na Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokwenda kwenye huu uchumi wa kipato cha kati tunaenda na nani, kama Serikali kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba hawa wazawa hawanyanyuki? Mwaka 2015 kuna Mhandishi mmoja alijiua kwa sababu kampuni yake ililemewa na madeni ya Ukandarasi, kwa sababu ya Kandarasi mbalimbali alizofanya kwenye Serikali, akajiua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kuwe na *affirmative action* ya kuhakikisha kwamba tunawanyanyua wazawa. Ukienda kwenye ile sheria ya mwaka 2004 ya kuwezesha wazawa waweze kushiriki kwenye uchumi na yenyewe ina walakini mkubwa. Naona Waziri Muhongo hayuko hapa, lakini mwaka 2015 nafikiri kuna mtu mmoja alitaka kuwekeza kwenye gesi na ni mtu maarufu, Dkt. Regnald Mengi akaambiwa yeye *level* yake ni uchuuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri leo atuambie, ili uwe mzawa unayeweza kupewa hadhi ya kuwekeza kwenye vitu ambavyo siyo vya uchuuzi, unapaswa uwe na uchumi wa namna gani? Kwa sababu uchumi wa Mengi kwa jinsi tunavyojua, ni uchumi mkubwa. Kama ni fedha anaweza akawanazo nyingi; kama ni mali zisizohamishika ambazo zinaweza kuwekwa dhamana, anazo ambazo watu wanazifahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama huyo anaambiwa kwamba ni mchuuzi, akachuuze, kwa vyovyote Watanzania walio wengi watakuwa wamekwazika sana na watakuwa wanaogopa kujitokeza kwa sababu watajipima, hivi mimi na Dkt. Regnald Mengi, naweza kwenda? Inawezekana ndiyo maana Mheshimiwa Waziri hapa kila siku anahamasisha watu wajitokeze, hawajitokezi kwa sababu havijatolewa vigezo vya Watanzania ili washiriki kwenye uwekezaji wanapashwa wawe na nguvu zinazofanana namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na hili naweza nikashika mshahara wako kama hautokuja vizuri. Kwa sababu ni suala

la kiseru, utuambie ni uwezo wa namna gani unatakiwa ili Watanzania nao waweze kushiriki katika kuwekeza kwenye uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *laxity* ya Serikali ya CCM, yaani uzembe wa Serikali ya CCM na kutokufuatilia mambo kwa Serikali ya CCM. Kwa sababu tumeambiwa hapa viwanda vimekufa, lakini viwanda hivi vimekufa na Mheshimiwa Waziri ametuambia katika taarifa zake mbalimbali kutoka kwenye Kamati kwamba viwanda vingine vilitumika kama dhamana kukopa kwenye mabenki, lakini mikopo hiyo haikwenda kutumika kwa ajili ya kuendeleza viwanda, ilitumika kwenye vitu vingine, Serikali ilikuwa wapi? Serikali ilikuwa wapi wakati mtu anakopa fedha akasema anakwenda kufua kiwanda akaenda akafanya mambo mengine ya kwenda China akaenda kuchukua bidhaa kwa ajili ya uchuuzi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba, kama tabia hii haitabadilika, kama mienendo ya namna hii haitabadilika, bado tutaendelea kupata matatizo kwa sababu hizi benki ambazo tunataka kuanzisha, zitaanzishwa, pesa zitawekwa kule, watakopa tena, kwa *laxity* hii hii ya Serikali za CCM, mambo yatakuwa yale yale, *business as usual*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuangalie ni namna gani. Limezungumzwa suala la kulinda viwanda vya ndani, *well and good*, lakini unavyozungumza suala la kulinda viwanda vya ndani, usiangalie tu uagizaji wa bidhaa kutoka nje; jiulize vile vile ni kwa nini bidhaa za nje zinakuwa bei rahisi? Zinakuwa bei rahisi kwa sababu mazingira yetu ambayo kimsingi ni jukumu la Serikali kuyafanya yawe yanayofanya viwanda vya kwetu vizalishe bidhaa zinazoweza kushindana kibeji, ni magumu. Watu wamechangia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Peter Surukamba asubuhi alizungumza akaorodhesha...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umemalizika, naomba ukae. (Makofi)

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Taska Mbogo!

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza nasimama mbele ya Bunge hili Tukufu, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na leo hii mimi Taska

Restuta Mbogo nimesimama hapa nachangia hoja. Napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Mkoa wa Katavi hususan akinamama walionichagua na kuniwezesha mimi kuwa Mbunge wa Viti Maalum ndani ya Bunge hili Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote wa vyama vyote mliomo humu ndani, mliofanikiwa kuja ndani ya Bunge hili Tukufu. Napenda nimpongeze Rais Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na napenda nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kupata ushindi mkubwa na kuongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwa hotuba yake nzuri, lakini ninayo machache ya kuchangia kuhusu hotuba yake. Kwanza kabisa, napenda nichangie suala la viwanda. Tunaposema kwamba tunakwenda kwenye nchi ya viwanda tunatakiwa tuwe na maji ya kutosha, tuwe na miundombinu bora kama barabara, reli ambazo zinapitika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano mdogo tu, kule kwetu Katavi hatuna miundombinu ya barabara mizuri, reli yenyewe ni ya kusuasua, siyo reli ambayo inaweza ikabeba mzigo mkubwa wa kiwanda. Kwa maana hiyo ni kwamba, hata kama kiwanda kinajengwa kule, bado tutakabiliwa na miundombinu mibovu ambayo iko katika Mkoa wetu wa Katavi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katavi inaunganika na Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma, lakini huwezi kusafirisha mazao kutoka Mkoa wa Katavi kuyapeleka Mkoa wa Kigoma kwa barabara kwa sababu barabara hiyo haipitiki, ni barabara ya vumbi.

Pia huwezi ukasafirisha mazao ukayatoa pale Mkoa wa Katavi ukayapeleka Mkoa wa Rukwa kwa sababu barabara ile ni ya vumbi ina vipisi vipisi tu vya lami ambavyo havijakamilika. Kwa hiyo, kama tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, nchi yetu ya Tanzania tunapaswa pia tuangalie miundombinu hiyo iwe bora, maji yawepo ya kutosha. Kule Katavi ni pale Mjini tu ambako ndiyo kuna maji, lakini sehemu nyingine wananchi wanatumia bado maji ya visima. Kwa hiyo, naomba suala hili la maji pamoja na barabara liangaliwe kabla ya hivyo viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mkoa wetu wa Katavi ni Mkoa ambao hauna kiwanda hata kimoja; na tangu nchi hii imeumbwa hakujawahi kujengwa kiwanda hata kimoja, hata kiwanda cha kiberiti hakuna, wala cha sindano. Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Waziri anapokuja kutoa ufafanuzi, labda atuambie kwamba kule Katavi ataanza kutujengea kiwanda cha

kutengeneza nini? Kwa sababu Katavi tunazo fursa nyingi; sisi ule Mkoa tunayo asali ya kumwaga, naweza nikatumia neno “ya kumwaga.” Tunazo karanga nyingi sana; tunayo tumbaku; tunao mpunga unalimwa. Ina maana mchele kule kilo ni shilingi 1,200/=, tunayo mahindi ambayo mpaka yananyeshewa na mvua nje. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Ndiyo, ndiyo!

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie utaratibu wa kujenga viwanda vinavyohusiana na hayo mazao. Kwa Mfano, Serikali ikijenga Kiwanda cha Kuchakata Asali, asali itapakiwa vizuri, itapelekwa nje. Asali inaleta pia nta; ile nta ni zao zuri sana ambalo likipelekwa nje ya nchi linaweza likaleta mapato kwa nchi yetu ya Tanzania. Nta inatumika kwa mambo mengi; inatumika kutengeneza mabegi, viatu; ina manufaa mengi ambayo ni pamoja na gundi zinazotumika maofisini. Mazao hayo yangeweza kuongeza kipato cha mwananchi wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye suala la tumbaku; inalimwa kule Katavi, Tabora lakini Kiwanda cha Tumbaku kipo Morogoro. Sasa inamkatisha tamaa mwananchi kulima tumbaku. Tumbaku yenyewe ina *grade 72*. Yule *classifier* anapofika pale anai-*grade* ile tumbaku, anaweza akamwambia mtu kwamba hii tumbaku yako nanunua kilo moja kwa sh. 500/=, lakini kama Kiwanda cha Tumbaku kingekuwa karibu, kwa mfano, kingejengwa Tabora au hapo Katavi, kingeweza kuwanufaisha wananchi wote ambao wanalima hilo zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Mheshimiwa Waziri angefikiria suala la kuleta kiwanda cha kutengeneza mafuta kama ya alizeti. Tunalima alizeti sana kule, pia tunalima karanga nyingi, tusingeweza kuagiza mafuta ya nje hayo ambayo yanakuja yamechakachuliwa hujui hata kama ni mafuta yametengenezwa na nini, unaambiwa tu ni *vegetable oil*. Tungeweza kutumia mafuta ya alizeti, tukatumia mafuta ya karanga na wananchi wakapunguza *cholesterol* mwilini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mikoa yetu ya Katavi, Tabora na Rukwa ni Mikoa ambayo ina ardhi safi sana, ambayo kuna sehemu nyingine ardhi ile tangu imeumbwa na Mwenyezi Mungu hamna binadamu ambaye ameweza kukaa. Naomba Mheshimiwa Waziri wawekezaji wanapokuja, jaribuni kuwapeleka pia mikoa ya pembezoni. Najua mnatuambia kwamba ile ni mikoa ni ya pembezoni ya mwisho wa dunia, lakini ni mikoa ambayo inazalisha mazao mengi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanapokuja kutaka kuwekeza Tanzania msiwape tu ramani za kusema kwamba wawekeze Dar es Salaam au

wawekeze Arusha, wapelekeni pia na mikoa ya pembezoni. Mikoa ya pembezoni kwa mfano kule Katavi, hiyo ardhi mwekezaji anapokuja, akichukua akalima mahindi yake akatengeneza unga na pia hayo mahindi akatengeneza mafuta ya mahindi ambayo ni mazuri sana kwa kupikia chakula, ambapo pia mwekezaji angeweza kuongeza pato na kuweza kuajiri vijana na kupunguza matatizo ya vijana ambao hawana kazi kwa sababu kiwanda kitakuwa pale, kitaajiri wale vijana ambao watafanya kazi pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi pia unazo mbao nyingi. Hili tatizo la Madawati ambalo sasa hivi Serikali inakabiliana nalo, lingeweza kutatuliwa. Kwa mfano, kama Serikali ingekuwa imewekeza ikaleta Mwekezaji mmoja akajenga Kiwanda cha Mbao kule Katavi ambapo kunapatikana mbao nzuri sana ya mninga ambayo hata mdudu anaogopa kuitoboa, ina maana madawati yangetengenezwa kwa wingi kwa sababu mbao zinapatikana nyingi sana, tungeweza kuondoa tatizo la madawati ambalo linawakabili wanafunzi na watoto Tanzania hii yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbao ni nyingi sana kule Katavi, Tabora na Rukwa; pia asali ni nyingi sana maeneo hayo. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja na majumuisho atuambie ni lini atatuletea hivyo viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba hao Maafisa Biashara ambao wameajiriwa kwenye Ofisi za Halmashauri, wajaribu kuwa wanaenda kutoa elimu ya biashara kwa wananchi, kwa sababu muda mwingi wanautumia ofisini na kutumia *computer*. Wanatakiwa Waonane na wananchi wawape elimu ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wao wanakuwa wana-*chat* kwenye *computer*, wanataka kufanya kazi kwa mtandao, lakini mwananchi wa kawaida hayuko kwenye *computer*, anataka asikilize ile elimu ya biashara na hiyo elimu iweze kumsaidia yeye na kuweza kujiinua kwenye biashara yao. Kwa sababu pia wao wanalipwa mshahara kwa ajili ya kuwa Maafisa Biashara wa Halmashauri, lakini huwa siwaoni wakitoa hiyo elimu ya biashara kwa wananchi, wanatumia muda mwingi kukaa ofisini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ni kengele ya pili, muda wako umekwisha.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. ZAINAB N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia leo katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ameniwezesha leo nami niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli; nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu; nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na timu yake yote ya Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo wanatukonga nyoyo zetu Watanzania, wametuonesha umahiri wao na kwamba wana ari kubwa ya kulitumikia Taifa na wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyingine, naitumia nafasi hii pia kuwashukuru wale wote ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia mimi uwepo wangu au wamerahisisha mimi Zainab Mwamwindi kuwepo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Nawashukuru kwa namna ya pekee na nasema Mungu awabariki sana, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inahitaji kwenda kwa kasi na ari kubwa. Tunasema tunahitaji Tanzania yenye viwanda. Kilimo kinatajwa kama uti wa mgongo wa nchi yetu na kinatajwa kwa sababu ya kwamba hakuna hata mmoja kati yetu Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ambaye hatujui kwamba bila kilimo nchi haitasonga mbele. Ni lazima tulime na tuweze kupata mafanikio mazuri, lakini pia ndoto yetu ya kuwa na viwanda vingi itatokana na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Mkoa wa Iringa. Mkoa wa Iringa kuna Kiwanda kikubwa cha Karatasi cha Mgololo. Kiwanda kile kinazalisha karatasi, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake, atueleze au awaeleze wananchi wa Tanzania kwamba ni kwa nini Kiwanda cha Mgololo kinachotengeneza karatasi soko lake halipo lakini pia karatasi zake hazipatikani sokoni na hata kama zitapatikana, karatasi zake huwa ghali sana? Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Mwijage naomba atusaidie sisi wananchi, ni kwa nini Tanzania hii tunatengeneza karatasi lakini kwa bahati mbaya sana karatasi zile zikipatikana bei inakuwa ghali kuliko zile ambazo zinaingizwa kutoka nchi za nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la kinu cha kusindika au kusaga sembe kilichoko Manispaa ya Iringa. Ni kiwanda ambacho kinasaga sembe. Inawezekana kikawa ni kiwanda pacha, kinahusiana na kilimo vile vile. Kiwanda kile kilikuwa kinafanya kazi vizuri sana huko nyuma wakati wa NMC lakini mara baada ya Shirika la NMC kufa, kiwanda kile sasa kimekuwa hakifanyi kazi kama ambavyo inatakiwa. Pia kuna vijana wetu na akinamama pia wapo ambao nao walikuwa wanapata ajira na wengi wao wakiwa ni akinamama ambao ndio wanaotunza familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, naomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie katika kiwanda hiki, Serikali iweke mkono wake kwa asilimia mia moja ili iweze kuwakomboa wananchi wa Mkoa wa Iringa ambapo wananchi wa Mkoa wa Iringa hasa ni wakulima wa mazao ya mahindi, wanazalisha mahindi kwa kiwango kikubwa sana, lakini mara nyingine tunakosa soko la kupeleka mahindi, tukauze wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, Serikali itie mkono wake kwa asilimia mia moja katika kiwanda kile ili tuweze kukuza ajira kwa vijana wetu, lakini pia wakulima wa Mkoa wa Iringa na mikoa jirani waweze kunufaika na kiwanda kile kwa kuuza mahindi yao pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mama. Vazi la mwanamke yeyote wa Kitanzania ni Kanga. Namwomba Waziri wa Viwanda atusaidie sisi wanawake wenye maumbile kama mimi, tumekuwa sasa hatuvai kanga, kwa sababu Kanga zinazidi kuwa ndogo siku hadi siku na akinamama wamenituma nije niseme katika Bunge lako hili. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, kanga zilizopo sasa zinatoshwa kuvaa wasichana wadogo na Tanzania hii wanawake wameshiba, wako vizuri, wanahitaji kuvaa kanga wapendeze watoke katika shughuli mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, hilo aliwekee kipaumbele sana maana wanawake ndiyo jeshi kubwa na tegemeo la Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya kwanza leo kuchangia, naomba kusema naunga mkono hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwamwindi. Tunaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema na baadaye atafuatia Mheshimiwa Sabreena Sungura akifuatiwa na Mheshimiwa Henry Amon.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Kitabu cha Mithali ambacho ameandika Mfalme Suleiman, hii ni sura ya 30 mstari wa 18 mpaka 19 anasema ifuatavyo: “Kuna mambo matatu yaliyo ya

ajabu kwangu. Naam, kuna manne nisyoyafahamu. Mwendo wa tai katika hewa, mwendo wa nyoka juu ya mwamba, mwendo wa merikebu katikati ya bahari na mwendo wa mtu pamoja na msichana."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfalme Suleiman angekuwa anaandika, angeandika; "na utaratibu wa uchangiaji wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi." Mnaikataa bajeti muda wote wa kuchangia, halafu mwisho mnaunga mkono hoja. Hili jambo pia lingemshangaza Suleiman. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwuliza Mheshimiwa Msigwa hapa, hivi sisi tukija upande huo na nyie mkaja upande huu, tukabadilishana Vyama lakini *status quo* ikabaki hivyo hivyo, mkabaki Mawaziri, Wabunge lakini mkawa CHADEMA na sisi CCM, mngeweza kubadilisha maisha ya Watanzania? Nikapata jibu msingeweza kwa sababu kimsingi tatizo siyo Chama chenu, ni akili zenu. Msingi kabisa, ni *attitude*. *Attitude...*

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde!

MBUNGE FULANI: Umeanza kutukana siyo eeh? Umeanza!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo matusi!

WABUNGE FULANI: Umeanza eeeh?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema!

MBUNGE FULANI: Umeanza eeh?

MBUNGE FULANI: Anaanza huyo eeh?

MBUNGE FULANI: Futa kauli yako mara moja wewe!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, naomba katika maongezi yako utumie lugha nzuri. Ukisema akili zenu, tujue akili zipi. Ina maana hakuna akili ama vipi? Kwa hiyo, naomba tuseme hivyo.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *attitude* siyo tusi; siyo tusi!

MBUNGE FULANI: Sasa *attitude* ni nini?

MBUNGE FULANI: Kuna *negative*!

MBUNGE FULANI: Kwani *baby* tusi?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MBUNGE FULANI: *Baby* halikuwa tusi. *Baby* halikuwa tusi.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi *attitude* ni tusi, naliondoa hilo neno "*attitude*" kwasababu nyie mnasema ni tusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti leo tunaongelea habari ya viwanda..

MBUNGE FULANI: Akili siyo *attitude*!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachopigiwa kelele hapa ni *opportunity*. Wabunge wote humu wa Upinzani na wa Chama Tawala, wanapigia kelele *opportunities* ambazo walipaswa kuzi-cease na ndiyo sababu nilipoanza na neno "*attitude*" mlipaswa kusubiri. Wabunge wote hapa...

MBUNGE FULANI: Ulisema akili wewe! Wewe nani asiyejua *attitude*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, naomba ukae. Naomba fuelewane. Umetumia neno akili ndiyo maana hawa huku wanalalamika. Kwa hiyo, naomba ufute hilo neno akili.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, akili ni tusi?

MBUNGE FULANI: Futa neno akili. Nani hana akili?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta neno "akili."

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la viwanda nchi hii na wala Serikali haiwezi kuleta viwanda vyote ambavyo vitaleta *transformation* katika Taifa hii. Ukienda nchi zote zilizoendelea, *transformation* ya viwanda imeletwa na *private sector*. Kwa hiyo, kama *private sector* ndiyo imeleta *transformation* ya viwanda, Waheshimiwa Wabunge wanaodai Serikali ya nchi hii lazima ilete viwanda, Wabunge wao ni lazima waanze kujua tofauti ya *liability* na *Assets*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge wanachaguliwa wapya. Anachaguliwa Mbunge mwezi wa Kumi; mwezi wa Kumi na Mbili ananunua gari ya shilingi milioni 400 halafu *full back position* ya kuendesha gari ile ni posho ya

kikao. Tatizo hapa siyo kiwanda! Gari moja ya thamani ya shilingi milioni 400 ni viwanda nane China.

Kwa hiyo, tunapoongelea suala la *transformation* ya viwanda siyo Serikali peke yake, ni pamoja na *transformation of the attitude*. Wananchi kutoka kwenye *negative mentality* kwenda kwenye *positive mentality* na hiki ndicho nilikuwa nataka mwelewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi mnavyosema hapa, havitakuja. Mtaonea Wizara hizi! Riba leo kwenye *Commercial Bank* ni asilimia 20 mpaka 22. Ukichukua shilingi bilioni moja Benki leo, utalipa riba ya shilingi milioni 220 kwa mwaka, maana yake ni takribani shilingi milioni 20 kila mwezi. Ndiyo sababu wananchi wengi ama watu wengi hawaingii katika mfumo wa *investment*, wanaenda katika mfumo wa *buy and sell* kwa sababu kununua kiwanda, kifike, ukijenge, kianze kufanya kazi upate leseni, ni jambo linachukua takribani zaidi ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki zetu siyo rafiki na urafiki huu unaondoka kwa sababu *base rate* ya *BOT* ni asilimia 16, maana yake Benki zote zinaanza kuanzia asilimia 16 kupanda juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ya kufanya *transformation* ya viwanda katika Taifa hili, ni lazima Wizara ya fedha na *BOT* waende wakashushe riba kwa watu ambao wanataka kufanya *investment* kwenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *investment* ya Viwanda haiwezekani. Leo ukitaka kufungua Kiwanda, unahitaji kwenda kuchukua fedha Benki, utaenda kuweka *property* yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wengi wanakufa na *pressure* kwa sababu ya riba. Ili viwanda nchi hii vifanikiwe, nendeni mkaongee. Wizara ikaongee na Wizara ya Fedha na Benki Kuu. Riba ya viwanda lazima iwe tofauti na riba nyingine zote katika uwekezaji. Sasa *attitude* haitawakwaza tena. (Makofi/Kicheko)

MBUNGE FULANI: Wameelewa! (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri, kuhusu *General Tyre*; niliwashauri kwenye Kamati, wakati *General Tyre* inajengwa pale palikuwa ni pori, leo *General Tyre* iko katikati ya *residential*, huku kuna nyumba za *PPF*, nyuma kuna mtaa wa Lolieni. Niliwaambia njooni tuongee na Halmashauri ya Jiji na mimi na-control lile Jiji, kila kitu ni mimi Kamati ya Mipango Miji ni mimi, Meya ni mimi kila kitu ni mimi. Kwa sababu mnataka shilingi bilioni 68 ili m-take off,

mkija Arusha kuliko lile eneo muendeleo kulazimisha kuweka kiwanda pale njooni tuwape heka 100 kilometa 20 kutoka Arusha Jiji na lile eneo muende mkatengeneze iwe ni *commercial areas*, mtengeneze *proper residential*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnawaza mkauza eneo la *General Tyre* kwa zaidi ya bilioni 30 ya Kitanzania, ikawa ni ubia wenu mkatafuta *partner*, lakini leo Mheshimiwa nakushauri ukifufua kiwanda cha *General Tyre* na mitambo iliyopo, tairi moja utauza shilingi milioni 10, ile mitambo ni mitambo ya siku nyingi, inatumia umeme mwingi na umeme wenyewe huu wa kusuasua, matairi yamebadilika, *moulding* zimebadilika. Leo kuna tairi za waya, pale kuna tairi za nyuzi, ni bora hiyo fedha mkaitumia kufanya *research* na *analysis*, mjue ni kitu gani mnataka kufanya kwenye kiwanda kile lengo siyo kufungua kiwanda, je, kiwanda kitakuwa *effective*? Lengo ni kiwanda kitakuwa *effective*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri njoo Arusha tukubaliane tuwatafutie heka 100 nje ya Mji, tupeni lile eneo tuwatafutie shilingi bilioni 30, pale fedha iko! Lakini leo ukiweka kiwanda cha *General Tyre* pale na usitoe nje ya Mji pale ni *residential*, barabara ni nyembamba, unaingiaje kupeleka *raw material*? Unaingiaje kutoa *raw material*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakushauri sana Mheshimiwa Waziri ukitaka kuleta *transformation* kwa *General Tyre* lazima uchukue mwelekeo ninaokuambia mimi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya nchi hii ni midogo, hakuna *purchasing power*. Leo mtu kuingia *supermarket* ni *prestige*, leo mtu akionekana anaingia *supermarket* nchi hii ama akipanda ndege ni *issue* yaani leo kupanda ndege *it's a dream*! Kwa hiyo, ili muweze kutengeneza viwanda na muweze kutengeneza wawekezaji waone kwamba nchi hii unaweza ukawekeza viwanda lazima kuwepo na *purchasing power*. *Purchasing power, number one* inakuwa *created* na mishahara ya Serikali pamoja na *private sectors*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba sana kwamba Serikali kama inataka kuona viwanda vinakuwepo katika Taifa hili ni lazima Serikali ifikirie kuongeza mishahara ya wafanyakazi. Lazima Serikali ifikirie kuongeza mishahara bora ya wafanyakazi ili kuwepo na *purchasing power*, siyo kupunguza kama ambavyo mnafikiria sasa, mtu wa shilingi milioni 30 apewe shilingi milioni 15. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi hapa kila siku anafuta *title* na anatangaza! Mnafikiri mnasaidia nchi, msiwanyang'anye watu ardhi mkatangaza. Mwekezaji mnayemuita kuja kuwekeza kwenye kiwanda halafu anasikia kuna mtu amenyang'anywa heka 3,000 huyo mtu atarudia Dubai kama alikuwa ana-*connect* ndege. Msinyang'anye watu ardhi. Hata kama

mkinyang'anya watu ardhi, imekaa muda mrefu msifanye *publicity* kwa sababu ina *threat* wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza. Huwezi kuwekeza kwenye viwanda kama huna ardhi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo dakika tatu zilikuwa zimebaki kwa sababu ya zile kelele kelele.

MWENYEKITI: Dakika zako zimemalizika, nakupa nusu saa.... aah! nusu dakika. (Makofi/ Kicheko)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa hiyo nusu saa, Mungu akubariki sana. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa nimekupa nusu dakika.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TRA. Wafanyabiashara wa nchi hii wakiwaona TRA wanawaogopa kama wameona *Field Force*. Ili wafanyabiashara wawe na malengo ya kufikiria maono makubwa ni lazima TRA ijenge *attitude* ya kuwa na urafiki na wafanyabiashara na siyo wakali kwa wafanyabiashara. Viwanda na Biashara ni Wizara ambayo imesambaa sana, kilimo kiko ndani yake, Wizara ya Fedha iko ndani yake, kila kitu. Lakini hawa ili waweze kufanikiwa lazima muwape nguvu zaidi ya kufanya *connectivity* na hizi Wizara nyingine kwa ajili ya *harmonize* shughuli zao za kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mazingira leo anaweza akatoka hapa ama Naibu Waziri wa Mazingira akaenda Tanga akafunga kiwanda kwa sababu tu anataka aonekane kwenye tv bila kum-consult Waziri wa Viwanda na Biashara.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Sabreena Sungura halafu atafuata Mheshimiwa Henry Amon.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwa kuwa ni mchango wangu wa kwanza napenda kutoa shukurani za dhati kwa chama changu kwa kunirudisha Bungeni kwa awamu nyingine ya pili, ahsanteni sana ninawaahidi ukombozi mpaka pale nchi yetu kitakapoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili; napenda kuchukua fursa hii kulaani vitendo vya kikatili na udhalilishaji vinavyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi vya kupiga, kudhalilisha na kuburuza Wabunge ndani ya jengo

takatifu, jengo linalotunga sheria, jengo linalofanya maamuzi katika nchi hii. Ni kitendo cha udhalili na ni laana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala zima la viwanda na biashara. Kinachoendelea humu ndani ni maigizo. Ni ndoto za alinacha kusema mtafanya mapinduzi ya viwanda na biashara ilhali zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania hawana umeme, hawana maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ni Mkoa wangu wa Kigoma, Mkoa ambao tunapata umeme kwa kutumia jenereta ambazo haziwezi ku-run heavy industry. Kwa hiyo tukisema tutaanzisha viwanda, alipita Mheshimiwa Rais Magufuli kwenye kampeni akasema kwamba atahakikisha Dangote anakuja kufungua kiwanda cha cement Mkoa wa Kigoma, swali langu ni kwamba kiwanda hicho kitafunguliwa kwa umeme upi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma hauna barabara za maana kwa maana ya barabara za kupitika. Leo hii naongea kuna wananchi walikwama zaidi ya saa 48 njiani kwa ubovu wa barabara. Mkoa hauna reli yenye standard gauge, mvua zikinyesha inakuwa ni shida. Mkoa hauna ndege za uhakika, Mkoa hauna boti ama meli za kisasa ambazo zitatusaidia kupeleka bidhaa mbalimbali katika nchi nne ambazo zinaungana na Mkoa wetu wa Kigoma. Ni viwanda gani hivyo mtakavyoleta kujenga, nchi imejaa urasimu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia Mheshimiwa Rais anasema kwamba kuna mishahara hewa, lakini nafikiri hajapewa information za kutosha, siyo tu mishahara hewa kuna fidia hewa nchi hii. Nimeshuhudia baadhi ya wananchi maeneo mbalimbali wakilipwa fidia hewa, mtu anahonga shilingi milioni 10 anapewa milioni 60. Sasa kama kuna fidia hewa hakuna kiwanda kitakachojengwa katika mazingira hayo, mnajidanganya na Serikali inajua kama fidia hewa zipo lakini kwa kuwa ni miradi yenu hamchukui hatua zozote za kudhibiti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu mitaji. Ni wajibu wa Serikali kuwawezesha wananchi wake kupata mitaji ya kuendeleza viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa. Mheshimiwa aliyemaliza kuongea hapa, amezungumzia matusi ambayo amepata mwekezaji wa ndani, mzalendo ndugu yetu Mengi. Lakini juzi juzi tumesikia Bakhresa naye akiambiwa kwamba ni mkwepa kodi, unaweza kukuta uhuni ule umefanya na management ya watu wachache tu katika kiwanda kile. Sasa nasema ni wakati muafaka wa Serikali kuweza kuwapongeza na kuwashikilia wawekezaji wa ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu kama Ndugu Mengi, mtu kama Ndugu Bakhresa na familia zao, rasilimali walizonazo wakisema waweke kwenye *fixed deposit* kwa mwaka fedha, watakayopata matatizo yao na familia zao wanamaliza, lakini wanawekeza kwa niaba ya Watanzania. *Please* Watanzania wanaojitokeza kwenye uwekezaji, Serikali iwaunge mkono. Kwanza kwa kutoa ardhi, pili kwa kutoa sheria zozote ambazo ni kandamizi kwao, lakini tatu kwa kumaliza migogoro ya fidia kwa wananchi mbalimbali na nne kuhakikisha kwamba mnawapa ruzuku. Serikali isiwe kikwazo kwa wawekezaji katika sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, napenda kuzungumzia zao la mchikichi. Mkoa wa Kigoma nilizungumzia hapa miaka 40 iliyopita tuliwapa mbegu nchi ya Malaysia, Malaysia sasa hivi inafanya vizuri kwenye zao hili kutokana na kuliendeleza. Ajabu na aibu ya Tanzania, zao hili halijafanyiwa utafiti, zao hili halina bodi wala Serikali hamna mpango madhubuti wa kuendeleza zao la mchikichi. Tunaiomba Serikali ituambie ni lini mtawekeza nguvu za kutosha kwenye zao hili kwa sababu zao hili linazalisha bidhaa zaidi ya 20 ndani ya zao moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache naweza nikataja mafuta ya mawese, naweza nikataja mafuta ya mise, zao hili linazalisha sabuni, zao hili linazalisha chelewa, zao hili linazalisha majani ambayo yanafunikia mapaa katika nyumba zetu, lakini zao hili linazalisha makafi ambayo tunatumia kama nishati ya kupikia. Serikali ya Chama cha Mapinduzi miaka 54 ya Uhuru haijaona umuhimu wa zao hili na kuweza kuliendeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nilizungumzia kuhusu bandari. Kulikuwa kuna kelele za sukari, imefikia mpaka shilingi 3,000, shilingi 3,500, shilingi 4,000 mpaka shilingi 5,000 baadhi ya maeneo, lakini wakati Serikali imelala hapa Dodoma, sukari mbovu inapitishwa kwenye mwambao kuanzia Pangani mpaka maeneo ya Mbweni kule Dar es Salaam. Bandari bubu zimejaa, Serikali inajua, watu wanakusanya kodi, Jeshi la Polisi liko pale, Serikali haipati mapato. Hii ni Serikali inafanya kazi kwa utashi ama ni Serikali inafanya kazi kama panya *road*? Lazima muamke, lazima muwe makini, fedha za nchi zinapotea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tanzania sasa hivi wengi ukienda hospitalini figo zinafeli kwa sababu ya kutumia sukari za KK.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wanaotengeneza *juice* na vijana na akina baba, kijiko kimoja cha sukari kinahudumia ndoo mbili za lita 20. Wananchi wanafeli figo na wakienda katika hospitali yetu ya Taifa Muhimbili hakuna matibabu wanayopata ya ziada. Napenda kusema kwa kusikitika niliwahi kukutana na mgonjwa mmoja ambaye figo zake zimefeli na sababu

kubwa ikiwa ni hizi *juice* ambazo zinaungwa KK. Mgonjwa yule figo zimefeli kwa sababu ya sukari hizi lakini kilichotokea gharama za matibabu zimekuwa ni kubwa akawaomba wauguzi arudi nyumbani nikapumzike nisubiri kuonana na muumba wangu kwa sababu siwezi kukidhi gharama hizi za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mnaweza mkaona kwamba sekta hii inaathiri vipi sekta nyingine. Mnaingiza sukari mbovu, Serikali mmelala, mnashindwa kuziba mipaka ya nchi, bidhaa mbovu zinaingizwa, Watanzania wanakufa, mnajiita Serikali ya hapa kazi tu. Mimi nawaita Serikali ya hapa kuchoka tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la uvuvi. Mkoa wa Kigoma tuna Ziwa Tanganyika na takwimu tu toka mwaka 2003 mpaka 2014 zaidi ya nyavu na mashine za bilioni sita zimeibiwa katika Ziwa Tanganyika. Lakini kama Serikali ingekuwa makini kudhibiti wizi huu basi ni imani yangu tungeweza kuvua samaki wa kutosha na tungeweza kutengenezewa viwanda vya kusindika samaki hivyo tungeweza kuuza samaki ndani na nje ya nchi. Sioni mkakati wowote wa viwanda vya kusindika samaki katika Ziwa Tanganyika. Tunaomba Waziri ukija kuhitimisha utuambie ni kwa kiasi gani utawekeza kwenye viwanda hivi ili vijana wa Mkoa wa Kigoma waweze kuajiriwa katika sekta hii ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna viwanda kama viwanda vya chumvi. Hivi ni viwanda ambavyo havijapewa kipaumbele kabisa. Ukiangalia Bagamoyo kuna chumvi inatengenezwa, ukiangalia Uvinza kule Kigoma kuna chumvi ambayo ilikuwa inatengenezwa, lakini Mtwara na kwenyewe walikuwa wanatengeneza chumvi, Serikali hatujaona hata siku moja mkitoa hata ruzuku ya madini joto kusaidia suala zima la chumvi. Kila mtu anayekuja hapa ni sukari, sukari, sukari, *How about* chumvi? Kwa nini mmesahau? Ama hamuoni kama Watanzania watakosa madini yenye chumvi yanaweza na yenyewe yakaathiri afya zao. Ningependa mtuambie mkakati gani wa kusaidia watu wanaosindika chumvi ili mambo yaweze kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ningependa kuzungumzia kuhusiana na suala zima la uwekezaji. Ukiangalia katika sekta ya uwekezaji maeneo mengi matumizi ya Taasisi na Mashirika ya Serikali, matumizi yamekuwa ni makubwa kuliko bajeti ya maendeleo. Huu ni udhaifu wa Serikali. Ukiangalia Taasisi nyingi hazina bodi, bodi zimeisha muda wake, *TR* ameikumbusha Serikali kwamba kunatakiwa kuundwe bodi mpya lakini Serikali bado imelala. Je, mna dhamira ya dhati ya hapa kazi tu ama mnaendelea kufanya mazingaombwe kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba Mawaziri mnapokaa kwenye mabaraza yenu mumkumbushe Mheshimiwa Rais aunde bodi mbalimbali ziweze kusaidia kilimo katika nchi hii. Ninashukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Saul Henry Amon na baadaye tutakuja upande wa Mawaziri. Tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atafuata Mheshimiwa Waziri wa Nishati na mwisho tutamalizia na Waziri wa Kilimo. Hayupo Mheshimiwa Henry? Haya.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja asilimia 100. Manyoni ni Wilaya ya zamani (kongwe) na Wilaya ya kwanza kuwa na Mkuu wa Wilaya Mwafirika. Tatizo kubwa Manyoni hasa Manyoni Mashariki hatuna kiwanda cha kati hata kimoja. Naipongeza Serikali imepata eneo kwa ajili ya Ukanda wa EPZ. Tunaomba tafadhali Serikali itenge fedha kwa ajili kuanza ujenzi wa viwanda ndani ya EPZ area.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ianze kutujengea kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti (*sunflower*) kwa kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti. kwa kufanya hili itakuwa imetoa hamasa kubwa kwa wakulima wetu wa alizeti katika Wilaya nzima ya Manyoni na hata Wilaya jirani za Chemba (Dodoma) na kadhalika. Aidha itatoa ajira kwa wingi kwa Wanamanyoni na maeneo mengine ya nchi. Mwisho viwanda hivi vitaongeza pato la Taifa kupitia kodi, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kuwezesha katika sekta ya viwanda. Serikali imefungua milango ya uwekezaji kwa kuleta wawekezaji wengi kutoka nchi mbalimbali waje kuwekeza nchini kwetu. Cha kushangaza kuna baadhi ya viwanda vimejengwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo kile cha ASPAM Mbagala. Kiwanda hiki kimejengwa maeneo ya Mbagala kina miaka zaidi ya mitano lakini hakijafunguliwa mpaka leo. Mwekezaji yule anahangaika hajui afanye nini, amewekeza fedha nyingi tena za mkopo mpaka sasa amekufa moyo. Je, Serikali hali hii inatia moyo kwa wawekezaji au inakatisha tamaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge ambaye ninaishi Mbagala. Masikitiko ya wawekezaji kwa kukosa aina mbalimbali za vibali vinavyoweza viwanda kuendelea. Niishauri Serikali kuwepo na mshauri wa viwanda ndani ya viwanda ili aweze kusaidia kuwashauri na kuwasimamia wawekezaji hawa kwa kuwa bado tunawahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo, naomba Serikali iboreshe SIDO ya Nyerere Road na elimu zaidi itolewe kwa viwanda vidogo

vidogo ambavyo Watanzania wanaweza kuvianzisha. Viwanda vya pipi, ubuyu, biskuti na juisi ni viwanda ambavyo katika nchi za China mtu anaweza kuviendesha hata kwenye eneo dogo la nyumbani. Niombe Serikali itoe elimu kwa wananchi wake jinsi ya uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vikubwa kwa mara nyingine tena naomba Serikali sambamba na kuanzisha viwanda vipya iangalie na viwanda vyetu tulivyokuwa navyo muda mrefu na sasa havifanyi kazi tena. Mlundikano wa viwanda vikubwa vya aina moja au vinavyozalisha bidhaa ya aina moja katika eneo moja ni tatizo. Kwa mfano eneo la Mbagala lenye makazi ya watu wamejenga viwanda vya cement viwili kwenye umbali wa robo kilometa ambapo maeneo hayo yana makazi ya watu na viumbe vingine vyenye uhai ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya matumizi ya maeneo ya viwanda vya Serikali, viwanda vingine vimegeuzwa *yard* za magari na vingine dampo la uchafu wa chupa na takataka nyingine. Kwa mfano Kiwanda cha Kubangua Korosho na Kiwanda cha Kioo Mbagala (*Sheet Glass*) kimegawanywa na miundombinu ya uendeshaji wa kiwanda kile umekufa kabisa, vipuli vyote vimechakaa. Nataka kujua kiwanda kile bado kiko *Twiga Cement* au kimeuzwa? Je, Serikali inafaidika na nini na eneo hilo? Naunga mkono hoja.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika azma ya Serikali kuwa nchi ya viwanda na hatimaye kuwa na uchumi wa kati lazima Serikali ije na mkakati wa kulitumia Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*) kwa mapana zaidi. Kwa hali ilivyo sasa hivi *SIDO* ina ofisi na kutoa huduma kwenye Makao Makuu ya Mikoa tu na Mikoa mengine haina, hali hii inafanya wananchi wanaotaka huduma kufuata huduma za *SIDO* Makao ya Mkoa ambako ni mbali. Lazima *SIDO* iwezeshe ili iweze kufuata watu na kuwapa huduma huko wanakoihitaji. *SIDO* isogeze huduma katika Wilaya, Kata na hata vijijin na kwenye miji mingine midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mazingira ya kufanya ama kuanzisha biashara katika nchi yetu siyo rafiki kwa wafanyabiashara na wawekezaji. Mwananchi akitaka kufanya biashara hapo hapo anafuatiliwa na *TRA* na vyombo vingine vya utozaji kodi. Kwa wawekezaji vilevile mwananchi huyu mara hii amepata wapi mapato au faida ili alipe kodi wakati mtaji amekopa na anatakiwa aanze kurejesha? Serikali itengeneze mazingira rafiki kwa kuwawezesha wananchi wafanye biashara na uwekezaji kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwa *sustainable* kwenye viwanda lazima pia wanasiasa na *private sector* waaminiane. Sasa hivi bado kuna kutokuaminiana kati ya wanasiasa au Serikali kwa upande mmoja na sekta binafsi kwa upande mmoja. Serikali iweke mazingira ya kuaminika kwa sekta

binafsi ikiwa ni pamoja na kuwa-assure wawekezaji wa nje na wa ndani kwamba waliwekeza mali yao itakuwa salama, haitataifishwa ama mazingira ya uwekezaji yasiwe yanayobadilika badilika sana kuashiria *risk* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uchumi wetu ufikie uchumi wa kati tunatakiwa tuwekeze katika viwanda vyetu vya ndani pamoja na kuvisimamia. Pia tukumbuke viwanda ndio njia pekee inayoweza kutoa ajira kwa vijana walio wengi nchini. Pia kuna vijana wengi ambao hawana ajira, niishauri Serikali iwawezeshe vijana hawa ili wasiwe wanatangatanga kwenda mjini kutafuta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna vijana wengi waliomaliza vyuo na hawana ajira, papo hapo wanaambiwa walipe mkopo waliokopa, vijana hawa watalipaje mkopo kama Serikali yao haijawawezesha kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyefahamu kuwa Wilaya ya Lushoto ni ya wakulima wa matunda na mboga mboga. Hivyo niishauri Serikali iweke kiwanda cha kusindika matunda, kwani matunda na mboga mboga vinaharabika hali inapelekea wakulima kupata hasara katika mazao yao hayo na pia wakulima wetu tunawakatisha tamaa kwa kupoteza nguvu zao nyingi shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wamejitahidi kujiajiri kwa kufanya biashara lakini wanasumbuliwa sana na watu wa TRA hasa wafanyabiashara wa Jimbo la Lushoto. Maafisa wa TRA hawana elimu ya biashara, halii inapelekea Maafisa hawa kuwa ndio wamepata uchochoro wa kuwanyanyasa wafanyabiashara hawa. Imefikia hatua mfanyabiashara akutane na simba lakini sio Afisa wa TRA. Naomba Serikali iliangelie hili ili wafanyabiashara wale waweze kufanya biashara yao kwa amani na kujipatia kipato chao cha kila siku.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya Moshi Mjini na Kilimanjaro kwa ujumla ambavyo vimefanywa maghala na vingine havifanyi kazi kwa ufanisi. Naishauri Serikali itekeleze ahadi ya Rais wakati wa kampeni kuwanyang'anya wawekezaji ambao hawajaweza kutimiza malengo ya awali yaliyotarajiwa katika viwanda vilivyobinafsishwa. Mahusiano ya kissekta ni muhimu sana (*forward and backward interlinkage*). Naishauri Serikali iwekeze katika *Agro Processing Industries (value added)* ambavyo vitaongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo. Pia nishati lazima iwe ya uhakika na ya bei rahisi ili viwanda vyetu vizalishe kwa bei nafuu kwa maana ya kuwa *cost effective*.

Vilevile ni lazima miundombinu ya reli iimarishwe ili iweze kubeba mizigo ya viwandani. Hatuwezi kutegemea barabara katika kusafirisha mizigo ya viwandani. Aidha, lazima Serikali iimarisha taasisi za kifedha *financial institutions* ili ziweze kutoa mitaji kwa wawekezaji wadogo, wakubwa na wa kati. Mikopo ikiwa na riba kubwa haiwezi kusaidia wawekezaji ndani wala wa nje. Nashauri Serikali iwe na mkakati wa kuacha kukopa mikopo mikubwa kwenye taasisi za fedha ili wawekezaji binafsi waweze kukopa kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ni muhimu sana katika kuhakikisha uwepo wa viwanda, nashauri mambo yafuatayo katika masoko:-

(a) Serikali ifanye jitihada za kuimarisha soko la ndani kwa kuongeza fursa za vipato kwa wananchi. Mataifa yanayokua kwa kasi kiuchumi kama China, India na mengineyo yamefanikiwa kuimarisha soko la ndani hivyo bidhaa zao wanazozalisha zinapata walaji wa ndani ya nchi na ziada ndio inauzwa nje. Kuimarika kwa soko la ndani kunavihakikishia viwanda uhakika wa kupata faida kwa bidhaa zinazozalishwa. Mojawapo ya mkakati wa kusaidia soko la ndani ni kuongeza uwezo wa kununua (*purchasing power*) kwa wananchi kwa kuhakikisha vipato vizuri vya mtu mmoja mmoja na wananchi kwa ujumla.

(b) Masoko ya nje lazima yatafutwe kwa kuanzia nchi jirani. Jambo hili litafanyika kwa kujifunza vizuri bidhaa ambazo tunaweza kushindana na jirani zetu. Pia ni vizuri wananchi wetu wasaidiwe jinsi ya kuingia kwenye ushindani na wananchi wenzetu katika masoko mbalimbali ya nchi jirani.

(c) Masoko yataimarishwa kwa kuziimarisha sekta za utalii, madini na Halmashauri zetu na sekta binafsi. Sekta ya utalii imekuwa kwa haraka katika nchi yetu, hivyo ni vizuri ikatumika katika kutoa ajira ambazo zitaongeza kipato cha wananchi na baadaye kupanua soko la ndani. Pia sekta ya utalii itafanya hivyo hivyo.

Aidha, Serikali ikizitumia Halmashauri zetu vizuri kwa kuimarisha sekta ya wajasiriamali wadogo wadogo kwa maana sekta isiyo rasmi itatengeneza kundi la watu wenye mitaji ambao wanaweza kuwekeza kwenye viwanda vidogo vidogo, viwanda vya kati na hata baadaye wanaweza kuunganisha mitaji na kuwekeza kwenye viwanda vikubwa. Zaidi ya hayo sekta binafsi inatakiwa itengenezewe mazingira rafiki ya kufanya shughuli zake ili iweze kuajiri wananchi wengi zaidi hivyo kuongeza kipato cha wananchi na kwa maana hiyo kuongeza nguvu ya kununua yaani *purchasing power*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima iwekeze katika teknolojia kwa kuimarisha mifumo yetu ya elimu na vyuo vya sayansi na ufundi.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na timu ya wataalam wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye kuonyesha nuru ya Tanzania ijayo ya viwanda kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie katika suala zima la viwanda hasa upande wa ajira kwa watu wenye ulemavu. Ninamuomba Waziri mwenye dhamana aliangalie suala zima la ajira kwa watu wenye ulemavu katika viwanda ikiwa ni utekelezaji wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaongelea viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Kuna kazi nyingi ambazo zitaweza kufanywa na watu wenye ulemavu hasa za kiufundi na zisizo za kiufundi. Hii itasaidia kupunguza ama kuondoa wimbi la ombaomba ama tegemezi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba pia Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kati ya viwanda vitakavyoanzishwa, kiwepo kiwanda ama viwanda vitakavyokuwa vinatengeneza vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia vifaa hivi saidizi vipatikane kwa gharama nafuu lakini pia ita-create ajira kwa watu wenye ulemavu kwani wengi wao wana utalaamu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali yangu sikivu ya CCM izingatie maombi ama ushauri niliotoa hapo juu. Vifaa saidizi vinauzwa kwa bei kubwa sana ikilinganishwa na uwezo halisi wa watu wenye ulemavu.

Pia ninapenda niongelee suala zima la viwanda na upatikanaji wa umeme ama *stability* ya umeme nchini. Kama tunavyofahamu viwanda vingi karibu asilimia zote mia vinategemea uwepo wa umeme sana.

Nimuombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya viwanda na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Nishati, washirikiane katika utendaji wao ili suala zima la umeme liweze toa mwelekeo wa uwepo na ustawi wa viwanda nchini kama Ilani ya chama changu cha CCM inavyosema. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atoe ufafanuzi wa mambo niliyozungumzia hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukerewe kama sehemu ya maeneo yanayozalisha samaki kwa wingi panahitajika kiwanda cha kusindika samaki. Hivyo tunaomba ushawishi wako kwa wawekezaji ili wajenge

viwanda vya kusindika/kuchakata samaki Kisiwani Ukerewe kitu kitakachosaidia upatikanaji wa ajira na hivyo uwezo wa kununua kwa walaji.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichangie katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Katika nchi yetu tuna rasilimali za kutosha ikiwa ni pamoja na madini, mazao, bandari, mbuga za wanyama, mifugo. Mkoa wa Njombe ni moja ya mikoa mitano inayozalisha mazao ya chakula na mazao ya biashara. Mazao ya chakula ni kama matunda, viazi, mahindi, ngano, maharage na kadhalika; mazao ya biashara ni pamoja na chai, mbao na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hadi sasa Mkoa wa Njombe hauna viwanda vinavyoeleweka. Naomba Serikali ione ni namna gani inapeleka wawekezaji watakaosaidia kuanzisha viwanda vya kripsi zinazotokana na viazi, viwanda vya mbao; viwanda vya karatasi, viwanda vya mafuta ya alizeti na viwanda vya juice.

Pia Serikali iwasaidie wajasiriamali wadogo wadogo ili kuanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile viwanda vya vikapu, mapambo, sabuni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Tanzania ya viwanda inawezekana sana, kikubwa ni Bunge hili na Serikali yake kuunga mkono azma ya Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yenye kauli mbiu ya Tanzania ya Magufuli ni Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili ya mvua ni mawingu, Serikali ya Awamu ya Tano imeanza vyema kwa kuongeza makusanyo ya kodi kwa kila mwezi. Makusanyo kupitia kodi mbalimbali yanaiwezesha Serikali kufikia hatua ya kuwa na akiba ambayo itapelekea fursa ya kuwekeza katika sekta hii muhimu ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali yetu itilie mkazo katika mabadiliko ya fikra katika vichwa vya Watanzania hasa wale wanaohusika katika kutengeneza mazingira wezeshi na kuvutia wawekezaji katika sekta ya viwanda na katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na matarajio ya walio wengi kuna Watanzania wenzetu wanaweka urasimu mwingi na usio wa lazima, ama kwa makusudi au kwa kutengeneza mazingira ya kuomba rushwa. Lazima Serikali yetu hasa kupitia Kituo cha Uwekezaji (*Tanzania Investment Centre*) wawekwe

Watanzania wenye nia njema na nchi hii, watakaokuwa na uchungu na wenye uzalendo na mapenzi mema wawasaidie wawekezaji wazawa na wawekezaji kutoka nje waweze kuwekewa mazingira wezeshi yatakayolitoa Taifa hili kwenye aibu ya kuifanya nchi kwenye orodha ya nchi zenye mazingira mabovu sana ya uwekezaji. Ni vyema tukajipanga upya kwa kuondoa urasimu usiokuwa wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) katika uwekezaji katika eneo la makaa ya mawe na chuma Mchuchuma na Liganga, Serikali ichukue hatua za makusudi kuharakisha uchimbaji wa makaa ya mawe na chuma, vilevile ili chuma kizalishwe hapa nchini na chuma hiki kitachochea mapinduzi ya viwanda nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ni la wakulima, asilimia zaidi ya 70 wanategemea kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara na ili waweze kunufaika ni vyema viwanda vidogo vidogo, vya kati na vikubwa vikatiliwa mkazo ili kuongeza thamani kwa mazao yanayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Geita ni mkoa mpya, hata hivyo unazo fursa mbalimbali kuanzia mazao, dhahabu, mifugo, uvuvi na kadhalika. Ninaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zones*).

Ninaamini maeneo yatakuwepo katika Wilaya mbalimbali ikiwemo Mbogwe. Tunawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje waje Mkoani Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikawekeza zaidi katika maeneo ya upatikanaji wa umeme wa uhakika, maji yapatikane kwa urahisi, miundombinu ya uhakika kwa maana ya reli, barabara, bandari, mapinduzi ya viwanda na mazingira wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 53 iliyopita (1962) ambapo ilikuwa ni mwaka mmoja tu baada ya Uhuru, Mwalimu Nyerere aliwaambia Watanganyika kuwa we *must run while they walk*, kwamba kama Taifa ni lazima tukimbie wakati wao wanatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaelekea katika mfumo wa viwanda ili kuwezesha Watanzania kuweza kuwa na uchumi wa kati, ni vyema kama Taifa tukajitathmini upya. Hatuwezi kufikia uchumi wa viwanda kama tutaacha nyuma sekta shirikishi, mfano sekta za miundombinu na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa viwanda vinategemea uwepo wa miundombinu kama barabara na reli ili kuweza kusafirisha malighafi kutoka shambani kwenda viwandani, vilevile kusafirisha bidhaa toka viwandani hadi sokoni, hivyo ni vyema kama Serikali ikazitupia jicho pia sekta wezeshi hizi ili kuwezesha viwanda vyetu kuwa na malighafi za kutosha kwa ajili ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema pia kama Taifa tuondoe kauli mbaya kuwa tunazalisha tusichokitumia na tunatumia tusichokizalisha. Tuungane kwa pamoja kumpa nguvu Mheshimiwa Rais katika kujenga uchumi unaozingatia mahitaji ya nchi na soko kwa ujumla, nchi ya viwanda vitakavyoongeza thamani ya mavuno kwa mkulima. Kujenga Taifa ambalo mkulima wa kahawa atanufaika kuliko mnunuzi wa kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Mkoa wa Songwe ni mkoa mpya hivyo kukabiliwa sana na changamoto ya kiuchumi, naishauri Serikali tunapoelekea uchumi wa viwanda ni vyema Serikali isiache nyuma mikoa mipya kama ya Songwe, Njombe na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kusikitisha, Mkoa wa Songwe hauna kiwanda chochote kikubwa ilhali Mkoa wa Songwe ni maarufu kwa kuzalisha mahindi na kahawa. Hivyo naiomba Serikali itujengee kiwanda kikubwa cha kukoboa mahindi ili kuweza kuzalisha unga ambao utauzwa ndani na nje ya nchi, sambamba na kiwanda cha kahawa ili kuwezesha wananchi wa Mkoa wa Songwe kunufaika pia na mpango huu madhubuti wa kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati.

MHE JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika hoja hii iliyo mezani inayohusu Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa tumekuwa tukipanga mikakati mingi na kujinasibu kwamba tunataka kuipeleka nchi yetu kwenda kwenye uchumi wa kati ili tuweze kuipata Tanzania ya viwanda, wakati tunasahau kuwa hatuwezi kuwa na nchi ya viwanda nchi nzima kama bado tuna tatizo sugu na kubwa la nishati ya umeme katika sehemu zetu nyingi za vijijini ambako ndiko tunataka na tunapaswa kupeleka viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tutakuwa tunafanya kazi bure kama hatutaweka mkakati wa dhati huku tukisukumwa na dhamira ya mioyo yetu ya kufufua sekta ya kilimo. Yatupasa kuwekeza zaidi kwenye kilimo mfano, pamba, kahawa, korosho, miwa na kadhalika ili tuweze kutimiza dhamira yetu ya kuipata Tanzania ya viwanda ambayo pia itatusaidia kutoa ajira kwa watu wetu na kuongeza kipato kwa wakulima wetu na kujiletea maendelea ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumekuwa kila siku tukisema tunataka kufufua viwanda ambavyo vimekufa lakini hatutaki kusema ni nini kimeua viwanda vyetu. Mfano Mkoa wetu wa Morogoro ulikuwa ni moja ya mikoa iliyoshamiri kwa viwanda kadha wa kadha ambavyo sasa vimebinafsishwa, vingine vimeshakufa kabisa na kuwa mabanda ya kufugia mbuzi na kuku na vingine vipo njiani kufa maana kama ni mgonjwa basi yupo ICU anapumulia mipira kupata hewa na ndugu wapo mbioni kuzima mashine yenyewe ya kupumulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana kwa niaba ya wananchi wa Mkoa mzima wa Morogoro, Mheshimiwa Waziri kabla ya kusema ni vipi atafufua hivi viwanda, pia atuambie hali halisi ya viwanda vyetu vya Mkoa wa Morogoro ambavyo vilikuwa vinatoa fursa ya ajira kwa wananchi wengi wa Mkoa wa Morogoro. Mfano, nataka kujua viwanda vyetu vya *Mang'ula Mechanical and Machine Tools Limited (MMMT)*, *Morogoro Canvas Mill Limited*, *Tobacco Processing Factory* na *MOPROCO* vipo kwenye hali gani na vinasaidia nini kwenye ubinafsishaji uliofanyika na kama vina tijakwa Taifa letu. Pia kwenye Jimbo langu la Mikumi kuna kiwanda cha *Kilombero Sugar Company Ltd.* ambacho kinajihusisha na utengenezaji wa sukari lakini kilibinafsishwa Aprili mwaka 1998 kwa Kampuni ya ILLOVO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwasisitiza wakulima wa Wilaya ya Kilosa walime miwa na kuacha kulima mpunga na mahindi lakini wakulima hao wa miwa wamekuwa wakilalamika sana kunyonywa kuhusu idadi ya asilimia ya miwa inayoingizwa kwenye kiwanda hicho cha ILLOVO. Lakini pia wakiwa na malalamiko mengi ya upimaji wa utamu wa miwa hiyo (*sucrose*) na pia mabaki ya miwa hiyo (*buggers*) ambayo ni mabaki ya miwa yamekuwa yakitengeneza umeme na pia kuna *morales* ambayo inatengenezea pombe kali (*spirits*) lakini wakulima wamekuwa hawalipwi zaidi ya tani za utamu wa sukari tu ambapo sasa ndani ya kiwanda cha ILLOVO pia kuna kiwanda kingine cha kuzalisha pombe na bado wanasema kiwanda kinapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupata sukari ya kutosha kama hatutaweka mazingira mazuri na salama kwa wakulima wa miwa. Wakulima wa miwa wa nje wanataabika sana na wanayonywa sana na wanahitaji sana msada wa Serikali kuwasaidia wakulima wao wapate mzani wao wa uhakika ili waweze kupima na kuingiza miwa yao kwa haki badala ya sasa kuwekewa mzani wasiouamini. Wapimaji ndio hao hao wenye kiwanda ambao pia ndio wanaopanga bei ya zao hilo, nasisitiza na naomba sana Serikali ifanye mpango wa kuwaletea wakulima mzani ili wapate haki yao na kufutwa machozi yao ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko makubwa sana ya wafanyakazi wa Kiwanda cha ILLOVO ambapo kumekuwa na mateso na

unyanyasaji mkubwa sana wa wafanyakazi wa ngazi ya chini wa kiwanda hicho. Nakushauri siku moja uende pamoja na mimi kwenye Kiwanda cha ILLOVO ili tukasikilize kilio cha wafanyakazi wao na ninakuomba usiende kuonana na uongozi wa kiwanda bali tuonane na viongozi wa vyama vya wafanyakazi au wafanyakazi wenyewe ambao wamekuwa kama watumwa ndani ya ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, lakini pia kumekuwa na malalamiko makubwa ya ajira za kindugu, ajira za kirafiki na ajira za rushwa ya ngono. Vyeo vinapandishwa kwa upendeleo mkubwa, lakini mbaya zaidi ni mishahara midogo sana ambapo Kampuni ya Sukari Kilombero (ILLOVO) imekuwa ikiwadanganya wafanyakazi kwamba wanapata hasara pindi linapokuja suala la majadiliano ya mishahara ingawa ukweli ni kwamba hakuna mwaka waliopata hasara bali ndiyo kwanza wanaendelea kuongeza kiwanda kingine cha tatu cha pombe, pamoja na ununuzi wa vifaa vyote vya usafiri kama magari, pikipiki ambavyo kila mtu akitumia kwa miaka mitatu tu viongozi hao wanauziwa kwa shilingi 100,000 tu.

Hii ni kama ile kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa John Magufuli, ni kwamba viongozi wa Kampuni ya ILLOVO wanaishi kama malaika na wafanyakazi wa chini ambao kimsingi wamekuwa wakifanya kazi ngumu kwa jasho na damu wanaishi kama mashetani. Sasa kuna wafanyakazi wa kigeni 23 pale ILLOVO, wakati wafanyakazi wa kigeni hawakutakiwa kuzidi wafanyakazi watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo kubwa sana la wafanyakazi zaidi ya 2000 waliokuwa wanafanya kazi kwenye kiwanda cha *Kilombero Sugar Company*, kwa masikitiko makubwa sana nataka nipate majibu ni lini watahendewa haki zao na kulipwa mafao yao kama wanavyostahili kwa kupitia mkataba wao na mwajiri Na. 4/1995 ambapo walilipwa miezi kumi badala ya miezi 40 kadiri ya Kifungu Na. 10.3.7 kinachohusu upunguzwaji kwenye mkataba huo wa hali bora za wafanyakazi, hivyo basi walipunjwa kiasi cha miezi 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri aje na majibu ya hoja hii ya msingi sana ambapo pia wafanyakazi hao walifutiwa malipo ya utumishi ya muda mrefu kama wanavyostahili kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na malalamiko mengi sana juu ya vipimo vya kazi kwa wafanyakazi wanaofanya kazi za vipimo. Sera waliyonayo ni kuhakikisha wanawapa vipimo vikubwa ili wasiweze kumudu kumaliza, hivyo kwao inawasaidia kubana matumizi kwani mfanyakazi asipomaliza kipimo kile alichopewa hawezi kulipwa hata kama kazi imebaki robo. Huu ni utumwa wa kiwango cha juu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inabidi ilifuatilie kwa kina na kuchunguza makampuni haya ya sukari yenye mashamba kwani wananchi hawa wanateseka sana. Serikali inaweza kufurahia kwamba wananchi wanapata ajira kumbe wamo utumwani ndani ya ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningeiomba Serikali ituambie ni lini itaanza kujenga viwanda vya kusindika viazi ambapo kilimo hicho cha viazi kimeshamiri sana katika Kata ya Kisanga ambapo tumebarikiwa kulima viazi kwa msimu mzima kwa wingi kushinda hata Gairo. Na pia napenda kuishauri Bodi ya Sukari itimize wajibu wake wa kuhakikisha inasimamia haki stahiki za wakulima wa miwa kuanzia kwenye mikataba yao dhidi ya makampuni ya sukari na wamiliki wa viwanda maana kwa sasa unyonyaji umezidi kwa wakulima wa miwa na kilio chao kikubwa ni kuwa na mzani wa kupimia sukari unaomilikiwa na wakulima wenyewe, tofauti na sasa ambapo mwenye kiwanda ndiye anayemiliki mizani hiyo na kuleta malalamiko ya miwa mingi kutupwa kwa kukosa ubora na utamu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Waziri aje na majibu, ni tani ngapi za wakulima maskini zimeshatupwa mpaka sasa na ni hasara gani ambayo wakulima wameipata mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mungu kwa fursa ya kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda pamoja na Naibu, Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara yake kwa hotuba inayoainisha mipango mizuri inayogusa maeneo yote muhimu yanayoleta maendeleo ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupitia Wizara hii kwa mpango unaozingatia uanzishwaji wa viwanda kwa kuanza na mazingira bora ya kuwekeza kwenye viwanda ambayo ni rasilimali zilizopo nchini kama ardhi, mazao ya kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu, mbegu za mafuta, pamba na kadhalika; miundombinu muhimu na wezeshi kama vile barabara, umeme, maji, mawasiliano na rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa rai kwa Serikali kupitia Wizara ya Viwanda kuhakikisha kuwa wawekezaji wanaandaliwa sera na sheria zinazokinzana zirekebishwe ili kuepuka migogoro na wananchi na taasisi za Serikali zinazosimamia ukusanyaji mapato. Sheria, sera na taratibu za taasisi zetu

zizingatie kuondoa urasimu na kuhakikisha kuwa maamuzi juu ya uwekezaji yanafanywa bila ucheleweshaji wowote na usumbufu kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano kati ya Wizara ya Viwanda na Wizara nyingine wezeshi na uchocheo uchumi uanze tangu mipango inapoanza kuwekeza viwanda. Kwa hiyo ni mategemeo yetu kuwa Mheshimiwa Waziri atatuainishia mfumo uliopo wa mipango kati ya Wizara ya Viwanda na Uwekezaji, Nishati na Madini, Miundombinu, Maji, TAMISEMI, Kazi na Elimu ya Juu na Ufundi ili kila mmoja aonyeshe jinsi gani atachangia katika kukamilisha mipango ya kuendeleza viwanda hivyo na utekelezaji wa mipango hii. Hii itatatua changamoto nyingi zinazotokana na kuwa kila Wizara inajiendesha yenyewe bila kuwa na mawasiliano ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mazingira ya viwanda vilivyopo kwa kuhakikisha kuwa wanapata huduma muhimu kujiendesha kama vile maji, umeme, miundombinu, masoko, maghala, mawasiliano na mitaji. Hii itakuza pato, kuongeza bidhaa na kuzalisha ajira za kutosha. Hii itasaidia kuwaaminisha wananchi na wageni wanaotaka kuwekeza kwenye viwanda na kuwavutia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kupitia Wizara ya Viwanda kwa kuzingatia katika mpango huu wa kuendeleza viwanda kila kanda ya nchi kwa uwiano unaoendana na rasilimali zilizopo na *comperative* na *competitive advantage*. Hii itaondoa kuwa maeneo machache ya nchi yanaendelea zaidi wakati mengine yako nyuma ilhali wana fursa nyingi za kuwa na viwanda. Wilaya kama Wilaya yangu ya Ileje na nyingine nyingi zenye kuzalisha nafaka na mazao mengine kwa wingi zipewe kipaumbele tunapopanga kuwekeza viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kutoa rai kwa Serikali kuhakikisha sasa kuwa sambamba na uanzishwaji wa viwanda tuanzishe viwanda vyenye kuzingatia soko la ndani. Serikali ijipange kuzalisha bidhaa zinazofaa kutumiwa nchini ili kukuza soko la ndani na kwa hiyo kuongeza ajira na kuondoa umaskini. Kwa hili tunamuomba Waziri ahakikishe kuwa mipango inazingatia kukuza soko la ndani na soko la Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla, tupatiwe mkakati wa kuanza kupunguza uagizaji wa bidhaa ambazo zinazalishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango na vipimo. Bidhaa nyingi ambazo hazikidhi viwango zinaingia nchini na nyingine ni hatarishi, vilevile nguo na bidhaa za nguo zinazozalishwa na kuagizwa nchini au hata bidhaa za vifaa vya ujenzi hazizingatii vipimo sahihi; wanapunja kwa kupunguza sentimeta katika bidhaa. Hii inawadhulumu wananchi, kwa hiyo natoa rai kuwa TBS na WMA wajengewe uwezo wa kupatiwa wafanyakazi wengi zaidi ili waweze kukagua viwanda na bidhaa hizi ili viwango na vipimo vizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko na vituo vya mipakani, Tanzania ina mipaka mingi na majirani zetu ambayo kwa mtazamo chanya ni fursa muhimu ya kuboresha biashara ya mipakani na nchi jirani. Yapo masoko mengi ya mipakani na yapo maeneo kama Ileje ambayo hayajaendelezwa lakini yana uhitaji mkubwa wa kuendelezwa ili wananchi wa maeneo haya ambao wengi wao ni wanawake na vijana wapate kipato na kuinua familia zao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje ina fursa ya kuwa na soko la kimataifa la mazao ya kilimo yaliyosindikwa ya ufugaji, uvuvi na misitu. Ileje inapakana na Malawi na Zambia lakini pia iko karibu na Mji wa mpakani wa Tunduma na hii kibiashara ni fursa kubwa. Ningependa Serikali itufahamishe jinsi ilivyojipanga kuboresha masoko yote ya mipakani kwa kuiwekea miundombinu muhimu na kujenga vituo vya forodha na soko la Kimataifa la Isongole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jinsia na maendeleo ya viwanda. Wanawake ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, pia ni wafanyabiashara wazuri. Tungependa kuishauri Serikali izingatie umuhimu wa kundi hili muhimu kuzingatia maendeleo ya viwanda tangu ngazi ya mipango hadi utekelezaji. Wanawake wanahitaji viwanda vya usindikaji, kufuma masweta na nguo za baridi, nguo kama khanga, vitenge, vikoi na hivi pamoja na viwanda vya kusindika matunda, mboga na mazao ya mifugo, karanga na mafuta ya kula. Ningependa kujua jinsi gani wanawake watazingatiwa katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgodi wa Kiwira utafufuliwa lini? Naunga mkono hoja.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, kwa hotuba nzuri ambayo inalenga Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa sekta ya viwanda na biashara kwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi na watu wake unahitaji mtazamo tofauti. Nchi za *Tiger (Tiger nations)* zimeendelea kiuchumi ukilinganisha na Tanzania kwa sababu ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa sekta hii inaleta ufunguo wa sekta nyingine hasa kilimo. Serikali iweke mkazo kwenye viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani za mazao ya kilimo. Kutokana na kazi nzuri ya REA, napendekeza kuangalia uwekezaji mdogo mdogo wa viwanda vijijini ili kuongeza thamani ya mazao yetu na pia kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la mitaji linaweza kutatuliwa na benki mpya ya kilimo (TADB). Napendekeza milioni 50 kwa kila kijiji, zipelekwe

TADB, kwa kusimamia hizo pesa ambazo ni mfuko wa kuzunguka (*Revolving Fund*) kwa kila kijiji. Hii itawezesha TADB kutoa huduma moja kwa moja kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuiongezea mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha ufanisi wa viwanda na biashara ndogo ndogo, ni muhimu kutoa elimu za muda mfupi kwa vijana na hasa wa vijijini, ili ujasiriamali uwe na tija na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa kufufua viwanda vyetu, zoezi hilo liendeshwe kwa uangalifu mkubwa kutokana na kubadilika kwa teknolojia na ushindani mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mbeya, imetenga eneo mahsusi katika kijiji cha Mjele kwa ajili ya Kiwanda cha Nyama na bidhaa zingine zitokanazo na mifugo. Hilo eneo ni mbadala wa eneo lililokuwa la *Tanganyika Packers* ambalo kwa sasa limezungukwa na makazi ya watu (Mji mdogo wa Mbalizi).

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya uhakika yatakayotupeleka kwenye nchi ya uchumi wa kati yatapatikana kwa kuwa na viwanda, tena viwanda vinavyotumia mazao yetu kama malighafi yake. Kufikia uchumi wa kati ni kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja ambao kwa ujumla wake ndio utakaopandisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza na kuunga mkono hoja ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza Mkoani kwangu Dodoma, Wilayani kwangu Chamwino na Jimboni kwangu Chilonwa, naomba kuomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mazingira rahisi kwa wananchi wa Jimbo la Chilonwa kuweza kukipa na kuanzisha viwanda vidogo vidogo vinavyochakata/process mazao yanayozalishwa jimboni kama vile mashine za kukamua alizeti, ufuta pia, mashine za ku-process mahindi na kuuza sembe mijini badala ya kuyauza mahindi (*value addition*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kipekee zao la zabibu ambalo kwa hakika ndio mkombozi wa uchumi wa wananchi wa Dodoma ambao bado unasinzia. Kwa zabibu naiomba Wizara ifanye kufuatilia Halmashauri ya Chamwino ili kuisaidia kufanikisha ujenzi wa kiwanda cha zabibu cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha kisasa ni kile kitakachoweza uzalishaji wa *juice*, mvinyo na *concentrate* ya mvinyo. Hiki ni kiwanda tofauti na vile vidogo vidogo na vichache vilivyopo vinavyozalisha mvinyo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kumpongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na watendaji wake kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti yao hapa Bungeni ili tuweze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo nilikuwa napenda kupatiwa ufafanuzi na kutoa ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, viwanda vilivyobinafsishwa. Serikali iliamua kubinafsisha viwanda vilivyokuwa vya Serikali na kubinafsishwa kwa wawekezaji lakini bado tunaona licha ya kuwa viwanda hivyo havifanyi kazi lakini vingine vimebadilishwa hata matumizi na vingine vimegeuzwa kuwa maghala ya kuhifadha bidhaa au mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango mkakati gani kwa sababu awamu hii Serikali ina mpango wa kufufua viwanda na ningependa kujua hatua gani watachukuliwa wawekezaji hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningependa kujua katika ujenzi wa viwanda je, itazingatia katika maeneo yenye malighafi ili kupunguza gharama za kusafirisha malighafi kutoka zinakopatikana mpaka viwandani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Iringa hasa katika Jimbo la Kilolo asilimia kubwa kuna kilimo cha nyanya, pilipili na vitunguu, lakini wakulima wamekuwa wakipata shida sana kupata masoko kwa kuwa Serikali inahimiza ujenzi wa viwanda na kuna eneo la EPZ je, mkakati wowote umewekwa na Serikali ili kupata mwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, maeneo yaliyoteuliwa na EPZ. Kwa kuwa Serikali ilitenga maeneo mengi sana kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda lakini maeneo mengi bado wananchi hawajalipwa fidia likiwemo lililotengwa katika Mkoa wetu wa Iringa. Nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha wananchi wanalipwa ili maeneo hayo yaweze kutumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubovu wa barabara zinazokwenda katika viwanda. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha barabara zote zinazokwenda katika viwanda zinajengwa kwa kiwango cha lami na barabara hizo zinahamishwa kutoka kuwa za Halmashauri na zinakuwa za TANROAD.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa kiwango. Mchango wangu utajikita katika sehemu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sekta ya masoko. Wakulima wa mazao ya nafaka wanakabiliwa na changamoto kubwa ya masoko ya uhakika kwa mazao mfano soko la mpunga na mahindi kila mwaka yanakabiliwa na kutokuwa na soko la uhakika. Nashauri Serikali kupitia Wizara ichukue hatua katika kutafuta masoko ya mazao haya katika nchi jirani kama Sudan ya Kusini, Kenya, Zambia na nchi jirani ambazo zina uhaba wa mazao haya badala ya wafanyabiashara binafsi kusimamia na utafutaji wa masoko kwa mazao hayo makuu ya nafaka. Aidha, Serikali kwa kupitia vyombo vya habari watangaze taarifa za masoko kwa wakulima ili wawe na uwezo katika kujadili (*debate*) vyema bei inayolipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu Bodi ya Leseni za Maghala. Naipongeze Wizara kwa mpango wake katika kuboresha na kuongeza wigo wa mkopo kwa wakulima vijijini ili kuongeza bidhaa za kilimo. Kwa kuwa Mkoa wa Morogoro ni ghala ya chakula la Taifa na moja ya Mikoa yenye viwanda vingi, naishauri Wizara ianzishe Ofisi ya Leseni ya Kodi za Maghala katika mkoa wa Morogoro ili kusogeza huduma zaidi na karibu ya wakulima ili kuongeza uwezo wao wa kuzalisha mazao kwa wingi/ufanisi kwa kuwezesha Mkoa wa Morogoro kutekeleza majukumu yake kiukamilifu kuwa ghala la chakula la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali yetu kwa hotuba nzuri kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda. Hotuba hii inaongelea mambo mazuri sana na kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda jambo ambalo litaleta fursa ya ajira kwa vijana wetu ambao wako mitaani, hawana ajira, pia tukiwa na viwanda tutainua kipato cha mwananchi na kipato cha Taifa kitaongezeka na uchumi wetu utakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufanikiwa ni lazima tuhakikishe tunaweka mazingira rafiki ambayo yatawapa fursa wawekezaji kuja kuwekeza nchini kwetu bila usumbufu yaani tuondoe urasimu uliopo, pia viwanda ambavyo vipo tuhakikishe tunavilinda. Niiombe Serikali yangu ili tuweze kufanikiwa na tuingie kwenye uchumi wa viwanda wa kati tuhakikishe tunakuwa na umeme wa kutosha ili viwanda vyetu vitumie umeme wetu kupunguza gharama za uzalishaji na ndipo kipato cha Taifa kitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa ili kupata malighafi za kupeleka kwenye hivyo viwanda, tuweke mazingira rafiki ili huyu mkulima anacholima kiwe na ubora kwa ajili ya viwanda vyetu hatuwezi kufanikiwa. Mheshimiwa Waziri tutumie huu umeme wa REA ambao umefika vijijini, tuwawezeshe na kuwapa elimu vijana wetu kufungua viwanda vidogo vidogo wapate ajira na kuongeza kipato cha Taifa.

Namuomba Mheshimiwa Waziri, Kyerwa kuna kahawa ambayo ni zao muhimu linaloingizia Taifa kipato. Serikali iongeze Benki zetu hasa hasa Benki ya TIB ipunguze riba ili wananchi wakopeshwe mashine za kukoboa kahawa, hili litaongeza kipato kwa mwananchi kitu ambacho kitapunguza wizi wa kahawa inayopelekwa nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kufikiria kufungua kiwanda Kyerwa cha kusafisha Tini ili kuinua kipato cha wachimbaji wadogo wadogo na hili litaondoa Tini nyingi inayovushwa kupeleka nchi jirani maana karibu asilimia 75 ya Tini inayochimbwa Kyerwa inanufaisha nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ipeleke viwanda maeneo husika ili kuongeza ajira kwa maeneo husika mfano, viwanda vipelekwe maeneo ya uzalishaji pamba, matunda, tumbaku na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa neema ya gesi tunaweza kuzalisha vitu vingi. Niombe Serikali tusiishie kwenye kuzalisha gesi kwa ajili ya umeme tu, bali kila kitu kinachotoka kwenye gesi maana gesi tunaweza kuzalisha vitu vingi sana.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri wa Viwanda, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge na uongozi wote wa Wizara. Pongezi za pekee kwa Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kufufua viwanda. Naomba Serikali ifufue Kiwanda cha Nyuzi Tabora kwani kiwanda hicho ni cha zamani, pia ni mitambo ya kizamani ambayo imepitwa na wakati. Ni vema Serikali ikamshauri mwekezaji kuagiza mitambo mipya ya kisasa. Serikali ikajiridhishe kuona kama kweli mitambo ipo, isiwe wameihamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa majengo yaliyojengwa na Serikali ambayo alipewa mwekezaji ameshindwa hata kukarabati, ni vema apewe mwingine. Kukosekana kwa viwanda Mkoa wa Tabora ni kuongeza ugumu wa maisha kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora, kusababisha ongezeko la uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Maziwa, niombe Serikali kuwawezesha wawekezaji wa ndani ambao uwezo wao ni mdogo kimtaji kama

vile mwekezaji anayemiliki Kiwanda cha Nyamwezi. Kukosekana kwa mitaji hiyo, pia kumechangia kufungwa kwa kiwanda hicho mara kwa mara, pia kufanya wafugaji kukosa mahali pa kupeleka maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kutafuta wawekezaji ambao wanaweza kuweka kiwanda cha kusindika asali kwani Tabora ni *centre* ya mikoa jirani ambayo nayo wanayo asali kwa wingi kama vile Katavi, Singida na Kigoma. Hivyo basi, ni rahisi kwa mwekezaji kupata mahitaji ya kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Tumbaku, naishauri pia Serikali kuleta wawekezaji Mkoa wa Tabora ili zao la tumbaku lisindikwe kwa urahisi na kuondoa usumbufu kwa wakulima. Pia wananchi wa Mkoa wa Tabora kupata ajira na mikoa jirani kuliko ilivyo hivi sasa ambapo mazao yote hupelekwa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke nguvu zote kwa kuwezesha bajeti ya viwanda vidogo vidogo (*SIDO*) kupewa fedha za kukuza uchumi kwa wajasiriamali, kwani *SIDO* imefanya kazi kubwa hapa nchini, imefanikisha kutoa elimu kwa wananchi wengi hapa nchini kwa kada mbalimbali hasa wanawake. Ofisi za *SIDO* zipewe vitendea kazi kama vile magari, vifungashio vya elimu ambavyo hujifunzia wajasiriamali hapa nchini.

Ombi langu kwa Serikali isaidie kiwanda cha *SIDO* ambacho hutengeneza sabuni, kusindika karanga, pia mikopo midogo midogo kilichopo Tabora; tumbaku ipewe kipaumbele kwa kutafuta wawekezaji kwani hulimwa Mkoa wa Tabora kwa 60%. Naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya Viwanda haiko kama Serikali haitakuwa na malengo makini kwa Watanzania. Kwanza, Serikali ijikite kwa kutoa vipaumbele ni viwanda vipi kwanza waanze navyo. Serikali ijali wawekezaji wa ndani wanapowekeza kwenye viwanda na iondoe sheria kandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuwe na miundombinu mizuri kama ya barabara bora zenye viwango, ambazo zitaruhusu bidhaa kusafirishwa kwa urahisi zaidi. Kuwe na uhakika wa umeme na siyo wa mafuta. Kwa upande wa biashara, wafanyabiashara wapunguziwe riba kwenye mabenki ili kwe na urahisi wa kufanya biashara na Watanzania wengi wawekeze kwenye biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wageni wakiwekeza kuwe na asilimia ya kuajiri Watanzania isiyopungua asilimia 90. Pia kuwe na masharti ya uwekezaji kuwa wanapowekeza, waboreshewe miundombinu katika eneo walilowekeza. Vilevile Serikali ifanye jitihada za makusudi za kupanua wigo na

fursa za kuanzisha masoko yenye masharti nafuu. Serikali ijifunze kutoka nchi nyingine vipi wamefanikiwa katika biashara na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuweze kuendeleza viwanda vidogo vidogo kama *SIDO* na vinginevyo ili wananchi wapate ajira na kuwe na soko la karibu na uhakika ili kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanahitaji Serikali iimarisha viwanda ambavyo kwa kuanzia vitaleta tija na kuendelea kama walivyoendelea nchi za jirani na za mbali na siyo kila siku hadithi. Wanatarajia kuona Tanzania ya viwanda vyenye neema mbalimbali na imeondokana na umasikini ulioenea. Pia Serikali itatue changamoto zilizopo katika sekta hii ili tufikie malengo tunayotarajia.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa hotuba yake nzuri yenye kulenga kukuza uchumi wa viwanda vidogo vidogo na kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hii ya uwekezaji wa viwanda iliyoainishwa katika utekelezaji wake wa Mpango huu wa mwaka 2016/2017, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea maeneo mbalimbali ya Majimbo yao juu ya uendelezaji wa upandishaji wa thamani ya mazao yao wanayolima, lakini juu ya vijana na wanawake kuwezesha kushiriki katika uchumi huu wa viwanda vidogo vidogo ili kukuza ajira na kuleta ustawi wa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ni mkombozi mkubwa wa wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini ni mkombozi mkubwa kwa vijana na wanawake katika kuyafanya makundi haya yaweze kushiriki katika uchumi huu wa viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kusaidia *SIDO* Mkoa wa Lindi fedha za kutosha ili kusaidia kundi kubwa la vijana na wanawake kupata elimu ya kutosha kupandisha thamani ya mazao yanayolimwa Mkoani Lindi. Naishukuru Serikali, imetenga bajeti ya shilingi bilioni sita katika Mikoa minne tu. Naomba Mkoa wa Lindi ufikiwe kuwezesha *SIDO* iweze kusaidia Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya uwekezaji *EPZ*, Lindi Manispaa ni wafaidika wa mradi huu. Eneo lilishatengwa lakini hatuoni chochote kinachoendelea juu ya mradi huu. Tunaomba Serikali itupe majibu juu ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza sera endelevu ya viwanda ya mwaka 1996 Mkoa wa Lindi ulikuwa na viwanda. Kwa mfano, Kiwanda cha Usindikaji wa Mafuta ya Karanga na Ufuta (Nachingwea); na Kiwanda cha Ubanguaji Korosho, Lindi Vijijini na Lindi Manispaa. Viwanda hivi havikuwahi kufanya kazi hata siku moja, Mheshimiwa Waziri analijua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake ya swali namba 19 la Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Viwanda 1996/2020 Mheshimiwa Waziri alisema, juhudi zinafanyika ili viwanda vilivyosimama vifanye kazi. Mheshimiwa Waziri anieleze, juhudi hizi zipo katika hatua gani za utekelezaji? Mheshimiwa Rais aliwapa matumaini Wana-Lindi na kuwaambia atahakikisha viwanda vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nangependa Mheshimiwa Waziri anieleze, Maafisa Biashara wana kazi gani katika Halmashauri zetu? Hatuoni chochote wanachofanya zaidi ya kusimamia ukataji wa leseni za biashara; kingine ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. MPAKATE D. IDDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani inatakiwa ifanyiwe marekebisho kutokana na upungufu, kwani ilishindwa kumfidia mkulima pindi mzigo wake ulivyopotea katika maghala makuu. Mzigo ukipotea ghala kuu sheria inamtaka mtunza ghala amfidie mweka mali, lakini sheria haimlazimishi kulipa, matokeo yake mweka mali anakuwa anadai mali zake bila mafanikio. Hivyo ninaomba sheria hii irekebishwe ili itoe msisitizo wa mtunza ghala kulipa mara moja pindi akipoteza mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo nyingi sana zinazotolewa na Serikali pamoja na Halmashauri bila kumfahamisha tozo hizo wakati mfanyabiashara anapata leseni ya biashara. Ni vyema mfanyabishara apewe orodha ya tozo zote anazopaswa kulipa wakati anapewa leseni ya biashara. Kuna ule ushuru wa vipimo, kodi ya majengo, ushuru wa mazingira, tozo mbalimbali kama EWURA, Halmashauri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna ukiritimba wa kupata vibali mbalimbali. Ni vyema mfanyabiashara akahudumia sehemu moja ili kuharakisha uwekezaji wa wafanyabiashara. Kwa mfano, vibali vya ujenzi, vibali vya mazingira, vibali vya Taasisi mbalimbali kama EWURA na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi vimebinafsishwa, lakini wafanyabiashara wamebadili matumizi ya viwanda hivyo bila kujali kuwa viwanda hivyo vilijengwa kwa madhumuni fulani ili kuwezesha mazao yetu kuongeza thamani. Ni vyema viwanda hivyo vifufuliwe kama ilivyokusudiwa ili kuongeza ajira kwa vijana wetu. Tuna malighafi nyingi sana tunazalisha, lakini tunauza ghafi badala ya kuongeza thamani ya mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ucheleweshaji wa huduma mbalimbali katika vitengo vilivyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ikiwa ni pamoja na kufumbia macho sekta ndogo ya biashara ndogo ndogo (Wamachinga) ambao wanaendesha biashara bila utaratibu maalum ambao ungewezesha kundi ili kuwa na leseni za biashara na kuongezea mapato Serikali kupitia leseni hizo.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, naipongeze sana Serikali kwa jitihada zake za uchumi wa viwanda kwenye nchi yetu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri na kwa namna ya pekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja moja kwa moja. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni namna gani iliyo rahisi kabisa viwanda vinaweza kupata malighafi ya gesi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme? Mfano, Kiwanda tarajiwa cha marumaru (*tiles*) cha *Goodwill Ceramic Tiles* kinahitaji gesi na wawekezaji hawa wapo tayari kabisa kujenga bomba kwa gharama yao wao wenyewe (Mkopo kwa *TPDC*): Je, Wizara itasaidiaje kuharakisha jambo la namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji hawa pia wa *Goodwill Ceramic* pia wameomba bei ya gesi iweze kuwa *stable* (imara). Naiomba Wizara ya Viwanda isaidie pia katika kuhakikisha inashirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuharakisha jambo hili pia. Mwisho, naipongeza tena Serikali kwa jitihada hizi na kusisitiza kuwa jitihada hizi ziendeleo kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sera ya kuwekeza kwenye viwanda, nashauri tujikite zaidi kwenye viwanda vidogo vidogo vyenye kuongeza thamani ya mazao yetu badala ya viwanda vya kuzalisha bidhaa kamili kama hatuna “*comparative advantage*” ya bidhaa za aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itafute mwekezaji wa Kiwanda cha kusindika samaki katika Kisiwa cha Mafia sambamba na kupata meli za

uvuvi zenye zana za kisasa zenye uwezo wa kuvua katika bahari ya kina kirefu. Mafia ipo karibu na mkondo wenye kina kirefu kunapopatikana samaki wengi na wakubwa wa aina mbalimbali kama Jodari (*Tuna*) nguva (*King fish*) samsuri (*Marley*) na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa viwanda vya sukari umekuwa mdogo na hautoshelezi kulisha soko la nchi nzima. Ipo hoja na haja ya kuvutia mwekezaji kuwekeza katika bonde la Mto Rufiji ili kuondokana na tatizo la kuagiza sukari kila mwaka. Naishauri Serikali pia katika kipindi hiki kuelekea kujitosheleza kama uzalishaji wa ndani wa sukari, Serikali itoe vibali kwa kuagiza sukari kwa viwanda vyenyewe, mfano, Mtibwa, Kagera na kahalika.

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali ya Marekani kuuongezea muda Mpango wa AGOA kwa miaka 10, mpango ambao unazipa fursa nchi za Kiafrika kuuza bidhaa zake kwenye Soko la Marekani bila kutozwa ushuru, Tanzania bado haijatumia fursa hii vizuri. Soko la AGOA katika Jumuiya ya Afrika Mashariki limetawaliwa na nchi ya Kenya ambapo mwaka 2013 nchi hiyo imeuza zaidi ya asilimia 96 ya bidhaa zote toka Afrika Mashariki, ikifuatiwa na Tanzania 3%, Uganda 0.4%, Rwanda 0.2% na Burundi asilimia 0%. Bidhaa zitokazo Kenya kwenda Soko la Marekani kwa asilimia kubwa ni mazao ya kilimo cha maua, chai, kahawa, pamba na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao makubwa yaliyofanywa na Kenya yamechangiwa na nchi hiyo kuwa na mkakati mahsusi wa Kitaifa wa AGOA unaoainisha maeneo ya vipaumbele. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo hazina mkakati mahsusi wa Kitaifa wa AGOA, hivyo kushindwa kuitumia fursa hiyo adimu na adhimu kikamilifu. Mwaka 2015 kulikuwa na jitihada za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na sekta binafsi kuandaa mkakati ya Kitaifa wa AGOA. Ni muhimu tujue tumefika wapi na hatua hiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya udhaifu tulionao Tanzania ni ufungashaji mbovu wa bidhaa zetu na usalama kiafya wa mazao tunayotaka kuuza nje, udhaifu ambao umetufanya tuwaachie Wakenya kununua vitunguu, hiliki, tangawizi, viazi, pilipili, mchele mzuri nakadhalika, kutoka mashambani mwetu kwa bei ndogo na wao kumaliza kwa ufungashaji bora na kuzingatia masharti ya afya ya usindikaji, hatua ambazo zinaongeza thamani ya bidhaa na kuwaingizia fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 tarehe 26 Februari, 2015 Tanzania tuliongoza nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye kikao muhimu cha kujadili masuala haya ya kibiashara na Serikali ya Marekani jijini Washington DC. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo uliwezesha nchi zetu kusaini makubaliano na Serikali ya Marekani ya urahisishaji wa biashara (*Cooperation Agreement on Trade Facilitations, Sanitary and Phytosanitary measure and technical Barriers to trade*). Makubaliano haya yametufungulia njia Watanzania kurekebisha upungufu wetu, kuomba msaada wa kiufundi pale tutakapokuwa tayari kusonga mbele. Moja ya hatua muhimu za kujiandaa ni kuja na huo mkakati wa Kitaifa wa AGOA niliouelezea awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wachapakazi ambayo imeonyesha utayari wa kuchakarika ili nchi yetu sasa ijenge uchumi wa viwanda. Hivyo nina imani kuwa mkakati huo wa Kitaifa wa AGOA utakuwa tayari na kuanza kufanyiwa kazi. Wilaya ya Kyela inasubiri kwa hamu fursa ya kuuza kwenye Soko la Marekani bidhaa zake kuu mbili; mchele wenye ladha nzuri ya pekee na unaonukia na kokoa “organic” ambayo haitumii mbolea zozote za kemikali na ambayo imepata sifa kubwa Ujerumani na Uholanzi. Tatizo letu kubwa ni afya ya mimea na bidhaa zetu kuendana na viwango vya Kimataifa na ufungashaji wa bidhaa zetu ambao bado una ukakasi. Hatua tuliyofikia na wamarekani ni nzuri, tuitumie bila kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa wingi wa rehema kwa jinsi ambavyo alituchagulia viongozi kwa ngazi zote; nikianza na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Joseph Pombe Magufuli; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu; na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

Pili, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Busokelo ni Jimbo ambalo tunalima mazao ya chakula na mazao ya biashara. Mazao ya chakula tunayolima ni kama yafuatayo: ndizi, mahindi, maharage, viazi mviringo na viazi vitamu, matunda mbalimbali kama maparachichi, matunda damu na mengineyo. Mazao ya biashara ni kama yafuatayo: mbao, chai, kokoa, kahawa pamoja na hiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazao hayo yote, hatuna hata kiwanda kimoja kwa ajili ya kuchakata mazao hayo yote. Inasikitisha sana kuona mkulima, tena wa jembe la mkono analima kwa taabu sana, pembejeo

haziwafikii kwa wakati, zinakuja wakati muda usiofaa. Kwa mfano, mbolea za kupandia zinakuja wakati wa kupalilia na mbolea za kukuzia zinamfikia mkulima wakati anavuna. Mbaya zaidi mkulima huyu akifanikiwa kuvuna, hapati sehemu za kwenda kuuza ama kuchakata (viwanda vidogo) ili mazao yao yapate thamani kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri awakumbuke wananchi hawa wa Busokelo kwa kututafutia wawekezaji wa mazao kama kokoa, ndizi na mahindi pamoja na viwanda vya mazao ya ng'ombe mfano, maziwa (kiwanda cha maziwa) Kata ya Bonde la Mwakaleli (Isange, Kandete, Lubeta na Mpembo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kutafuta wawekezaji kwenye viwanda vya gesi aina ya *cabondioxide* gase CO_2 , pamoja na umeme wa joto ardhi *Geothermal* eneo la Ntaba, Kata ya Ntaba ndani ya Busokelo Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana tuwe na kiwanda cha kusindika kokoa kwa sababu wakulima hawa wanalima kwa wingi sana hasa maeneo ya lufilyo, Ntaba na Kambasegela ili thamani ya kokoa ipande na mkulima aweze kupata zaidi kuliko hivi sasa na itaongeza morali zaidi kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya Jimbo la Busokelo ni mibaya sana hasa kipindi hiki cha mvua na hivyo imepelekea zaidi ya tani nyingi sana za ndizi na maparachichi kuharibika na hivyo kusababisha umasikini zaidi kwa wakulima hawa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, ni muhimu sana viwanda hivi vikajengwa maeneo husika ili hasara ambayo inatokana na kuharibika kwa miundombinu iweze kuepukika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo hapo juu, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Naomba Serikali itengeneze mnyororo wa huduma na kuhudumiana (*chain supply*) ili uzalishaji wa viwanda vyetu ulenge kwanza kuhudumia mahitaji ya ndani (soko la ndani). Yapo mahusiano kati ya viwanda, masoko na ubora wa miundombinu ya umeme, maji, barabara, mawasiliano na uzalishaji wenye tija. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri awasiliane kwa karibu na Wizara nyingine ili kuwe na matokeo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu itolewe ili wananchi na wataalamu, viongozi waliopo vijijini waelewe viwanda vinaanza na viwanda vyenye kuajiri watu 1, 2, 3, 4 - 9 hadi viwanda vikubwa. Wananchi hawaelewi kama shughuli wanazofanya kama usindikaji wa vyakula ni viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utunzaji wa *data*, naishauri Wizara iwe na utaratibu wa kuweka kumbukumbu (*data*) ili kuweza kuchambua maendeleo ya uendeshaji viwanda na matokeo yake kama vile idadi ya walioajiriwa Kiwilaya hadi Kivijiji. Hii itasaidia kufanya maboresho ya mara kwa mara. *We need to have proper and useful information.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nashauri utafiti ufanyike mara kwa mara ili Wizara iweze kutoa ushauri, maagizo na maelezo ya namna Sera ya Uchumi wa Viwanda uweze kutekelezeka. Utafiti ufanyike pia ili tujue changamoto za uendeshaji wa viwanda na utatuzi wa changamoto kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la ufafanuzi kwa Waziri: Je, Mheshimiwa Waziri, Wizara ina mpango gani wa kuhimiza ushirika na wenye viwanda hususan viwanda vidogo vidogo ili iwe rahisi kuwafundisha kupima maendeleo yao na kuona kwa kiasi gani viwanda vimepunguza hali ya umasikini na kuongeza ajira?

Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani kuhimiza mafunzo ya uendeshaji viwanda kwa ufanisi hususan Jimboni Ushetu?

Je, tutawatumiaje vijana waliohitimu mafunzo ambao hawana ajira kushiriki na kutumika katika ukuzaji wa viwanda?

Je, Sekta ya Viwanda inapunguza kwa kiasi gani mfumuko wa bei kwa kusogeza huduma ya masoko karibu na wananchi?

Je, hadi sasa kuna changamoto zipi za kiteknolojia kifedha, kisera na kiutawala ambazo bado hazijatatuliwa na zinazokwamisha maendeleo ya haraka katika viwanda vyetu na kwa namna gani changamoto hizi zitatatuliwa?

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iwasaidie wakulima wa mazao ya baharini:-

(i) Kuwatafutia masoko ya uhakika wakulima wa zao la mwani;

(ii) Kusaidia kuwapatia elimu juu ya mbegu bora ya mwani inayokubalika katika masoko ya nje ya nchi; na

(iii) Kuhamasisha wawekezaji wawekeze katika kujenga viwanda vya usindikaji wa mazao ya bahari, mfano mwani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora unaokubalika kwa matumizi na zinazohatarisha maisha ya mtumiaji na hasa bidhaa za chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa viwanda uzingatie ujenzi wa viwanda visivyoharibu mazingira, malighafi zake ziwe zinapatikana hapa nchini, Wizara iweke vipaumbele vya aina ya viwanda tutakavyoanza navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napongeza juhudi za Wizara katika juhudi zake za kufufua viwanda na kuanzisha vipya kwa nia ya kuongeza pato la Taifa na kupunguza tatizo la ajira kwa wananchi na kuweza kunyanyua hali zao za maisha. Ahsante.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya mbao laini (*soft wood*) inatoka kwenye viwanda vilivyoko Mafinga, ambapo kuna kiwanda cha SAO-Hill na viwanda vya wajasiriamali wa kati ambao wanaajiri kati ya wafanyakazi 100 - 200 kwa kila mwenye kiwanda, hii ni *direct employments*, achilia mbali *indirect employment*. Kwa ufupi, uchumi Mafinga, Makambako, Iringa na maeneo yote ya jirani unategemea sana suala la uvunaji wa misitu kwa nia ya kuvuna mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika kitabu chako Mheshimiwa Waziri, sijaona ukigusia viwanda vya mazao ya misitu, hususan viwanda vilivyopo katika Mji wa Mafinga. Kitakwimu, Mafinga na Mufindi inachangia pato la Taifa kwa kiwango cha juu. Mara kadhaa kama Wilaya imekuwa *ranked No.3* katika kuchangia pato la Taifa, mchango mkubwa ukitoka katika uzalishaji wa mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Serikali iwasaidie wenye viwanda vya kati kwa kuwadhamini ili wapate mashine za kisasa za kuchania mbao. Ilivyo sasa, hata kama mtu ana shamba la miti, mabenki yanaogopa kukopesha kwa dhana ya *risk* ya moto. Hawa wajasiriamali wakipata mashine za kisasa wataweza kutumia mabaki kuzalisha vitu vingine kama ulivyosema *tooth pick, chip board* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu umeme. Kiasi cha asilimia 30 ya muda wa kufanya kazi unapotea kutokana na kukatika kwa umeme. Nashauri Wizara ya Nishati TANESCO wafunge *sub-station* Mafinga ili kuondokana na tatizo la umeme. Kwa sasa umeme unaotumika unatoka Mgololo; na kwa kuwa Mji wa Mafinga umekua na viwanda vya kuchana mbao vimeongezeka, umeme unapofika, unakuwa umepungua nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitashukuru kusikia kutoka kwako kuhusu namna gani viwanda vya mbao vya wajasiriamali wa kati vitakuwa

incorporated kwenye michango ya Wizara na siku ufike na kuhakikishia hatutaagiza tenda *tooth pick* nje. Ahsante.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa hongera sana kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 60 ya tumbaku Tanzania inalimwa Urambo Mkoa wa Tabora. Je, Serikali hii haioni kuna umuhimu wa kiwanda cha Tumbaku? Kwa sasa tumbaku inasafirishwa kwa magari kwenda Morogoro jambo ambalo limepunguza kiwango au daraja la tumbaku, wakati huo huo barabara zinaharibika. Aidha, kuwakosesha ajira vijana wa Urambo na Tabora kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni umuhimu wa kuokoa matunda ya Tanzania kwa kushawishi wawekezaji?

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Nyanza Cooperative Union* wameshindwa kuendesha viwanda vya pamba kutokana na kuwa na madeni makubwa Benki. Pia kutokana na kupitwa na teknolojia ya viwanda walivyonavyo ambavyo sasa haviwezi kushindana katika soko kutokana na gharama za uzalishaji, kwa kuwa Serikali hivi sasa inataka kufufua viwanda vyote. Napenda kushauri Serikali kwanza kuwasaidia Nyanza kupata mbia ambaye atasaidia mitaji na teknolojia mpya katika *ginneries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita tunalima mananasi bora kabisa hapa Tanzania. Kwa muda mrefu zao la nanasi halijatumika kama kivutio cha uwekezaji na hivyo kupunguza uzalishaji kwa kuwa wakulima hawana soko la uhakika. Naiomba Serikali kupitia agenda ya Tanzania ya viwanda kutupatia mwekezajiwa Kiwanda cha Nanasi Geita na soko la nje la zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania inataka kuwa nchi ya viwanda, nashauri kila Mkoa upewe maelekezo ya kupima maeneo maalumu ya viwanda, yaani *industrial area*. Maeneo haya yatengenezewe hati na yamilikiwe na Halmashauri ili mwekezaji akifika usiwepo usumbufu wa kupata maeneo. Maeneo haya yapewe miundombinu ya umeme, barabara na maji ili kumfanya mwekezaji kuvutika na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa mitaji, naomba kushauri kwamba Serikali mara itakapokuwa imefanya utafiti katika eneo fulani na kuona panafaa kiwanda, lakini hakuna wawekezaji, utumike mtindo uliotumika Rwanda ambao ni kwamba watu wenye mitaji ya wastani wanaunganishwa kwa hisa na kupewa access ya kukopa kwa *collateral* kwenye Benki maalumu kama *TIB* na kuwafanya wazawa kadhaa kumiliki kwa pamoja kiwanda. Haya yamefanyika Rwanda na viwanda vingi vinafanya kazi.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa namna unavyoliongoza Bunge. Naomba kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kigoma Kusini liko Wilaya ya Uvinza, Mkoa wa Kigoma na ni Jimbo ambalo wananchi wake wanajishughulisha na kilimo cha michikichi pia ni wavuvi. Naomba Waziri aone namna ya kuwapatia wananchi wa uvinza miche ya michikichi ya kisasa inayozaa kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema wawekezaji wako tayari kuja kuanzisha viwanda vya mawese Uvinza. Namwahidi Mheshimiwa Waziri kama Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, niko tayari kuhamasisha wakulima wa zao la michikichi, kulima zao hili kwa nguvu zote na mimi pia nitakuwa mfano wa kulima zao hili la michikichi. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atupe kipaumbele kutuletea mbegu ya michikichi ya muda mfupi ili na sisi wananchi wa Uvinza tuweze kupata wawekezaji wa kuja kuanzisha viwanda. Pia nampongeza sana Waziri kwa mipango yake mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie viwanda vya uvuvi. Wananchi wa Uvinza pia ni wavuvi wa samaki na dagaa, hivyo, kwa kuwaanzishia viwanda itawasaidia wavuvi kupandisha thamani mazao haya ya uvuvi. Hivyo naomba Mheshimiwa Waziri, mipango yako hii mizuri izingatie kuwaletae wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini viwanda vya Mawese na Viwanda vya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara ya Ardhi mwaka 2011/2012 Bunge lilipitisha matumizi ya kuanzisha mabaraza ya ardhi na nyumba Wilaya ya Matano na Tunduru ikiwa ni mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Baraza la Ardhi la Nyumba halikuanzishwa na Serikali kutokana na bajeti ya Wizara kwa muda uliopangwa. Ndipo Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ikafuatilia Serikalini mipango hiyo ya uanzishwaji wa Baraza. Jibu lililotolewa ni kwamba Serikali kwa sasa haina uwezo wa kuanzisha Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba wananchi wa Tunduru wanapata taabu ya kusafiri kilometa 264 hadi Songea kufuata huduma za baraza. Halmashauri ikaona ni vema itoe jengo miongoni mwa majengo ya Idara ya Ujenzi na samani japo chache ili angalau Baraza liweze kufanya kazi. Je, ni lini Serikal itaajiri Mwenyekiti wa baraza la Ardhi la Wilaya ya Tunduru? Kwa

sasa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Songea Mheshimiwa Norbet Ndimbo ndiye anaetembelea Baraza la Tunduru kila baada ya mwezi mmoja na mara nyingine miezi miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaajiri watumishi na wahudumu wa Baraza? Kwa sababu sasa kuna mtumishi mmoja Bi. Vumilia Chipasura anafanya kazi ya Uhudumu, Ukarani na Uchapaji. Ikiwezekana basi, hata huyo kibarua aangaliwe kama ana sifa aajiriwe na aongezewe watumishi wengine kwani amejitolea kwa muda wa miaka miwili sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali ijenge jengo la kudumu kwa ajili ya Baraza la Ardhi badala ya kuazima jengo Halmashauri. Hii iendane na ununuzi wa thamani za Ofisi.

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inahitaji kwenda mbele kwa kasi. Ni jambo linalofahamika duniani kote kuwa tofauti muhimu ya nchi tajiri na masikini ni uzalishaji bidhaa za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kimetajwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu; kilimo hakiwezi kustawi bila ya viwanda. Wakati Serikali imelivalia njuga suala la viwanda hapa nchini, naomba kuishauri Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kutazama nyuma wapi tulikwama kama Taifa na wapi tulipo na changamoto ipi tunazokabiliana nazo. Kwa mfano, mimi nimetoka Iringa ambako kuna kiwanda kikubwa cha karatasi kilichopo Mgololo Wilayani Mufindi. Namwomba Waziri wakati wa majumuisho anisaidie kuwaeleza Watanzania, ziko wapi karatasi za Mgololo katika soko? Kwanini zikipatikana bei yake huwa ghali kuliko karatasi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinu cha kusaga unga Iringa Mjini kilikuwa chanzo muhimu cha ajira na soko la uhakika la zao la mahindi Mkoani Iringa na mikoa jirani. Mheshimiwa Waziri pamoja na kuwa na ulinzi, kinu hicho kipo katika sekta pacha ya kilimo na viwanda, tunaomba na kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa kinu hicho kiwe katika asilimia mia moja ya uzalishaji ili kukuza ajira na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amebainisha kuwa Sekta ya Viwanda ni msingi wa maendeleo wa Sekta ya Kilimo umetueleza kuwa asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo Iringa kama ilivyo baadhi ya Mikoa nchini kama vile Tanga, Morogoro na kwingineko, kuna uzalishaji mkubwa wa matunda ambayo mengi huishia kuoza mashambani kwa kukosekana kwa viwanda vidogo vya kati katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kuhusishwa kwa viwanda vidogo hasa katika maeneo ya uzalishaji ni ukombozi mkubwa kwa wakulima ambao wengi wao ni wanawake. Ufufuaji na uanzishaji wa viwanda utakuwa na maana endapo Wizara husika itaweka vipaumbele, kwani mwisho wa siku tunachotaraji ni kuwepo kwa viwanda vyenye tija. Tunapofufua kiwanda cha mbolea tutakuza ajira na kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima na kuongeza uzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiona ari na hamasa kubwa aliyonayo Mheshimiwa Waziri ya kuhakikisha kuwa Tanzania ya viwanda inawezekana. Wanawake wa Tanzania vazi lao ni khangha, naomba kushauri kwamba kifufuliwe Kiwanda cha Mutex na Urafiki.

Viwanda vilivyopo vimesababisha wanawake wengi sasa hawavai khangha kwa sababu ukubwa wa khangha kiurefu na upana ni mdogo sana. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na timu yake Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na *team* yake nzima ya wataalam inayoongozwa na Katibu Mkuu mzoefu Dkt. Meru. Nawapongeza kwa kutuletea Mpango mzima na mzuri wa mwaka huu 2016/2017. Hotuba yako imefafanua vizuri kwa muhtasari kabisa mwelekeo wenu kwa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze Serikali yetu kwa kuona umuhimu wa kuwa na uchumi wa viwanda. Mimi binafsi naona ni hatua kubwa sana na mwelekeo ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri masuala machache ili yafanyiwe kazi katika kuboresha dhana nzima ya uchumi wa viwanda. Tanzania suala la viwanda linawezekana sana. Tuna rasilimali nyingi na fursa ya malighafi za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni muhimu, Wizara ya Viwanda, Biashara iwe ndiyo Wizara inayoratibu masuala yote ya biashara na uwezeshaji. Iwe ndiyo kiunganishi (*coordinator*) baina ya Wizara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi na tozo zinazotozwa na Serikali na taasisi za udhibiti (*Regulatory Bodies*) pamoja na Serikali za Mtaa. Nyingi hujirudia na shughuli za taasisi za udhibiti hujirudia. Tunashauri nyingi ziondolewe au kupunguzwa na pawe na *One Stop Center* wakati wa malipo na wakati wa ukaguzi wote kama *team* moja ya Serikali na siyo kila taasisi kwa wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Regulatory Bodies* zisitoze na badala yake Serikali itoe bajeti za kuziendesha na itoze kwa wafanyabiashara sehemu moja na kugawa kwa taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nashauri pia tuwe na mfuko maalum wa kupata fedha za utafiti. Fedha za utafiti kila mwaka ni ndogo sana. Bila utafiti katika sekta zote hatutasonga mbele. Nashauri kwa kuanzia tutoze shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta kwenda kwenye mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa ndani wapo na wanahitaji msaada wa utafiti ili waweze kuwekeza katika viwanda vidogo na kati. Mitaji kwao siyo shida bali ushauri wa kitaalam na msaada wa kufuata sheria na kanuni ili waweze kuwekeza. Wizara ya Viwanda na Biashara inaweza kusaidia kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni katika eneo la uwekezaji wa kimkakati (*strategic flagship investments*) ya 2015 - 2020. Nashauri suala la Kiwanda cha Mbolea inayoendana na gesi asilia (*Urea plant*) ili tuweze kuzalisha aina zote za mbolea hapa nchini badala ya kuagiza urea ambayo ni moja kati ya msingi (*foundation compound*) ya mbolea zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie namna ya kukuza Sekta ya Biashara ya Mbegu ndani ya nchi. Tulikuwa tumefikia katika hatua nzuri sana kabla ya miaka ya 2004. Baada ya sera kubadilika na kutotoa fedha za kutosha katika taasisi zetu za utafiti na kuondoa kodi na tozo zote katika uagizaji wa mbegu za nje na kuendelea na kutoza uzalishaji wa ndani kwa aina zaidi ya kodi na tozo 26, sekta hii ilidorola na wazalishaji wengi wa nje walihamia nchi zinazopakana na sisi kuzalisha mbegu huko na kuleta nchini bila kodi na tozo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia ni kwa Sekta ya Madawa ya mimea na mifugo ambapo uzalishaji wa ndani hutozwa kodi na tozo nyingi lakini bidhaa hiyo hiyo kutoka nje haina kodi wala tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Wizara iangalie namna ya kuwa na Ofisi za *BRELA* kimkoa, tuanze na ofisi katika Kanda. Leo hii ingawa ipo *online* lakini bado ni lazima ufike ofisi za Dar es Salaam kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Serikali iangalie namna ya kuboresha huduma katika viwanja vya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Songwe. Leo hii mazao ya Sekta ya Mboga Mboga (*horticulture*) ya Kanda ya Kaskazini yote hupitia Kenya (Nairobi) badala ya KIA. Je, utafiti umefanywa kuwa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninashauri kama sababu ni biashara, tuangalie namna ya kuunganisha bodi zote za mazao kuwa moja na kila zao liwe na idara katika bodi hiyo. Hii itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa bodi hizo na pia wataalam waliobobea katika biashara ndio waongoze bodi na siyo uwakilishi wa kisiasa na uwakilishi sababu tu ya uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba bodi hiyo moja iangalie namna ya kusaidia sekta husika bila kuwatoza. Gharama za kuendesha itokane na uwekezaji na faida itakayotokana na biashara ya kuhudumia sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali iangalie namna ya kuondoa kodi kwenye vifaa na mitambo ya ujenzi na kuchimba maji zinapoagizwa (*import duty and VAT on earth moving equipment and drilling equipment*) na itoze kwenye shughui za kazi na siyo kwenye uagizaji. Hii itafanya ziwe nyingi nchini na zikiwa nyingi ushindani utakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri ili kulinda viwanda vya ndani, tutoe kodi ya VAT kwenye mafuta yanayozalishwa ndani ya nchi na tutoze mafuta ya kupikia yanayoagizwa kutoka nje. Pia tutoze tozo maalum kwenye *concentrates* za *juice* zinazotoka nje na tozo hiyo itumike kuboresha kwa kuagiza miche ya matunda tuzalishe ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutoze *dumping charge* kwenye chuma. Leo hii viwanda vyetu vitafungwa kutokana na mzalishaji mkubwa duniani kuleta chuma kwa bei nafuu. Wanafanya *dumping* kumwaga kwa bei ya chini ya gharama za uzalishaji wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie upya sera ya kulinda viwanda vya ndani badala ya kuangalia upatikanaji wa kodi inayotokana na uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Wizara ya Viwanda na Biashara ibadilike na wataalam wake badala ya kuwa wakusanyaji wa kodi na tozo tu, wawe washauri wa wafanyabiashara na wanaotarajia kuwekeza; wawe washauri katika kila sekta kwa kufanya utafiti na kushauri jinsi ya kuboresha sekta hiyo; jinsi ya kupunguza gharama, kupata mitaji, kupata teknolojia mpya na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *coordination and advice* hii iwe katika kila ngazi kuanzia Wilaya, Mkoa na Taifa. Wafanye utafiti katika gharama mbalimbali na tozo na kuishauri Serikali namna ya kuboresha biashara ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya TRA tu, huwa na uwezo wa kutoa ushauri na elimu ya kodi. Wizara pia inaweza kusaidia kutoa elimu hiyo. Muhimu hapa ni *mindset change* kuwa na mabadiliko katika fikra.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itumie Sheria ya PPP (*Public Private Partnership*) kufanikisha maendeleo ya biashara nchini na kuboresha mfumo ili uwekezaji ufanyike kwa tija. Naamini Waziri na *team* yake nzuri ya wataalam wanaweza na wataongoza mabadiliko ya kuelekea katika uchumi wa viwanda. Naunga mkono hoja.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya sukari; changamoto hii suluhisho lake ni uzalishaji. Tatizo ninaloliona ni kukosekana kwa utaratibu ndani ya Serikali. Hotuba ya Waziri ukurasa 140 ibara ya 191 inaeleza malengo ya kisékta ikiwemo viwanda. Hata hivyo, katika malengo tisa hakuna hata lengo moja kuhusu kuzalisha bidhaa zinazotumiwa zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya bidhaa hizo ni sukari, nguo na mafuta ya kula. Hata hivyo, ukisoma hotuba ya Wizara ya Kilimo ukurasa wa 25 na ukurasa wa 44; Wizara hiyo imeelezea mikakati ya kulima miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari. Ili miwa iwe sukari, tunahitaji viwanda. Wizara ya Viwanda na Biashara haina malengo haya. Je, Serikali haina uratibu? Serikali inasema sema tu bila uhakika isemalo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya miradi kwenye Wizara ya Kilimo inaweza kuzalisha tani 1.5m za sukari kwa mwaka. Kwa bei ya jana ya sukari na kupata \$500m za Marekani kama *forex*. Hii ni robo ya lengo letu la mpango wa maendeleo kwa sekta nzima ya viwanda. Naomba mlete *addendum* ya hotuba ili tuweze kuwa na lengo la kuzalisha sukari na kuondokana kabisa na tatizo la sukari. Napendekeza muongeze lengo katika ibara ya 191 *amendment* ukurasa wa 140, ongezea (i) na rekebisha (i) iwe (ii) na kuendelea.

(i) Kuhamasisha kuanzisha na kuendeleza viwanda vya bidhaa zinazotumika zaidi na wananchi kama sukari na mafuta ya kula. Hii ni pamoja na kuhamasisha viwanda vidogo vya wakulima kwenye maeneo yanayolima miwa ya ziada kama Kilombero na Mtibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapendekezo hayo hapo juu, naomba pia kuisitiza kuhusu viwanda vya kusindika mafuta ya kula. Tanzania ina mawese na alizeti ambapo iwapo tukiweka nguvu kubwa kwenye kuzalisha mawese na alizeti tutaweza kuwa na mafuta mengi zaidi na hata kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma tuna mpango/mradi wa kulima hekta 100,000 za michikichi kwa mpango wa hekta moja kwa familia

moja. Iwapo tutafanikiwa tutaweza kuzalisha tani 200,000 za mafuta kutoka nje yenye thamani ya dola milioni 240 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda inabidi ifanye kazi na Wizara ya Kilimo na Mkoa wa Kigoma ili kufanikisha jambo hili. Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Singida inaweza kuwa Mikoa ya kimkakati ya kumaliza kabisa uingizaji wa mafuta ya kula kutoka nje. Mipango iwekwe kwenye mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo litaondoa kabisa tatizo la ajira muhimu ni viwanda vya nguo (*Textile Industries*). Ukisoma hotuba ya Wizara ya Kilimo, unaona namna uzalishaji wa pamba umeshuka mwaka 2014/2015 kwa 47%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo azma ya Wizara ya Viwanda lazima iendane na malengo ya Wizara ya Kilimo kuongeza uzalishaji wa pamba nchini. Kuna hatua za kuchukua sasa hivi ikiwemo udhibiti wa ukwepaji kodi unaofanywa na waagizaji wa nguo nchini. Viwanda vya ndani vya nguo vinapata shida kubwa sana kutokana na magendo ya nguo. Pambaneni na magendo ya nguo ili tulinde viwanda vya ndani vya nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda ifanye kazi na Wizara ya Kilimo ili kuongeza uzalishaji wa pamba nchini na tuongeze thamani ya pamba kwa kuzalisha nyuzi, vitambaa na nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia; viwanda vya sukari, mafuta ya kula na nguo viwe vipaumbele vya juu kabisa kuanzia mwaka 2016/2017. Tuwe *focused*, tuwe na *sequence*; narudia; nguo, mafuta ya kula na sukari.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake za kuhamasisha viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni kuwa kutajengwa kiwanda cha samaki na utengenezaji wa boti: Je, mpango huo ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kufuatilia TBS kwa ajili ya kujenga shades za kukaushia samaki na dagaa, ikiwa ni sehemu ya kusaidia MSMEs na SMEs. Napenda kufahamu je, Wizara ina fahamu juu ya hilo ili kuendelea kuwasukuma TBS ikiwa ni sehemu ya mafunzo katika suala la usindikaji wa dagaa na samaki wenye ubora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hao wamekuwa waki-process dagaa katika mazingira duni, mbaya zaidi kuondoa sura nzuri ya fukwe za Ziwa Nyasa. Angalau basi tusaidiwe eneo la *Mbamba Bay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Waziri atasaidia kwa kuagiza taasisi zake *TBS*, *SIDO* na wengine anaowajua ili kusaidia na kuleta tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, asaidie kabla wananchi hawajanitumbua.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kidogo katika hoja hii muhimu katika kujenga Taifa letu. Ili nchi iendelee ni lazima iwe na viwanda vinavyozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka Mkoa wa Kilimanjaro ambao ulikuwa na viwanda kadhaa ambavyo vilichangia pato la Taifa, lakini kwa bahati mbaya hakuna kiwanda kinachofanya kazi kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee Kiwanda cha Magunia Moshi. Kiwanda hiki kimeshindwa kwa sababu kumekuwa na uingizaji mkubwa wa magunia toka nje na bei ya magunia hayo iko chini kuliko haya magunia yanayotengenezwa nchini kwetu na sababu kubwa ni kodi nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwanini nchi yetu kupitia Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki hamkai na kukubaliana kuzuia uingizaji wa magunia toka nje ili viwanda vilivyo ndani ya nchi zetu hizi viweze kufanya kazi na kuzalisha na kutoa ajira kwa wananchi wa nchi hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna umuhimu wa Serikali kukaa na wawezeshaji ili kujua matatizo waliyonayo ili kuondoa matatizo hayo waweze kuzalisha na hata kuuza bidhaa zao wanazozalisha toka kwenye viwanda vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie Mkoa wetu wa Kilimanjaro, tuna tatizo la ardhi. Je, Wizara ina mpango gani wa kututafutia wawekezaji wa viwanda vidogo vidogo kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wetu pamoja na Wabunge tunaotoka kwenye Mkoa huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo niliyotaka kuchangia kuhusu Mkoa wangu. Nategemea Mheshimiwa Waziri na wataalam wake wanafanyia kazi mambo hayo ili Mkoa wetu uweze kurudi kwenye hali yake ya zamani ya kiuchumi na kutoa ajira kwa wananchi wa Mkoa wetu.

MHE. ONESMO K. NANGOLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani ambayo inahitaji maendeleo ya watu wake, panahitajika pawepo na viwanda (Viwanda ni uchumi mama). Tanzania baada ya kupata uhuru wake tulikuwa na viwanda 125. Serikali ilisimamia viwanda hivyo kwa kupitia mashirika yake ya Umma, hasa baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki 1977. Viwanda hivyo vimeendelea kudhoofika hadi kufa kabisa. Kutokana na hali hiyo Serikali ilibidi kubinafsisha viwanda hivyo kwa sekta binafsi hapo mwaka 1990.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa nchi yoyote duniani inategemea uwepo wa viwanda. Bila viwanda maendeleo ya watu kwa sekta mbalimbali ni tatizo na matokeo yake ni watu kuendelea kubaki katika lindi kubwa la umasikini kwa wananchi wake. Hivyo basi, bila kuwepo viwanda, maendeleo yanarudi nyuma na uchumi unabaki kuendelea kuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara na Uwekezaji aliyotoa Bungeni hapo tarehe 5 Mei, 2016, nimesoma hotuba hiyo kwa makini sana. Serikali bado haijaonesha nia thabiti ya kukuza viwanda vyetu. Jambo kubwa hapa ninaloona siyo lazima kuanzisha au kuigiliza nchi zilizoendelea kuwa ni lazima kuanzisha viwanda vikubwa. Kutokana na bajeti hii ilivyo ndogo hatuwezi kufikia lengo la uchumi wa kati (itakuwa ndoto tu). Bajeti hii haioneshi matumanini ya dhati katika kukuza na kuendeleza viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kuangalia kwa umakini mkubwa, ni vyema sana tuanze kuimarisha viwanda vidogo hatimaye kufikia hatua ya viwanda vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora sana kwa Wizara hii kuungana na Wizara nyingine kama Wizara ya Kilimo, mifugo na maji katika kuanzisha tena viwanda vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Mkoa wa Arusha wananchi wengi wanajishughulisha na kilimo, ufugaji, utalii na biashara. Napenda kushauri kwamba Wizara hii ingeungana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, wawekezaji wakapatikana wakaanzisha viwanda vidogo kama vile eneo la Arusha, pakawepo na kiwanda cha maziwa; Longido, Monduli, Ngorongoro pakawepo kiwanda kwa ajili ya nyama na ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi nchi jirani wanafaidi sana na mifugo mingi huenda Kenya kwa njia za panya. Faida kubwa wanayopata kutokana na mifugo yetu ni ushuru kwa Serikali za Mitaa, kusafirisha nyama kupeleka nje na kupata fedha za kigeni. Viwanda vya Kenya wanapata sana ngozi ya mifugo kwa kukuza viwanda vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Mikoa ya Tanga ni vyema pia pawepo na kiwanda kwa ajili ya kutengeneza juisi. Machungwa na maembe yanayolimwa Korogwe na Muheza, mengi yanaoza kwa kukosa soko. Mengi yanapelekwa nchini Kenya kwa ajili viwanda vyao. Tumeshindwa kuanzisha viwanda hivi vidogo kwa ajili ya maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma sana hotuba hii, kwanza tunataka kujenga viwanda vikubwa na kujifananisha na nchi kubwa kama vile China na kadhalika; hatuwezi kufika huko. Hotuba hii imejaa sana historia na hamasa, hatufikii huko!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ifike mahali Serikali iijipange kwa upya na kuchagua maeneo machache ambayo nguvu ikiunganishwa kwa Wizara nyingine hasa Wizara ya Kilimo kuanzisha viwanda vitatu kwa kuanzia. Tuanze kwa viwanda ambavyo vitawagusa kwa haraka na mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda kama cha mbolea, Kiwanda cha Sukari na Kiwanda cha Mafuta; viwanda hivi vinatosha sana kwa kuanzia kukuza na kuendeleza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ina umuhimu wa pekee sana katika uchumi wa nchi, hasa katika kutoa ajira nyingi kwa wananchi wake, pia katika kuchangia pato la Taifa. Sekta ya Viwanda ni msingi wa maendeleo ya kilimo na ufugaji.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa weledi wake katika kuhakikisha juhudi za kujenga Tanzania ya Viwanda zinafanikiwa. Kusini mwa Tanzania ni eneo ambalo viwanda vya korosho vilijengwa kwa kuwa ndiko mali ghafi hii inakozalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa juhudi za Serikali zinahitajika katika kufufua viwanda hivi kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi yetu pamoja na wakazi wa maeneo husika. Jimbo la Masasi lina kiwanda cha kubangua korosho ambacho hakifanyi kazi kwa muda mrefu sasa. Naomba majibu ya Serikali kuhusu mpango wa kuhakikisha kuwa kiwanda hiki kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakusudia kutoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri ikiwa katika majumuisho Serikali haitatoa kauli kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LAMECK O. AIRO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo: Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa kuwa na aina nyingi za

matunda. Ninaishauri Serikali kama bado wataruhusiwa wafanyabiashara kuingiza *powder* ya kuchanganya na maji na kutoa *juice*, hapo itafanya wawekezaji wa viwanda vya kutengeneza *juice* kushindwa kuwekeza, kwa sababu kijiko kimoja cha *powder* kinachanganya lita tano za maji na kutoa *juice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kuhusu kiwanda cha maziwa Utegi; kiwanda hiki kilibinafsishwa kwa mwekezaji, lakini ameshindwa kwani mwekezaji huyo ameng'oa mashine zote na majengo kubaki magofu. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuchukua kile kiwanda na kumkabidhi mwekezaji mwingine ili wananchi zaidi ya 500 waliokuwa wakipata ajira kwenye kiwanda hicho waweze kupata ajira, hicho kiwanda kina eneo la hekta 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mchango wangu.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, nchi hii ina matunda mengi kama vile maembe, mananasi, machungwa, zabibu na mengineyo, Serikali haina sababu ya kuagiza *juice* na *wine* nje ya nchi kwa kuwa uwezekano wa kuanzisha viwanda vya *juice* na *wine* hapa nchini ni mkubwa, kuagiza *juice* nje ya nchi ni upotevu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mafuta ya kupikia ambayo ni ya pili kuingizwa nchini yakitangulia mafuta ya magari, Serikali ipige marufuku uingizaji wa mafuta ya kupikia kwa kuwa mazao ya kutengenezea mafuta kama vile karanga, alizeti na mawese vinapatikana hapa nchini. Alizeti inalimwa katika Mikoa ya Singida, Iringa, Mbeya, Rukwa, pamoja na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, uagizaji wa *toothpick* ungepigwa marufuku kwa kuwa tuna miti mingi inayoweza kutengenezea *toothpick*. Serikali ikizingatia haya yote tutaokoa fedha nyingi sana, lakini pia tutatengeneza ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa rasilimali tulizonazo za watu, mazao ya biashara tukiamua kwa dhati, tunaweza tukapiga hatua kubwa hasa tukijipanga vizuri. Ndani ya miaka mitano tuliyofunga mkataba na waliotuchagua, fursa zipo tukiamua hasa kwa kuanza na viwanda vidogovidogo ambavyo tunaweza kuanza navyo. Ili kuvilisha viwanda vya kati na baadaye viwanda vikubwa, kinachotakiwa ni kuundwa kwa mazingira mazuri ya uwekezaji, katika miradi mbalimbali kutokana na jiografia ya nchi yetu. Miradi hiyo ndiyo itakayounda ajira kwa Watanzania walio wengi na hao ndiyo watakaokuza uchumi wetu.

Kama nilivyoanza hapo juu kuwa tunayo rasilimali yetu ardhi, siasa safi na wajasiliamali. Hivyo tukiwatumia vizuri wajasiliamali, tukawawezesha tukawawekea mazingira mazuri kwa kila eneo, kufuatana na uzalishaji wao hasa katika mazao yanayotokana na ardhi, mito, maziwa, miti, mifugo na kadhalika huko waliko, ile idadi ya vijana kukimbilia mijini itapungua. Hebu tuisome ile Sera ya Taifa ya Biashara ndogo, na viwanda vidogo na tuitekeleze kwa kuisimamia. Sote twajua kilimo ndiyo kinachotoa, mapato kwa watu waishio vijijini, tukiamua kuanzisha viwanda vidogo vijijini vitaleta mabadiliko chanya, katika uchumi wa nchi yetu. Hasa vijijini kwa mazao yetu kuongezewa thamani, badala ya mkulima kuuza mazao yao kama yalivyo, viwanda vidogovidogo vitatumika kuyasindika mazao hayo. Mfano badala ya kuuza mahindi vijijini viwe na mashine za kusaga na kukoboa unga badala ya kuuza mpunga wauze mchele uliofungwa katika pakiti ndogo za kilo moja, mbili au tano huko huko vijijini tayari kupelekwa mjini kwa walaji, badala ya kuuza karanga na alizeti kama zilivyokuwepo, na viwanda vya kukamua mafuta, badala ya kuuza matunda kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujengwe viwanda vya kukamulia juisi, viwanda hivi mbali na kuongeza thamani katika mazao hayo, vitaongeza ajira huko huko vijijini na itasaidia vijana kubaki vijijini. Serikali itambue uongozi katika ngazi za Wilaya, na Mikoa kushawishi wawekezaji katika maeneo yao kufuatia fursa zilizoko zitenge maeneo kwa wawekezaji kwa kuondoa urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ile dhana ya kujitegemea ya ki-ujasiriamali nashauri Waziri wa Viwanda, awasiliane na Waziri wa Elimu ili kuingiza somo la ujasiriamali katika mitaala ya shule. Kuanzia ngazi ya elimu ya msingi, sekondari, na katika mafunzo ya ufundi stadi, hii itasaidia kupanua elimu na matayarisho ya kazi ili kuongeza hali ya kupenda kuanzisha na kuendeleza ujasiriamali, ili kuwafanya vijana kubaki vijijini. Vijana wakifundishwa ujasiriamali kuanzia msingi, sekondari na katika mafunzo ya ufundi stadi, watabadili mitazamo yao watapenda kujiajiri tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nijikite hasa katika suala zima la ujasiriamali, huko vijijini ili kupunguza idadi kubwa ya vijana kuja mijini kutafuta kazi (ajira) ambazo nazo hapo naomba tujipange vizuri. EPZ tutazipata katika Wilaya zetu na Mikoa yetu, fursa zipo tukiamua na kila mtu akatekeleza na kutimiza wajibu wake ndani ya muda mfupi tutapata matokeo chanya na tutabadilisha maisha ya vijana na kuinua uchumi wa nchi yetu Tanzania. Naomba niwaombe wataalam wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara yako wafanye kazi kwa kuzingatia weledi wao, tuangalie wapi tulikosea na tuparekebishe na tusonge mbele kwa ari mpya. Ili ile ndoto ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Watanzania kwa ujumla, Tanzania iwe nchi ya viwanda ili tuweze kuzalisha kwa matumizi ya ndani na baadaye tusafirishie nje ya nchi ili tupate pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza ajira na vijana wetu waweze kubaki katika maeneo yao ya uzalishaji, Mheshimiwa Waziri tulikuwa na viwanda vingi sana kabla ya kubinafsishwa ningependa kujua ni jinsi gani agizo la Mheshimiwa Rais umelitekeleza. Hasa kwa wale waliojitwalia viwanda na kuvitelekeza mbali na kwamba hadi leo hawajalipa pesa zote kufuatia na mkataba wa mauziano (MOU), ni hatua gani umezichukua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha nguo, kiwanda cha zana za kilimo asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima wa pamba, nyuzi, matairi, korosho, kahawa, asali, nyama na kadhalika, ni kichocheo cha upatikanaji wa ajira fedha za kigeni lakini nchi yetu itaitwa nchi ya viwanda. Nchi haiwezi kuitwa nchi ya viwanda wakati viwanda vilivyopo havizalishi katika uwezo wake na havizidi 200-500 tunakuamini Mheshimiwa Waziri, lakini tunakuomba ukaze buti wewe na Wataalam wako, ndiyo mtaifanya nchi hii kuitwa nchi ya viwanda. Ushirikiano na Wizara zingine nchini hii ni kutokana na kutegemeana. Pia chuo chako cha CBE Dar es Salaam nilichosoma mimi kitazamwe upya, elimu inayotolewa pale ni tofauti na zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba ya bajeti. Viwanda vidogovidogo vilivyokuwepo kwa tathmini ya mwaka 2012 imeonesha kulitolewa ajira milioni 5.2 na kuchangia Pato la Taifa (GDP) ambapo ajira hizo zilisaidia kuwezesha familia kujiendesha na kupunguza uzururaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, kiasi cha shilingi bilioni 81, kilichoombwa kwa mwaka 2016/2017 kinashabihiana na kasi ya Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli cha kutaka kujenga Tanzania ya viwanda kwa sababu asilimia 49.3 ya pesa zote zinaenda kwenye shughuli za maendeleo na asilimia 50.7 iende kwenye matumizi ya kawaida. Ili tuwe na viwanda ambavyo vitazalisha kwa uhakika, suala la miundombinu ya umeme, barabara na reli iwe imeimarika zaidi tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda, biashara na uwekezaji ni muhimu sana katika kuinua uchumi wa nchi yetu tunaomba Serikali kufufua viwanda vilivyokufa kwa kuzingatia gharama za kufufua viwanda hivyo. Kabla ya kuanza kazi ya kufufua viwanda hivyo, lazima kufanya *cost analysis* ili kujua gharama halisi ya viwanda hivyo, kama gharama ni kubwa ni heri kujenga viwanda vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanda vipya, kabla ya kujenga viwanda vipya, Serikali lazima kuangalia maeneo ya kujenga viwanda hivyo. Vitu vya kuangala ni miundombinu kwa mfano, barabara, umeme, gesi, umeme na ardhi, Serikali ihakikishe inaboresha miundombinu ili kuwezesha usafiri na uzalishaji wa bidhaa unakuwa imara na unaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya viwanda. Serikali lazima kutumia *technology* katika kuimarisha viwanda vyetu, vijana wetu lazima wasomee elimu ya kuendesha viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko. Serikali lazima ihakikishe inatafuta soko la bidhaa ambazo zitakuwa zinazalishwa katika viwanda. Tunajua Serikali haifanyi biashara lakini inaweza kuwezesha wafanyabiashara kupata soko la bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyetu. Viwanda ambavyo Serikali inaweza kuviboresha ni viwanda vya chai, korosho, pamba, ngozi, sukari na viwanda vya mbao ambavyo vipo Wilaya ya Mufindi katika Mkoa wa Iringa. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilima mia moja, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda; kwa kuwa wananchi wa Dodoma wanalima sana zabibu lakini hawana soko la kuuza na kiwanda cha kutengeneza au kukamua mvinyo wao ndiyo maana wananchi wanakata tamaa kulima zao la zabibu. Je? Serikali itawasaidiaje wananchi wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma wanalima sana karanga, zao la alizeti na ufuta, lakini hawana viwanda vidogovidogo vya kukamua mafuta, Serikali isaidie wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa mwelekeo wa bajeti uliowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi alisema Serikali inataka Tanzania kuwa nchi ya viwanda, kuelekea uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwenye hotuba hii imesema itawavutia wawekezaji waje kujenga viwanda hapa nchini, kwa mwendo wa kusubiri

wawekezaji waje wajenge viwanda hatuwezi kwenda na kufikia malengo ya Taifa tuliojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa miaka 10 sasa kila hotuba ya Viwanda na Biashara inaeleza kuwaita wawekezaji wa kujenga viwanda, ni kwa kiasi gani tumefanikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza Mkoa wa Tabora kunajengwa kiwanda cha Tumbaku ili kutoa ajira kwa vijana na ku-process tumbaku ambapo asilimia 60 ya tumbaku inalimwa Tabora. Tuelezwe ni mipango gani ya awali iliyofanywa ili kufanikisha azima hii ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Makaa ya Mawe kwa wingi sana kule Namtumbo-Songea. Kuna Malori zaidi ya 80 hadi 100 yanabeba makaa yale kila siku na kupeleka Kenya na kwingineko. Serikali itueleze, makaa hayo yanapelekwa huko kwa utaratibu gani, tunanufaika na makaa hayo ili kutuongozea nishati na kuokoa misitu yetu inayoteketea kwa uchomaji wa mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tuna misitu na mbao zenye thamani kubwa. Mbao zile zinasafirishwa kwenda nje na Mikoa mingine kutengeneza Furniture (Samani). Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tunapata kiwanda cha mbao Mkoa wa Tabora ili vijana wa Tabora wapate ajira na mbao ya Tabora iweze kuwa na thamani zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa ni dampo la bidhaa ambazo hazina viwango kwa kila kitu, vifaa vya umeme, nguo, viatu, vifaa vya ujenzi na kadhalika. Kwa nini Serikali imeshindwa kuweka sheria za bidhaa hapa nchini? TBS wameshindwa kabisa kudhibiti bidhaa duni hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango gani wa kuhakikisha bidhaa feki, duni na dhaifu haziingii hapa nchini? Sheria ya Uwekezaji inamtaka mtu anayekuja hapa nchini kuwekeza anatakiwa kuwa na mtaji wa kuwekeza na kutoa ajira kwa wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itueleze, Wachina na Wahindi wanaozagaa Kariakoo na maeneo mengine wakiuza maua, karanga, mitumba na kadhalika wanaruhusiwa na nani? Serikali imeruhusu ajira za wananchi wake zichukuliwe na watu wa nje ambao wanaitwa wawekezaji, tunakwenda wapi? Ni lini Serikali itahakikisha biashara ndogondogo zote hapa nchini zinafanywa na wazawa na hivyo kuwaondoa Wachina wote waliopo Soko la Kariakoo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa wawekezaji wamebadilisha matumizi na kufanya magodauni, vingine havijalipiwa fedha ya

kununuliwa na vingine vimeng'olewa mashine zote zilizokuwepo. Serikali inasema nini kuhusu viwanda hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe mazao yote yanachakatwa ndani ya nchi na hivyo kuongeza thamani tofauti na sasa ambapo mazao mengi yanasafirishwa ghafi na hivyo kukosesha mapato mengi Taifa na kupoteza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaacha kuagiza samani za maofisini kutoka China na hivyo kununua samani ndani ya nchi kutokana na mbao ya Tanzania. Hii ni aibu kubwa!

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake ikiwemo uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimp ongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba ambayo pia ameisoma kwa umahiri mkubwa sana. Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya Viwanda, napenda kuishauri Serikali kama tunataka kufikia lengo hili kwa ufanisi ifuatavyo:

Maeneo yote ya EPZA na SEZ ambayo hayajalipiwa fidia yakiwemo ya Kurasini, Bagamoyo na Mtwara wahakikishe kuwa fidia hiyo inalipwa kwa wakati na kusafishwa ili wawekezaji wasipate usumbufu juu ya upatikanaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu wezeshi, umeme wa uhakika, barabara na reli ni muhimu sana ili kuhakikisha tunazalisha bidhaa ambazo zitaweza kushindana na bidhaa nyingine kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata majibu kutoka kwa Waziri kuhusu suala la kiwanda cha Mbolea Msangamkuu Mtwara, ningependa kufahamu ni lini kiwanda hicho kitapatiwa uhakika wa kupewa gesi ili kiwanda hicho kianze kujengwa ninafikiri kushika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kweli kuwa nchi ya Viwanda, Serikali yangu ni lazima tuweke sheria za maksudi kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu. Nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha alizeti na mafuta ya alizeti na kulisha Afrika Mashariki, lakini tunashindwa kwa sababu ya mafuta ya kutoka nje ambayo hatuna hata uhakika wa usalama wa afya zetu. Naomba Serikali iondoe usumbufu kwa wawekezaji, tuangalie sheria zetu za kodi, utaratibu wa kupata ardhi kwa wawekezaji na kuthubutu kutoa maamuzi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, viwanda vya korosho ni muhimu sana kwa maendeleo ya wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kuchangia mambo yafuatayo zaidi ya yale niliyochangia;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara itoe elimu ya biashara kwa wananchi kwa kupitia Maafisa Biashara wa Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara ijitangaze kwenye *internet* kwa maana ya kutangaza fursa zilizopo Tanzania ili wawekezaji waweze kuona fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya *SIDO* vijengwe mpaka Wilayani ili viweze kutoa elimu kwa vijana kwa sababu viwanda vingi viko Mikoani sehemu nyingi Wilayani hakuna viwanda vya *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamiliki wa viwanda waangalie afya za wafanyakazi kwa sababu kuna viwanda vingine vinazalisha sumu kama maji ya sumu na unakuta wafanyakazi hawapewi *Boot* za kufanyia kazi au vitendea kazi. Nashauri Wizara iwe na Wakaguzi watakaokuwa wanakagua viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri katika hotuba yake, ukurasa wa 13 anasema kuna viwanda 37 vimefungwa, nashauri Waziri aje na *plan* kuonesha kwamba atafufua vipi viwanda vilivyobinafsishwa, ambapo tulikuwa na viwanda takribani 474. Pia atueleze mikakati ya hivyo viwanda 37 ikoje. Je, inaweza kuvunjwa kwa sababu katika kubinafsisha kiwanda kuna mkataba umesainiwa, je mikataba ya viwanda hivyo ikoje? Inaweza kuvunjwa bila madhara kwa Serikali kulazimika kulipa fedha nyingi kwa ajili ya kuvunjwa mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aje na *Plan*, atuambie ataanza kujenga viwanda vya aina gani, vya kilimo nikiwa na maana, viwanda vya mbolea au viwanda vya nguo au viwanda vya chuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara iwasiliane na Halmashauri ili ziwe zinatenga maeneo makubwa ya kujenga masoko na Mikoani ili wananchi waweze kuuza biashara zao. Mara nyingi unakuta Halmashauri inatenga maeneo madogo ya masoko tena mengine hayana hata *Parking*, matokeo yake wananchi wanapanga bidhaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu kama barabara, reli iboreshwe ili wawekezaji waweze kuvutiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni wa shida, Mkoa wa Katavi hauna umeme wa *Grid* wanatumia umeme wa jenereta. Kwa hiyo ili kuwezesha Katavi kuwa Mkoa wa viwanda inatakiwa Mkoa upate umeme wa *grid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji bado ni tatizo nchi nzima, viwanda haviwezi kijengwa bila maji, maana viwanda vingi vinahitaji matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijengwe viwanda vya kuchakata mazao ya asili kama pamba, mahindi, karanga, alizeti, ngozi, na tumbaku katika maeneo yanayozalisha hayo mazao bila kusahau mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itumie ardhi kama mtaji kwa wananchi.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa njia ya maandishi juu ya hoja ya Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufa kwa viwanda Morogoro; Mwalimu Nyerere alipendekeza Mkoa wa Morogoro kuwa Mkoa wa viwanda tangu miaka mingi iliyopita kwa lengo la kusaidia Jiji la Dar es Salaam kutokana na miundombinu iliyopo ikiwemo umeme, barabara, reli, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vilitegemewa na wananchi wa Morogoro, vilisaidia kupunguza tatizo la ajira, ambapo hata wananchi wale waliweza kuendesha maisha na kupeleka watoto shule, hali hii ilisababisha *population* na kupelekea kuwepo kwa vyuo vingi vikuu ambavyo vilitengeneza wanafunzi waliofanya kazi katika viwanda, lakini viwanda hivi leo hii vimekufa baada ya Serikali kuvibinafsisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kubinafsisha lilikuwa ni kuongeza uzalishaji na kupanua viwanda, lakini hivi sasa viwanda vimebaki kuwa magodauni, vingine vinafuga mbuzi na vingine vimebaki tupu baada ya wawekezaji wasio na nia njema kuuza vyuma vilivyopo ndani ikiwemo kiwanda cha Kanivas cha maturubai na kiwanda cha Asante Moproko kilichokuwa kinatengeneza mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijitapa kuwa inataka kuingia katika uchumi wa viwanda, lakini tutafikaje bila ku-review upya matatizo yaliyosababisha kufa kwa viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa Serikali, ipitie upya mikataba ya ubinafsishaji, ambapo baadhi ya wawekezaji wasio na nia njema walichukua viwanda kwa lengo la kujinufaisha ambapo wengine walichukua viwanda kwa lengo la kupata mikopo katika mabenki, ambapo wengine walichukuwa

mikopo na kufungua biashara zingine zikiwemo biashara za mabasi na malori badala ya kuwekeza kwenye viwanda na matokeo yake viwanda vimekufa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi zaidi ya 4000; mpaka sasa wengine wameshakufa, walikuwa wanadai fidia baada ya ubinafisishaji kwa lengo la kuwaendesha na kulipa vinua mgongo, lakini wafanya biashara hawa hawakuwalipa Wananchi hao hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka ama kupitia upya mikataba, ukaguzi wa viwanda vya Komoa, Kanvas, Asante Moproco, *Ceramic Unats, Tanaries, Tanzania Shoe*, ambavyo vyote vimekufa na vimegeuzwa kuwa mazalia ya popo na kufugia mbuzi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kufungia viwanda vya *Plastics* nchini; hivi sasa kuna zaidi ya viwanda 20 vya kutengeneza *plastics* vinavyotengeneza mifuko, ambavyo vingi vimefungiwa kwa sababu vinasababisha uchafuzi wa mazingira, kiwanda kimoja cha mfuko wa *plastic* kinaajiri watu 200 kwa viwanda, hivi 20 tunawanyima ajira watu 4000! Kwa nini Serikali isiye na *plan B* ya kuwataka wawekezaji hawa wa viwanda vya biashara kama vya mifuko kuagiza *material* ya kuoza mifuko badala ya kuja na hoja ya kuongeza *micro*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imevifungia viwanda hivi kwa kuvitaka vitengeneze mifuko minene yenye unene wa macro 50 kutoka kwenye *micro* 30 ya hivi sasa. Wawekezaji hao wana mikopo na walifuata utaratibu wote wa kupata vibali na kuwekeza, lakini badala ya kuja na mkakati rahisi kusaidia nchi iendeleo kuwa na viwanda sasa inaua viwanda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Uingereza, Kenya, Ethiopia, viwanda vya *Plastics* ndiyo vinasaidia kuongeza ajira na kuinua uchumi. Katika hili wamefanikiwa kutokana na ubunifu ambapo ungesaidia kuwezesha mifuko hii badala ya hapa nchini kuja na mkakati wa kufungia viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ije na *plan B* ya kusaidia viwanda hivi kwa kuruhusu ku-*import material* kuwezesha mifuko na hii itasaidia hata bidhaa zingine zinazotumia mifuko kama chumvi, viroba, sanzu na kadhalika. Lakini tukija na mpango wa kuwa na mifuko *macro* 50 mifuko hii itakuwa ghali na watu wa kawaida hawataweza ku-*afford*.

MHE. ISSA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajielekeza katika eneo la viwanda vidogovidogo kwani eneo hili likisimamiwa na kupewa kipaumbele litachochea na kukuza ajira, Wizara isimamie *SIDO* kuanzisha mitaa ya viwanda, mfano katika Jimbo la Mbagala Kata ya Chamazi, Charambe, Tuangoma, Kilungule na Kiburugwa zina maeneo ya kutosha kwa

ajili ya mpango huo, kutokana na idadi kubwa ya watu katika Jimbo langu naomba mpango huo utambuliwe na Wizara na kuanzishwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili; mchango wangu unajielekeza katika uwezeshaji wa wajasiriamali wa kati na wa chini kabisa. Uwezeshaji huu utasaidia sana kuinua kipato, pia uwezeshaji wa zana kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tatu; Wizara ifanye uhakiki wa viwanda vilivyobinafsishwa kama vinafanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa kwani viwanda vingi vimebaki kuwa maghala na magofu mfano *TANITA* kiwanda kilichopo Mbagala kimegeuzwa ghala la kuhifadhiya chupa chakavu. Serikali ikirejeshe kiwanda ili kiweze kuendelezwa kwa madhumuni yaliyo kusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nne; kumekuwa na ongezeko kubwa la viwanda vidogo vidogo vilivyoanzishwa lakini vimekuwa hatarishi katika mitaa na maeneo ya makazi. Wizara ihakiki viwanda hivi ili visilete madhara katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tano; Wizara iangalie uwezekano wa kuisaidia Halmashauri kujenga na kuboresha masoko yawe ya kisasa ili kutoa huduma bora na masoko yawe ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sita; Wizara ina hakika gani kupitia *TBS* kuhakikisha kuna mawakala wa ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi mfano magari yaliyopo Uingereza, Japan, Dubai na kadhalika. Uhakiki wa mapato, ubora wa uhakiki huo, umakini na uaminifu wa mawakala hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani, nawasilisha.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache sana ya kuchangia kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa ni wavuvi wamekuwa wakichomewa nyavu zao ambazo ni haramu, nyavu hizo zimeendelea kwa kiasi kikubwa kuzalishwa na viwanda na kusambazwa na wanafanya biashara kila kona hapa nchini. Kwa kuwa, hali hii inaendelea kuwafanya wavuvi kuwa maskini, wengi wa wavuvi wanachukua mikopo benki na taasisi zingine za fedha kama *PRIDE*, *FINCA*, *SACCOS* na kadhalika. Kwa muda mrefu sasa Wabunge tumekuwa tukitaka Serikali ya Awamu ya Tano kukomesha uzalishaji na usambazaji wa nyavu hizo ili zisiwafikie wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni mkakati gani uliopo kuhakikisha kwamba, nyavu hizo haramu hazizalishwi na kusambazwa ikiwa ni pamoja na

kudhibiti uingizaji wa nyavu hizo kutoka nje ya nchi? Naomba maelezo ya kina juu ya kuwepo kwa mkakati huo kama upo au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kwa kuwa nchi yetu ilianzisha mpango mahsusi wa uwekezaji wa EPZ wa kutenga maeneo ambapo baadhi ya maeneo Serikali ililazimika kuwaondoa wananchi. Je, mpaka sasa kwa nini eneo la EPZ Wilayani Bunda Mkoa wa Mara halijatekelezwa? Ni vema tukajua utaratibu wa uwekezaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo machache naunga mkono hoja!

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada na mikakati mbalimbali ambayo Serikali imechukua kufufua viwanda na kujenga viwanda vipya nchini bado naona kuna changamoto ambazo ni vema Mheshimiwa Waziri akazifahamu.

- Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kwanza kujifunza kwa nini viwanda vya zamani vilikufa?
- Ni vema kujifunza wapi tulikosea kama Serikali na kama nchi mpaka viwanda vikafa
- Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema tukajifunza changamoto zinazokabili viwanda vilivyopo sasa na namna ya kuzitatua. Sambamba na kukaa vikao vya kimkakati na wamiliki wa viwanda waliopo saa hapa nchini na kupata mawazo na ushauri wa uhalisia wa hali ya uendeshaji wa viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, viwanda vilivyopo vinakabiliwa na changamoto zipi?

- Kimasoko ya bidhaa zizalishwapo nchini?
- Upatikanaji wa nishati ya umeme ya kutosha na uhakika?
- Gharama za umeme?
- Sheria mbalimbali, rushwa na urasimu na kadhalika

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni lazima Wizara hii ishirikiane kwa karibu sana na sekta za kimkakati kama Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu na ofisi nyingine wezeshi ili kuweza kufanikisha dhamira hii ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kuwa na mpangokazi unaonesha ratiba ya utekelezaji wa kila hatua kuanzia sasa mpaka 2025. Pia ni vema Waziri atupe majibu ya changamoto zilizopo na namna atakavyozitatua na Wabunge tuko tayari kumpa ushirikiano kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuongeze bidii ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na kupunguza urasimu na vikwazo visivyo vya lazima ili kuhakikisha maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini, sekta binafsi kuwa nguzo muhimu katika kufikia lengo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni lazima Serikali isimamie taasisi za kifedha nchini kwa kufunga sera wezeshi ili Watanzania waweze kushiriki kikamilifu kwenye uwekezaji ni lazima kuwe na upatikanaji wa mitaji yenye masharti nafuu toka kwenye benki zetu nchini ikilinganishwa na benki za nje yanayokopesha wawekezaji wa nje ambao wanashindana na wawekezaji wa ndani kwenye soko moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ni vema nikamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye rehema. Ninakupongeza pia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kulisimamia Bunge hili Tukufu kwa umakini mkubwa. Pia nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipatia fursa na mimi kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie hapa “kufufua viwanda” na kufanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Ingekuwa busara kama kwanza tungefanya utafiti wa kina hadi tukaelewa chanzo cha kufa viwanda vyetu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kwanza tukaandaa miundombinu itakayoweza Tanzania kuwa ni nchi ya viwanda kweli. Umeme bado ni tatizo, umekuwa siyo wa uhakika unakatika hovy hovy, maji pia ni tatizo ni vema tungeboresha miundombinu hii kwanza.

Mheshimiwa Spika, ni vyema viwanda vyetu vikaanza na sekta hii ya kilimo kwani ni rahisi kupata malighafi. Tungetumia zana za kisasa sana pamoja na mbolea hata mbegu za kisasa ili kupata tija baadaye tukipeleka kwenye viwanda vyetu. Nyanya zipo kwa wingi, miwa ya kutosha na matunda mengine. Hata mpunga kama tutalima kisasa tutavuna vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenda kwenye viwanda vya *general tyre*. Mimi hapa napata mashaka kidogo, sidhani kama tutaweza kumudu soko vizuri.

Bahari yetu pia ina samaki wengi wa aina tofauti, samaki hawa wanavuliwa na wageni, ni vyema viwanda pia vikaangaliwa kushindika samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Tanzania ya viwanda tunayotaka ikaangalia mapema kuimarisha bandari zetu zote ambazo zitaweza kutuunganisha vizuri, tuweze kuuza vizuri mali zetu zitokanazo viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kabla ya kuanzisha viwanda tukaandaa mpango mkakati wa kuvilinda viwanda hivyo. Lakini pia ni vema kukawa na maelewano ya karibu sana baina ya Wizara ya Kilimo, Miundombinu, Biashara, Viwanda na Uwekazaji wakatengeneza “unit” ili wakafanyakazi kwa pamoja, kwa baadhi ya wakati ikawa ni rahisi sana njia za mawasiliano na kukamilisha kwa wepesi lile lililopangwa mashirikiano baina ya Wizara hizi yanahitajika ili tupate Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa hotuba yake nzuri na iliyosheheni mipango mizuri ya uchumi wa viwanda hapa nchini. Katika hii ninapenda kusisitiza Serikali ihakikishe uchumi wa Viwanda unajielekeza kwenye kuongeza mnyororo wa thamani (*value chain*) kwenye shughuli za asilimia 70 ya Watanzania ambazo ni kilimo, mifugo, uvuvi na Biashara ndogo na kati (*SMEs*) *The focus should be at the bottom of the population pyramid* ndipo kuna asilimia 70 ya wananchi au zaidi. Kwa kufanya hivi uchumi wa wananchi hawa ambao karibu wote ni maskini utakuwa na malengo ya nchi yetu wa kufikia uchumi wa kati (*MIC*) ifikapo 2025 yatafanikiwa. Aidha, tutakuwa tumepata uchumi wa viwanda wenye tija na weledi kwa Watanzania walio wengi. Ninaomba sana Serikali izingatie ushauri huu. Ninashukuru Mheshimiwa Waziri Mwijage kwa kutambua hili katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karagwe ni moja ya Wilaya nchini ambazo zinazalisha mazao mengi na kusaidia kulisha Watanzania hasa wanaoishi Mjini. Pamoja na mchango huu mkubwa wa kuzalisha kwa wingi mazao mengi hasa maharage na kahawa, sijaona Serikali ikileta wataalamu kuwapa mafunzo wakulima kuhusu namna ya kulima kwa tija na kuwasaidia mikakati ya kuwaunganisha na masoko. Kushindwa kufanya hivi kwa Serikali kumesababisha mazao kuharibika mashambani, (*Post harvest loss*) kwa miaka mingi kwenye Wilaya ya Karagwe na kwingineko Nchini. Je, kwa nini Serikali haijatenga bajeti ya kuwasaidia wakulima wa Karagwe na mafunzo ya kufanya kilimo cha biashara na kuwapa mikakati ya kuwaunganisha na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi wananchi wa Kagera kwamba Mkoa utajengwa uwanja wa Kimataifa kwenye

eneo la Omukajunguti lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mwijage sijaona wala kusikia fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza ahadi hii ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Aidha, sambamba na hii ahadi ya Mheshimiwa Rais, pia wananchi wa Kagera waliahidiwa na Mheshimiwa Rais *Special Economic Zone (SEZ)* sambamba na mipango ya uwanja wa ndege wa Kimataifa. Mkoa wa Kagera kijiografia umezungukwa na Miji mikubwa ya Afrika Mashariki ambayo kuwepo kwa SEZ na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa utakuza biashara za Mkoa wa Kagera na kusaidia kukuza uchumi wa Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapo simama kujibu hoja za Wabunge name nijibiwe katika SEZ na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Omukajunguti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewaahidi wananchi wa Kagera Kiwanda cha kusindika nyama kwa miaka mingi sana. Kuna eneo kubwa lililotolewa kwenye *Ranch* ya RAHCO ya kitengule takribani hekta 36,000 kwa mwekezaji huyu ila hakuna uwekezaji wa kiwanda cha nyama mpaka hivi sasa. Hii haikubaliki na ni mfano mzuri wa matumizi mabaya ya ardhi. Je, kwanini Serikali inatoa maeneo kwa wawekezaji ambao ni waongopaji na wakati kuna Watanzania wanakosa maeneo ya kufanya uwekezaji katika sekta ya mifugo? Naomba tamko la Serikali juu ya uwekezaji wa Kiwanda hiki cha kusindika nyama kwenye *Ranch* ya Kitengule. Aidha, Mkoa wa Kagera tuna maziwa mengi sana. Tunaiomba Serikali ituletee Wawekezaji wa kujenga kiwanda cha kusindika maziwa. Jirani zetu wa Rwanda wana ardhi na hali aya hewa inayofanana na Kagera.

Rwanda inasindika Maziwa yanaitwa Nyamo UHT na yanauzwa Afrika Mashariki nzima, Iweje Kagera ambayo ina ardhi kubwa kuliko Nchi ya Rwanda na tuna rasilimali ya ardhi na hali ya hewa ya kuwezesha uzalishaji wa maziwa mkubwa tusipate wawekezaji wa kusindika maziwa? Tunaiomba Serikali iweke *diary zone* Mkoa wa Kagera na miundombinu stahiki iwekwe ili kuvutia uwekezaji huo. Ninaomba tamko la Serikali kuhusu hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya saruji Mkoa wa Kagera ni mara mbili ya gharama ya saruji Mkoa wa Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvutia uwekezaji wa saruji kwenye Kanda ya Ziwa ili wananchi wa Mikoa ya ukanda huu wapate saruji ya bei nafuu kama wenzao wa Kanda ya Pwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuwapongeza Serikali na mpango wa Tanzania wa Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa unapoongelea viwanda unahitaji *infrastructure* iliyokamilika ambazo ni umeme wa kutosha na barabara ya kupitika kwa urahisi ambazo tunaipongeza Serikali kwa kuliona hilo na mnalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya sasa hivi ni dunia ya *processing*, ni vizuri Serikali iweke utaratibu mzuri kwa wawekezaji wa ndani na wa nje, wakubwa na wadogo wa kuweza kuanzisha viwanda kwa urahisi ikiwezekana kuwe na *one stop centre* ya kumaliza taratibu zote za leseni na vibali mbalimbali. Vilevile Mheshimiwa Waziri lazima akae na taasisi zake na wawe na *speed* ya kuweka Mazingira mazuri kwa yeyote anayetaka kuweka kiwanda *especially* vya *processing (processing Industry)*, napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri akija kwenye majumuisho ni vizuri awaeleze na kuwaelimisha Wabunge kwamba viwanda vya zamani huwezi kuvifungua, Hata mashine zilizopo sidhani kama zina vipuri vyake maana yake ni teknolojia ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa kufanyika ni kuhakikisha viwanda vya zamani vinapatiwa Wawekezaji ambao wataleta mitambo ya kisasa na kuanza upya. Hatuwezi kujadili yote haya kuhusu Viwanda bila umeme wa uhakika. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri awe na angalau taarifa za juu ni lini gesi yetu itakuwa tayari kuanza kutumika na kutoa umeme mwingi ambao utavutia wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba pia Waziri aje atoe ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali haifanyi Biashara na Serikali haijengi Viwanda, kinachofanywa na Serikali ni kuweka mazingira mazuri kwa Wawekezaji wa aina yote kuweza kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa kuwa wabunge wengi wanasimama na kuomba Serikali iwajengee Viwanda nadhani wakieleweshwa nia ya Serikali wataweza kuwa katika mstari mmoja wa kauli yetu ya Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwa kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ningependa kujua sababu ambazo zimefanya kiwanda cha Chai-DABAGA kutofanya kazi sasa ni miaka zaidi ya 15 wakati wananchi wanalazimishwa kulima chai, nitaomba ufafanuzi.

Ningependa nijue hadi sasa Serikali imejipanga vipi kuwawezesha wazawa zaidi kupunguza ukiritimba ili waweze kujenga viwanda vya matunda na nyanya katika sehemu za Ilula ambako nyanya nyingi zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iringa kiwanda cha usagishaji cha N.M.C kilichopo Iringa Mjini kimekuwa kikifanya kazi kwa kusuasua. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe ufike Iringa na utembelee Kiwanda cha Chai-DABAGA-Kilolo na Kiwanda cha usagishaji ili uone hali iliyopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Waziri na Wizara yake wawasaidie wananchi, wakulima kuona uwezekano wa kuleta sheria ambayo itamsaidia mkulima kuweza kuuza mazao yao sokoni na kwa kutumia mizani na siyo lumbesa. Tumeshuhudia hata viwanda vimekuwa vikinunua mazao ya wakulima kwa bei ndogo tena bila kutumia mizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri amtembelee Mtanzania Mzee Sallawa George aliyegundua jinsi ya kutengeneza Ulanzi na kuweka kwenye chupa bila kuharibika. Ninaomba Wizara yako imsaidie ili utaalamu wake usipotee. Wenzetu wa Kenya wanatengeneza juice ya Ulanzi, Bamboo Juice na mimi nitakuwa tayari kumuwezesha Mtanzania huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa jitihada na matarajio makubwa ya nchi kuwa na Viwanda na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Watendaji wote walioteuliwa nae, kwa kasi yenye uchungu wa maendeleo ya wananchi wa Tanzania kwa kuwapatia ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili.

Madhumuni ya kuanzisha *SIDO* ni kuwezesha kutoa ushauri na mafunzo kwa vijana wetu wajasiriamali kuboresha uwezo wa kujijaji kwao. Lakini Mkoa wa Rukwa kuna mapungufu ambayo yamekwamisha utekelezaji wa ufanisi na wenye tija wa *SIDO* kwa vijana na wajasiriamali wetu.

Majengo yapo, mashine zilizokuwepo hazipo kwa sasa, ambazo zilitoa ajira na mafunzo kutokana na hali hiyo majengo yamepangishwa kwa wafanyabiashara wa mashine za kukoboa mpunga na kusaga unga. Naomba Serikali kufuatilia majengo hayo na kurejesha mashine zilizokuwepo ili kufufua *SIDO* madhumuni yake kwa vijana na wajasiriamali wengi wao ni kina Mama.

Mapungufu yafanyikayo *SIDO*-Rukwa, kwa namna watoavyo mafunzo kwa vijana wetu na wajasiriamali kwa kufanya mchango kutoka kwa washiriki hao ndiyo wafanye maandalizi ya mafunzo. Inakatisha tamaa na mafunzo

hupatikana kwa wachache. Serikali ipange fungu maalum la kuendesha mafunzo kwani watalamu wapo bila ya kufanya hivyo watakuwa wanapata mishahara bure.

Serikali kuona umuhimu kwa Mkoa wa Rukwa kufufua SIDO kwa kuhakikisha majengo yake yanarejeshewa mashine zake na vijana, akina mama wajasiriamali waweze kufaidika na uwepo na SIDO Nchini

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa wapo vijana wa kutosha wanaomaliza elimu ya msingi na Sekondari wanakosa elimu ya kujiajiri, wanajishirikisha kwenye Ujasiriamali pasipo na uwelewa wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga wametenga eneo la kujenga chuo cha VETA lakini hakuna kinachoendelea. Ni vema Serikali ikaona umuhimu wa kujenga Chuo hiki kwa maslahi ya Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Waziri napenda kupata utaratibu na mikakati ya kufufua SIDO-Rukwa na ujenzi wa VETA-Rukwa katika kutukwamua huku pembezoni ambako hakuna hata viwanda vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tundaendelea na Mawaziri, tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atafuatia Waziri wa Nishati na baadaye Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujaalia neema ya uhai na jioni ya leo tunahitimisha mchakato wa Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika Wizara hii. Tatu naomba niseme naunga mkono hoja asilimia mia moja hotuba iliyoletwa na bajeti iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Naomba nikupe pongezi sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako nzuri ambayo uliwasilisha vilivyo, hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme masuala machache ambayo yameonekeni kwamba yanatakiwa kusemewa na Wizara yangu ya Fedha.

Sehemu ya kwanza kabisa naomba nianze na maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira alipopendekeza kwamba Serikali itoe fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kupelekea utekelezaji wa bajeti zetu katika Wizara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana na wazo hili, inakubaliana kabisa na mapendekezo haya na tunaona umuhimu kama Serikali wa kutoa pesa hizi kwa muda muafaka pale inapohitajika. Pia naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba utoaji wa fedha za bajeti unategemea upatikanaji wa mapato kwa mwaka husika, hivyo naomba pia tukubali kwamba sote na tunafahamu ni mashahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi tumedhamiria vilivyo kukusanya mapato, kuziba mianya yote na sote tunaona sasa tunaweza kukusanya zaidi ya asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika hilo, Serikali ya Awamu ya Tano pia imedhamiria kwamba Tanzania ya viwanda inawezekana na tunaanza mwaka huu na tumedhamiria kuanza kweli na ndiyo maana tumekuja na asilimia 40 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Tunaomba sana kama Serikali mtuunge mkono bajeti zetu, tupitishie, tumedhamiria na tumeonesha kwamba tunaweza kukusanya na sasa tunazipeleka pesa katika maendeleo asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja namba mbili ilikuwa ni Serikali na mamlaka zake ipunguze utitiri wa tozo na ushuru ikiwemo kuziondoa zile zisizo na tija. Mapendekezo haya pia tumeyapokea, tumeanza kuyafanyia kazi na kama sote sisi ni mashahidi tulimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema tozo zisizo na tija zote zitaondolewa. Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba kikosi kazi kiko kazini na kikao cha kwanza cha kushughulikia tozo hizi zisizo na tija kinafanyika kesho na tuna uhakika mpaka tunaleta bajeti ya Wizara ya Fedha hapa tutakuwa tumeainisha tozo zote zisizo na tija na zote zitafutwa ili tuweze kwenda kwa mwendo unaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba tu Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono pale ambapo tutaleta mapendekezo yetu na muweze kutushauri ili tuweze kwenda mbele kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu, maendeleo ya Watanzania na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ilikuwa imetoka kwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ambaye aliomba majibu ya kina yatolewe kuhusu ukomo wa bajeti. Akaenda mbele zaidi kuita kwamba uhuni wa Waziri wa Fedha katika kutenga ukomo wa bajeti. Naomba niseme hakuna uhuni hapa, kilicholetwa kama ukomo wa bajeti hakijatoka Wizara ya Fedha peke yake, haya ni maamuzi ya Serikali kwamba asilimia 40 sasa inakwenda kwenye maendeleo na asilimia 60 inakwenda kwenye matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba ukomo wa bajeti hautolewi na Wizara ya Fedha, unapita katika vikao maalum, tunaanza na vikao vya wataalam, nimewasikia Wabunge wakisema kwamba Mawaziri tunafika pale na tunawadharau wataalam, hapana. Kikao cha kwanza kabisa cha jambo lolote huwa ni wataalam wetu, wanatuletea

mapendekezo na mwisho Baraza la Mawaziri linapitisha ili kuleta hapa. Kwa hiyo, hata ukomo wa bajeti haukuwa uhuni, ila ilikuwa ni maamuzi sahihi kabisa na lengo sahihi kabisa la Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwamba sasa tunahitaji kuiona Tanzania ikikimbia, Tanzania ya viwanda inawezekana chini ya Dkt. John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja namba nne pia ilitoka kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba tupitie upya utaratibu wa kufanya *uplifting* ya kodi, naomba niseme pia katika tatizo hili, siyo tatizo *in such* au naweza kuita ni tatizo kwa sababu ya wafanyabiashara au sisi *final consumers*. Sisi ndiyo tunapelekea kuwa na hii *uplifting* na mimi siiti ni *uplifting* kwa sababu tunakwenda kwa *standard*, tunakwenda kwa sheria, hatuendi tu bila kufikiri, ukadiriaji wa bidhaa zinazolingia nchini, tunafahamu unafanyika chini ya Kifungu cha 122 cha Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki. Hivyo tatizo hii linaonekana kwamba ni kubwa ni kwa sababu tu kama nilivyosema wafanyabiashara wengi au watumiaji wengi wa bidhaa za kutoka nje, huwa wanafanya *under invoicing* yaani wanapoleta pale hawasemi ukweli bidhaa hii imelipiwa kiasi gani kutoka kule ambako imetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo sheria hii niliyoitaja haikutuacha hivi imetupa mwongozo, linapotokea tatizo kama hili sheria inaipa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania uwezo sasa wa kuangalia kutoka kwa *country of origin* ya ile bidhaa, bidhaa ile inauzwa kiasi gani na pia tunaangalia *data base* ya bidhaa zinazolingana, zinazofanana na bidhaa hiyo ili tuweze kufanya ukadiriaji halisi wa dhamani ya bidhaa ambayo imeingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa pamoja tushirikiane hii ni nchi yetu, tuipende nchi yetu, tunahitaji maendeleo siyo maendeleo kwa Chama cha Mapinduzi tu, ni maendeleo kwa ajili ya Taifa letu kwa ujumla na watu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaweza kuendelea kama tusipoweza kulipa kodi husika, kodi ambayo inaendana na bidhaa tunazolingiza nchini, hivyo, kama Mamlaka ya Mapato tutaendelea kusimamia sheria hii, hatuwezi kuwaumiza wateja wetu lakini tunasimamia sheria na pale ambapo mteja anafikisha bidhaa yake, pale kwetu tunafanya uthaminishaji kwa sheria hii na analipa kodi anayostahiili kulipa, hatuna sababu ya kumuumiza mteja wetu katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limeongelewa tatizo kwamba kumekuwa na vikwazo kwa wafanyabiashara kutoka Zanzibar kwamba bidhaa zao zinatozwa kodi mara mbili. Naomba niliseme pia jambo hili. Hakuna kodi zinazotozwa mara mbili kwa bidhaa zinazolingia Zanzibar kuletwa Tanzania Bara, kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, nilijibu hapa mbele ya Bunge lako Tukufu

kwamba kinachofanyika ni ukadiriaji kwa sababu sheria inayotumika kule upande wa Zanzibar siyo sawa na mifumo tunayoitumia huku Bara, kwa hiyo kinachotokea hapa bidhaa inapoingia Zanzibar inakuwa haijathaminishwa kwa kiwango kile kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo inapokuja huku hatutozi kodi mara mbili tunachokifanya sasa ni kuangalia ile tofauti ya kodi iliyotozwa kule thamani ya bidhaa ile Zanzibar na thamani ya bidhaa huku kwa hiyo tunachaji ule utofauti tu wa kodi ile ambayo haikuchajiwa na siyo kodi mara mbili. Serikali inawaangalia wafanyabiashara kutoka Zanzibar kwa jicho chanya kabisa, naomba mtuelewe Serikali ina nia njema na wafanyabiashara wake wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iliongelewa tatizo la kwamba Serikali itoe *temporary documents* kwa magari yanayokuja Tanzania Bara kutoka Zanzibar. Hili pia napenda kulieleza Bunge lako Tukufu ni kwamba hatuna sababu ya kutoa *tempoprary documents* kwa magari yanayotoka Zanzibar kuja huku Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya, magari yanayolipiwa ushuru wa dola ishirini siyo magari yanayotoka Zanzibar kuingia Tanzania Bara hapana. Ni magari yanayotoka nchi za jirani, nchi tunazopakana nazo kwamba watu wameingia nchini humu na magari yao wanataka kuyatumia na huwa tunawapa muda wa siku sitini, ndani ya muda wa siku sitini hiyo huwa wanalipa dola ishirini. Kwa magari yote yanayotoka Zanzibar kuingia humu nchini, kwa mfano Waheshimiwa Wabunge wamekuja na magari yao huku hakika huwa hawalipi hii dola 20, wanachotakiwa tu wao ni kueleza kwa Mamlaka ya Mapato kwamba ameingia nchini kwa muda upi atakaa hapa nchini, hivyo hakuna tozo yoyote anayotozwa mwenye gari anayetoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinacholalamikiwa kama nilivyosema mwanzo ni kwa gari zinazolingia huku moja kwa moja au zinazolingia huku kutoka Zanzibar kuja kuuzwa huku, kama nilivyosema mifumo yetu ya kodi haifanani kwa hiyo lazima tunafanya uthaminishaji upya kwa sababu hii ni gari inaingia sokoni kwa hiyo na pia kinacholipwa siyo kodi mara mbili kinacholipwa ni utofauti tu wa kodi ambayo ililipwa kule Tanzania Zanzibar na hatimaye inapoingia huku kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Raphael Japhary Michael pia aliongelea kuhusu tuiangalie upya *tax regime* kwa kupunguza *cooperate tax* na VAT kwa wafanyabiashara wa ndani, kwa sababu inapelekea *compliance* kuwa ni ndogo.

Naomba niseme kwamba kodi ya ongezeko la thamani ni kodi inayolipwa na mnunuzi wa bidhaa au huduma na wala siyo kwa mfanyabiashara, hivyo kodi hii wala haipelekei watu kutokulipa kodi au

compliance kuwa ndogo hapana, kwa sababu mfanyabiashara ni *agent* tu wa kodi hii kwa Serikali. Fedha yake huwa inarudishwa kwake pale ambapo anakuwa amerejesha na amelipa kodi husika kule Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *cooperate tax*, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hutozwa kwa faida baada ya kuondoa gharama za uendeshaji kwa mujibu wa sharia, kimsingi pia naomba niseme kodi hii haiathiri gharama za uendeshaji wa kampuni, kwa sababu hii inakuwa ni ile faida ambayo mfanyabiashara ameweza ku-*declare* kwamba amepata faida ndipo anapolipa *cooperate tax*. Kwa hiyo, katika kodi hizi mbili pia hazizui uwekezaji, wala hazisababishi *compliance* ya kulipa kodi kuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo napenda kuliongelea jioni ya leo ilikuwa ni kutozwa kwa kodi ya VAT kwa *transit goods*. Jambo hili pia limeleta changamoto kubwa sana na naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba kwa mujibu wa Sheria ya VAT ya mwaka 2014, mizigo inayopita nchini kwenda nchi za jirani haitozwi kodi ya VAT, hivi haya malalamiko yanayoletwa kinachotozwa kodi ya VAT ni zile tunaita *auxiliary services* ni zile huduma za msaada kwa ajili ya bidhaa hii kuweza kufika kule nchini. Kwa mfano, tunapokuwa na ulinzi tunapokuwa na *storage charges* hizi ndizo zinazotozwa VAT na siyo mzigo ule wala *transportation* yake haitozwi kodi hii. Hivyo naomba pia Waheshimiwa Wabunge, tuwaelekeze wafanyabiashara wetu, tuwaelekeze ma-clearing agency kwamba mizigo ya *transit* haitozwi kodi ya VAT hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha sasa ninamkaribisha Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na baadaye atamalizia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, mmi pia nitajielekeza kwenye sayansi na teknolojia, na maelezo yangu ni dakika tano hadi kumi tu kwa sababu ni sayansi na takwimu peke yake. Nimesoma kwa kina sana taarifa ya Mheshimiwa Waziri na nimesikiliza kwa makini sana michango ya Waheshimiwa Wabunge, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, ninakiri na kuamini kwamba wasiwasi walionao Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na ushamilifu wa tasnia ya nishati ya miundombinu mingine pamoja na viwanda, inatakiwa iangaliwe kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau niunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na takwimu za kisayansi. Tunapozungumza viwanda na biashara, tunapozungumza karne ya viwanda vya kati na ikiwezekana vya juu tunamaanisha miundombinu mingi sana na lazima nikubali kuna changamoto, siyo suala la siku moja wala mwaka mmoja. Lakini nishati kwenye viwanda ndiyo uchumi wenyewe, huwezi ukazungumza viwanda, huwezi ukazungumza chochote kama hujazungumza nishati ya umeme, kwa hiyo nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wengine wanaochangia kwa hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kutaja takwimu, Serikali namna ambavyo imejipanga na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lililopita kwa sababu mlipitisha mipango hii na sasa ni utekelezaji wake. Leo Tanzania tumegundua kiasi kikubwa kweli cha gesi ambacho mnajua sasa ni trilion *cubic feet* 57 wote tunajua, ni gesi nyingi kwa Afrika sisi ni wa kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza uwezo wa kuzalisha umeme, Tanzania kwa leo anayetuongoza kwa Afrika Mashariki ni Kenya peke yake mwenye *megawatts* 2,357, Tanzania ni ya pili. Tanzania tuna *megawatts* jumla wake 1554.12; Wanyarwanda wana *megawatts* 49, Waburundi wana *megawatt* 185; Waganda wana *megawatts* 185.6; kwa hiyo sisi ni wa pili na tunatembea. Tunakwenda mbali na hapa tunazungumzia umeme utakaozalisha viwanda vidogo vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza tuna uhakika wa umeme nimezungumza kwa ujumla wa *megawatts* nilizotaja, lakini bado tunaendelea na kugundua umeme wa maji, wenzangu wa Kigoma wamezungumza, Kigoma wanatumia umeme wa mafuta ni kweli na wanatumia zaidi ya shilingi milioni sitakwa siku, sasa umeme wa Malagarasi unakuja, tunaanza kujenga Malagarasi kuanzia mwezi wa tisa mwakani na ni ujenzi wa miaka mitatu, 2019/2020 umeme wa maji Kigoma unatembea na tunawatundikia umeme huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema umeme wa viwanda ndiyo huo tunaosema umeme unaotabirika. Sasa hivi wananchi wa Kigoma wanatumia takribani *megawatts* 15, sasa *megawatts* 44.8 za Malagarasi zinawatosha na maeneo ya jirani watautumia. Kwa hiyo, viwanda vya tumbaku vya Kigoma, viwanda vya samaki vya Kigoma, viwanda vyote vya nguo na kadhalika vitatembea sasa kwa umeme wa maji. Kwa hiyo, nataka kuwaondoa wasiwasi wanachi wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili niunge hoja mkono vizuri kwenye hoja ya viwanda nilikuwa nazungumza ugunduzi wa umeme, tunatoka sasa kwenye umeme wa mafuta tunaelekea kwenye umeme wa gesi na maji. Mwaka huu

tarehe 1 Aprili, tumeachana na umeme wa mafuta *megawatts* 70 wa Aggreko, kwa sababu tunataka kutumia umeme wa gesi tunaanza sasa kusafirisha umeme naomba wananchi na Waheshimiwa Wabunge ninapokuwa nataja zile *megawatts* muwe mnashangilia basi kwa sababu ni juhudi zenu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa na hizi ni juhudi zenu Waheshimiwa Wabunge leo *Kinyerezi I* tunazalisha *megawatts* 150 na tunaongeza *megawatts* 185 *extention* yake. *Kinyerezi II* Mheshimiwa Rais amezindua tena *megawatts* 240, *Kinyerezi III* *megawatts* 300, *Kinyerezi IV* itakuja baada ya miezi miwili *megawatts* 320, huo ni umeme wa gesi peke yake na bado tunaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara kuelekea Songea, *Symbion* na TANESCO wataanza tena *megawatts* 600. Waheshimiwa Wabunge, suala la umeme, suala la viwanda ni la kufa na kupona, Waheshimiwa Wabunge nizungumzie usafirishaji wa umeme. Tunaanzia Zambia, tunachota umeme Zambia unaoitwa ZTK tunasafirisha kwa *kilovolt* 400, tunautoa Zambia kuuleta Iringa – Mbeya kilometa 292, tunasafirisha *kilowatts* 400. Lakini tunautoa huo huo wa *megawatts* tunaupeleka mpaka Arusha mpaka Namanga, kilometa 412; sasa huu umeme unapita wapi siyo kwa watu na viwanda? Lakini bado tunapeleka umeme *North West Grid* wenzangu wanajua, umeme huo unatoka Mbeya unapita Sumbawanga, unapita Mpanda, unapita Kigoma mpaka Nyakanazi kilometa 1,284. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni *kilovolt* 400 za umeme na hapa tunataka tuwaeleze wananchi kwamba sasa umeme utakuwa ni uhakika, lakini bado tuna umeme unaotoka *North East Grid* kutoka Dar es Salaam *Kinyerezi* unapita kwa mwenzangu Chalinze Mheshimiwa Kikwete unakwenda mpaka Tanga, una kwenda mpaka Arusha kilometa 664 za umeme, zote ni *kilovolt* 400 lakini bado tunatembeza umeme huo kutoka Makambako kwenda Songea *kilovolt* 220 na ni kilometa 100 zote hizo tunatembeza umeme, tunatoa umeme kutoka Geita kwenda Nyakanazi *kilovolt* 220 kilometa 133, huo ni umeme na yote haya yanajenga viwanda vyetu. Waheshimiwa Wabunge naomba tukumbuke sasa tumedhamiria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya umeme, bei ya kuunganisha umeme sasa hivi ukijaza fomu ni bure, ukishaunganishiwa *service charges* sasa hivi ni bure, sasa tunataka umeme gani wananchi, Waheshimiwa Wabunge tutajenga viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelea kutaja ndugu zangu juhudi ambazo tumezifanya, sasa hivi tunapozungumza kuhusu ugunduzi pale Madimba - Mtwara leo tunazalisha trilioni themanini *cubic feet* za gesi na tunaweza

tukafikisha 130 tunachohitaji watu wajitokeze kuusomba umeme wa gesi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazalisha umeme mwingi wa gesi kuliko mahitaji pale Mtwara, lakini bado pale Songosongo tuna uwezo wa kuzalisha sasa hivi triloni *cubic feet* 130 hadi 200 na hakuna wanaousomba, tunasubiri viwanda. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, takwimu tunazosema ni za kisayansi na tunataka tujenge viwanda vya kisayansi na siyo maneno. Nilisema nitatumia dakika tano tu kwa sababu nikibaki humu nitawa-bore, lengo langu ni kuwaletea takwimu za kisayansi zilizokusudia kujenga umeme, viwanda pamoja na miundombinu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungemze jambo la mwisho ambalo tulieleza kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kwamba leo Watanzania wanaopata umeme kweli ni wachache asilimia 40 lakini tunakusudia ifikapo mwaka 2025 Watanzania zaidi ya asilimia 75 watakuwa wanatumia umeme wa uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani niendeleo lakini nataka wananchi na Wabunge wabaki na kumbukumbu hizi, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba sasa Awamu ya Tano inakuja na umeme unaotabirika wenye gharama nafuu na ambao pia sasa hautakuwa unakatika, tukishaunganisha hizi *kilovolt* 400 leo ni kweli umeme unakatika kwa sababu tunatumia msongo mdogo zaidi 132 na 220, ifikapo mwaka 2019, tutakuwa tumeshaunganisha miundombinu yote ya *kilovolt* 400 na umeme sasa utakuwa ni wa uhakika ambao utakuwa haukatikikatiki. Tunajipanga kwa hilo ili kusudi viwanda vya sasa viweze kujengwa kwa uhakika na wananchi wafanye biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache maneno mengi sipendi, nataka mtakapokuja hapa kupitisha bajeti yetu tutaendelea kutundika umeme katika viwanda ili vianzwe kujengwa na maendeleo yaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana, namkaribisha sasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, karibu.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri

wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, pacha wangu ambaye tunategemeana. Kwanza naunga mkono hoja hii kwa sababu watu wangu hata wakizalisha namna gani, kama bajeti ya pacha wangu haijapita watakosa mahali pa kupeleka bidhaa zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niseme kwamba bajeti hii ya leo tunayoipitisha ni jambo jema sana kama Waheshimiwa Wabunge wote tutaelewa dhana yake halisi iliyo kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kwanza hii ni bajeti ya kwanza ikiwa imebeba dhana hii ya kwenda kwenye Tanzania ya Viwanda na hivi tunapopitisha tunatengeneza pamoja na miundombinu yake ambayo inahusiana na suala hili la kukuza viwanda.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote tuelewe kwamba suala la viwanda siyo suala la Serikali peke yake wala si suala la Waziri wa Viwanda peke yake, ni suala ambalo linaanzia kuanzia uzalishaji, linakwenda mpaka kwenye kujituma kwa Watanzania na linakwenda mpaka kwenye uwekezaji ambao unatumia sekta binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno mengi ambayo yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge, Wizara imezingatia na mimi kwa sababu pacha wangu nakaa naye karibu hapa, kuna hatua ambazo ameendelea kuzichukua hapa ambazo ni maelekezo ya ufanyaji kazi wa mawazo ya Wabunge hata kabla hajasimama kujibu hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nijibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza ambazo zinalenga kwa pamoja kwenye Wizara yangu na pamoja na mwendelezo wa ushirikiano wa Wizara yangu pamoja na Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye jambo alilolisema Mheshimiwa Leonidas Gama, Mbunge wa Songea Mjini ambalo lilikuwa linahusisha kiwanda cha kuchakata mihogo kifanyikie hapa hapa Tanzania badala ya mihogo kusafirishwa. Wizara zetu tayari zimeshachukua hatua kwenye hilo kuanzia kwenye mahitaji ambayo yanahitajika katika kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa. Nimpongeze sana kwa hoja hiyo na kwa concern yake, lakini nimhakikishie kwamba hicho ndicho ambacho kitafanyika. Hivi tunavyoongea mwekezaji mmoja wa *Tanzania Agricultural Export Processing* tayari alishajenga kiwanda Pwani, na anategemea kujenga Lindi, Mtwara, lakini hivyo hivyo ndivyo itakavyofanyika katika maeneo mengine ambayo yanalima muhogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge, tuwahamasishe wananchi wetu waweze kujikita katika kilimo hiki kwa ajili ya

soko lililopatikana, lakini pia kwa mimi wa kilimo niseme kama moja ya chakula cha akiba ambacho kinastahimili katika maeneo mengi ambayo yana mtawanyo hafifu wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Mbunge Mukasa wa Biharamulo, Mheshimiwa Innocent Bashungwa Mbunge wa Jimbo la Karagwe na Mheshimiwa Mbunge wa Innocent Bilakatwe Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum mgeni kabisa hapa Mheshimiwa Oliver na yeye amesema, pamoja na hawa wanaotokea Ukanda wa Tabora pamoja na Shinyanga wameongelea zao hili la muhogo. Sisi kama Serikali tunawahakikishia uhakika wa soko, lakini pia maabara ambayo imeshapitishwa ya kisasa kabisa ya kuweza kufanyia tathmini zao hili, ili liweze kuuzwa popote pale duniani. Kwa maana hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunapoongelea viwanda Serikali tumedhamiria na tuna uhakika hatubahatishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania siyo mara ya kwanza kwa Serikali ya CCM kuamua jambo na likafanikiwa. Tuna mambo mengi ambayo yamefanikiwa na ninyi ni mashahidi. Niwaambieni siyo miaka mingi sana ilikuwa ukitaka kupiga simu inabidi uende kusubiria simu za kuzungusha zile. Hili sijasimuliwa nimeshuhudia mwenyewe, lakini kwa sasa hivi hata wanafunzi wa shule za msingi wana simu za mkononi, hiyo ndiyo CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siku nyingi ilikuwa mtu akitaka kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo lingine inabidi apange safari ya wiki nzima kwa hiyo, kama ana bidhaa zake atazipata baada ya mwezi mmoja. Lakini tuliposema tutaunganisha nchi hii Mikoa kwa Mikoa ili watu waweze kuwekeza na kusafirisha bidhaa, sasa hivi unaweza ukatoka na *taxi* Mtwara na *taxi* na ukaenda mpaka Mtukula kule kwa *taxi*. Ama ukatoka mpaka wa Zambia ukaenda Holili kwa *taxi*. Kwa hiyo, tunaposema tunaenda kwenye Tanzania ya viwanda tuna uzoefu wa kuamua jambo na tukatekeleza likafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza kuhamasisha uzalishaji kwa sababu, viwanda tunavyotaka kujenga siyo viwanda vya kuzalisha kwa wiki moja, tunataka viwanda ambavyo vitazalisha katika msimu wa uzalishaji na vizalishe katika msimu ambapo vina akiba ya malighafi. Kwa maana hiyo, jambo hili ni vema Watanzania wote tukaitikia kauli ya Mheshimiwa Rais ambaye ameshatoa dira kwamba tunaenda kwenye Tanzania ya viwanda badala ya kuanza kauli za kukatishana tamaa ambazo zinaweza zikawaacha wengine wasijue ni lipi la kufanya. Ni vema tukawa na kauli moja kwa sababu nchi hii ni yetu sote na mafanikio haya yakiwa ya Taifa itakuwa ni heshima kwetu sisi sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hili tulilosema la jembe la mkono kupelekwa makumbusho, jamani ni jambo ambalo linawezekana. Hatuwezi tukaendelea kujilaani kila leo kwamba sisi tutakuwa watu wa jembe la mkono. Tumedhamiria, tutatumia sekta binafsi, tutatumia jitihada za Serikali, tunaunganisha zote za sekta binafsi pamoja na jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba, tunaenda kwenye kilimo cha kisasa kwa sababu hatuwezi tukazalisha bidhaa za kutosha viwanda kwa kutumia jembe la mkono. Jambo hili lazima liwe na mwanzo na sisi tumepanga mwanzo ni sekta binafsi pamoja na sisi wenyewe Serikali, tayari tunakaa pamoja na Wizara ya Viwanda kwa ushirikiano wa Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayasema haya kwa sababu ndiyo tunaanza. Huu ndiyo wakati wenyewe wa kusema tumepanga nini na baada ya hapo tunaenda kwenye kutekeleza. Watu ambao mnakuwa na mashaka niwaambieni hiyo hairuhusiwi hata kwenye vitabu vya Mungu maana Mungu mwenyewe anasema mwenye hofu hatapokea kitu kwangu; *and a person who is incapable of even trying, is incapable of everything. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie, nimeshuhudia nikiwa mdogo Mkoa wa Singida watu walikuwa wanaenda kusaga unga wa kula mara moja katika miezi sita, lakini sasa hivi lile jiwe la kusagia lilishapotea. Kwa hiyo, hata jembe la mkono nina uhakika litabaki maeneo matatu; eneo la kwanza kwenye makumbusho, eneo la pili makaburini kwenye kuchimba makaburi na eneo la tatu kwa ajili ya kumbukumbu litabaki kwenye bendera ya CCM, ili itukumbushe tulitoka wapi.! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitumie fursa hii tunapochangia bajeti ya Viwanda na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote tuzingatie, tuwahamasishe wananchi wetu waepuke kuibiwa, wanaibiwa kwenye uuzaji wa mazao kwa lumbesa. Nimesikia malalamiko hayo kwa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, kwa Mheshimiwa Bosnia kule, nimesikia malalamiko kwa *Jah People* kutoka kule Njombe, kwa Mheshimiwa Hongoli pamoja na ndugu zangu wa Ludewa na maeneo mengine ambako wanazalisha mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaelimishe wananchi wote watumie vipimo rasmi. Hii wanayouza kwa lumbesa ni namna ambayo wanunuzi wasio waaminifu wanawadanganya kwamba hii ni namna ya kupakia lakini ndivyo ambavyo wanawaibia wakulima wetu. Baada ya kuwa tumeshaanza mwaka mpya wa fedha, vyombo vya dola visimamie ili wakulima wetu waache kuibiwa, likienda sambamba na wale wanaonunua mazao mashambani wakiita wanachumbia, kwamba kama ni migomba inakuwa bado ndizi hazijawa tayari kwa ajili ya kuuza, wao wanawekeza fedha kwa bei ndogo

wanaita kuchumbia na baadaye soko likiwa zuri wanakuwa tayari walishazinunua zikiwa bado ziko mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine limesemwa na shangazi yangu, Mheshimiwa Hawa Ghasia, la kuhusu kiwanda cha mbolea. Katika ukurasa wa 24 wa hotuba ya Waziri limeongelewa na hii ndiyo *connection* ambayo Mheshimiwa Zitto alikuwa anaitafuta. Niseme tu kwamba kwenye kitabu kuna maeneo ambayo yameongelewa *connection* ya uzalishaji pamoja na viwanda, mojawapo ni hili la kiwanda cha mbolea ambacho sisi tunakitegemea sana na liko katika ngazi ya Serikali pamoja na wawekezaji na Mheshimiwa Waziri atalielezea pia, atakaposimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utitiri wa tozo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ameliweka vizuri na niseme tu tayari Waziri mwenye dhamana alishaelekeza kupitia kwa Katibu Mkuu anayeshughulikia mambo ya uwekezaji kwamba ataratibu ile timu ya Makatibu Wakuu, ili kuweza kujua tozo gani za kuondoa, lakini pia na kuweza kuunganisha zile ambazo zitaonekana zinatakiwa ziwepo ijulikane ni nani anatoza ili pasiwepo na huu utaratibu wa kila mmoja kwenda kwa wakati wake na kuleta usumbufu kwa wanaochangia ili waweze kufanya shughuli zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili litaenda sambamba hata katika utaratibu wa kupata leseni ama vibali vya kufanyia kazi. Mtu akishamaliza eneo moja ajue kwamba tayari ameshamaliza katika utaratibu wa kupata vibali ili aweze kufanya shughuli zake za kibiashara. Serikali inalifanyiakazi kuweza kutengeneza mazingira ya kufanyia biashara katika nchi yetu ambayo ina fursa kubwa kuliko nchi nyingi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limeongelewa, amelisemea sasa hivi Mheshimiwa Mwamwindi linalohusu kinu cha Iringa. Vinu vingi vya Serikali vilikabidhiwa kwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na utaratibu huu tuliona pamoja na kwamba tuna *NFRA* ambayo yenyewe ni Hifadhi ya Chakula, tuliona tuwe na chombo kingine ambacho kinashughulika na mambo ambayo yanaweza yakawa ya kibiashara zaidi na hapo ndipo ambapo ilianzishwa hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Katika jambo hili tumesema hawa wakiwa sehemu ya ununuzi na tukachukua na lile wazo alilolisemea Mheshimiwa Serukamba la kuunganisha na sekta binafsi wanaotaka kufanyakazi katika maeneo haya ya kununua mazao, tuna uhakika kwamba wakulima wetu watakuwa wamepata soko pia, watu hawa wataweza kuweka uwiano wa bei, wakati bei ziko chini waweze wao kujitokeza na wakati bei ziko juu waweze wao kujitokeza ili wakulima wetu wasipate hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wazo lake tunalipokea na wafikishie wana-Iringa kwamba, hoja yako uliyoitoa Mawaziri wote wawili mapacha

wamelipokea kwa nguvu zote na watalifanyia kazi na waendeleo kukupa heshima ya kukuchagua kwa sababu umewasemea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo lilisemewa na Mheshimiwa Sabreena, amelisemea suala la zao la mchikichi kwamba halina Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Serikali jambo pekee ambalo tunaungana naye, Mheshimiwa Zitto Kabwe na yeye amelisemea mara nyingi kuhusu zao la mchikichi ni kwamba tunahitaji kuimarisha uzalishaji wa mazao haya ambayo bidhaa zake tunaagiza kutoka nje. Jambo la kusema tuanze na Bodi kabla ya zao lenyewe halijaanza kuzalishwa ama halijaanza kuwa na tija, tutaleta mgogoro na tutaleta gharama ambazo hazihitajiki. Kwa hiyo, jambo ambalo tunalifanya kama Wizara ni kuhamasisha wakulima waone kwamba pana fursa katika jambo hilo. Sisi kama Serikali kuweka kila jitihada kusaidia pale ambapo patahitaji msaada kuhakikisha kwamba wakulima hawa wanasaidiwa, lakini tukianza kusema kila zao tuliwekee bodi hata ambayo hayajaanza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hata juzi wakati nahitimisha hotuba yangu, nikasema ni lazima tufanye tathmini, kila taasisi tunayoiunda uhalali wake uonekane kutokana na kazi unazozifanya. Leo hii kwenye mpunga hatuna bodi, lakini nchi yetu inapiga hatua, inajulikana hapa Afrika na inajulikana hapa duniani, kwenye mahindi hivyo hivyo tunafanya vizuri, hatuna kesi ya kuibiwa, hatuna kesi ya wizi, hatuna kesi ya utapeli. Leo hii tukiwaza kwamba uwepo wa Bodi ndiyo utaibua mchikichi au utaibua alizeti, hili ni jambo ambalo mimi mwenye sekta nawashawishi lazima tutathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwenye mpunga, kwenye mahindi, wanayo tu bodi inaitwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, tunasema bodi zisipoweza kuondoa uozo unaojitokeza kwenye mazao haya yenye bodi na kwamba kama uwepo wao haujaweza kusaidia, tutawaza uwepo wa chombo kimoja ambacho kitaitwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaondokana na haya ambayo yanawakera watu wanaovuja jasho kila leo huku wakitozwa makato mengi kwa ajili ya uwepo wa taasisi nyingi ambazo tukienda kwenye uhalali haziwasaidii ama zimepunguza uhalali wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongelea kuhusu kushuka kwa uzalishaji wa pamba. Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Kiswaga, Mheshimiwa Kemirembe, Mheshimiwa Njalu pamoja na Mheshimiwa Nyongo na Wabunge wengine wanaotoka maeneo yanayolima pamba akiwemo Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani ambaye nimemuona ameongelea vizuri sana suala

la umeme, akanikumbusha enzi za Mheshimiwa Rais akiwa Waziri, jinsi alivyoweza kutaja maeneo yale anayoyasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameliongelea kwa machungu suala hili la zao la pamba akiwemo ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola kutoka kule Mwibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tunarejea katika misingi tujue kitu gani kimepotea hapa hata uzalishaji ukashuka. Tumeshaweka timu yetu na tunategemea baada ya kuwa tumeshamaliza bajeti na pacha wangu hapa akamaliza ya kwake tunaenda sasa kwenye utekelezaji ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza hii *chain* kuanzia kwenye uzalishaji tunaenda kwenye kutunza iliyozalishwa, tunaenda kwenye ku-process ambayo ndiyo inayoangukia kwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge tumpitishie Mheshimiwa Waziri bajeti yake, tumpe kazi, ili tuweze kuanza hii ramani ya kwenda kwenye Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia na niendeleo kusema kama mnaitaka mali mtaipata shambani na mali yenye tija inapatikana kwenye viwanda. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninampa fursa mtoa hoja, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili ahitimishe hoja yake. Karibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ninamshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kuongoza na kusimamia vema Mkutano huu wa Bajeti na mahususi majadiliano ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa usikivu na uchangiaji makini kwa hoja za maandishi na kwa kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Natambua na kuthamini dhamira na nia njema iliyotawala mjadala ambao kimsingi ulilenga kuboresha mikakati na mbinu za kisekta zitakazotekelezwa katika mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, Mbunge wa Igunga, Makamu wake Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata Likwelile, Mbunge wa Viti Maalum kwa

ushauri na mwongozo ambao umechangia katika kuboresha mipango ya kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Mheshimiwa Anthony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini, Waziri Kivuli wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa maoni yenye kulenga kujenga, kutoa chachu na hivyo kupanua mawazo katika kuinua ufanisi wa sekta hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa pongezi nyingi za utendaji wa Wizara na taasisi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Sisi kama Wizara tunaahidi kuendeleza jitihada zetu ili kuleta mafanikio endelevu. Aidha, tumepokea ushauri na michango mingi yenye chachu na changamoto ambazo kwetu tunazichukulia kuwa fursa muhimu katika kuleta maendeleo endelevu kwa sekta ya viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo sana, viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa na uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasilisho haya yanatambua na kuzingatia pia, hoja mbalimbali za Sekta yangu yaliyojitokeza wakati wa kujadili na kupitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais na Makamu wa Rais na pia Wizara zilionitangulia kuwasilisha bajeti zao hapa Bungeni. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, ushauri wenu na maelekezo ya Bunge hili katika kujadili bajeti ya sekta hii, tutayazingatia na kuyafanyia kazi ikiwemo kutoa mrejesho na utekelezaji wake.

Aidha, kutokana na muda mfupi nilionao katika kuhitimisha hoja za bajeti hii, maelezo na majibu ya kina ya michango mbalimbali yameandaliwa na yatawasilishwa rasmi kabla ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza katika kujibu na kufafanua hoja mbalimbali zilizojitokeza napenda kutambua michango ya jumla ya Waheshimiwa Wabunge 117 ambapo kati yao Wabunge 64 wamechangia kwa kuongea moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 53 wamechangia kwa maandishi, ahsante sana msiondolewe hapo.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa nijielekeze katika kujibu na kutoa maelezo kwa hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa mjadala wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo napenda niyakatae, niweke kumbukumbu sawa! Wizara yangu tangu nikabidhiwe, siwasemei walionitangulia, *it is not business as usual*. Wizara yangu tangu nikabidhiwe kuna mabadiliko na hata Mzee Komu nikutume Mheshimiwa Dkt. Komu, nenda kamuulize Mwenyekiti wa *Tanzania Private Sector Foundation* kwamba Mheshimiwa Mwijage mnamuonaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza katika mambo yatakayotekelezwa kwamba nitapigana kufa na kupona kuhakikisha Watanzania wote wanashiriki kwenye uwekezaji, *this is not business as usual!* Nimekaa na wataalam wangu, nina Profesa mmoja nguli wa uchumi, nina Profesa mmoja ana *Ph.D.* ya Uhandisi, mainjinia na wataalam wengine. Tumefanya kazi, ngoja niwaoneshe. (Kicheko/ Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkakati, ngoja niwaambie bwana! Wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Nimesimamia mimi na wataalam wangu tumetengeneza mkakati ambao Mheshimiwa Bashe anaulilia unaitwa *Cotton to Cloth Value Chain Strategy*, mkakati huu kazi nimeimaliza tarehe 2 Mei, Mheshimiwa Kabwe Zitto nihurumie nimefanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetengeneza Mkakati tarehe 2 Mei nimeuzindua, nimesafiri usiku kuja hapa. Mkakati unaitwa *Sunflower Sector Development Strategy*. Ntoa maelekezo Wizara yangu naomba mlete mikakati hii muiweke kwenye *pigeon holes* kabla Waziri wa Fedha na Mipango hajawasilisha, watu wanafanya kazi! *it is not business as usual any more.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza Mkakati unaitwa *Leather Sector Development Strategy*. Mheshimiwa Mabula anapozungumza kiwanda cha *Leather* cha Mwanza, nimekwenda Kashenamboni nikakuta kiwanda kile ambacho ukikiangalia unamkumbuka Mwalimu, mtu anaweka makatapila na matrekita, inatia uchungu. Nimetengeza mkakati wa ngozi. Nimemfuata mwekezaji wa ngozi ambaye alikuja hapa akizungushwa, amekwenda kuwekeza Kigali. Nambembeleza arudi hapa mnasema sijafanya kazi. *it is not business as usual.* (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie, unajua kuna mambo unapaswa kumwambia mtu usije ukamwambia mtu wa kwetu kwamba hufanyi kazi au hujaenda shule. Ukitaka kumuudhi mtu wa kwetu mwambie hujaenda shule, ndiyo maana nimekuja na mambo haya, ngoja niwaeleze, tumetengeneza mkakati, huu ni mkakati unalenga watu wa Lindi, *Value Chain Road Map for Pulses*, tarehe 2 Mei, ninao wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Faida, naingia saa mbili ofisini natoka saa nne usiku, *is not a matter of writing*, watu wanaumia na ndiyo maana Mheshimiwa Rais, akaweka Makatibu wawili wote ni nguli. Tunazungumza usiku na mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie *it is not business as usual* tumemshawishi mwekezaji toka Singapore, tarehe 23 mwezi wa kwanza nilikwenda Morogoro katika mradi wa AGOA nilikuta watu wa Mazava

wanahangaika, hawana mahali pa kufanyia kazi, nikawauliza nikiwapa eneo mtafanyaje, wakasema tutaajiri watu 7000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezindua eneo la *Star City Economic Zone*, ninatengeneza *shed* tatu, kuna watu wako tayari ku-relocate kutoka China na Pakstani kuja kuwekeza katika sekta ya nguo, wewe unasema *business as usual*, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisema hilo, niende kwenye suala la pili ambalo nasema na lenyewe siyo sawa. Watu wanasema hatuna mikakati, aah! Mikakati tunayo, kuna mkakati mwingine mdogo unaitwa *Development Strategy for Tanzania Textile and Apparel February 2016*, italetwa brother Chei. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *we trying to do everything*, soma mkakati wa *Integrated Industrial Development Strategy 2025*, soma hotuba yangu page 24 imeeleza tutafanya nini. Tutawekeza kwenye *fertilizer* na kwenye *petrochemicals*. Nimjibu Mheshimiwa Hawa Ghasia, *Ferrostaal* sasa hivi wako na matarajio, wako Kilwa wanaangalia kujenga kituo cha kuunganisha gesi, kutengeneza mbolea ya gesi kwa kushirikiana na Minjingu. Mtu wa *HELM A.G.* ambaye anategemea kuwekeza Msanga Mkuu matatizo yake kwa nini hajaanza ni kwa sababu anataka uthibitisho wa maandiko kwamba gesi itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatoa suluhisho la kitaalam na gesi itapatikana, mamlaka zitaamua na watu wa Mtwara mtatengeneza mbolea. Waheshimiwa Wabunge niwaambie mambo ya Mtwara, mbolea ya Mtwara ikianza zinazalishwa tani nyingi za mbolea, tutaweza kupata mbolea, muwe na subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Hawa Ghasia Mbunge wa Mtwara Vijijini. Mheshimiwa Mbunge huyu nilikwenda Misri nilimwakilisha Mheshimiwa Rais kwenye *business forum, Business for Africa*, nikakutana na mwekezaji anataka kutengeneza Kiwanda cha *sulphur*, nikamwambia nitampa kiwanja bure yule mwekezaji. Kiwanja mimi Mtwara nimekipata wapi. nikazungumza na Mbunge Mheshimiwa Hawa Ghasia ametoa eneo ambako huyu mwekezaji ataweka kiwanda. Mwekezaji huyu ametoka Misri, amepanda ndege, amekuja hapa, asubuhi ameonekana. Mheshimiwa nakuomba na katika Mstari huo hayuko peke yake, Mheshimiwa Bashe ametoa ekari 200 Nzega kujenga *Special Economic Zone*. Mheshimiwa Prosper Mbena ametoa eneo Morogoro Kusini. Waheshimiwa Wabunge tufuate namna hiyo, tutengeneze maeneo tutaweka utaratibu wa kuyaendeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo yaliyokuwa yananikereketa, ngoja niendeleo kujibu hoja zenu. Eeee! Mtu hawezi kusema *we are trying to do everything, we will end up doing nothing*, siyo kweli. Katika mkakati tumezungumza ni mbolea, ni mazao ya kilimo, halafu niwaeleze, ukisoma page 24 na ukasoma jedwali namba 16(c) inaeleza na nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Nsanzugwanko na Mheshimiwa Nswanzugwanko usimame uwaambie watu kama siyo mimi *Kigoma Sugar*, mradi wa kulima miwa kwa ajili ya kiwanda cha sukari ungeanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nazungumza sukari soma jedwali namba 16, wananchi wa Mbeya kuna mtu ametoka Marekani anataka kuweka kiwanda wanamzungusha, nimesharipoti kwenye mamlaka. Anataka kutengeneza tani nyingi za sukari halafu unasema *you are trying to do everything, you end up doing nothing*, usiniambie hivyo siwezi kukubali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende kwenye majibu ya jumla. Hakuna tofauti ya takwimu, Mheshimiwa Komu hakuna tofauti ya takwimu. Mheshimiwa Komu, Waziri mwenzangu lakini wewe ni Kivuli, hapa mwenzako aliyetoa hoja ndani ya Kamati yenu, tulipoletewa pesa nyingi kwenye *General Tyre* hoja ilitolewa na amerudia hapa. Ninyi ndiyo mlimwambia toa pesa hizi, nenda mkajitafakari muweke pesa zinazostahili. Tukatoka kwenye mamilioni yaliyopangwa tukabakiza shilingi milioni 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *General Tyre* ninachokwenda kufanya nitaleta watafiti nguli waanze *General Tyre* kwa mtazamo mpya ikiwemo mawazo ya Mheshimiwa Lema, amesema hapa mmemsikia. Sasa Mheshimiwa Komu kuna mtu mmoja ameniambia kwamba Mheshimiwa Komu alipokuwa akisoma ile *speech* ukimwangalia inaonekana mambo aliyokuwa anasoma alikuwa hakubaliani nayo. Haya ulikuwa hukubaliani nayo. (Makofi)

Kwa hizo takwimu Kamati ni kwamba ilipanga milioni 150, huwezi kujenga kiwanda cha *General Tyre* kwa shilingi bilioni mbili. Ameshatangaza tajiri namba moja *Social Security* zote amesema Arusha nenda muone Waziri wa Viwanda awaambie pesa zenu mtaweka wapi muache kutengeneza majengo tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Kivuli mwenzangu, huwa unanishauri na unayonishauri hapa uyasemi. Ananishauri vizuri sana huyu lakini akija hapa anabadilika, kwa hiyo mimi sina matatizo nayo, takwimu zangu ziko sawa sawa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda tunavyolenga vipo page 24 nimeshavisema na vimezungumzwa kwenye *Integrated Industrial Development Strategy*. Hakuna kitu chochote ambacho hatukusema. Kama alivyosema

pacha wangu kwamba ukitaka mali utaipata shambani, lakini ili upate tija yapitishie kiwandani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini, anakuja ndugu yangu anasema Mwijage unataka kujenga viwanda kila mahali, ndiyo nataka kujenga viwanda kila mahali. Sifichi, wala sipepesi macho nitavijenga kila mahali. Kiwanda cha kuchakata asali ni dola 40,000, Tabora ni asilimia 36 tu ya asali ya Tabora inachakatwa. Mimi hapa nina *order* za asali kwenda Oman, siwezi kuzipata. Katavi asali yenu yote haichakatwi. Ni Mbunge gani anaweza kwenda benki kukopa dola 40,000 akanyimwa. Nani anaweza kunyimwa? Nakushukuru, unajua tatizo la Mheshimiwa Lema anachangia mambo mazuri ukiondoa yale aliyoyafuta halafu anatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nunua kiwanda watakukumbuka. Uzuri wa viwanda, kwa nini mimi napenda viwanda vidogo, unaweza kufanya biashara ya *apples* au mvinyo wa zabibu, meli ikifika Dar es Salaam unauza kontena bila kuliona, unaweka pesa yako hapa unakwenda Kilimanjaro unashusha mvinyo. Lakini ukitengeneza kiwanda wewe mwenyewe unafaidi na jirani anafaidi. Ndiyo maana Mheshimiwa Magufuli anasema tujenge viwanda, ufaidi wewe mwenye mtaji na jirani afaidi. Mama nipigie makofi umeipenda hiyo. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kujenga viwanda hakuna itikadi, kwa hiyo tutajenga viwanda vidogo sana na tutajenga viwanda vya kati. Niwasimulie mfano mtakaupenda tena niwaambie ninyi rafiki zangu, Mheshimiwa Lema, ame-order kiwanda cha *toothpick* kwa ushauri wangu dola 28,000, ame-order kiwanda cha *Tomato Souce* kwa ushauri wangu, anataka kufuga samaki, mimi nina kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki, *the best in this country*. Msilogope kumiliki, watu wanaogopa kumiliki, mtu ana malori, anayaficha eti siyo ya kwangu, useme! tatizo ni kwamba uliyapataje? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, kwa hiyo ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mhamasishe watu wetu na tutajenga viwanda. Mheshimiwa Jitu Soni ninakushukuru pia. Mheshimiwa Jitu amesema kujenga *Petrol Station* moja ni milioni 700, hivyo ni viwanda vingi, mimi nimetoka kwenye *oil industry*, nawashawishi sasa wale nguli wa *oil industry* watoke na kundi la kwanza nalipekeka kwenye maziwa. ASAS ni nguli wa *petrol* amashakwenda kwenye maziwa, *Oil com* ameshakwenda kwenye maziwa, na nitakwenda kwa Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi, ndiyo maana nikamshukuru, nataka kuomba maeneo ya ile *nuclear farm* kusudi tutengeneze *farm*. Nina ajenda ya kwenda Musoma, nimekuwa namfuata kila siku Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, kuna shamba la Utege ili kusudi tutengeneze maziwa. Mnaweza mjiadini, mnaweza Waheshimiwa Wabunge na muwaambie wapiga kura wenu

wanaweza, msipothubutu ninyi waliopo nyuma yenu hawataweza kwenda kwenya uchumi wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba fedha uliyopangiwa ni kidogo, katika maazimio yangu ambayo nitayaboresha kumridhisha mjukuu wangu Mbunge wa Kigoma amesema uyaboreshe babu, nikasema nitayaboresha. Nitamuwekea kile anachopenda afurahi. Sasa mjukuu kama anapenda kitu mpe.

Katika maelezo yangu nimesema viwanda vitajengwa na sekta binafsi. Kitu kingine niwaambie, maelekezo ya Mheshimiwa Rais anasema tunaanza na viwanda vilivyopo, vizalishe *maximum capacity*. Kwenye ripoti yangu nimezungumza, viwanda vingi vinazalisha *below 40 per cent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaishangaa TANELEC, Mheshimiwa Rais alipokwenda Monduli ile ziara ya kwanza ya Jeshi, Mkuu wa Mkoa ambaye na yeye ni mjukuu wangu wa Arusha, akamfuata akamlalamikia TANELEC. Mheshimiwa Rais kwa utaratibu wake akamwambia anayeshughulika na viwanda ni Mheshimiwa Mwijage, akaja na watu wa TANELEC. Mimi lile nikalipeleka kwa Mheshimiwa Muhongo, tatizo la TANELEC ni sawa na *East African Cable*. Tumetengeneza umeme kwa Mpango wa REA II karibu kilometa 45,000 lakini hakuna waya ulinunuliwa hapa, *East African Cable* inatengeneza cable zile zile, haijauza kwa miezi 36. Lakini huwezi kunilaumu mimi ndiyo naanza sasa nije nione mtu anaziagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema katika hotuba yangu kwamba nitakuwa mboni ya kuhakikisha Wizara yoyote, Mtendaji yeyote, Shirika lolote la Umma linalokiuka nitawasemea na mnajua nitawasemea wapi. (Makofi)

Kuhusu mipango ya Wizara haiunganiki siyo kweli, huyu ni Waziri mwenzangu wa Kilimo, ni pacha wangu, hata juzi Mheshimiwa Mtolea wakati tunahangaika namna gani tulipeleke jembe kwenye makumbusho, tumekutana mimi nilikuwa *chairman* na chini yangu walikuwepo Makatibu Wakuu watano. Wawili kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Makatibu Wakuu watatu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Tunajadili namna gani tunaweza kupata zana za kilimo, kuzitoa huko tuzitoako, kwa riba nafuu, tukapeleka kwenye vituo ili kusudi jembe libaki kwenye bendara ya chama na watakaokwenda makaburini mlikute basi mambo yawe mazuri Mheshimiwa Mtolea.

Kwa hiyo usiwe na wasiwasi, tunafanya kazi kwa kuunganisha Wizara, lakini kama alivyozungumza mrithi wangu Mheshimiwa Kalemani ni kwamba mimi bila nishati sifanyi lolote, bila barabara sifanyi lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachumi mnaelewa. Kuna kitu kinaitwa *production cost na transaction cost*. *Transaction cost* ni zile gharama za miundombinu, unaweza kuzalisha kwa gharama ndogo lakini kama usafiri ni mbaya bidhaa itafika sokoni imeshakuwa mbaya. Ninawategemea watu wa miundombinu na tunafanya kazi wote na ndiyo maana wanasema bajeti ya viwanda ni triloni 29 kwa sababu sasa tunatengeneza mazingira wezeshi. Miundombinu wezeshi, ni pamoja na maji umeme, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa Bagamoyo. Bagamoyo haiwezi kufanya kazi mpaka Kidunda ifanye kazi, litatatengenezwa birika lingine la kuchuja maji, kwa hiyo *we are connected, we are related and intergrated*. Kwa hiyo, kwamba hatuna mahusiano, hatukuunganika haiwezekani, *brother*. Mheshimiwa Rais, ana Mawaziri 19 kwenye *cabinet*, anatuona na ana simu zetu kila wakati tunazungumza, sisi ni timu moja inayokwenda kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini miradi ya Mchuchuma na Liganga, Engaruka Soda, *General Tyre*, miradi ya Ngaka inaitwa kuwa ni miradi ya kimkakati. Akaniuliza rafiki yangu, ninampenda sana Mheshimiwa Hussein Bashe, ana michango ya kiuchokozi, amenikumbusha zama zangu nikikaa pale, nilikuwa na michango ya namna hiyo muulize Mheshimiwa Ngeleja. Nilikuwa naweza kutetemeshwa *microphone*, ananiuliza uniambie *comperative advantage*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi hii kuna *comperative advantage*, kuna *competitive* na *absolute advantage* zote zimeunganishwa hapo. (Makofi)

Kuhusu *General Tyre* siyo kwa ufahari, *General Tyre* sina shida na matairi, nataka *General Tyre* irudi nyuma ichochee kilimo cha mpira Pemba na Unguja, ichochee Morogoro, ichochee Tanga tulime mpira. Lakini *General Tyre* tuna *advantage*, tuna *population* inayokua vijana wa sasa kila mtu akipata mshahara kwa kwanza anapeleka ile *salary slip* kwenda kununua gari. Niwaambie nimewahi kuwa Mtafiti Msaidizi wa Benki ya Dunia kuangalia usalama wa barabarani, *percent* kubwa ya hatari za barabarani zinasababishwa na matairi mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshwamwambia mtu wa TBS, na nitawaonesha *show* kama mnapenda *show*, watu wakienda na *video* mnasema wanakwenda na *video*, wasipokwenda nazo mnasema *business as usual*. Nimemwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa TBS, tutakagua matairi yote hata kama ni mapya, kama hayana siku ya kutengenezwa na siku ya ku-expire tutakwenda kuyateketeza. Piga makofi na hiyo mbona hampigi makofi? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuambizane, kwa hiyo *General Tyre, comparative advantage*, tuliyonayo tuna watu wanaweza kulima mpira, *but the comparative advantage we have, we have a young population* itakayopenda kuendesha magari. *That is the comparative advantage, comparative advantage* nyingine tuna ardhi, Mheshimiwa Lema amenipa heka 200. Hauwezi kupata heka 200 Ulaya, utaipata wapi? Kwa hiyo, tutaangalia *comparative, competitive* na ikibidi tuangalie *absolute advantage*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampenda Mheshimiwa Bashe, nililazimika kwenda kusoma Michael Potter, Tom Peter na Charles Andy kuangalia hivyo vitu vinazungumzaje. Kwa hiyo hii iko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchuchuma na Liganga ina maneno. Tunataka chuma pale, ndicho kiwanda mama. Lakini chuma ya Liganga inasema ukiweza ku-*extract* yale madini mengine, unapata faidi nyingine. Ukasema Mheshimiwa Bashe kwamba kuna makando kando ameyaona CAG. CAG alipokuja kuona makando kando mimi nilishayaona. Tarehe 23 Januari niliwaita watu wa NDC wakafanya *presentation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno nilikuwa nayasikia nikiwa kijiweni, nikawauliza, Katibu Mkuu ambaye alikuwa ni mfanyakazi wa NDC wakati anaanza kazi, akaita timu ya wataalam kutoka nje ya Wizara yangu, wameandika ripoti nzuri, tutaweka sawa, tuondoe makando kando, lakini mkakati wa Mchuchuma na Liganga uweze kuendelea. Ukitaka kuujua mradi huu muulize Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, akueleze, ni mradi muhimu. Lakini kuja kumpata huyu mtu haikuchukua siku moja imechukua miaka mingi, kuna mtu mmoja mshindani alisema naapa Mchuchuma na Liganga haitafanya kazi, kwa sababu yeye ana migodi sehemu zingine za dunia hii.

Kwa hiyo tupigane Watanzania, kama mtu atakuwa na makandokando tuyaondoe. Watu wa kwetu wanasema *osangile amazi, oshorome eboga* yaani unafukia kinyesi kusudi uchukue mboga uende, ukikataa utakula chakula bila mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini viwanda vilikufa, ngoja niwasimulie mlischangia siku mbili siyo mchezo. Kwenye kitabu changu ukurasa wa nane aya ya 14, nimezungumza ngoja niende taratibu mnisikie. Mfumo wa kiuchumi ulikuwa mfumo hodhi, ndiyo maana viwanda vilikufa. Huwezi kununua *raw materials* mpaka upewe kibali na Kamati Kuu tumemaliza hiyo sasa ni soko huru. Kutozingatia viashiria vya nguvu za soko katika kuendesha uchumi wa viwanda, ndiyo maana vilikufa, lakini msisahau lilikuja lile wimbi la *globalization* (utandawazi), ule upepo tusingeweza kuuzuia na ninyi mnajua madhara ya upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana upepo ulitaka kupita hapa, *alhamdulillah* Mwenyezi Mungu akatuokoa upepo ulikuwa umekuja vibaya, upepo ulikuwa umekuja vibaya kwa hiyo huwezi kuzuia upepo. Mpaka akatokea jamaa mmoja akazuia mafuriko kwa mikono, ni mambo ya ajabu ajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine viwanda vililenga kukidhi mahitaji ya ndani, viwanda vililenga kukidhi mahitaji ya ndani tu sasa tumekataa, ni *import substitution cum export promotion*, nimesema kwenye hotuba yangu wazalishaji wa Tanzania nitawalinda lakini msibweteke, nitawalinda wasibwete walenge kuzalisha katika soko la dunia, hata tairi tutakazozalisha zitakuwa zinalenga dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni menejimenti ambazo hazikuzingatia ujuzi pamoja na *study*, na *technical know who*, iliingia pale. Nataka niwaeleze ninayoyajua bila kuwaficha kitu. Mtoto wa shangazi unampa kazi mambo yanaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuyumba kwa uchumi wa Taifa hili, kulikosababishwa na kuyumba kwa uchumi wa dunia, ukumbuke *oil crisis* ya miaka 70 lakini msisahau na nichukue fursa hii kuwashukuru Watanzania mliokuja kupigana vita ya Kagera hadithi ingekuwa nyingine, vita ya Kagera ilitusumbua, wengine mikanda haijawahi kufunguliwa, kwa hiyo na yenyewe ilituyumbisha. Viwanda vikayumba tukaingia kwenye mgao wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaeleze Watanzania haya mnayajua ila mnataka kujifanya hamyajui. Ujenzi na uendeshaji wa viwanda ulitawaliwa zaidi na matakwa au matashi ya kisiasa bila kuzingatia zaidi nguvu ya soko. Kwa hiyo, viwanda tutakavyovijenga, nimeeleza kwenye hotuba yangu itazingatia upatikanaji wa malighafi, soko na teknolojia, lakini na utulivu. Ngoja niwaambie *research* moja imefanyika, nazungumza na watu mbalimbali Morogoro iko juu katika *disciplined labor force worldwide* Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitawaambia mambo yote *disciplined work force* Tanzania wanasema iko Morogoro, mtoto wa Kiluguru anashuka na mzigo anapanda na mzigo, anaweza kufanyakazi. Lakini ukimchukua mtu kwenye *pool table brother* amepiga *pool table* miaka mitatu, umuweke kiwandani saa sita hajazungumza Simba na Yanga au kigodoro, hawezi kufanya kazi. Habari ndiyo hiyo, tutazingatia mambo yote hayo. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji mdogo, *under capitalization* mtalelewa hiyo, nalo lilikuwa tatizo, utamaduni wa utegemezi wa wahisani kupita kiasi. *Donor over dependence syndrome*, mmemsikia Mzee Magufuli, anasema hata kama ugali nakula bila mboga ni wa kwangu. *Donor over*

dependence syndrome amelisema Mheshimiwa Magufuli, kwamba itabidi tutembelee kwa nguvu zetu na haya yalituangusha, wanakuletea kiwanda wanachotaka kukuletea siyo kile unachokihitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano ya kisekta na uratibu wa Wizara nimeyazungumza sina tatizo nayo, kuna vikao vingi vinahusika, dhana kuwa Serikali haina sera na mikakati endelevu kutoka awamu moja hadi nyingine hapana, wenzangu wamelizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *vision 2025*, ilipokuwa inaandikwa akiwemo Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, alikuwa bosi wangu mimi nikiwa Meneja wa gas, nilikuwa namuona anaandika imemalizika 1996, haijaanza leo ni Mzee Mkapa huyo. Tunapozungumza *sustainable industry development strategy* ya 2011/2015 alikuwa Mzee Kikwete, kwa hiyo kuna uendelevu, kinachowasumbua watu ni kutokusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza hizi nyimbo zina mafundisho yake, kwa nini Rais wetu anaitwa tinga tinga? Ni kwa sababu yeye ni kama tingatinga, tingatinga likifanya kazi baada ya masaa fulani hufanyiwa service tena kwa gharama kubwa, likimaliza kufanyiwa service linafanya kazi kama jipya, kwa hiyo wanaona kwamba ni mpya lakini ndiyo tabia ya tingatinga, ametoka service brother kwa hiyo tunachapa mwendo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera zipo zimeandikwa na zote nimekuja nazo ni hizi hapa, *sustainable industry development policy* ya 1999 inakwenda mpaka mwaka 2020, Rais alikuwa Mzee Mkapa, ngoja niwaoneshe *Integrated Industry Development Strategic* ya 2011, Rais alikuwa Mzee Kikwete, kwa hiyo kuna uendelevu, ndiyo tabia ya magari makubwa, likiharibika gari kubwa huwa linafanyiwa service linarudi barabarani utadhani gari jipya, gali kubwa halitupwi, CCM ni gari kubwa, huwezi kulitupa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *SIDO*. Wanasema *SIDO* imetengewa Mikoa mitano tu, hapana siyo hivyo, *SIDO* haijatengewa Mikoa mitano tu, hiyo Mikoa iliyotajwa ikiwemo Arusha tunaweka vitu vinaitwa *incubator*. Watanzania wakiwemo wanafunzi watakaonekana na ubunifu, tutawapeleka pale, watawekwa kiatamizi, wataangalia utaalam wao, Canada na India watatusaidia waki-graduate, tukiona wanaweza wanakwenda mtaani, itakuwa Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, zimeandikwa hapo, kwa hiyo pale ni center.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa yote, nitahakikisha kunakuwa *SIDO* na niwaambie, najadiliana na TAMISEMI Maafisa Biashara wa Wilaya nataka wapewe mamlaka zaidi siyo kukata leseni tu. Wawe wanawafundisha watu namna ya kufanya biashara na ujasiriamali, waingie hata kwenye mikutano ile

ya Halmashauri ile Menejimenti ya Halmashauri waingie pale, wafanye kazi, hakuna kwenda kukusanya leseni, unakusanya leseni biashara mtu ulimfundisha? Hiyo tutaizuia, tukubaliane hapa waende wafanye kazi na *SIDO* atakuwa *coordinator* wangu, yaani Meneja wa *SIDO* wa Mkoa, anaripoti kwa *Minister* moja kwa moja na mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaagiza *SIDO* watengeneze *catalogue* za mitambo yote midogo midogo ya milioni kumi, milioni ishirini, milioni thelathini, muwaoneshe Waheshimiwa Wabunge wakawaoneshe wananchi wao namna ya kuchakata maziwa, asali, kuchakata mihogo, kama ndugu yangu Mheshimiwa Bilago wa Kigoma nimemuonesha mtambo wa kuchakata muhogo, unahitaji shilingi milioni 12 unatengenezwa Morogoro pale, unachakata muhogo. Kwa hiyo, ndugu zangu vitu vipo ni jukumu la *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Mchuchuma na Liganga na CAG nimeishaizungumzia.

Kuhusu umuhimu wa *NDC* katika ujenzi wa viwanda nchini. *NDC* ni kutambua fursa, mimi bwana mkisema napendelea kwetu basi mtanilaumu tu, nirudi tena kuwapongeza watu wa kwetu Kigoma. Watu wa Kigoma wanafanya kazi nzuri, Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma na uongozi wao wa Mkoa wameanzisha utaratibu wametambua kaya laki moja, kila kaya ilime mawese heka moja, watengeneze ekari laki moja na nimewaahidi mniombee nidumu kwenye cheo hiki, nitawaletea wawekezaji wawekeze katika kiwanda cha mafuta ya mawese. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo inapaswa kuwa siyo kazi ya Serikali, kwa hiyo ndugu zangu kazi ya *NDC* niwaeleze watu wa Kigoma, wako Kibaha - Pwani, wanatengeneza shamba la ekari 4,000 na *outgrowers* watazalisha tani 60,000, mahitaji ya sasa ya mafuta ni 400,000 wanatengeneza 60,000 nimewaagiza waende Mbeya, nimewaagiza waende Rukwa, nimewaagiza waje Kigoma. Mtaalam wa mbegu za miwese nimeishampata anaitwa Mushobozi, anafanya kazi na Koffi Annan yuko Arusha, aje awatengenezee mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakuambia *business as usual* haiwezekani *it is not business as usual*, ngoja niwaambie, kuna mambo mawili napaswa niyazungumze nimetulia, moja la rafiki yangu Mheshimiwa Sungura. Mheshimiwa Sungura amezungumza maneno makali. Ubora wa vyakula niwasihi msinunue chakula chochote ambacho hakina alama ya *TBS*, maneno aliyoyasema Mheshimiwa Sungura siyo ya kuchekea, msinunue chakula ambacho hakina alama ya *TBS* kwamba mtu anachukua chakula sijui anaugua figo, sijui anakwenda kumsubiri Mungu amchukue siyo habari nzuri, kwa hiyo hilo naisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu utendaji wa CBE, CBE inasaidia kufundisha vijana wetu, CBE ninaisimamia, CBE nitaisimamia, tuhuma alizozisema ndugu yangu Mheshimiwa Waitara, watu hao waliniletea taarifa Ijumaa ile iliyopita nikazichukua mwenyewe nikazipeleka ofisini, nikampa Katibu Mkuu, nikamwambia mambo ya kufanya. Mambo ya kufanya ni pamoja na kumhusisha CAG, lakini mambo mengine ni ya kimamlaka zaidi, ni ya PCCB ni ya Polisi, nikayaancha kule. Waziri hawezi kwenda kupeleleza, na yule msichana aliyeko gerezani tangu mwaka 2012 aitwaye Rose ni mahabusu siyo mfugwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema mahabusu huwa hanyimwi mshahara, mimi sijawahi kwenda shule ya sheria na kwa umri huu sitegemei kwenda kwenye shule ya sheria lakini niwahakikishie kitu kimoja, nitaisimamia CBE.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie CBE mnisikie sasa, wasionijua wakawaulize niliosoma nao shule. Nitahakikisha CBE inakuwa shule ya viwango, kuanzia muonekano, ukimuona mwanafunzi wa CBE anapita utasema yule anasoma *marketing*, yule ni mtawala, hakuna mtepesho, hakuna mtu anavaa kama anakwenda kwenye vigodoro, CBE nitahakikisha naiweka kwenye viwango. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengine nimeishaweka wataalam Mheshimiwa Waitara tulia. Tukitoka hapa nitakwenda niwaone wajukuu zangu huko. Suala la kuangua mayai Mheshimiwa Waitara wewe una pesa za kununua *incubator*, *incubator* ya mayai ya shilingi milioni 20 inatosha ndugu zangu wa kule, nitasaidiana na wewe kutafuta eneo, tutengeneze eneo katika mpango wa Mitaa Mheshimiwa Waitara mimi sina ugonvi na wewe, kuniacha kwenye chama hiki haujakosea, nitakwenda kushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri waliochangia bajeti yangu. Nimshukuru Mheshimiwa Omary Mgumba, mfano wake wa korosho ulikuwa mzuri sana. Ametoa *literature* ya korosho, lakini tatizo la korosho watu wa korosho, mimi nimepewa maelekezo na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi na Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi tutakaa chini, matatizo mnayo wenyewe. Wamarekani wametoa *order* ya korosho tani 15,000 wako tayari kununua kwa bei zaidi ya 40,000 kwa kilo iliyokobolewa lakini kwa masharti, kwamba lazima ikobolewe na wananchi, *the poor* mnaowatetea

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nasikia za Chama chenu cha Ushirika zinakataa, imeishafika kwa Mheshimiwa Mwigulu na ninyi mtaitwa wadau na nimezungumza hata na makampuni yanayohusika ORAM walinifuata, nilizungumza hapa wadau wa korosho walinifuata, tutakaa chini jioni tujadiliane twende mbele. Hii sayansi ya korosho ina mambo mengi, ngoja niwaambie sayansi ya korosho, wameniambia kwamba unaweza ukaona korosho iliyotoka

Tanzania tani 150,000 korosho iliyotoka Tanzania India, unakuta ni 250,000 nimeyaona. Kwa hiyo, ukubali Shekhe nakushukuru kwa nipigia makofi, mtu akisema *business as usual* mkatalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja binafsi moja moja, nimeishamshukuru Mheshimiwa Omary Mgumba, lakini kuna watu akiwemo Mheshimiwa Nsanzigwanko, wamezungumzia suala hili, suala la *ease of doing business*. Kama wazungu wakirudi leo, kutupima kwenye wepesi wa kufanya biashara, Tanzania hali imebadilika, mojawapo ya eneo tulilokuwa tunapimwa ni wepesi wa kupata viwanja vya kuwekeza. Kwenye bajeti yangu nimeshukuru TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, wamefanya kazi nzuri. Mimi nimepewa hekta 800 kwa kazi ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na Mheshimiwa Lukuvi, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisha mwambia Mheshimiwa Muhongo tutoe bomba la gesi kutoka Mbagala, likatishe moja kwa moja liende Kigamboni. Tunaendelea nahangaika, sasa aliyenichekesha kwenye *ease of doing business* ni rafiki yangu Mheshimiwa Kubenea, akataka kuzungumza Omukajunguti, akasema nimesoma kitabu chote Mwijage hajazungumza Kagera, usinichonganishe. Watu wa Kagera wanajua kwamba Mwijage alilelewa na bibi yake, na bibi yake Mwijage Mko Omwami alimfundisha hadithi 1002, hadithi moja inasema hivi, bibi yangu aliniambia mwanangu ukiamka asubuhi kwanza unawe uso. Uso wangu mimi ni Kagera na wala simfichi mtu, kwa hiyo Omukajunguti itajengwa, tutaishughulikia Omukajunguti, maua yatatoka pale, ufugaji wa samaki nitajisahauje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utaratibu siyo kukimbilia haya, nataka niondoe kwanza mambo ya kwanza, Bagamoyo wananidai pesa sijazilipa nikachukue Omukajunguti niongeze nitaongeza matatizo. Lengo letu kwenye SEZ tutalipa maeneo tuliyopewa kwanza, tukishamaliza tunatafuta wawekezaji kwenye yale maeneo yenye vivutio, kuna watu wanataka ku-relocate kuja Tanzania. Tunataka tuyachukue yale, tuya-service hata kwa kukopa pesa, pesa tutakazopata twende kwenye maeneo mengine, wengine wanasema Mwijage mmekamata maeneo mengi, *we are not aiming for the next election, we are aiming for the next generation*. Tunakamata maeneo watakaokuja miaka 50 chama ni hiki hiki, watakwenda kwenye hayo maeneo watajenga. Kwa hiyo ndio mpango mzima. *It is not for next election, it is for next generation.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vietnam nimewaandikia wana *Special Economic Zone* 150, lakini Vietnam ni moja ya saba ya nchi yetu. Sasa ndugu yangu mimi naota kesho kutwa, ningependa vijana wakija wakiwa wanaangalia waseme alikuwepo Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles John Mwijage. Kwa hiyo hilo nimelijibu kwa hiyo *ease of doing business* tunaijua, na mojawapo ya *ease of doing business* ni katika kutoa haki. Mheshimiwa Rais ameliona, ametoa pesa za kutosha katika Mahakama

kusudi ipunguze, ninacho hiki kitabu, na nimeagiza kiwekwe kwenye *website* ya Wizara yangu, utakisoma hiki tunapimwa vipi, lakini ndugu zangu wasikudanganye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza na Mmarekani mmoja juzi, baada ya hotuba yangu imejadiliwa nchi nzima, na *CTI* wameijadili. Mmarekani amenipigia simu akasema Mwijage, yote uliyoandika ni bure nikasema eeh bure. Akasema *you didn't include important element* nikamwambia *what?* Akasema *peace*, amani yetu inatusaidia kufunika haya mapungufu lakini hatutabweteka, haya mapungufu tutayaondoa, na akaniambia kitu kimoja, Tanzania katika Afrika ndiyo nchi ambayo inatembelewa na Marais wengi wa Marekani wastaafu, hawawezi kwenda mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa nakushukuru sana, kwa hiyo fedha ya *General Tyre* nimeishajibu, dira ya maendeleo ya Taifa kuifanya nchi yetu kuwa ya uchumi wa kipato cha kati imetimiza miaka 21 bila mageuzi nimeisha lizungumzia. Kitu kimoja ambacho watu hawaelewi, kuna ule mpango wa kuanzia mwaka 2010, mpaka 2025 kipande cha kwanza ilikuwa ni kuondoa vikwazo. Vikwazo vimeondoka, sasa tunakwenda kwenye kujenga uchumi wa viwanda, tukimaliza tunakwenda kwenye ushindani. Kwa hiyo, kazi imeondoka sasa hapa kama ni ndege tunaanza mwendo wa kupaa, tumeshatenga maeneo, nimewaeleza taarifa za ukweli kuna viwanda vina-*relocate*, vina-*relocate* kutoka Asia kuja hapa, someni majedwali yangu nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu niingie Ofisini nimekutana na makampuni zaidi ya 32, kuna kampuni inaitwa *Goodwill* inakuja Mkuranga, muulize Mheshimiwa Mbunge wa Mkuranga, kuna Kampuni inaitwa *Goodwill* inakuja Mkuranga, itatengeneza kiwanda cha vigae kitakachozalisha *square* mita 80,000 kwa siku, *production* ya mwaka itaweza ku-*generate* dola milioni 150. Lakini kuna kiwanda ambacho mimi niliwezesha kupata ardhi Mkuranga Mzee Lukuvi nitakushukuru mara mia moja, kile kiwanda kitatengeneza ajira za watu 20,000 Mbunge wa Mkuranga anajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shamba Mkuranga ndio maana nakwenda kule kwa hiyo kazi inafanyika. Kwamba tumefanya nini, basi tulikuwa tunatoka kwenye *runway* sasa tunapaa, na tukipaa tunakwenda, kwa hiyo muwe na imani. Lakini nimezungumza kwenye mipango ya kazi yangu, kwamba nawaomba tukubaliane twende safari, asitokee mtu akawa na mashaka. Tukifika njiani mkaona tunapotea mniambie tunapotea na niwahakikishie, hii hotuba na michango yenu, kuna michango imeandikwa ya maandishi inastahili kuandikiwa kitabu. Wale ambao michango yenu itakuwa ina mapungufu, nitawarudishia mui-*edit* vizuri, nitaweka picha zenu pale na nitaandika majina yenu, mchango wa Mbunge fulani ili kusudi muweze kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuangalia suala la Omukajunguti, nimelijibu, uwanja wa ndege utajengwa Serikali isuke upya taasisi zinazoshugulikia viwanda, biashara na uwekezaji ili kuziba mianya ya ukwapuaji fedha za umma ambazo zingetumika kuendeleza sector ya viwanda, ushauri huo naupokea na nitaufanyia kazi.

Kwa hiyo, mwaka 2016/2017 Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, haijaweka bayana mkakati wa Serikali wa kufufua viwanda 33 vilivyobinafsishwa na kufa. Ngoja niwaambie, viwanda vilivyopo lazima vifanye kazi, na bidhaa mnazona madukani, lakini vile vilivyokufa vina njia mbili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja una dakika kumi bado.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vile vilivyokufa vina njia mbili, ama ukirudishe ama ukiendeleze na namna ya kukiendeleza tafuta mbia mwenzako. Kwa nini tunavitafuta ni kwa sababu mikataba ya mauziano inasema hivyo lakini faida nyingine vile viwanda vina miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi kuliko kwenda kupasua misitu kuweza kujenga sehemu mpya.

Suala la korosho nimelizungumzia, tutakaa chini tulizungumzie, viwanda vya Mwalimu tutavifufua, Serikali itimize ahadi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aliahidi wakati wa kampeni kuwa kiwanda cha kubangua korosho kitaanzishwa eneo la Mkuranga. Tutakapomaliza matatizo ya korosho na kile kiwanda kitaweza kufanya kazi. *Sunshine* wako tayari kutengeneza viwanda wana kiwanda kimoja Mtama, wanataka kwenda Nachingwea wako tayari kwenda kokote, lakini muondoe yale matatizo ya msingi yaliyopo kwenye sekta hiyo.

Serikali iwezeshe vijana wasio na ajira ili wasiwe wanatanga tanga, kwa kushirikiana na TAMISEMI tunatenga maeneo, hapa ni mshukuru Mheshimiwa Azzan Zungu, nakubaliana naye mipango ya kurasimisha sekta isiyo rasmi inafanyika na njia mojawapo ni hiyo. Leo nimezungumza na Mheshimiwa Mangungu wa Mbagala, wameshanitegea eneo, nikitoka hapa nakwenda kukutana na Mheshimiwa Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam tukaangalie eneo tutaanzia pale. Kwa hiyo, Mikoa yote imeshaambiwa kutenga maeneo na tunawalenga Vijana. Watu wa *BRELA* na *TRA* tutaangalia namna ya kuondoa mambo ya *TIN*, kumlipisha mtu kabla ili watu waweze kurasimisha shughuli yao. Tutafuata maelekezo yenu ambayo mmetupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Kioo Mbagala, nitatoa maelezo kwa kuandika. Katika miaka 1970 *NDC* imechukua eneo la hekta 350, Mbunge wa Nyamagana tuonane, nitakupa maelekezo namna ya eneo hili, tuko tayari

kulitoa kwa ajili ya Halmashauri kama mtaona kwamba mtalifanyia kazi vizuri, lakini tafuta wawekezaji tuweze kulifanyia kazi sina tatizo nao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya chai navishughulikia, nimemaliza cha Lushoto, nitakwenda Lupembe na Mheshimiwa Spika aliyemaliza kipindi chake anafuatilia suala hilo.

Mheshimiwa James Millya suala la *Diamond, Tanzanite* kule tunalishughulikia nimeshamaliza kulipa pesa zilizokuwa zimebaki zote, kwa hiyo tutakwenda kuangalia namna gani ya kutengeneza *Special Economic Zone*.

Mheshimiwa Adadi Rajab nimekukubalia kwamba tukutane kesho kutwa leta wawekezaji wako, tuweze kwenda mbele na mpango wa kuwekeza kwenye matunda.

Mheshimiwa Kasuku Samson aliuliza je, viwanda dira ya Rais au ya nchi? Hii ni sera ya CCM hilo sina tatizo nalo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Dodoma wasaidiwe kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika karanga na alizeti. Mheshimiwa George Malima Lubeleje tutafanya hivyo, nimekubaliana na Serengeti waende waanzie kwenye Jimbo la Mtera, watachukua hekari nyingi wawafundishe wale wakulima wa kawaida watumie matrekta wazalishe mtama, tunawahakikishia kwamba mtama utauzwa Serengeti, kutoka kwa bwana kibajaji kule Mtera, kwa hiyo Mbunge wa Mtera pamoja na swali lako hili, uje unione nitakuunganisha na mtaalam wa Serengeti walime mtama kwako, mwezi wa saba nitakwenda kukagua hilo shamba tulime. Tutawachukua mmoja mmoja muwe na imani tunakwenda ili mradi safari ianze.

Kambi Rasmi ya Upinzani wanasema wafanyabiashara wadogo kuelekezwa katika viwanda badala ya kuonekana kero, tutafanya hivyo sina matatizo.

Kuhusu kuiwezesha *SIDO* isogeze huduma zaidi Wilayani hadi vijijini, huo ndiyo mpango wangu na itategemea bajeti na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa wa Ushetu Wizara isimamie *SIDO* ili vijana wapate ajira, nitaismamia *SIDO*, ipo chini yangu tunaanza na *centre* kubwa zile tano, ninawaomba Mheshimiwa Wabunge mtembelee *SIDO* mkaone mambo, kuna mambo mazuri sana.

Kuna hoja kuhusu *SIDO* itoe elimu zaidi kwa viwanda vidogo ili Watanzania wengi wavianzishe, tutafanikiwa tukiwekeza kwenye viwanda, mchezo upo kwenye viwanda. Baba Mchungaji Mheshimiwa Msigwa mni hukumu kwa viwanda vidogo. Viwanda vya wakubwa vinatumia teknolojia

kubwa haviajiri watu wengi, kwa hiyo nitavihimiza hivi nawashukuru sana kwa mchango wenu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kupigiwa kengele michango yote nimeizingatia, natafuta mchango wa Mheshimiwa Msigwa ambaye alitaka kuona kama ninaweza kumwonesha *40 percent*. Mimi leo ndiyo ninaomba bajeti, ninamaliza Ilani ya Chama ya 2010-2015 sasa naanza ya 2015-2020. Kwa hiyo niko *year zero* nina *take off*, huwezi kunihukumu leo kwamba nimetengeneza wangapi? Lakini nimeandika kwenye maelezo yangu kwamba tutatafuta wajihi wa kila kiwanda na kila kampuni. Lengo la kutafuta *profile* za kila kampuni ni kuweza kubainisha *at every stage* kwamba watu wangapi wameweza kupatiwa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tumeanzisha viwanda? Tumeanzisha viwanda kwa sababu vinaweza kutoa ajira, na ndiyo maana tunalenga viwanda vinavyotumia watu wengi. Mheshimiwa Msigwa akasema Mwijage ninazungumza kama ninapiga kampeni. Nimesema kazi yangu kubwa itakuwa kuhamasisha Watanzania wakubali hii dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu, inahitaji mhamasishaji na mhamasishaji aliyepewa ni mimi, sasa Mzee Msigwa unauliza makofi polisi? Ndiyo kazi yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute masoko ya matunda nje ya nchi. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Raza, amekubaliana na mimi atanisaidia kunipatia masoko ya mazao na masoko ya mazao ya matunda yako Oman. Walikuja watu wa Oman Waziri wa Oman nilizunguka naye mjini, watu wake wakaniuliza, Mheshimiwa Waziri, nikasema naam, wanazungumza kiswahili wa Oman, wakasema mnanunua na ninyi matunda kutoka Mombasa? Matunda ya Muheza yanauzwa Mombasa kwa hiyo watu wa Oman wakadhani matunda ninayanunua kutoka Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, soko lipo ninamshukuru Mheshimiwa Raza na TANTRADE nawapa jukumu, lakini Watanzania mchangamke kufanya biashara inawezekana. Tatizo kubwa la Watanzania walio wengi wanaogopa kumiliki, mtu anapita kwenye nyumba yake anaangalia huku, eti wasimwone ana nyumba, kwenye gari lake hawezi kulipanda, anapanda gari nyingine, gari yake inapita. Mmiliki, msilogope kumiliki ili mradi mmiliki kihalali ndiyo utaweza kufaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia fursa za uanachama wa Jumuiya za Kikanda angalia takwimu zangu, Tanzania tumeuza mno *East Africa*, tumeuza mno SADC, tunakwenda COMESA. Kwa hiyo, Watanzania tujiamini na nitaendelea kuhamasisha mambo ya Kikanda ya *bilateral*, kikanda, kieneo na

ninyi msilogope, Watanzania msilogope kwenda *Southern Sudan* sasa hivi mchangamkie fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania kuna wakati tulikuwa tunashangilia fursa, *location advantage*, haina maana, ushishangilie fursa, ichangamkie fursa. Katika hilo ndiyo maana viwanda vidogo, viwanda vya kati, tunataka kuanzisha mashindano ya kimkoa ningependa kuona mtu analeta sembe imekuwa *packed* kwenye mfuko, anasema sembe safi kutoka Ileje, mchele mzuri kutoka Mbarali, tushindane Kiwilaya na tushindane Kimkoa, hii ni asali nzuri ya kutoka Katavi, hilo haliwezekani mpaka muweze kuyahamasisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusaidia wahitimu kusajili makampuni. Nitaliangalia hili tuweze kuangalia namna gani tunaweza kuwasaidia wahitimu hata ikibidi kuwasajili siku wanafanya mtihani, lakini lazima tuzingatie sheria, na kama kuna vikwazo mtaweza kuondoa ninyi mnaopitisha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumaliza tatizo la sekta ndogo ya sukari. *Kigoma Sugar* amepewa na watu wa Kigoma niwashukuru tena, hekta 47,000; akifanya kazi mpiganie kwa namna yoyote asikwamishwe na mtu yeyote na mimi nitawasaidia. Atazalisha tani 120,000; RAK wameomba ardhi watazalisha zaidi ya tani 60,000; *Kagera Sugar* anataka kupanua mpaka tani 120,000; lakini Oman wamesema wanataka watumie *facilities* za *Kagera Sugar* wazalishe tani 180,000 kama alivyosema Mheshimiwa Zitto Kabwe tunaweza kuzalisha tani 1,500,000 tukapata mamilioni mengi ya pesa. Kwa hiyo hili tatizo la sukari ni suala la muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze muazime uzoefu wa Wabunge wa Bunge la Kumi, Taifa lilikuwa linasumbuliwa na sekta ya mafuta namna hii, kwa hiyo kinachokuja tutakuwa na *coordinated importation* kwani kuna suala la *quality*, kuna suala la *quantity*, kuna suala la *price*, ulikuwepo udanganyifu kwa hiyo udanganyifu unakwisha wanaoshangaa kwa nini Mheshimiwa Rais anasema ndiyo, akishamaliza kusema mwenye nyumba sasa mje muone watoto watakavyofanya tutalishughulikia hili, kwa hiyo itakuwa na *coordinated importation* na msiwe na wasiwasi hakuna Ramadhani sijui sukari itakosa hakuna, kuna wengine sijui Mikoa gani huko, wanachagua maduka mawili ya kata kuuza sukari, sukari itauzwa kila duka na itakuwepo sukari ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka mwenye sukari, na ukitaka mambo yakuendee vizuri hakikisha sukari inakwenda kwa wananchi, *distribute* kusudi tuone kwamba hakuna sukari. Lakini sukari ndiyo ilikuwa inakwamisha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni waambie siri moja, waulize wawekezaji, *Kigoma Sugar*, muulize hata RAK, Mheshimiwa Jitu Soni anataka kutengeneza

kiwanda cha sukari kwenye Halmashauri yake cha kuzalisha tani 50, Abdul Salim aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, anataka kutengeneza kiwanda cha tani 50, siyo gharama kubwa ni shilingi bilioni mbili tu unakwenda Benki unaweka *guarantee* ninakudhamini, wewe Mbunge mimi nitakosa kukudhamini? Ndiyo faida ya Ubunge mnakopa. Msiogope kukopa huwezi kuwekeza kwa pesa yako mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo usinipigie kengele, baada ya kuzungumza yote hayo, nimeahidi kwamba mengine yote nitaweza kuyaweka kwenye kitabu vizuri, niwashukuru wote mliochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa mtoa hoja Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa kuhitimisha kwa namna ambayo umelichangamsha Bunge. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nina tangazo moja hapa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, amepotelewa na miwani ambayo hakumbuki ni wapi ameisahau na miwani hiyo ilipotea siku ya Jumamosi tarehe 7 Mei, 2016 katika maeneo ya Bunge. Kwa yeyote ambaye ameiona ama ataiona miwani hiyo anaombwa aiwasilishe kwa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi au Ofisi ya Katibu wa Bunge.

MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI: Imeshapatikana.

MWENYEKITI: Afadhali imeshapatikana, Katibu tuendeleo.

NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida ukurasa wa 278.

Kif. 1001 Admn. & HR Mgt..... Sh. 10,355,266,000

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tayari nimeshaletewa majina matano hapa kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri, wa kwanza ni Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa mwingine ni Mheshimiwa Rashid Chuachua na mwingine ni Mheshimiwa Antony Komu na wa mwisho ni Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma. Kwa hiyo tunaanza na Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, mshahara wa Waziri, nimewasikiliza vizuri sana Waheshimiwa Mawaziri wawili, Waziri wa Kilimo pamoja na Waziri wa Viwanda. Kilimo ni uti wa mgongo, lakini katika maelezo yao, wanasema kwamba jembe tutakutana nalo labda huko makaburini na sehemu zingine, lakini ukiangalia takwimu hatujapata maelezo ya kutosha ni jinsi gani tutaondokana na hili jembe la mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu matumizi ya jembe la mkono, katika ile asilimia 70 ya Watanzania wote wanaolima asilimia 62 wanatumia jembe la mkono, asilimia 24 ni wenye maksai, wanaotumia trekta ni asilimia 14 tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate maelezo ya kina sijaona mkakati tutaondokana vipi na jembe la mkono. Lakini lingine baya zaidi ni kwamba majembe haya, mapanga, mafyekeo yanatoka India na China ambapo Serikali inagharamika kulipa pesa nyingi zaidi za kigeni, sijaona mkakati naomba Serikali iniambie ni jinsi gani tutaondokana na jembe la mkono kwa maelezo ambayo Serikali imeyaeleza? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ndassa kwa kufuatilia suala hili, lakini jambo hili siyo la sehemu moja, ni muunganiko wa jitihada nyingi, jitihada moja ukiunganisha na shughuli ya leo ni kwamba panapokuwa na viwanda ambavyo vinaongeza thamani mazao ni moja ya kichocheo kizuri kitakachoweza mtu hata katika

ngazi ya uzalishaji kuona kwamba anaweza akaaminiwa, akakopa na akapata matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, tunapowapeleka vijana katika shughuli hizi kwa hamasa hii tunayoifana vijana kuingia katika shughuli hizi pia ni watu ambao hawatalima kwa jembe la mkono.

Kwa hiyo, hamasa yenyewe ya kuona kwamba uhitaji wa kulima kwa kisasa unahitaji trekta utaona unaongezeka na utapatikana kwa kutumia sekta binafsi, benki yetu ya kilimo, lakini pia na jitihada za Serikali ambazo nilitoka kuzisema siku ya bajeti na ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Mheshimiwa Ndassa, atuelewe kwamba tunaposema tunatumia jitihada za Serikali, sekta binafsi, TIB, Benki ya Kilimo pamoja na hamasa yenyewe ya mtu mmoja mmoja kwa sababu katika mazingira ya sasa katika kipindi kilichopita, kama mtu hapati soko bora la mazao ni vigumu kusema mtu wa aina hii anaweza akapata matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata upatikanaji wa soko, upatikanaji wa uongezeaji wa tija kwa mazao ni moja ya mkakati ambao utatuchangia kuweza kufikia katika ndoto hiyo. Tunaposema hivi ni moja ya kitu kingine ambacho tunaweka hamasa kwa watu wetu waweze kuona kwamba dira na mwelekeo tunaokwenda ni huo wa kuhama kutoka jembe la mkono, kwenda kwenye matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo kauli mbiu tu, bali ni dira ambayo tunataka tuende nayo ili tuweze kubadili kilimo hiki hatuna njia mbadala lazima tuende kwenye uzalishaji wa aina hiyo na huo ndiyo uzalishaji ambao utatosheleza viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye nchi ambazo zimekuwa za viwanda, utaona kwamba mazao mengi ambayo tunazalisha katika maeneo yetu, unaweza ukayaita mengi lakini ukienda kwenye *serious industry* unaweza ukakuta wana-*process* kwenye wiki mbili na baada ya hapo wakawa *idle*, kabla hatujafika huko ndiyo maana tunaenda kuanzia kutoa dira, kuweka hamasa lakini pia kuchukua hatua na hicho ndicho ambacho kitakachotufikisha katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliipenda kauli ya Mheshimiwa Serukamba ya kilimo ni sayansi, maana yake tunatakiwa tuende katika *mechanization*, ili tuweze kuzalisha kwa ubora, wingi na kuweza kumudu kwenda kumpatia malighafi za kutosha mwezetu wa kiwanda hata atakapohamasisha wengine waweze kujua kwamba tuna malighafi za kuweza kuweka kiwanda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, hoja yangu ya msingi Mheshimiwa Waziri, mpango ni mzuri, lakini Serikali ingekuja ikatuambia mpango wetu wa sasa ili tuondokane na kulima kwa kutumia jembe la mkono mikakati yetu kwa sasa, kwa sababu tulikuwa na Kiwanda cha UFI ambacho kilikuwa kinatengeneza majembe ya mkono, majembe ya kukokotwa na ngo'mbe, mapanga, chepeo na kadhalika. Lakini pia tulikuwa na kiwanda cha zana za kilimo Uyole, hivyo hivyo kilikuwa kinatengeneza zana hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya sasa Mheshimiwa Waziri mnaposema, mipango ni mizuri, lakini kwa asilimia hii Mheshimiwa Waziri, asilimia 62 jembe la mkono huwezi ukaondokana nalo leo. Tasisahau kwamba majembe yanayokuja kutoka China na India ubora wake ni duni. Tunataka tumsaidie huyu mkulima huyu, tunamsaidiaje? Ninachosema ni kwamba naomba mikakati ya Serikali itueleze tunataka tuende huko tuondokane na jembe la mkono, tuondokane na majembe ya kukokotwa na ngo'mbe tutafikaje huko, mipango ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitegemei kuondoa shilingi, lakini nataka nipate maelezo ya kina. Mheshimiwa Waziri unajua tulikuwa na UFI haipo, tulikuwa na Uyole haipo. Kwa sasa lazima tuendeleo kutumia jembe la mkono, hatuwezi kuacha leo kutumia jembe la mkono hata siku moja. Hatuwezi kuacha leo kutumia jembe la kukokotwa na wanyamakazi. Tuambiwe jembe la mkono bado tutaendelea kuagiza kutoka nje, hizi plau tutaendelea kuagiza kutoka nje, Mapanga na vitu vingine? Nataka maelezo ya Serikali!

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee maelezo ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri mwenye dhamana ya Kilimo.

Naelewa concern ya Mheshimiwa Ndassa, nadhani maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu *Machineries, tractors* ameyaelewa. Concern yake ni zana za kilimo hizi za mapanga. Katika hotuba yangu, katika mambo ambayo nimesema nitayafanya ni kuhamasisha Watanzania wapende bidhaa zinazotengenezwa Tanzania. *Wheelbarrow*, jembe linalotoka nje, sitaki kutaja Mataifa wasije wakanipeleka mahakamani, diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye viwanda vyangu vya *SIDO*, ukienda kwa yule mjasiriamali ambaye analelewa na Mheshimiwa Sukum, Mheshimiwa Sukum ana mjasiriamali anamlea aliyefundishwa na *SIDO* Brazil. Waheshimiwa Wabunge mmuulize Mheshimiwa Sukum ana mwekezaji

anamlea, zana zipo. Kwa hiyo, ninachowaomba mpende kuzitumia hizi zana. Ukienda *SIDO* Arusha majembe yenye ubora yapo, lakini kitu kingine kilichokuwa kinatukwaza Watanzania tulikuwa na utamaduni wa kutokupenda kununua vitu vyetu. Yuko mtengenezaji wa zana za kilimo hayo *ma-wheelbarrow*, mapanga anaitwa ndugu Mushi, anatengeneza zana nzuri, lakini ipo ile kasumba ya watu kupenda vitu vya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kukwepa jukumu hiyo ni kazi yangu, nitahakikisha kwamba bidhaa yoyote ambayo, hailingani na ubora wa bidhaa za hapa haitaingia nchini na nimeisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mpango wetu ni kwamba tutahamasisha vituo vyetu vinavyozalisha zana hizo zinazozungumzwa (mapanga na *wheelbarrow*) tutazihamasisha tutazitangaza kwenye biashara Watanzania wazione. Mniunge mkono, ndiyo njia rahisi ya kuweza kupata hizo zana bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matrekta amelizungumza vizuri. *TADB* na *TIB* na yamekuja mapendekezo humu kwamba *TIB* ilete fedha nyingi kusudi watu walete matrekta yaende kwenye vijiji, kwenye center tuweze kwenda mbele. Hayo ndiyo maelezo yetu, bidhaa zipo. Ila hayo majembe mazuri ya UFI ya ZKK, lakini mtu wa ZKK alipoitwa na Msajili wa Hazina alijitetea kwa sababu hizo hizo kwamba mimi nikitengeneza *wheelborrow* ambalo ni imara halinunuliwi, nimepewa maelezo hayo hayo na wajasiriamali Arusha *SIDO* kwamba nikitengeza hayanunuliwi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mmenihakikishia kwamba mtanunua bidhaa ya Tanzania basi ninakwenda kuwahimiza wawekezaji wangu wenye viwanda wazalishe na tutasimamia kuhakikisha bidhaa yenye viwango inaingia ndani tuweze kujenga uchumi wa kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndassa hayo ndiyo majibu niliyonayo.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea sasa tunakuja na Mheshimiwa Antony Calist.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote number 44*, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba maelezo ya Serikali kabla sijachukuwa hatua zaidi ya kushika shilingi kuhusiana na maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya *EPZ* na *SEZ* karibu katika mikoa yote ya Tanzania ambapo ni hekta zaidi ya 31,000. Maeneo hayo mpaka tunavyozungumza moja

ya tatu haijafanyiwa uthamini na hayo yaliyokwisha kufanyiwa uthamini hayajalipwa fidia mpaka sasa hivi na ukiangalia bajeti hii hakuna fedha iliyotengwa. Kwa hiyo naomba maelezo ya Serikali kwamba kuna mpango gani kuhusiana na maeneo haya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli yapo maeneo yametengwa nchi nzima. Kuna eneo la *Special Economic Zone* Bagamoyo, kuna sehemu imefanyiwa tathmini na ikalipwa. Kuna sehemu nyingine imeainishwa haijafanyiwa tathmini, kuna eneo la Kigoma limefanyiwa tathmini halijalipwa, kuna sehemu ya Bunda imefanyiwa tathmini ikalipwa yakatokea yaliyotokea huko. Kuna sehemu ya Manyara karibu na Mgodini wa *Tanzanite*, namushukuru Mwenyezi Mungu tumemaliza kulipa mwezi uliyopita. Kuna sehemu ya *Kurasini Logistic Center* tumemaliza kulipa mwezi jana. Kuna sehemu ya Mheshimwa Gama, Songea inadai, kuna sehemu ya Makambako mkinipitishia bajeti yangu nimetenga kwa ajili ya kulipa. Ndiyo, yapo maeneo yaliyolipwa na yapo ambayo hayajalipwa. Hoja ya Mheshimiwa Komu ni kwamba tutayalipaje na hapa hakuna pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida moja, ukichukua sehemu ya *Kurasini Logistic Center* ambayo tumeshalipa fidia, ukachukua sehemu ya Bagamoyo, *Phase I* na *Phase II* ambayo tumeshalipa fidia. Ukachukua TAMCO Kibaha ambayo ni mali ya Serikali, maeneo yale kuna watu tayari wako tayari kuhamia. Unawawekea miundombinu wezeshe *they are ready to pay*. Kwa hiyo, kwa lugha ya kitaalam au ya watu waliyosoma pesa yale maeneo ni *bankable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *proposal* ambayo mimi nimeipeleka Serikalini nimesema waniruhusu hizo pesa hasa za watu wa Bagamoyo; ukisoma ule Mpango wa Kwanza wa Waziri wa Fedha na Mipango aliouwasilisha, ilikuwa imetengwa shilingi bilioni mbili, lakini wanazodai watu pale Bagamoyo ni shilingi bilioni 56 unatakwenda na shilingi bilioni mbili kuwalipaje wale shilingi bilioni 58. Kigoma, walikuwa wametengewa bilioni moja, utakwendaje watu wanakudai zaidi shilingi bilioni sita unakwenda na shilingi bilioni moja unamlipa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo busara ambayo tumetumia kitaalam kwamba, haya maeneo ambayo ni *bankable* Serikali imruhusu EPZA kwa sababu wawekezaji wanajulikana twenda kupitia TIB, EPZA iruhusiwe kukopa, haihitaji *government guarantee* ikope, ikimaliza kukopa tupate pesa ya kulipa fidia maeneo yote bila kubakiza eneo, lakini tupate pesa ya kuendeleza *Phase I* na *Phase II* ya Bagamoyo, kwa kumaliza hiyo wale watu wanao-relocate kutoka Asia watakuja pale waweze kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo utaratibu wa Serikali barua ilishafika kwa mhusika na kikao kinachopaswa kujadili kwamba njia hiyo ni sahihi, riba zitakuwaje, uwezekano, hao watu unaowasema ni kweli au siyo kweli, kikao kinakaa kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo mradi ni mzuri, *bankable*, ndiyo njia rahisi ya kuweza kumaliza matatizo ya hizi fidia na tunalenga yale maeneo yaliyokwishatengwa. Maeneo mengine nitakayoyafuata ni haya yanayotolewa kama hili la Nzega, la Mheshimiwa Bashe, nikimaliza haya hilo ni la kwanza, ni kama hili la Mheshimiwa Hawa Ghasia, la Mtwara ambalo halihitaji fidia, ni kama lile la Mzee Mbena, la Morogoro ndiyo nayafuata. Kwa hiyo ndiyo utaratibu huo, ndiyo tutakavyoweza kumaliza hilo suala la SEZ ambazo zimetathminiwa zikalipwa kidogo na wananchi wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana siyo ile ya kulipa nusu nusu ni kulipa moja kwa moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Komu nakuomba chondechonde wewe niruhusu kesho siyo mbali wanipitishie hiyo fedha halafu wewe ndiyo mshauri wangu kila mtu anajua tuweze kuwalipa hawa watu mambo tuweze kuendelea mbele.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza maneno mengi na marefu ya Mheshimiwa Waziri. Sasa ninatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi kwa sababu hii hadithi ni ya muda mrefu. EPZA imeanzishwa 2006 na baada ya kuya- *earmark* hayo maeneo Wananchi kote huko kwenye hiyo Mikoa ambayo inazungumzwa ni kwamba wamefungwa mikono hawawezi kufanya chochote katika maeneo yao kwa sababu wanasubiri fidia au wanasuburi tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingekuwa makini, ingefanya hata uthamini kwenye hayo maeneo ili watu wajue kwamba sasa mimi natarajia kulipwa kiasi hiki. Lakini ukiangalia toka mwaka 2006 mpango huu ulivyoanza mpaka leo ni muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho anachosema kwamba wanakwenda kukaa kesho ili benki iweze kutoa fedha na kadhalika ni jambo vilevile halipimiki. Maana yake ukiangalia hapa ni kamali nyingine ni *gambling*. Huku ni kucheza na maisha ya Watanzania na hatuwezi kuendelea namna hiyo. Jambo hili linagusa kila mahali katika nchi. Kwa hiyo, nafikiri itakuwa haki sana kama utaturuhusu, naomba nitoe hoja kwamba sasa baada ya kutoa shilingi Bunge zima sasa lifanye mjadala ili tuone kwamba muafaka ni upi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Komu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia kwenye EPZ, babu kuna majipu humu ambayo unatakiwa uende ukayatembelee. Kuna fidia hewa, watu wamepiga pesa. Nilipokuwa Mbunge wa Viti Maalum nilizungumzia katika Jimbo langu la Bunda Mjini, Mungu amuweke mahali pema Mheshimiwa Marehemu Kigoda alinipigia simu, Halmashauri imeingiziwa shilingi bilioni 2.5. EPZ na Wizara ya Viwanda na Biashara ikafanya tathmini ambayo wananchi waliridhika nayo, akaja Mkuu wa Wilaya na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wakasema tathmini ya Wizara ni batili. Wakatumia fedha za fidia kujilipa posho kwenda kufanya tathmini yao iliyoleta matatizo. Juzi anasema anatumbua jipu wakati yeye ni jipu la kwanza. Mheshimiwa Mwijage, Babu yangu nione nikupe nyaraka uende ukaanze kutumbua majipu pale Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamedhulumiwa, wananchi maskini, wamepewa hundi feki wanaenda kwa Mkuu wa Wilaya, anamwambia usimuonyeshe mtu nitamwambia Mkurugenzi akulipe kwa awamu na hizo barua ninazo nitakupa hata sauti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la EPZ ni bomu, ni bomu, ni bomu! Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Komu, kuna jitihada za dhati zinatakiwa zichukuliwe kuhakikisha muende mwekeze, watu wamechukuliwa maeneo yamekaa muda mrefu, fidia ndogo na bado fidia zinapigwa! Leo watu hawana pa kwenda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Komu, hili ni jipu, anza nalo. Ahsante!

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kangi Lugola.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Komu, mimi nitajikita pale aliposema kwenye EPZ ukiangalia hata kitabu cha maendeleo wametenga fedha sifuri, lakini kwenye kitabu cha hotuba kuhusu EPZ, Mheshimiwa Waziri ametuambia kuna mambo 16 ambayo yatatakiwa kufanyika ikiwemo Bagamoyo, Kurasini pamoja na haya maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Ester Bulaya ameyazungumzia ya Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshachukua uamuzi wa kuwanyang'anya wawekezaji viwanda ambavyo hawaviendelezi kwa sababu wamefanya ma-godown. Aidha, Serikali imeshachukuwa uamuzi kunyang'anya Wawekezaji mashamba kwa sababu hawaendelezi. Sasa EPZ na yenyewe imechukua ardhi kwa wananchi, sasa najiuliza Serikali kama haitaki kuwavutia

Wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo ya EPZ na yenyewe sasa itakuwa haiyaendelezi; Je, nani atainyanga'nya Serikali mashamba hayo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana dhana ya kusema usione boriti kwenye jicho la mwenzako angalia kwenye jicho lako kwanza. Naiomba Serikali yangu iwe *serious* juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Waziri, hoja ya Mheshimiwa Komu ni rahisi sana ujibu tu isiendele. Kwenye ukurasa ule wa 72 wa Kitabu cha maendeleo, bajeti ya maendeleo ya EPZ ni sifuri. Kwa hiyo, maeneo yote haya uliyosema, Bunda mtafidia, Bagamoyo kule mtafidia, Mtwara wapi, fedha hizo Wabunge tunataka tuzione Mheshimiwa Waziri Mwijage tusicheleweshe mjadala, ziko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa asante, tunaendelea na Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa kilichonifanya nisimame ni dhuluma ambayo naiona waziwazi inafanywa na Serikali kwa wananchi, wamechukuwa maeneo ya wananchi tangia mwaka 2006, maeneo mengine mwaka 2009, maeneo mengine 2010, wananchi yale maeneo hawayaendelezi, kwa bahati mbaya hawana wanachokijua, pesa hawalipwi, lini watapata hawajui!

Tunakuomba Mheshimiwa Mwijage hapa umejitamba sana umepiga blablaa nyingi, toa jubu lini wananchi watalipwa fedha zao? Kama jibu hili ni gumu tuambie utakapo kuja kulipa utalipa kwa kutumia tathmini ya wakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majibu mawili naomba uyajibu vinginevyo ninaunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu wananchi wanadhulumiwa. Leo watu hawaendelezi maeneo yao, wamekaa wanakuwa maskini kwa sababu ninyi mmeyazuia. Halafu mnakwenda kufanya tathmini ya kulipa hayo mnayosema mnakwenda kulipa mtalipa kwa kiwango cha mwaka 2009, leo mwaka 2016 *brother!* Lingine ni lini mnakwenda kulipa? Naunga mkono asilimia mia moja kwa sababu hakuna *straight answer* juu ya swali hili, bla bla nyingi, tunataka majibu hapa.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, uzito wa jambo hili kwa Serikali wala haitegemei shilingi kuondolewa bali ni dhamira ya Serikali mara zote kuhakikisha kwamba inakuwa na maslahi mapana ya Kiserikali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hata sisi tunaungana nanyi kwamba

tuna maslahi mapana ya Kitaifa ambayo yanatakiwa yazingatiwe, kwa maana hiyo, jambo la ulipaji wa fidia na jambo la tathmini huwa siyo la siku moja. Hata hivi tunavyoongea kuna maeneo ambayo yalikuwa yamepimwa, kuna maeneo ambayo yalishatathminiwa na kuna maeneo ambayo malipo tayari yalishaanza kufanyika na kuna maeneo ambayo yalishalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali haiwi na jukumu moja, Mheshimiwa Komu, shemeji yangu inabidi uridhie kwamba huwezi ukalipa maeneo yote kwa wakati mmoja, na ukalipa yote kwa wakati mmoja kwa kila mikoa. Jambo ambalo tunalichukua kutoka kwenu ni ile *serious commitment*, kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Bobali kwamba vipindi vinapita, lakini pia wananchi walikuwa wanahitaji kwa ajili ya matumizi mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge kwa kuzingatia maslahi mapana turidhie kwamba Serikali inachukua na inaipa uzito kwa ajili ya kulipa yale ambayo yameshafanyiwa tathmini na kuharakisha tathmini kwa yale ambayo hayajafanyiwa tathmini, lakini tusije tukaondoa uhitaji ule wa maeneo ya aina ile kwa Serikali kwa ajili ya mipango mipana yenye maslahi mapana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo la mambo ajira. Waheshimiwa Wabunge, ajira ni uwekezaji, ni lazima tukubaliane wote kwamba lazima tuwe na maeneo ya aina hiyo ambayo mwekezaji akitaka kuwekeza akute eneo lipo. Ukitaka kufidia watu baada ya mradi kuwa umeshapatikana, Waheshimiwa Wabunge tunajuana wote ni Watanzania, mtu ataweka hata mihogo ambapo hapakuwepo na shamba, ataweka kibanda ambapo mahali atakuwepo, kwa hiyo ni dhahiri kwamba ni lazima tuzingatie uzito wa lengo la Serikali lakini pia tuzingatie umuhimu huu ambao mmeusemea kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ninyi msipate shida sana kuhusu fedha imetengwa wapi. Serikali ina mifuko mingi, eeh!, Serikali ina mifuko mingi, ina Mfuko Mkuu...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: (Hapa hakutumia kipaza sauti).

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Yah! itakuwepo, kwani tumeshamaliza bajeti Mheshimiwa Msigwa? Utaratibu wa bajeti ulishabadilika. Jambo la msingi ambalo tunatakiwa tukubaliane wote ni ile hoja ya kwamba panatakiwa pafanyike tathmini na watu wapate *commitment* ya Serikali. Tunaposimama hapa tunasema au Mheshimiwa Waziri anaposema na sisi tunapounga hoja hii mkono maana yake ndiyo *commitment* ya Serikali, ndiyo maana maeneo mengine yameweza kulipwa na Waheshimiwa Wabunge walikumbushia maeneo ambayo yalikuwa yanahitaji kulipwa, yamelipwa.

Maeneo ambayo hayajalipwa na yenyewe yatafuata uzito huo huo kwa ajili ya kuweza kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba mridhie mkakati ambao amesemea Mheshimiwa Waziri na ameyabainisha maeneo yale, ndiyo uzito na ndiyo *commitment* ya Serikali. Kwa yale ambayo yana madhaifu, Mheshimiwa Waziri amekuwa akitembelea maeneo mengi na hatasita kufanya hivyo na atachukua hatua. Hii ni Serikali ya kuchukua hatua, na hilo liko wazi hata kwa Watanzania na wana imani na Serikali yao na wana uhakika kwamba Serikali itachukua hatua pale ambapo hatua zinatakiwa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja ya mipango ya Mheshimiwa Waziri, nimuombe Mheshimiwa Komu, ameshaonesha uzito wa jambo hili, amuachie Mheshimiwa Waziri na baada ya hapo Waziri atafanya kazi yake kwa sababu ndiyo anaanza kuchukua hatua hizi.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kigwangalla.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Komu kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, falsafa ya kumiliki ardhi kwenye nchi yetu siyo kwamba mtu anamiliki ardhi, hapana. Kwa mujibu wa sheria mwananchi yeyote yule anapewa mamlaka ya kutumia ardhi fulani, ruhusa kutumia ardhi fulani kwa kipindi fulani, lakini siyo kumiliki, hii ni falsafa pana ya ardhi na umiliki wa ardhi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye ana-own ardhi bali mtu anapewa kibali cha kutumia ardhi. Kinachojitokeza sasa ni uwepo wa baadhi yetu kuamini kwamba wanamiliki ardhi wakati sivyo. Wanapewa kibali cha kutumia ardhi cha miaka 33 ama cha miaka 66 ama cha 99, lakini siyo kumiliki. Kwa maana hiyo tunapozungumzia hii dhana ya watu kujitwalia misitu na kudai ni ardhi yao, nayo ni dhana ambayo imekuwa ikikwamisha miradi ya maendeleo na huu ni ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo miradi kama hii, sasa tujifikiria kwenda kwenye Tanzania ya viwanda, tunaanzisha taasisi kama mamlaka ya EPZ, tunahitaji viwanja kwa ajili ya kuwapa wawekezaji wajenge viwanda, tunakwama kwa sababu tunalazimika kulipa fidia kumbe tunalipa fidia kwenye misitu wala siyo kwenye mashamba ya watu. Hili nalo ni tatizo ni lazima Serikali ya Awamu ya Tano ilitazame kwa uhalisia wake, kwa sababu gharama sasa za

kuwekeza kwenye miradi zinakuwa kubwa mno kwa sababu ya kulipa watu fidia na sidhani kama ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kupongeza jitihada za Serikali, hususan taasisi ya EPZA kwa kuanza kutenga maeneo maalum kwenye mikoa yetu yote nchini, kwa sababu ninaamini *chance favours prepared mind*, tayari tukiwa na maeneo tumejiandaa kujenga viwanda, hata tusipovijenga leo, lakini kama tumetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda, hata ikachukua miaka 30 viwanda vitakuja kujengwa na watoto wetu na wajukuu zetu, lakini tuwe na viwanja kwa ajili ya kujenga viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipinga vikali hoja ya Mheshimiwa Komu, mpango wa Serikali uendele kutekelezwa kama ulivyo.

MWENYEKITI: Haya, tunaendelea Mheshimiwa Lukuvi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo hoja ya Mheshimiwa Komu juu ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wote tunasoma sheria. Ukisoma Sheria Na. 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 unaweza ukajua kabisa kwa marekebisho ya sheria ile mpya masuala ya fidia yanasema nini, imeandikwa waziwazi. Kwa hiyo, nilitaka nianzie hapa ili angalau niwatoe wasiwasi, maana yake tunapozungumzia hapa fidia naona tunachanganya mambo mawili, kuna watu wanakwenda zaidi wanafikiria kama vile Serikali ina nia ya kudhulumu haki ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanafikiri kwamba Serikali ina nia ya kudhulumu inapochukua ardhi kwa ajili ya shughuli za maendeleo, ina nia ya kudhulumu kwamba watu hawatapata haki yao, hapana. Kwa hiyo, dhuluma haitakuwepo. Lakini pia upo wajibu wa Serikali kutwaa maeneo kwa shughuli za maendeleo na siyo suala tu msielekeze leo mishale kwa EPZ. Ninyi wote kwenye Halmashauri zenu mnafanya, wote ninyi hapa, Halmashauri zenu zote mnapima, mnachukua mashamba ya watu, hamlipi fidia mnauza viwanja, na ninyi mnakaa kwenye council. Kwa hiyo, suala hili haliko upande wa EPZ, sheria inatambua na inakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo miji yetu yote lazima ikue, kila inapokua vijiji vina-shrink, lazima unatanua miji kwa kuchukua vijiji, vile vijiji ni mashamba ya watu. Waziri wa Ardhi akishatangaza eneo fulani limeiva kuwa Mpango wa Mji, lipangwe kimji, nikishatoa lile gazeti maana yake ninyi watu wa Manispaa mnaotaka kupima lile eneo lazima mlipe fidia. Jambo hili limekuwa halifanyiki vizuri, kwa wote wanaotaka kutekeleza shughuli za maendeleo, siyo EPZA kwa

sababu EPZA kwa Sheria hii ya Tathmini hana sheria yake, sheria ni moja na Sheria ya Ardhi ni moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dhuluma haitakuwepo. Nataka niwaondoe mashaka watu wote wanaofikiri kwamba yale maeneo yaliyochukuliwa EPZA basi EPZA watawapa tu fidia ya mkeka wanayotaka Serikali, hapana. Utaratibu utatekelezwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Hakuna hata mahali pamoja ambapo Serikali imelipa fidia kwa utaratibu wa mkeka, najua upo udanganifu wa baadhi ya Maafisa, *Valuers* wetu, anaweza kufanya tathmini kubwa lakini wakawapa watu kiduchu, sasa huo ni udhaifu wa watu, lakini nataka kuwahakikishia sheria itafuatwa wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawa wananchi wenye maeneo ambayo yamechukuliwa kwa shughuli fulani za maendeleo, Wizara yangu ingawa tuko ndani ya Serikali wote tuna *interest* moja, lakini mimi moja ya kazi zangu ni kusimamia sheria hii na kuhakikisha kwamba wananchi wanalipwa malipo stahili kulingana na ardhi waliyochukuliwa. *Chief Valuer* wangu ndiyo kazi yake kusimamia kwamba kila fidia inapotolewa inafanyiwa tathmini kwa mujibu wa sheria. Ikicheleweshwa upo utaratibu wa mtu kulipwa fidia kulingana na muda uliocheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nasema tu nawaondoa wasiwasi Wabunge. Nataka kuwaambia kwamba mimi ndiyo nimepewa Mfuko wa Fidia, mliunda Sheria ya Mfuko wa Fidia hapa na mwaka huu nimeamua kuunda na Bodi ya Mfuko wa Fidia, na mimi nitaweka shilingi bilioni tano kwenye mfuko huu kama mbegu ya kuanza kulipa fidia lakini *revolving*, nitalipa mradi mmojammoja kwa sababu hivi viwanja vya EPZA hatugawi bure, watakuja wawekezaji kama wanavyofanya Tamar pale, tunauza tunasonga mbele. Lakini pia sekta binafsi tutaihusisha katika kulipa fidia kwa sababu wao ndiyo wanufaikaaji wa *prime areas* kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba ndugu zangu, nimesimama tu kutetea hili kwa sababu usimamizi wa haki ya mwananchi kulipwa fidia stahili kulingana na ardhi yake mimi ndiyo msimamizi. Jambo hili litafanyika kwa mujibu wa sheria na hakuna mtu atapunjwa. Alipwe leo, alipwe kesho, watu watalipwa fidia kwa mujibu wa sheria. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka niliyopewa kwa Kanuni ya 104 (1), naongeza muda wa dakika 30 ili Kamati ya Matumizi iweze kukamilisha kazi yake. Mtoa hoja tuendeleo.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasilikiliza Wajumbe waliochangia hoja ya Mheshimiwa Komu, Waziri Kivuli wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuamka nikaja na mtazamo huu, hayo maeneo yote yanayozungumzwa nimeyaona kwenye maandishi na baadhi ya maeneo nimeyatembelea. Nimekwenda mimi mwenyewe Bagamoyo nimewaona watu, wamekuja wabia katika ile *Special Economic Zone* ya Bandari ambao wanataka kuwekeza pale. Unakutana na mtu anakuita bwana kijana wewe nakujua, mbona hujalipa hii pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimewaeleza, kuna nguvu inayotusukuma, tunasukumwa ili maeneo haya tuyafidie, haya maeneo tuyatumie kujenga viwanda, lakini tusingependa kujenga viwanda sehemu zile kwa kuwatupa watu porini. Ikaja mtindo wa kutumia njia mbadala nje ya bajeti, nikawaandikia mamlaka na hii njia mimi ndiyo naiona mkiniwekea nguvu kwamba hiyo njia Serikali iruhusu katika hali ambayo ni ya riba ndogo nitaweza kwenda haraka ku-cover nchi nzima, lakini utaratibu wa awali ndiyo ulileta matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaeleza, soma maandiko ya mwanzo ambapo Kigoma walikuwa wametengewa bilioni 2, Bagamoyo wametengewa bilioni 2 mtu anadai bililioni 50, kwa hiyo ikaja njia mbadala ya ku-finance hizi shughuli. *For the same spirit* hata ule mradi wa *General Tyre*. Huwezi kujenga kiwanda kama kile kwa kupewa bilioni moja moja, itakuchukua miaka 100, tunahitaji matokeo haraka. Kwa hiyo, mimi nina imani lile andiko lilivyoandikwa, wenye mamlaka, vikao vya kisheria vitakaa na hii pesa itatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja cha kuwa na imani nacho, mimi ukivivusha hapa Mheshimiwa Komu, kabla bajeti haijasomwa tarehe 9 na hiki kikao kimekwama kwa sababu Waziri mwenye dhamana ambaye ni Waziri wa Fedha, ambaye ni Mjumbe kwenye kikao hicho, yuko Arusha kwenye *East Africa*, wanajadili bajeti za *East Africa*. Kwa hiyo, nina dhamira nzuri, natafuta njia, siyo ya kumaliza mmoja mmoja, ya kuwamaliza wote kwa jumla, halafu nikishawamaliza wote kwa jumla nichukue eneo la kwanza kusudi niweze kukidhi haja ya kuonyesha vile viwanda vya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kumaliza zoezi *once and for all*, nafanya hivyo kwa nia njema siyo mambo ya kwamba nataka kupoteza lengo, sina sababu yoyote, lakini wananchi ninyi mnasikia mnakuja kuambiwa kama wasimamizi wangu, watu wanakuja ofisini kwangu, mtu anatoka Bunda, Mheshimiwa Ester unaowasema walidhulumiwa wamekuja ofisini kwangu. Mtu anakuja kuniambia ametoka Bunda na akikueleza alivyokuja kwa kudandia malori, ndiyo maana nikasukumwa nataka kumaliza hili moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tabia moja, sitaki kuzungumza mambo ambayo hayajaiva. Wamekuja watu kutoka Misri wanataka kuwekeza Kigoma kusudi waweze kutumia Kigoma kwenda Congo, lakini ile sehemu ina mgogoro halijaisha lote. Kwa hiyo nina kasi, kasi nitaitafuta kwenye *alternative way of*

financing the budget ambayo ni *borrowing from the bank*, TIB atatumika kutafuta pesa nje ambazo zina riba nafuu. Pesa haitakopwa humu ila TIB atatangulia kwenda kuchukua pesa nje, tutatumia mabenki ya Kimataifa yenye riba ndogo tuweze ku-finance.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, mkisema tukazanie kwenye bajeti shughuli hizi hazitakwisha. Nitapewa pesa ya kutoa Bagamoyo, ndugu zangu wa Kigoma nitawaambia nini, Musoma nitakwendaje Bunda, nitakwendaje Songea. Ningeomba mnisaidie hii *model* niliyokuja nayo ili kusudi iweze kupita tumalize hili tatizo *once and for all*, siyo bla bla, inatoka kwenye sakafu ya moyo wangu nina dhamira safi, kwa nini nije kuwaumiza watu. Ningependa nimalize haya mambo na mimi niache *legacy*, napenda *legacy* mimi, napenda kuwatumikia wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa mnhurumie, ndugu yangu Mheshimiwa Bobali uniamini mimi, nitakuletea maandiko yangu. Tunataka kuboresha Mtwara, lakini huwezi kuboresha kwa kutoa bilioni moja. Bajeti yetu inatosha shilingi trilioni 29, lakini keki hii inagawanywa kwa mapana, na mimi sitaki kwamba unipangie pesa leo mje mnipe mwaka kesho, kwenye bajeti hiyo, nataka pesa yangu mara moja namaliza shughuli halafu tunaanza kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Baba Mchungaji Msigwa anataka viwanda leo, hawezi kusubiri, kwa hiyo siwezi kusubiri pesa mwaka kesho, Mheshimiwa Msigwa ataninyima huduma ya kikanisa. Mheshimiwa Komu naomba unirudishie shilingi yangu, mwalimu anayekufundisha ndiye anayekupotosha. Mheshimiwa ugomvi wetu ule unisamehe kusudi tusikilizane, Mheshimiwa Komu hoja yangu ninayotoa unaisikia, ni *alternative way of financing the budget*. Lakini wewe una *plan B*, Mheshimiwa Komu una mahali pa kuangukia, bajeti ya Serikali haijapita ni tarehe tisa. Kwa hiyo, ninachokizungumza nimekwambia kesho kikao kinakaa kwa hiyo Serikali haiwezi kuepuka, itakuwa na namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo yangu. (Kicheko)

MWENYEKITI: Sawa, haya, namkaribisha Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza maelezo ya upande wa pili ambayo kimsingi ni maombi ambayo hayana *argument* zinazoshikika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anataka aonewe huruma kwenye mambo ya msingi, mambo ambayo yanakwamisha maisha ya watu. Sasa hao watu ambao unasema una nia njema nao halafu hutaki kuwafanyia yale ambayo

yatafanya ili nia hiyo njema iendeleo kutendeka, nafikiri tunafanya mambo kama mazoea, maana yake nikitumia neno *business as usual* ndugu yangu atakasirika sana, lakini tunafanya mambo kwa mazoea, mambo ya kuombana bila kutoa hoja ambazo zina mashiko kwa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hapa wamechangia na ukiangalia michango ya Wabunge, ucheleweshaji unasababisha mambo mengi sana ambayo ni athari kwa Watanzania ikiwa ni pamoja na kudhulumiana, masuala ya hewa, masuala ambayo yanafanya watu washindwe, wanakuwa *crippled* washindwe kujiendeleza kimaisha na wengine wanakufa wakisubiri hizo fidia, hawawezi kufanya chochote, wanaishi kwa matuamini tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ndugu zangu hapa wengine ambao kwa kweli ni wasomi wazuri lakini wanazungumza mambo ambayo ni ya ajabu. Serikali inatoa hati, inasema watu wamiliki maeneo, Serikali inakwenda inafanya tathmini inasema mko *entitled* kulipwa fidia, halafu mtu anakuja hapa mbele ya Bunge zima anasema kwamba hawa watu wanafanyiwa kitu kama huruma, sasa huo ndiyo mwanzo wa dhuluma, hapa ndipo hofu inapoanza kujengeka. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa nakuomba kwamba kwa maelezo yaliyotolewa hayajaniridhisha. Labda kwa busara zako na kwa taratibu za Kikanuni, Bunge liamue ili Watanzania waweze kuona ni namna gani tunawatendea haki na tunavyowajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya, kwa vile hujaridhika naomba sasa niwahoji Wajumbe wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Komu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Chuachua.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nasimama kwa vote hiyo ya 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda na ni wazi kabisa kwamba ili tuweze kufanikiwa tunapokwenda kwenye uchumi wa viwanda ni lazima pia tuwe tayari kupokea malighafi kutoka katika sekta ya kilimo ili ziweze kuchakatishwa na hatimaye ziuzwe kwa thamani kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Serikali za kutaka kwenda kwenye uchumi wa viwanda zinaonekana lakini bado naomba nisimame hapa siyo kwa nia ya kutoa shilingi, bali kwa nia ya kutaka *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wake ni upi ili kuhakikisha kwamba zao ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa sana katika Pato la Taifa yaani zao la korosho nalo linachakatishwa na viwanda vyetu ambavyo kimsingi vimekuwa havifanyi kazi kwa muda mrefu na korosho zaidi ya asilimia 90 inasafirishwa ikiwa ghafi. Naomba *commitment* ya Serikali katika Jambo hili. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mtoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhamira ya wazi ya Serikali, wakati nahitimisha hapa nimezungumza kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliniagiza pamoja na Mheshimiwa Mwigulu kwamba tukae chini tuangalie sekta nzima ya korosho. Nimeifanyia kazi na tutafikia hatua tutawahusisha wadau wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *dilemma*, hili zao mimi nasema sayansi ya korosho, sayansi ya korosho ina utata wake ndiyo maana wadau inabidi tufike twende tukaamue, wale watu wananunua korosho yetu India na Vietnam, wanatambua kwamba korosho ya Tanzania ndiyo jumbo ndiyo *premium* duniani. Kwa hiyo, wanaitumia korosho yetu kama kiungo na nimekwenda nimepata habari zaidi, wanaposema korosho yenye bei ya juu ni ile ya Tandahimba. Kwa hiyo, wanachofanya wao wako tayari kulipa bei yoyote kusudi kuichukua korosho yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunayazingatia mambo yote hayo tuweze kuyamudu na wamekuwa wakishindwa wapi? Wamekuwa wakishindwa kwa sababu mnapoweka bei wale wanaweza kutoa bei kubwa kwa hiyo huwezi kuwaambia wananchi mtoe bei ndogo viwanda vyetu vibangue. Kumbe kwa kutaka bei kubwa tunapoteza ajira. Wahindi wanachukua ajira, lakini wanachukua korosho yetu kama kiungo cha korosho nyingine lakini wanachukua yale maganda ambayo wanatumia kutumia kama *break fluid* ku-extract *break fluid*, wanatumia yale maganda kama *ant-oxidant*, ukichanganya na rangi ya kuzuia kutu wanasema maganda ya korosho yana dawa nzuri, nimeyafuatilia yote hayo nimeyajua,

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshajua mengi, hata kuna watu wamejitolea kutoa oda kwamba korosho ya kutoka Mtwara tani kumi na tano elfu wako tayari iende Marekani lakini ibanguliwe na wananchi wa kawaida. Kuna vipengele vinavyotukwamisha. Kuna sheria inayosema ni mpaka *board* sijui ndiyo ifanye nini? Eti mkulima alime korosho zake azilete kwenye *board*,

akishazileta kwenye *board* azinunue tena ndipo azibangue. Kwa hiyo kuna makandokando ambayo nimepewa jukumu mimi na Mheshimiwa mwenzangu hapa. Kwa kasi tuliyonayo, Mheshimiwa Chuachua tutashungulikia shughuli hii na wewe ni Mjumbe mmojawapo, muda tutakaokuwa Dodoma *information* ulizonazo uzilete, ndiyo maana katika mchango wangu nikampongeza Mheshimiwa Omary Mgumba, yeye ametoa *information* tunakwama wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi uwe na korosho za kutosha ili uweze kuanda kiwanda kiweze kufanya siku 260, mazingira hayo yanakuwezesha ununue korosho nyingi, kwa sasa uwezi kufanya hivyo kwa sababu wanunuzi wapo na wako tayari kulipa bei yoyote. Nimekwenda zaidi tunazo taarifa na bahati nzuri zinaletwa na wadau wenyewe, korosho ambayo tunapewa shilingi elfu tatu, ikishabangukiwa huko nje inafikia hata shilingi 60,000, hata 70,000. Kwa hiyo kuna mazingaumbwe na hayo ndugu zangu ugonjwa umepata dawa mimi hapa kwa mapacha wawili hapa hakiponi kitu. Nina dhamira ya kweli wadau mnikamate salamu yenu iwe korosho popote inapokwenda.

Mheshimiwa Chuachua utakumbukwa katika historia kwamba wewe ulipigania zao la korosho na ninakuambia suluhu tunaipata. Ujanja ni mmoja kama sheria inayoipa mamlaka bodi ya korosho ndiyo inaleta shida katika sheria zitakazo badilishwa muombe iletwe hapa ibadilishwe. Ninawahakikishia watu wa Tandahimba, watu wa Newala niko tayari kuwaletea mtu ambaye yuko tayari awape mashine wananchi kubangua, masharti yake anataka watu wa kawaida (*the poor people*) wanapomaliza kubangua wanapeleka kwenye soko la Amerika na masharti mengine wale wananchi wa kawaida, yuko tayari kuwapa hata *passport* kusudi wakafike kwenye soko wakauze wenyewe, niseme nini zaidi ya hapo Bwana Chuachua? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chuachua naona ameridhika tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nasimama kwa vote hii ya 44 mshahara wa Waziri. Naomba nipate maelekezo ya kina kwa haya maelezo ambayo naenda kuyatoa vinginevyo nitashika shilingi katika mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchana wa leo niliweza kuchangia bajeti hapa ya Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Kimsingi Serikali imeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba inaandaa mazingira rafiki ya kuvutia wawekezaji kutoka nje na wawekezaji wa ndani. Mheshimiwa Waziri hapa amezungumza kwa kutamba kwelikweli wakati anajibu hoja za majumuisho juu ya kuvutia wawekezaji hawa na kwamba mazingira sasa hivi ni rafiki kwa wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali moja kwamba sijaona kwenye hotuba yake hii, namna gani atasimamia ama Serikali itasimamia suala zima la wawekezaji ndani ya nchi yetu sambamba na kumlinda mlaji wa bidhaa hizi ambazo zitakuwa sasa zinazalishwa kwa wingi kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri hapa alivyozungumza. (Makofi)

Kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi wa kina na wa kutosha kabisa ni namna gani Serikali italeti mkakati wa kumlinda mlaji hasa wa Tanzania waliowengi ambao ni maskini sana? (Makofi)

MWENYEKITI: Mtoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge ana hoja na Serikali kwenye hoja hizo ambazo anazisema tayari imekuwa ikichukua hatua. Ameelezea kuhusu mazingira ya uwekezaji na akaelezea kuhusu kumlinda mlaji. Kama umemsikia Mheshimiwa Rais mara nyingi sana amekuwa akisisitiza moja ya hatua ambazo zitatuwezesha kuhakikisha kwamba mlaji analindwa ni kuwa na bidhaa zetu wenyewe ambazo zimezalishwa kwa uhakika na zimetimiza vigezo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kulinda uwekezaji Mheshimiwa Rais, ameonyesha dhamira yake ya dhati kuanzia mwanzo tu pale aliposisitiza kuhusu kulinda uzalishaji kutokana na bidhaa zile kutumika katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba zinachochea uzalishaji. Taasisi ambazo zinahusika na kulinda mlaji moja iko Wizara ya Afya, lakini nyingine iko chini ya Wizara ya Viwanda, zote hizi utaona katika siku za hivi karibuni zimekuwa zikifanya operesheni kuhakikisha kwamba vile vitu ambavyo vinawafikia wananchi ni vile ambavyo vinakidhi vigezo kwa ajili ya kuwalinda walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Mheshimiwa Mbunge achukue *commitment* ya Serikali kwamba Serikali iko makini kuanzia kuchukua hatua za uzalishaji wa bidhaa zetu ili kuondokana na bidhaa ambazo ziko *inferior* ambazo zingeweza kutoka Mataifa mengine na kuja hapa kama *dumping*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ni kuhakikisha tunazalisha zile bidhaa ambazo ni za kiwango, ambazo soko la kwanza ni la kwetu wenyewe na tukitosheleza tupeleke na masoko ya majirani zetu. Hayo ni kwa ajili ya bidhaa nyingi zikiwa ni pamoja na mafuta ya kula, sukari, pamoja na bidhaa zingine za matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kuhakikisha kwamba uangalizi unafanyika *control* imekuwa *strengthen* kuanzia bandarini, Mamlaka ya Mapato lakini pia kwenye Taasisi hizi ambazo ziko kwenye udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge upitishie bajeti hii pacha wangu aingie kazini na wewe utaendelea kupata ripoti tena siyo kwa kuandikiwa bali kwa kuona shughuli inayoendelea *site* kama ambavyo umeendelea kuziona katika shughuli zingine. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, bado sijapata majibu ya msingi juu ya hoja yangu niliyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni sisi wote ni mashahidi kwamba Serikali imetoa kauli ya kwamba kuna walanguzi wana lingua sukari kwa mfano na wakasema kwamba bei ya sukari lazima iwe ni bei ile elekezi ya shilingi 1,800 kwa kilo na tumeshuhudia pia kupitia vyombo vya habari kwamba, sukari imenyang'anywa kwa wawekezaji ambao ni mabepari kwa wafanyabiashara na kuweza kugaiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ambayo nilizungumza pia mchana wa leo hii wakati nikichangia bajeti, kwamba kiwanda cha Dangote kinazalisha *cement*, kwa mfano kule mikoa ya Kusini Mtwara na Lindi bei ni shilingi 13,000 mfuko mmoja, lakini *cement* hiyo ikisafirishwa kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kilometa takribani 500, *cement* bei yake ni shilingi 11,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la ajabu sana kwamba Serikali hii inashindwaje kusimamia bei hii ya *cement* pale inapozalishwa mikoa ya Kusini iwe ni bei kubwa lakini ikisafirishwa na huyu huyu mwekezaji kuleta Dar es Salaam na maeneo mengine inakuwa ni bei ya chini wakati imesafiri kwa umbali mrefu. Nilikuwa naomba nipate ufafanuzi wa kutosha juu ya hili kwamba Serikali inatoa kauli gani? Hivi sasa juu ya kudhibiti bei hii ya *cement* mikoa ya Kusini ifanane na mikoa mingine ya Tanzania? Kama sijapata maelezo ya kutosha naomba kutoa shilingi. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja!

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maftaha Abdallah, nawajibika kulinda maslahi ya mlaji kwa kuangalia ubora, ujazo, bei na ndiyo maana nina vyombo kama *TBS* kuweza kuangalia vitu kama hivyo *weights and measures* kuangalia shughuli kama hizo.

Mheshimiwa Maftaha mimi nina maslahi makubwa na Mtwara, tukipata muda nitakusimulia sitaki kutonesha kidonda kilichokwisha kukauka. Hata ukiwauliza wazee wa Mtwara wanafahamu vizuri sana. Busara ya kawaida bei inapaswa kuwa *cost plus* gharama ya kuzalisha na faida kidogo ya mzalishaji kujumlisha gharama ya usafirishaji. Ndiyo maana mafuta Dar es Salaam,

yanauzwa bei nafuu kuliko yanavyouzwa Dodoma. Umelizungumza la Dangote hatuwaingilii watu wanaopanga bei, lakini hili la Dangote nitakwenda nimueleze kwa sababu nina mamlaka naye. Dangote anatutegemea tuweze kumpa gesi, hajaanza kuchakata kutumia gesi. Kwa hiyo, lakini na yeye ni Mwekezaji mzuri, nitazungumza naye, nianze niangalie ni mkakati gani anataka kutumia. Mimi ni mtaalamu wa masoko yeye kitu anachotaka kufanya anataka kushambualia soko la Dar es salaam kuwazuia hawa akina *Twiga cement* na *Simba cement wa-suffocate*, lakini anaisahau Mtwara nimekwambia sitaki kukumbusha mambo ya zamani. Lakini waulize wazee wa Mtwara wa kusimulie wananifahamu vizuri nimesoma dua mimi Mtwara! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi na ninakueleza kukuonesha uwezo wangu, wewe nirudishie shilingi yangu, kanuni inasema *cost plus* nitamuita huyo Meneja wa Dangote nitamueleza anaweza kuwa amepotoshwa, lakini mkakati wake ambao nimeshagundua hapa anachotaka kufanya ni kumzuia Simba na Twiga wasimkabili. Niwaelezee kitu kimoja Watanzania mkubali, sasa hivi tunazalisha saruji, uwezo wetu wa kuzalisha ni tani milioni 8.7. Mahitaji ya nchi ni milioni 4.3, kwa hiyo kuna ugavi mwingi kuliko mahitaji yetu, wameanza kuminyana hata *clinker*, nakwenda kuzuia *clinker* isitoke nje, watumie *clinker* ya Mtwara watumie ya Tanga hakuna kuitoa nje, atakaye itoa nje tutaizuia bandarini.

Kwa hiyo tumeshashika mpini Mheshimiwa Maftaha tumeshashika mpini bei zitarekebisha tuende taratibu, sina sheria za kumwambia shusha lakini najua dua nitakayomsomea nitamsomea dua hiyo mambo yatakuwa mazuri. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Kangi Lugola.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko kwenye *General Tyre*. Wabunge wengi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri walikuwa wanahoji kwa nini bajeti imetengwa kidogo kwenye suala la ujenzi wa viwanda? Wabunge walidhani kwamba Serikali yenyewe ndiyo itakayojenga viwanda, lakini Mheshimiwa Waziri akatueleza vizuri kwamba sera ya Serikali yetu, ya nchi kwenye viwanda ni kwamba Serikali haijengi viwanda isipokuwa yenyewe itaandaa mazingira wezeshi ili watu binafsi waweze kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje kama hiyo ndiyo sera ya viwanda, imekuwaje kwenye *issue* ya *General Tyre* mambo sasa ni tofauti. Serikali yenyewe sasa ndiyo imeamua tena kununua na hisa zingine 100, zile 26 na kwamba sasa Serikali inamiliki hisa zote 100 za *General Tyre* na kwamba sasa Serikali ndiyo itakayoendesha kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwishoni Mheshimiwa Waziri nikukumbushe katika ukurasa wa 49, umesema mradi huo ambao ni kielelezo tunataka ujiendeshe kwa kuwa na menejimenti huru yenye watu weledi katika biashara ya matairi na bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba mkishafufua hicho kiwanda kwa menejimenti huru hutakuwa na mamlaka tena ya kuteua kuanzia *Chief Executive Officer* ni watu huru maana yake tena wataenda kwenye *private sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiye nilisimama kwenye Bunge la Kumi juu ya *General Tyre* ilipotaka kuuzwa kwenye mnada wa bei ya kutupwa. Serikali kupitia Mahakama Kuu wakapitisha *injunction order* ya kusimamisha uuzaji wa *General Tyre*. Pia nilikuwa kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma ambapo kiwanda hiki *under government guarantee* waliweza kuwapatia *General Tyre* dola za kimarekani milioni kumi, kufufua kiwanda hiki, fedha zote zikaliwa hawakufufua kiwanda. Lakini pia kwenye Bunge la Bajeti mwaka jana tulitenga shilingi bilioni mbili, milioni 150 kufufua kiwanda hicho, lakini mpaka leo hakijafufuliwa na hakuna maelezo juu ya fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatenga tena milioni 150, nahitaji maelezo ya kina kwa nini tunakuwa na ndimi mbili kama nyoka? Tunasema viwanda Serikali haingii ni kuweka mazingira wezeshi, lakini kwa *General Tyre* tumeingia asilimia mia. Fedha hizi zitapotea nina wasiwasi nataka maelezo ya kina kwa nini *General Tyre* pia isiende kwenye mfumo huu wa *private sector*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante mtoa hoja kwa ufupi kabisa.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jambo moja linalonipa faraja Mheshimiwa Kangi Lugola anaonekana ana *information* kuhusu *General Tyre*. Amekumbuka kwamba iliwekwa milioni mbili kufufua kiwanda cha *General Tyre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, busara ya kawaida itakuonyesha kwamba bilioni mbili haziwezi kufufua *General Tyre*. Bahati mbaya ameondoka Mheshimiwa Lema hapa, ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira. Ukitaka kuifufua *General Tyre* kwa mtindo mliokuwa mnakwenda nao, ule mliopendekeza wa kutumia ile mitambo ambayo Mwalimu alinunua miaka ya 1960, kwa kiwanda amabako kimekaa miaka kumi hakijafanya kazi mtakuwa mnatwanga maji kwenye kinu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo nikaamua na wataalamu wangu kwamba hapa tulipo *enough is enough*, tuende tutafute wataalam nguli katika biashara ya matairi watuandikie andiko la uhakika tufanye nini? Lakini baadhi

ya pesa hizo ziendeele kuangalia mashamba yetu ya mpira yaliyoko Muheza na yaliyoko Morogoro, wakati tutaya-*maintain* mashamba yetu tuje tuletewe jibu, tunaletewa mitambo ya namna gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutumia bilioni mbili, ukaweka kwenye zile *mould* za kizamani ambazo matairi yalikuwa yanaendeshwa kwenye *land rover* za 108, magari ya siku hizi hayatafanya kazi. Kwa hiyo, mimi nataka majibu na majibu ya wataalam ndiyo yataniongoza nifanye nini? Sintalaumiwa kwenye hilo, nimelisimamisha hilo na hilo sipepesi macho, ni msimamo ambao nimeusimamia nawajibika kwao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ni kwa dhamira nzuri tunao mpira utaandaliwa wa Muheza na Morogoro, pia tutawaajiri ma-*consultant* watueleze kitu gani, kwa hiyo siwezi kuendelea na utaratibu wa kutwanga pesa kwenye mitambo ile ya kizamani. Kwa nia hiyo nimeamua kwamba tutenge shilingi milioni 150, zi-*maintain* yale mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tupate wataalam watuongoze, tukishaongozwa na wataalam tunaanza, dhana ninayokuja nayo, na inayotumika mjini ni hii, kuleta wataalamu weledi siyo kwamba tunapotosha, tutabaki na *share* zetu, ukisoma maandiko yangu vizuri inasema viwanda vyote vitakwenda kwenye soko la hisa la *Dar es Salaam Stock Exchange* Watanzania wote tutamiliki pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Dar es Salaam Stock Exchange* tuta-own lakini itakuwa ni shirika letu, tutakuwa na mamlaka tutaleta *management* za wale nguli, wataalamu wakutoka Malaysia na wapi, waje waendeshe kwa amri zetu. Nataka kutumia viwanda hivi ndiyo maana ninaviita vya kimkakati, kuwapatia fursa watoto wetu waweze kuuonja Ukurugenzi, mimi nimepitia katika mikono hiyo, nimeajiriwa *TPDC*, nikasoma *TPDC*, nikakua mpaka kufikia hatua hii. Kama nisingekuwa kwenye shirika la namna hiyo ingekuwa ni taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti niwaeleze, Mheshimiwa Rais amezungumza leo Arusha kwamba *NSSF* ambayo alipoteza dola milioni kumi, kwa nini asiwekeze humo. Kwa hiyo watu wa kuwekeza ni *Social Security*, tutapata pesa za kitaalamu. Sitaki *story* kwamba nimenunua waya, *connector*, *wire* bilioni mbili hizo sitaki, nataka utaalam, ikibidi nitakuja Bungeni niwaoneshe wataalam, mimi sina siri, siri yangu ninayotaka ni mafanikio ya kuona tunakuwa na matairi yenye usalama nchini kwetu na mpira unapata soko. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2), tunaendelea na mafungu (*guillotine*). Katibu tuendeele.

Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

MATUMIZI YA KAWAIDA

Kif.1001 Admn. and HR Mgt.	Sh. 10,355,266,000
Kif.1002 Finance and Accounts.....	Sh. 427,497,000
Kif.1003 Policy and Planning.....	Sh. 3,420,446,000
Kif.1004 Gvt. Comm. Unit	Sh.152,482,000
Kif. 1005 Internal Audit Unit	Sh.196,089,000
Kif. 1006 Legal Service Unit.....	Sh. 85,048,000
Kif. 1007 Mgt. Info. System.....	Sh. 243,663,000
Kif. 1008 Procurement Mgt. Unit.....	Sh. 245,374,000
Kif. 2001 Industry.....	Sh. 5,137,005,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif.2002 Small & Medium Enterprises Division...	Sh. 5,386,458,000
Kif. 3001 Commerce.....	Sh. 2,871,303,000
Kif. 4002 Commodity Market Dev.....	Sh.13,351,361,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

Kif. 1003 Policy and Planning.....	Sh. 17,000,000,000
Kif. 2001 Industry.....	Sh. 13,360,000,000
Kif. 2002 Small & Medium Enterprises Div.....	Sh. 3,040,000,000
Kif. Commodity Market Dev.....	Sh. 6,600,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mtoa hoja taarifa!

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Taasisi zake zote, kifungu kwa kifungu na kuvipitisha bila marekebisho yoyote, kwa hiyo naomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2016/2017
ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge natangaza kwamba, bajeti ya matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepitishwa na Bunge hili, na nimtakie kila la heri Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, ili Tanzania yenye viwanda iwezekane. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Bunge kuna matangazo hapa mawili.

Moja linatoka kwa Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM, anaomba Wabunge Wanawake wote wa CCM wahudhurie kikao cha leo mara baada ya kuahirisha kikao hiki, katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Halima Bulembo, anatangaza kupotelewa na simu yake aina ya *Iphone 6* humu Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo na kwa vile shughuli za leo zimeishia hapa, naliahirisha Bunge hili hadi kesho tarehe 10 Mei, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne,
Tarehe 10 Mei, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*